

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 5 Mei, 2016**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu lakini Kikao cha Kumi na Tatu. Katibu!

**KATIBU WA BUNGE – DKT. THOMAS KASHILILAH:** Hati za Kuwasilisha Mezani.

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MHE. CECILIA D. PARESSO – (K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Parezzo asante sana. Katibu!

**KATIBU WA BUNGE – DKT. THOMAS KASHILILAH:** Maswali kwa Waziri Mkuu!

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba usogee hapo mbele. Simwoni Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kwa hiyo, tunaendelea na walioomba kama kawaida. Leo tutaanza na CUF, Mheshimiwa Katani Ahmad Katani, Mbunge wa Tandahimba, swali la kwanza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza naishukuru Serikali yako kwa kuondoa tozo kadhaa kwenye zao la korosho. Swali langu ni je, pamoja na kuondoa tozo hizo, Serikali imeendelea kumnyonya mkulima kwa kukata asilimia 15 ya bei ya soko. Je, Serikali ina mkakati gani kuendelea kumwondolea mkulima tozo hii ambayo ni kubwa sana?

**SPIKA:** Jibu swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katani, Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Katani pamoja na Wabunge wote wanaotoka mikoa inayolima korosho kwa kazi kubwa waliyoifanya kubainisha matatizo makubwa yanayowapata wananchi wanaolima korosho na hasa wanapolalamikia mfumo ulio bora na imara, lakini kutokana tu na kuwa na tozo nyingi, kama ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya maamuzi ya kupunguza tozo zote za hovy ambazo zilipangwa tu kwa lengo la kutaka kuvuruga mfumo na hatimaye wananchi wakachukia kutumia mfumo ambao unawaletea tija kwenye zao lao la korosho. Hii ni pamoja na tozo za asilimia 15 ambazo zipo miongoni mwa zile tozo, lakini tozo hii ya asilimia 15 kwenye orodha ya zile tozo, ilikuwa iko kwenye eneo la manunuzi ya vifungashio. Vifungashio; kuna magunia ambayo bei yake ni ya juu kidogo, pamoja na nyuzi.

Mheshimiwa Spika, tozo hii sasa itakuwa imeondoka kwa kuwa tumeupa Mfuko unaoitwa Mfuko wa WAKFU, ambao unasimamia maendeleo ya zao la korosho. Mfuko huu umeundwa na wadau wenyewe na unachangiwa na tozo za korosho zinazouzwa nje ya nchi. Inaitwa *Export Levy*, ambayo inachangiwa kwa asilimia 65 na tozo hii huwa inatozwa na TRA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mfuko wetu wa WAKFU kwa asilimia zile 65, sasa hivi wana hela nyingi sana kwa ajili ya kukamilisha madhumuni ambayo yamepangwa na wadau ikiwemo na kuhakikisha kwamba, masoko ya zao la korosho yanapatikana. Pili, kuhakikisha kwamba, wananunua pembejeo kwa maana ya mbolea na mbegu, kusimamia uboreshaji wa mbegu hizo na kupanua mashamba ya korosho; pamoja na kugharamia tafiti mbalimbali ambazo zinatakiwa ziwe zinafanywa kwa ajili ya kupata ubora wa zao la korosho.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Katani na Wabunge wote wanaotoka mikoa ya korosho, tozo hii iko sasa kwenye Mfuko wa WAKFU ambao umeingia kwa ajili ya kununulia vifungashio na kwa hiyo, mkulima kwa sasa hana tozo hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani, swali la nyongeza!

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru. Swali langu la nyongeza ni je, wale wakulima ambao korosho zao zimepotea zikiwa ghalani na Serikali ndiyo ilifanya uzembe kwa kuweka dhamana ndogo kwa mwendesha ghala, Serikali iko tayari sasa kuwalipa wakulima wale ambao pesa zao bado wanawadai? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Katani, Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli uko uendeshaji wa hovyoyote wa Vyama vya Msingi, pamoja na Vyama Vikuu, vinavyosimamia korosho na ndiyo sababu Serikali imesimamia kidete kwenye mazao yote; korosho, pamoja na mazao mengine, kuweka usimamizi wa dhati wa kuhakikisha kwamba wakulima sasa wanapata tija kwenye masoko ambayo wanapeleka mazao yao ili waanze kunufaika na mazao waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Katani anataka kujua wale waliopoteza korosho. Mifumo inayotumika pale, mara nyingi haisimamiwi na Serikali bali na Vyama vyao wenyewe vya Ushirika ambapo wao wenyewe wamechagua ushirika wao, ukisimamiwa na Mrajisi ambaye ndiye pia tumemtaka asimamie kwa dhati namna ya kuuza mazao hayo, pamoja na kutafuta masoko yake ili

wakulima waweze kupata fedha. Sasa wakulima wote ambao wamepoteza korosho, wajibu wao wa kwanza ni kuwauliza viongozi wao wa Chama cha Msingi na Chama Kikuu, kupitia mikutano yao. Wanayo mikutano yao ya haki kabisa na ya msingi na wanayo nafasi ya kuwahoji viongozi wao wa ushirika wa Chama cha Msingi AMCOS pamoja na Chama Kikuu, kwa vyama vile vikuu vinavyoongoza zao hilo la korosho.

Mheshimiwa Spika, pale itakapoonekana hawajaridhika na majibu hayo, wanachama wenyewe wanao uwezo wa kuwapeleka Mahakamani ili Sheria iweze kufuata mkondo wake. Mahakama maamuzi yake yatakayotolewa, ndiyo yale ambayo yataweza kuwawajibisha viongozi wa hovy, ambao pia wanawasababishia wakulima kupoteza mazao yao. Hii sasa siyo kwa korosho tu; kwa mazao kama pamba, tumbaku, kahawa; yote haya ni mazao ambayo yanauzwa kwa utaratibu ambao sasa tunataka tuusimamie, tuhakikishe kwamba wakulima wanapata tija. Mazao haya ndiyo yanaipatia pato Serikali, lakini wakulima ndiyo wanategemea sana katika kuendesha shughuli zao.

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Swali linalofuata litaulizwa na Mbunge wa Sikonge, Mheshimiwa Joseph George Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu; katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na migogoro mingi sana baina ya wafugaji na wakulima kwa upande mmoja, kugombea maeneo; lakini pia baina ya wakulima, wafugaji na maliasili, kwa upande mwingine. Hii ni katika maeneo mengi ya nchi. Sasa kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi yako maelekezo kwamba Serikali itapima maeneo mapya kwa ajili ya wakulima na wafugaji hususan kuongeza eneo la wafugaji kutoka hekta milioni moja hadi milioni tano:-

Swali, je, ni lini Serikali itateua Kamati ya Kitaifa ambayo itapitia maeneo yote na kutoa mapendekezo yatakayotekelezwa ili kuondoa migogoro hii na watu waendeleo kuishi kwa amani? Hii kazi inahitaji msaada zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante kwa swali lako. Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakunda Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba sasa hivi tunayo migogoro mingi sana ya wafugaji na wakulima, lakini pia hata migogoro ya ardhi yenyewe tu baina ya jamii zetu; mtu mmoja mmoja lakini pia na jamii na jamii. Migogoro hii tumefika wakati sasa tunatakiwa kuitafutia ufumbuzi. Jambo ambalo amelieleza Mheshimiwa Mbunge ni miongoni mwa mikakati ambayo sisi tunayo pia.

Mheshimiwa Spika, moja, tumeanza kutafuta njia sahihi ya kuondoa migogoro ya ardhi na hii inatokana na kuongezeka kwa matumizi na mahitaji ya ardhi na thamani ya ardhi. Pili, kumetokana na matatizo makubwa yaliyojitokeza kwenye maeneo yale ya mipaka kutokana na mahitaji ya kupanua eneo; kuongezeka kwa mifugo mingi; lakini wakati mwingine ni utendaji wa hovyotwa wa Watendaji wetu wa Serikali ambao tumewapa dhamana kwenye maeneo yale. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia tunao wawekezaji ambao wanaingia kinyemela kwenye maeneo yetu na wanapoingia kule wanajichukulia ardhi na kuongeza maeneo bila ridhaa ya wananchi wenyewe na kusababisha migogoro mingi. Kwa hiyo, jukumu la Serikali ambalo pia Mheshimiwa Mbunge amesema, ni kweli tuliamua tuunde *task force* inayounganisha Wizara tatu; Wizara ya Ardhi yenyewe, Wizara ya Maliasili, pamoja na Wizara ya Kilimo ili tuweze kubaini mipaka yote, tuweze kubainisha maeneo haya ili kila mmoja ajue anakaa wapi na vinginevyo, kwa kupima maeneo haya na kuweka mipango bora ya matumizi ya ardhi yanayobainisha maeneo ya wafugaji, wakulima, viwanda na maeneo ya makazi ya kawaida. Kwa hiyo, *task force* hii kwanza tumezipa Wizara zenyewe majukumu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili ituambie kwenye maeneo yale na ukomo wake, wanaishia wapi. Wizara ya Kilimo nayo watuoneshe wananchi wanaishia wapi na kilimo wapi baadaye sasa tumwite Waziri wa Ardhi wakae pamoja, tuweze kuweka mipaka mipya. Hii ikiwemo na kuongeza maeneo ya wafugaji kama ambavyo sasa tumeamua wafugaji wote sasa kuwatengea maeneo, kutumia *ranch* zetu za Taifa na mkakati huu ni ule wa kuboresha mifugo yetu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaofuga kawaida, watakuwa wanapeleka mifugo yao kwenye maeneo ambayo tumewatengea kama *ranch* ambayo mimi mwenyewe nimetembea; nimekwenda Mkoa wa Kagera kuona kule Misenyi, Karagwe lakini pia nimekwenda na Ngara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wetu ni kuwapeleka wafugaji kwenye maeneo yale, tunataka tuwamilikishe kwenye zile *blocks*. Wafugaji wote wenye mifugo mingi wakae kwenye maeneo yale ili sasa waweze kulisha, kuogesha, wanenepeshe, waweze kuuza maeneo ya nje. Huku vijijini kutakuwa na ng'ombe hawa wachache ambao watakuwa wanaenda *ranch* kwa kuwapa maeneo hayo ya wafugaji, baada ya kuwa tumeweka mpango bora wa matumizi.

Kwa hiyo, Tume ile itakapoundwa, tutaita maeneo hasa yenye migogoro. Simiyu nimekwenda nimeona migogoro mingi, kwa hiyo, maeneo kama hayo yatapata kipaumbele katika kuanza na zoezi hili. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda swali fupi la nyongeza!

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni lini atakuwa tayari kutembea Tabora ili nako ajionee migogoro hasa katika Wilaya ya Sikonge?

**SPIKA:** Swali hilo fupi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kwamba, nimeamua kufanya ziara katika Mkoa wa Tabora baada tu ya Bunge hili kwa sababu mbili. Moja, kufanya hilo, lakini pili nakuja kuongea na wadau wa zao la tumbaku; nakuja kufanya mapitio ya zao la tumbaku ambalo limekuwa kero kubwa. Nakuja kuongea na wakulima wenyewe, Viongozi wa Vyama vyao vya Msingi, kuongea na wafanyabiashara na wenye viwanda ili tubaini tatizo liko wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mkakati ambao tumeufanya kwenye zao la korosho, tunahamia kwenye tumbaku na baadaye tunakwenda kwenye pamba, tutakwenda na kwenye kahawa vile vile, kwa lengo la kuwapa tija wananchi waone kabisa kwamba sasa ni wakati wao wa kupata tija ya mazao wanayoyalima ili waweze kupata manufaa. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa tunahamia CHADEMA, Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha, uliza swali lako.

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Serikali yetu ya Tanzania ilisaini na kuridhia ule Mkataba wa Kimataifa wa 2006 kuhusu haki za watu wenye ulemavu, uliridhiwa, yaani ulikuwa *ratified* mwaka 2009. Utaratibu ni kwamba baada ya miaka miwili baada ya kuridhia, Serikali inatakiwa kuandika *State Report* na kuiwakilisha kwa ile Kamati ya Umoja wa Mataifa inayosimamia utekelezaji wa huo mkataba.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali yetu haijaandika hiyo *State Report*, sasa ni miaka minne *overdue*. Ni kwa sababu gani, Serikali yetu haijapeleka *State Report* kuhusu huo Mkataba wa Watu Wenye Ulemavu? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Macha, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeridhia mikataba mingi sana, kwa lengo la kuunganisha Taifa letu na mataakwa yetu na Mataifa na Taasisi mbalimbali za Kimataifa ili kuweza kufungua milango ya huduma mbalimbali, mahitaji mbalimbali ya nchi na Mataifa ya nje ikiwemo na jambo ambalo Mheshimiwa Macha amelieleza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu imedhamiria kufungua milango na kutoa huduma na kuweza kuwafanya ndugu zetu wenye mahitaji maalum kuwa ni sehemu ya wachangiaji wakubwa wa shughuli mbalimbali za maendeleo nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumefungua milango hiyo, Serikali ya Awamu ya Tatu, Serikali ya Awamu ya Nne imeweza kuwashirikisha kikamilifu Watanzania wote ambao wana mahitaji maalum na katika kuweza kuona katika kupata mchango wao ili pia waweze kutoa mchango wao kikamilifu, ikiwemo na mikataba hii. Mikataba hii baada ya kuwa tumeunda Serikali yetu, tutafanya mapitio ya kazi zote zile za Awamu ya Nne ambazo zilikuwa zimefikiwa na sasa tuweze kuunganisha na mkakati ambao Mheshimiwa Rais ameueka wa kuunda Wizara inayoshughulikia eneo la hilo na baadaye itafanya mapitio na imeshaanza kufanya mambo mengi ya kuweza kuridhia mikataba yote au kupitia mikataba yote ambayo tunadhani inaweza kuwaunganisha Watanzania wote kuweza kuridhia jambo ambalo tumekubaliana nalo. Kwa hiyo, hili ni pamoja na lile ambalo Mheshimiwa Macha amelieleza.

Mheshimiwa Spika, kwa mkakati tulionao, Mheshimiwa Dkt. Possi ameanza kukutana na wadau wenyewe kuanza kupitia mikataba ile kuona kama ina tija kwa Taifa, ina tija kwa ndugu zetu Watanzania ili sasa tuweze kuridhia. Kwa hiyo, taratibu zinaendelea na pindi itakapokamilika, tutaweza kukushirikisha Mheshimiwa Mbunge. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Elly Macha, umeridhika eh!

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Spika, swali moja dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante kwa majibu yako mazuri. Nafikiri huo mkataba una tija ndiyo maana Serikali yetu ulisharidhia. Naomba kuuliza, ni lini sasa hiyo ripoti itaandikwa na kupelekwa kwenye ile *Committee*?

**SPIKA:** Swali fupi, ni lini Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa sasa tuna Waziri mwenye dhamana na anayeshughulikia jambo hili au watu wenye mahitaji maalum na ameshaanza kazi ya kupitia shughuli mbalimbali na mahitaji yao na kuingiza kwenye mipango; na kwa kuwa pia mmesharidhia hata kwenye bajeti yetu, basi wakati wowote na wewe ukiwa



mmoja kati ya Wabunge hapa na Mheshimiwa Waziri yupo hapa, tunaamini unaweza kuwa mshiriki wa kwanza kati ya washiriki ambao tunataka tuwaingize kwenye orodha ya watakaokuwa wanafanya mapitio haya ili tuweze kuona kama jambo hilo sasa litakamilika wakati gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wakati wowote kuanzia sasa. Kwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Possi yupo, mtashirikiana naye katika hili na amelisikia, nimtaka tu sasa aanze mchakato huo mara moja kuwakusanya wadau wote ili tuanze kupitia mahitaji yale ili yaweze kutekelezwa katika kusaini mikataba yetu kama ambavyo tumekubaliana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tunarudi CCM, Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa Hassan Elias Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana...

**SPIKA:** Natumaini swali lako siyo la korosho, endelea. *(Kicheko)*

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo imenadiwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli mwaka 2015; moja ya ahadi kubwa ambayo ilitolewa kwa Watanzania ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Naomba kufahamu kupitia Serikali yetu, imejipanga vipi katika kutekeleza ahadi hii ambayo kimsingi inasubiriwa na Watanzania walio wengi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masala, Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, Mkoani Lindi, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nataka niwaambie Watanzania kwamba Chama cha Mapinduzi kupitia Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2015 imefafanua mambo mengi ambayo tumeamua tuyatekeleze katika kipindi cha miaka mitano. Jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua utekelezaji wake ni lini, nataka nimhakikishie kwamba ahadi zetu zote zilizoahidiwa na Chama cha Mapinduzi zitatekelezwa kama ambavyo zimeahidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumedhamiria kujenga barabara zetu kwa kiwango cha lami na tumeanza na mkakati wa kuunganisha barabara za ngazi za Mikoa, zinazounganisha Mikoa kwa Mikoa; tukishakamilisha hizo, tundaingia kwenye barabara zinazounganisha ngazi za Wilaya na barabara zote



ambazo zimeainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa awamu hii ni barabara ambazo zitakamilishwa kupitia bajeti ambayo sasa mnaipitisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi itakapokuja hapa, naomba niwashawishi Waheshimiwa Wabunge kuweza kuipitisha ili tuanze kazi ya kukamilisha barabara ambazo nimezitaja. Pale ambapo barabara za Mikoa hazijakamilika, tunataka tuzikamilishe. Tukishakamilisha hizo zote, tunaanza ngazi za Wilaya ili tuendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania wote kwamba ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais kwa kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 zitakamilishwa kama zilivyoahidiwa. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Masala, kama una swali la nyongeza!

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Waziri Mkuu swali hili nimekuuliza kwa makusudi kabisa na nimesoma vizuri Ilani yetu, lakini pia nimesoma uelekeo mzima wa Serikali yetu katika kutekeleza ahadi zake. Swali langu ambalo ningependa kukuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara kutoka Nanganga kwenda Nachingwea kilometa 44...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea, huwa hatubadilishi maswali.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Barabara ya kutoka Masasi kwenda Nachingwea nafikiri ni barabara ambazo toka tumepata uhuru bado ahadi zake...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea, bahati mbaya sana hujajiandaa vizuri.

Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke sasa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini tufanye mabadiliko, aliyekuwa unamwambia hajajiandaa vizuri sio Mheshimiwa Abdallah Mtolea. Abdallah Mtolea ndio mimi sasa.

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru umeweka vizuri. (Makofi)

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami kwa niaba ya wananchi wa Temeke niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunatambua kwamba mmiliki wa ardhi ya nchi hii ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kimsingi Serikali imekuwa iki-enjoy mamlaka hayo kwa kuchukua baadhi ya maeneo kwa ajili ya kukaribisha uwekezaji. Hili ni jambo zuri sana kukaribisha uwekezaji. Isipokuwa inasahau kitu kimoja, pale ambapo inawakaribisha hao wawekezaji, haizifanyi Halmashauri husika kuwa sehemu ya uwekezaji ule kwa maana ya uanahisa. Je, Serikali yako imejipangaje sasa kubadilisha mwelekeo huu ili kila unapowekwa uwekezaji ile Halmashauri iwe sehemu ya mwanahisa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mtolea, Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu imefungua milango kwa wawekezaji nchini kuwekeza kwenye sekta mbalimbali kulingana na matakwa ya mwekezaji. Uwekezaji huu unafanywa na unajikuta upo kwenye mamlaka zetu za Halmashauri ya Wilaya, Manispaa na maeneo mengine. Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama Serikali imejipangaje na Halmashauri hizi kuweza kunufaika na uwekezaji huu?

Mheshimiwa Spika, ni kweli. Sasa uwekezaji huu uko wa aina mbili; kuna uwekezaji ambao tumeutaka upitie kwenye Taasisi yetu ya Uwekezaji (*TIC*) ambapo *TIC* inayo Benki yake ya Ardhi na kwa kuwa ardhi ni ya Serikali, kwa hiyo *TIC* tumeweza kuwapa ardhi ambapo wao sasa wakipata mwekezaji mkubwa, wanaweza kwenda kuwekeza mahali. Kwa uwekezaji huu, wanapokwenda kuwekeza kwenye eneo lolote lile Halmashauri ndiyo ambayo itakuwa imetoa ardhi hiyo lakini kupitia *TIC* na uwekezaji huo, Halmashauri wanaweza kunufaika kwa tozo ya ile ardhi.

Mheshimiwa Spika, pia Halmashauri inaweza kunufaika pia kwa mwekezaji huyo kushiriki kikamilifu kwenye mipango ya maendeleo ya Halmashauri kwa kuchangia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yale. Pia kama kuna tozo nyingine na manufaa ya uwepo wa mradi wenyewe kama kuna bidhaa zinatengenezwa tunatarajia eneo hilo linaweza kunufaika kwanza kwa gharama nafuu kupitia uwekezaji ule.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji mwingine ni ule ambao Halmashauri yenyewe inakuwa na Benki yake ya ardhi ambayo inaamua sasa kutafuta wawekezaji ili kufanya maendeleo. Hii inanufaika zaidi kwa sababu kwanza

atapata tozo ya ardhi, lakini pili, naye anaweza kuwa ni sehemu ya mwanahisa wa mradi wenyewe kulingana na utaratibu atakaotumia; lakini atanufaika na manufaa yale yote ambayo nimeyataja kwamba mwekezaji anatakiwa atambue kwamba yeye yupo pale na wananchi waliopo maeneo yale watanufaika kupitia mradi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namna ambavyo Serikali tunasimamia jambo hili, kwanza tunahakikisha wawekezaji tunawatambua na uimara wao, ubora wao katika uwekezaji na tunawaunganisha na maeneo hayo ili waweze kujenga mshikamano katika kuwekeza ili pia na yeye aweze kupata *security* na Halmashauri kwenye maeneo hayo ziweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uwekezaji wa aina mbili; uwekezaji ambao wananufaika zaidi ni ule ambao Halmashauri yenyewe imetengeneza mpango wa matumizi ya ardhi lakini wametenga maeneo ya uwekezaji ili mwekezaji anapokuja, anakwenda kuwasiliana na Halmashauri. Kwa hiyo, pale wana-*negotiate*, wanaweza kukubaliana yale mambo ya msingi ili kuweza kupata tozo mbalimbali ikiwemo na Halmashauri yenyewe kutumia ardhi yake kuwa mwanahisa wa ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utakuta kuna tofauti kati ya ardhi inayomilikiwa na *TIC*, Taasisi ya Uwekezaji ambayo inakwenda kumpeleka mwekezaji ili awekeze chini ya Taasisi ya Uwekezaji na ile ardhi ambayo mwekezaji anakwenda kwa uwekezaji chini ya Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, maeneo haya yote utofauti wake ni kama ambavyo nimeweza kuutofautisha na namna ambavyo unaweza kunufaika. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, swali la nyongeza!

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru kwa majibu yako mazuri, lakini pamoja na hayo, hizi tozo zinazotokana na ardhi kwa maana ya *Property Tax* na *Service Levy*, *it's just a peanut* kwenye uwekezaji ambao umekuwa ukifanyika. Kwa mfano, katika uwekezaji wa *EPZA* ambao unafanyika katika Kata ya Kurasini kwenye Halmashauri ya Temeke; ardhi ambayo Halmashauri tumeitoa, kwa sasa ina thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 100. Unatoa ardhi ya shilingi bilioni 100 halafu uende ukasubiri mrejesho kwa kupitia *Property Tax* na *Service Levy* vinakuwa havifanani. Hivi kweli Ofisi yako haioni umuhimu wa kuifanya Halmashauri ya Temeke kupata angalau hisa 10 katika uwekezaji huu? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtolea Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Wakati huu tukiwa tunafanya mabadiliko makubwa na mapitio makubwa kwenye uwekezaji katika maeneo yote, tunaanza kugundua baadhi ya changamoto ambazo zinajitokeza, lakini pia usimamizi wa maeneo hayo pia tumeanza kuona kwamba upo umuhimu wa mamlaka yenyewe kuwa inaweza kuweka mipango yake ili iweze kupata manufaa ya uwekezaji uliopo. Moja kati ya mifano niliyonayo kwenye Halmashauri ya Temeke ni pale Temeke mwisho eneo ambalo mmebomoa majengo na sasa mmepata mwekezaji wa kampuni moja ya Kichina.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ndiyo inafanya maamuzi ya uwekezaji ule na ndiyo aina nyingine ya uwekezaji nilioutaja kwamba Halmashauri inaweza kunufaika zaidi. Sasa hivi mpo kwenye mjadala wa manufaa yenyewe na tozo ambazo mtazipata kutoka kwenye kampuni ile. Kwa hiyo, utaratibu ule pamoja na usimamizi wa Halmashauri yenyewe, lakini bado Serikali sasa tunataka tuipeleke ili iweze kuona kwamba je, Halmashauri yetu inaweza kunufaika?

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema sasa ni kwamba, Serikali inaandaa utaratibu wa kusimamia uwekezaji wa namna hii ili Halmashauri zetu za Wilaya, Manispaa ziweze kupata tija kwenye uwekezaji ambao sasa tumefungua milango kwa wingi na watu wengi wanaingia kwa ajili ya uwekezaji ili Halmashauri zetu zisiweze kukosea.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa Halmashauri zote nchini na Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani, tuzingatie sana kwamba uwekezaji huu unaofanywa kwenye maeneo yetu unaleta tija kwenye Halmashauri zetu na lazima tusimamie hilo kwa pamoja na Serikali itaanza kufanya ufuatiliaji wa kina kuona kuwa uwekezaji ule kwenye Halmashauri zile za Wilaya unawaletea tija Wanahalmashauri hiyo wakiwemo Baraza la Madiwani ambao ndiyo wasimamizi wakuu. Kwa hiyo, tutaendelea kufuatilia uwekezaji huu tuone tija ambayo inaweza kupata pia Halmashauri zetu kote nchini. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunarudi sasa CCM wanawake, Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi!

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, mvua zimenyesha pasipo kueleweka, zimekwenda kuua mazao mengi sana katika maeneo mbalimbali, hali ambayo inaonesha kabisa kuna viashiria vya njaa huo mbele tunapokwenda. Je, Serikali yetu imejipanga vipi katika kukabiliana na janga kubwa la njaa ambalo linaweza kuja baadaye kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa? Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kisangi, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia swali hili kwanza naomba nitoe pole kwa wananchi wote ambao wamekumbwa na matatizo makubwa ya mafuriko. Mafuriko haya yameleta madhara makubwa ya vifo, uharibifu wa mali, lakini pia mashamba yetu yote yamesombwa na maji. Nilisema hapa nilipokuwa nahitimisha hoja yangu wiki iliyopita kwa kuwatahadharisha Watanzania baada ya kuwa tumepata taarifa kutoka chombo chetu cha hali ya hewa kwamba mvua hizi bado zinaendelea. Ntoa pole kwa watu wa Kilosa, ntoa pole kwa watu wa Moshi Vijijini na Rombo ambako pia ndugu zetu wengi wamepoteza maisha na madhara hayo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kuwahudumia Watanzania wote wanaopata madhara na mpango huu upo kwenye Ofisi yangu kupitia Kitengo cha Maafa. Tunaendelea kufanya tathmini na tathmini hii inafanywa kwanza na Halmashauri zote zote za Wilaya ambazo ndiyo zimeunda Kamati ya Maafa kwenye maeneo yao. Wakishafanya tathmini, Mkoa unafanya mapitio na mahitaji yao halafu wanatuletea ofisini kwetu; nasi tunapeleka misaada kadiri walivyoomba kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tuna hifadhi ya chakula, yaani tunacho chakula cha kutosha cha kupeleka kwenye maeneo hayo na tayari tumeshaanza kupeleka chakula kwenye maeneo yote yaliyopata maafa. Tumejiimarisha tena kwa ajili ya maafa haya yanapoweza kutokea hapo baadaye na kutumia msimu huu wa kilimo kwa maeneo ambayo hayajapata madhara.

Nataka nitoe wito kwamba tulime sana, tupate chakula kingi tuweze kutunisha hifadhi yetu ya chakula ili pia tunapopata tatizo la mahitaji ya chakula, basi chakula hicho tuweze kukipeleka maeneo yote yenye maafa.

Mheshimiwa Spika, pia kitengo hiki sasa tunakiboresha, tunaanza mazungumzo ndani ya Serikali kuifanya kuwa agency ambayo itakuwa inaratibu shughuli zote za maafa popote nchini, ambapo tutakuwa tunatengea fedha ziweze kutafuta maturubai au vibanda vya kujihifadhi kwa muda mfupi lakini pia kununua vyakula, madawa na mahitaji mengine ili yanapotokea tu maafa kama haya, basi kitengo chetu kiende mara moja.

Kwa sasa tumejiimarisha vizuri, maeneo yote yenye maafa tumeshayapitia na wataalam wetu wapo huko kwenye maafa ili kunusuru

maisha ya Watanzania wenzetu ambao sasa wamepata mahangaiko kutokana na mvua nyingi ambazo zimenyesha.

Mheshimiwa Spika, pia tahadhari kwa wale wote ambao wako kwenye mabonde, narudia tena, nataka niwasihi Watanzania wote ambao wako kwenye maeneo hatarishi wapishe maeneo hayo, watafute maeneo mazuri. Viongozi wa Serikali za Vijiji, Kata na Wilaya wawasaidie Watanzania hao kuwapeleka maeneo sahihi ili waweze kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza itakapotokeza mvua nyingi kunyesha tena ambazo zinaendelea kwa sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, CHADEMA; Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa na mimi nimwulize Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni dhahiri kwamba wanafunzi hawatakiwi kufanya siasa Vyuoni, lakini kumekuwepo na ama mkakati au maelekezo ambapo Menejimenti ya Vyuo inawanyanyasa wanafunzi wanaokuwa hawapendezwi na siasa ya Chama cha Mapinduzi. Je, ni kweli kwamba kuna hayo maelekezo? Kama hakuna maelekezo, Serikali inazieleza nini sasa Menejimenti za Vyuo kuhusu hii tabia ambayo imejengeka ya kuwanyanyasa vijana na hata kuthubutu kuingilia Uongozi wa Serikali za Wanafunzi? Mojawapo ya Chuo ambacho kimekithiri ni Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sina hakika kama swali hili linakubalika! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka nikanushe kwamba siyo kweli kwamba kuna maelekezo kwenye Vyuo vyote vya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, hakuna unyanyasaji wowote unaofanywa kwenye Vyuo kwa wanafunzi ambao... *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Uongo! *(Kelele/Makofi)*

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Wamepigika sana hao!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, narudia tena. Hakuna unyanyasaji wowote wa Vyuo... *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Upo!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Watanzania wote wanao uhuru wa kujiunga na vyama vyovyote wanavyovitaka, lakini kila eneo limeweka utaratibu wake. Hakuna zuio la wafanyakazi kujiunga na vyama vyovyote lakini liko zuio la mtumishi anapokuwa kazini kuendesha siasa. Hakuna zuio la mwanafunzi yeyote kama Mtanzania kujiunga na Chama anachokitaka yeye, lakini zuio ni kwamba hutakiwi kufanya siasa wakati wa masomo ili u-*concentrate* na masomo yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaweza kutokea labda vijana wawili wenye itikadi tofauti huko wakafanya mambo yao, wakatofautiana huko, huo siyo utaratibu wa Serikali, ni utaratibu wao wao wenyewe. Kwa hiyo, nawaomba sana niwasihi Viongozi wa Vyama vya Siasa, tusilione hili kama ni msimamo wa Serikali, badala yake tulione hili kama ni mapenzi ya watu wengine, kama ambavyo vijana wafanyabiashara huko wanavyoweza kukorofishana mahali pao, lakini haina maana kwamba yule wa Chama Tawala anapokorofishana na mtu mwingine wa Chama cha Upinzani huko kwenye biashara zao tukasema labda soko lile, Chama Tawala kimepeleka watu wake kuzuia watu wa Vyama vingine wafanye vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwasihi Watanzania wote; Tanzania hii ni yetu sote na tunahitaji maendeleo ya Watanzania wote. Kila mmoja anao uhuru wa kupenda Chama anachokitaka. Kama kuna maeneo yanabana kisheria na kwa utaratibu wa matumizi au matakwa hayo kuyapeleka maeneo hayo, lazima yazingatiwe. Serikali hii itaendelea kuwatumikia Watanzania wote bila kujali Vyama vyao; tutaendelea kuwahudumia Watanzania wote bila kujali Vyama vyao; pia tutatoa elimu kutoka ngazi ya awali mpaka elimu ya juu bila kujali mapenzi ya Chama chako. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikusihi tu uamini bado kwamba Serikali hii haina jambo hilo wala haina maagizo hayo mahali pa kazi na uwe na amani. Nami nasema Watanzania hawa ni ndugu, wanaishi pamoja na bado tunapenda washiriki kikamilifu katika masomo yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana. Muda wa maswali umekwisha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza! *(Makofi)*



**MHE. ALLY M. KEISSY:** Kafanye siasa Manzese! (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu unaweza ukarudi kwenye kiti chako. Nakushukuru sana. (Makofi)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katibu!

**KATIBU WA BUNGE – DKT. THOMAS D. KASHILILAH:** Maswali ya Kawaida!

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Rais, TAMISEMI. Swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve.

Na. 105

#### **Mpango wa Serikali Kuwawezesha Wanawake na Vijana Kupitia Halmashauri**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Serikali imeweka utaratibu wa kuzitaka Halmashauri zote za Wilaya kutenga asilimia tano ya mapato ili kuwawezesha wanawake na vijana kupata mikopo:-

Je, ni akinamama wangapi au vikundi vya wanawake vingapi vimenufaika na mikopo hiyo katika Halmashauri za Wilaya ya Mufindi, Kilolo, Iringa Mjini na Iringa Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake, Halmashauri za Mkoa wa Iringa zimewezesha vikundi vya wanawake 430 na vikundi vya vijana 47 kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi iliwezesha vikundi vya wanawake 331, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo vikundi vitatu, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa vikundi 73 na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa vikundi 23.

Kwa upande wa vikundi vya vijana; Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi vikundi 13, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo vikundi sita, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa vikundi 28 na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa hakukuwa na kikundi hata kimoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaimarisha makusanyo ya mapato ya ndani kupitia mfumo wa *electronic* ili kuongeza mapato yanayokusudiwa kufanya mifuko hiyo kutengewa fedha zaidi. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 sharti la kupitisha makisio ya bajeti ya kila Halmashauri ilikuwa ni kuonesha kiwango kilichotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake. Napenda kulihakikishia Bunge lako kuwa tutaendelea kusimamia kwa karibu suala hili na kuchukua hatua yoyote itakayobainika kuhujumu mpango huu wa kuwawezesha wananchi.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu yako Mheshimiwa Waziri, kwangu naona hayajitoshelezi. Nilitegemea ungenipa ni kiasi gani pesa zilitolewa kwenye hivi vikundi vya akinamama kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na urasimu mkubwa sana wa utoaji wa hizi pesa kwa akinamama *especially* kwa Wilaya zangu za Mufindi, Iringa Mjini, Kilolo na Iringa Vijijini: je, huoni umuhimu wa kutoa tamko rasmi kwa Wakurugenzi ambao watakwenda kinyume na utaratibu wa utoaji wa pesa hizi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, huoni wakati sasa umefika kwa Wabunge wa Viti Maalum kusimamia zoezi zima la utoaji wa pesa hizi kwenye vikundi vya akinamama? *After all*, wao ndio wametuchagua sisi kuwa wawakilishi wao. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Ninyi wenyewe ndio Madiwani. Mheshimiwa Jafo!

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Rose Tweve kwa ajenda yake na swali lake. Ni kweli, katika *analysis*, maana yake nilizungumza jinsi gani wanawake na vijana wamefikiwa. Nilichambua mchanganuo mbalimbali katika kila Halmashauri. Kwa *figure* halisi ni kwamba wanawake walipata sh. 339,487,000/= wakati vijana walipatana shilingi milioni 98. Hapa kuna mchanganuo mdogo wa kila Halmashauri kuona ni

jinsi gani ilishiriki katika vile vikundi ambavyo i nimevibainisha awali kwamba vilipewa zile fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika Mkoa wa Iringa ni kwamba, kila Halmashauri, kama nilivyosema, kwa *figure*, akinamama walipata karibu shilingi milioni 339 na vijana milioni 98. Kwa suala zima la kutoa maagizo kwa Wakurugenzi, hili lilikuwa ni jambo langu la msingi zaidi. Nilizungumza siku tulipohitimisha bajeti yetu hapa, tukasema kwa sababu mwaka huu karibu takriban shilingi bilioni 56 zitakwenda kwenye vikundi vya akinamama na vijana, katika ule mgao wa asilimia tano tano. Nilisema katika bajeti yetu kwamba Wakurugenzi wote wa Halmashauri wana kila sababu kuhakikisha wanatekeleza hili.

Pia niliainisha tena, nikasema kwa sababu pesa za ndani maamuzi yake yanafanyika ndani ya Halmashauri, baada ya kupokea kwamba ni kiasi gani kimekusanywa, Kamati ya Fedha sasa inaweza kuhakikisha kwamba katika mwezi ule ule inatoa ule mgawanyo wa asilimia tano kwa tano kwa vijana na kwa akinamama.

Kwa hiyo, niliwahimiza Wabunge wote, kwa sababu sisi ni Wajumbe katika hizo Halmashauri zetu, tuhakikishe tunapokusanya *own source* tuwe wa kwanza kuhakikisha kwamba tunazielekeza pale pale, kwa sababu pesa hizi haziendi Hazina wala haziendi TAMISEMI, zinaishia katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Wakurugenzi wetu kwamba waende wakalisimamie hili. Vile vile niseme tena, Madiwani wote wanaingia katika Kamati ya Fedha na yale Mabaraza yetu ya Madiwani wahakikishe fedha hizi tano kwa tano zinakwenda kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wabunge Wanawake kusimamia jambo hili kwa karibu; naomba niwaambie, hili ni jukumu letu sisi sote. Akinamama, vijana na Wabunge wote humu tuna jukumu hilo. Mimi lengo langu ni nini? Ni kwamba kila Mbunge ataona kwamba jambo hili ni la kwake. Mama akinufaika katika Jimbo hilo, maana yake unakuza uchumi wa watu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, vijana wakinufaika, maana yake unakuza uchumi wa vijana katika eneo hilo. Kwa hiyo, ni jukumu letu sisi sote, twende sasa tukalisimamie hili kwa nguvu kubwa kwa ajili ya mustakabali wa uchumi wa nchi yetu.

**SPIKA:** Tunahamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura.

Na. 106

### **Ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Eneo la Msalato lenye kilometa tisa katika ujenzi wa barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati kwa kiwango cha lami bado halijakamilika.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kipande hicho kilichobaki cha Dodoma – Manyara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara chenye urefu wa kilometa 8.65 cha eneo la Msalato ni sehemu ya barabara ya Dodoma – Kondoa hadi Babati yenye urefu wa kilometa 251. Barabara hii inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni barabara ya kutoka Dodoma mpaka Mayamaya yenye urefu wa kilometa 43.65; sehemu ya pili, ni barabara ya kutoka Mayamaya mpaka Mela yenye urefu wa kilometa 99.35 na sehemu ya tatu, ni barabara ya kutoka Mela mpaka Bonga yenye urefu wa kilometa 88.8. Aidha, barabara ya kutoka Bonga hadi Babati yenye urefu wa kilometa 19.6 ilishajengwa kwa kiwango cha lami na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa sehemu ya Dodoma hadi Mayamaya yenye urefu wa kilometa 43.65 unaendelea. Utekelezaji umefikia asilimia 80 ambapo jumla ya kilometa 35 zimeshawekwa lami na zimebakia kilometa 8.65 katika eneo la Msalato.

Mheshimiwa Spika, ujenzi ulikuwa umesimama kwa muda kutokana na Mkandarasi kutokulipwa kwa wakati. Kwa sasa Serikali inaendelea kulipa madai ya Wakandarasi akiwemo Mkandarasi anayejenga barabara hii ya Dodoma hadi Mayamaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea malipo, Mkandarasi anayejenga barabara hii sasa yuko kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi na kazi inatarajia kukamilika mwezi Desemba, 2016.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa barabara hii ni sehemu ya *Great North Road* iliyokuwa inasubiriwa kwa hamu na Watanzania; na kwa kuwa ni sehemu ya Tanzania tu ambayo haijakamilika mpaka sasa; na kwa kuwa baadhi ya Wakandarasi wanasuasua; kazi zimesimama kwa baadhi ya maeneo; je, Serikali inatuhakikishiaje Watanzania kwamba barabara hii itakamilika kwa wakati? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Rais wakati akiwa Waziri wa Ujenzi katika Mkutano wa Wadau uliofanyika *Saint Gaspar* aliwaahidi Wanadodoma kwamba atajenga *ring roads* ili magari yanayotoka mikoa mbalimbali yaishie nje ya Mji kupunguza msongamano wa magari; je, ni lini upembuzi yakinifu utaanza kwa ajili ya kujenga barabara hizo za *ring roads*? (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bura. Mheshimiwa Engineer Ngonyani, Naibu Waziri wa ujenzi, majibu mafupi kwa maswali hayo!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kuhusiana na kipande kilichobakia cha Msalato na vipande vichache vilivyobaki vya kukamilisha hii barabara ya *North Great Road*, kwa vyovyote vile muda si mrefu barabara hii itakuwa imekamilika na naomba kumhakikishia hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la *ring roads*, aliyeahidi ambaye wakati huo alikuwa Waziri wa Ujenzi, hivi sasa ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, labda tu nimjulisha; hapa nina ramani nitamwonesha, labda kwa niaba ya wengine, hasa Waandishi wa Habari... (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, tayari tuna mpango mkubwa kabambe wa kujenga za *ring roads* ndani na nje ya Manispaa ya Dodoma katika kipindi cha miaka mia moja ijayo. Mpango huu utatekelezwa kwa kadiri mahitaji yanavyokuja. Barabara ambazo tunazo hapa za miaka mia moja ijayo, ziko barabara nane kubwa na jumla yake ni Kilometa 147.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu hayo. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, nilikuona; swali fupi sana la nyongeza!

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii ya kwenda Kondoa – Babati inafanana kabisa na ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Mstaafu na Rais huyu wa sasa, Mheshimiwa Magufuli, kwamba barabara ya kutoka Mbande – Kongwa – Mpwapwa mpaka Kibakwe itajengwa kwa kiwango cha lami; na ahadi hii ni ya miaka nane: sasa namwuliza Mheshimiwa Waziri, je, katika bajeti ya mwaka huu barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, majibu ya swali hilo muhimu sana. Hiyo ni barabara ya Spika. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa lubeleje pamoja na Wabunge wengine wa maeneo husika kwamba barabara inayoongelewa ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha mwaka 2015/2020, kwamba itakamilishwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naomba tusubiri tarehe 17, bajeti ya Mheshimiwa Waziri itasomwa ambayo itatoa majibu yote kwa undani zaidi na nisingependa kueleza sasa nikagusa hotuba yake.

**SPIKA:** Ahsante sana. Wananchi wa Kongwa, mmesikia majibu ya Waziri, msiwe na wasiwasi. Tundaendelea na Mheshimiwa David Ernest Silinde. Hayupo! Kwa niaba yake Mheshimiwa Mwakajoka!

Na. 107

### **Kukuza Uchumi Bonde la Ziwa Rukwa**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Ili kurahisisha msukumo wa kimaendeleo na kukuza uchumi katika Bonde la Ziwa Rukwa, Serikali iliahidi kujenga daraja linalopita katika Mto Momba kati ya Kata ya Kamsamba (Jimbo la Momba) na Kata ya Kipera (Jimbo la Kwela) mwaka 2009. Je, ni lini ahadi hiyo ya Serikali itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali kuhusiana na ujenzi wa daraja la Momba lililoko kwenye barabara ya Sitalike hadi Kilyamatundu, Mkoa wa Rukwa katika Jimbo la Kwela na vile vile Kamsamba hadi Mlowa, Mkoa wa Songwe, zinaendelea, ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni pamoja na kuandaa na nyaraka za zabuni imekamilika mwaka 2015. Kazi ya Ujenzi wa daraja la Momba imepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017 kama ambavyo Waziri wangu wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano alivyomwahidi Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela. (Makofi)

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Mwakajoka, nakupa nafasi.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Barabara hii ahadi yake ilikuwa ni kujengwa kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010 na daraja lile ilikuwa ni 2009/2010, lakini mpaka leo daraja lile halijajengwa. Je, majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri yataleta matumaini kwa wananchi wa Jimbo la Momba hasa eneo la bondeni kwamba itaanza kujengwa mapema mwaka 2016/2017?

Swali la pili, Momba ni Wilaya mpya ambayo inaunganisha Mji wa Tunduma na kutoka Tunduma kuelekea Makao Makuu ya Momba, eneo la Chitete ni Kilometa 120. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na kutujengea daraja katika Mto Ikana katika Kijiji cha Chitete, Kata ya Msangano ili wananchi wa Tunduma waweze kufika kule wakiwa wanatumia barabara ile ambayo itakuwa na kilomita 68?

**SPIKA:** Ahsante sana. Daraja kujengwa huko kulikotajwa; Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Ngonyani, majibu mafupi tafadhali!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema na kama nilivyoelekezwa na Waziri wangu wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ahadi yake kwa Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, ambaye ndiye amekuwa akifuatilia ujenzi wa daraja hili pamoja na barabara kwa upande ule wa Mkoa wa Rukwa, utatekelezwa kama ulivyoahidiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali dogo la pili linalohusu Mto Ikana, namwomba Mheshimiwa Mbunge alilete swali hili rasmi Wizarani ili Watalaam walipitie kabla mimi Naibu Waziri sijatoa *commitment* ili *commitment* yangu izingatie ushauri wa Watalaam.



**SPIKA:** Ahsante sana. Tunahamia Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, swali la Mheshimiwa Makame Mashaka Fom, Mbunge wa Kijini. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Ndaki, Mbunge wa Maswa.

Na. 108

### **Mikopo ya Elimu ya Juu Nchini**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI (K.n.y. MASHAKA MAKAME FOM)** aliuliza:-

- (a) Je, tangu Serikali ilipoanza kutoa mikopo ya Elimu ya Juu, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa mpaka bajeti ya mwaka 2015/2016?
- (b) Je ni kiasi gani kimerejeshwa ndani ya kipindi hicho?
- (c) Je, Chuo gani kinaongoza kwa wanafunzi wake kupata fedha nyingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Makame Mashaka Fom, Mbunge wa Kijini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ilipoanza kutoa mikopo ya Elimu ya Juu mwaka 1994/1995 hadi mwezi Machi, 2016, kiasi cha shilingi triloni 2.44 kimetolewa kwa wanafunzi 378,504 kwa kusudi hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, urejeshwaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika ulianza mwaka 2006/2007 na hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 kiasi cha shilingi bilioni 93.9 kilikuwa kimerejeshwa kati ya shilingi bilioni 256.2 ambazo zilikuwa zimeiva kwa kurejeshwa.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kilichoongoza kwa wanafunzi wake kupata fedha nyingi za mikopo ni Chuo Kikuu cha Dodoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza!

**MHE. MASHIMBA M.NDAKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa wananchi walionufaika na fedha hizi za mikopo wanakatwa kupitia waajiri wao, lakini hawapati taarifa

kwamba ni lini deni lao hilo litaisha. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kutoa taarifa hizo kwa wanufaika hao wanaokatwa? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mheshimiwa Stella Manyanya!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana hao ambao tayari wameshatambua wajibu wao wa kurudisha mikopo, kwani heshima ya mtu ni kukopa kwa staha, lakini pia dawa ya deni ni kulipa.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, napenda kusema kwamba katika mfumo wetu wa kulipa kupitia sheria zilizopo, tumegundua pia kulikuwa na upungufu wa aina mbalimbali ikiwemo na baadhi ya maeneo mengine, badala ya kukata kwa kutumia 8% ya mshahara, wamekuwa wakikata aidha kwa kusema ni shilingi nane au vinginevyo. Pia hizo taarifa zimekuwa hazipatikani siyo kwa wale ambao wanakatwa, lakini pia hata kwa bodi katika kuhakikisha kwamba watu wote wanalipa.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, tunashukuru kwa ushauri, lakini pia na sisi wenyewe tumekuwa tukifanyia kazi ili kuona kwamba wanufaika wanaolipa na sisi Serikali, wote tunakuwa na taarifa zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, tunaelekea kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, linaulizwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi.

Na. 109

### **Bomoa Bomoa**

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiendeleza zoezi la bomoa bomoa katika maeneo tofauti hapa nchini. Zoezi hili limekuwa likiwaathiri wananchi kiuchumi na hata kisaikolojia kwa kuwaacha wakiwa hawajui waelekee wapi:-

Je, kwa nini Serikali isiwapidie wananchi hawa ukizingatia kwamba wakati wanajenga, Serikali ilikuwa inawaona, lakini haikuchukua hatua stahiki?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali namba 109 la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Mwingwi, kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Wingwi. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali namba 109, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, suala la bomoa bomoa katika maeneo tofauti hapa nchini limesababishwa na sababu zifuatazo:-

(1) Ni wananchi kuvamia kwenye maeneo hatarishi na oevu kinyume cha sheria;

(2) Ni kuvamia maeneo au viwanja vya watu wengine au maeneo ya wazi na ya umma bila kufuata utaratibu;

(3) Ni kujenga ndani ya hifadhi ya barabara, misitu, mbuga, mikoko, fukwe, kingo za bahari na mito; na

(4) Ni kujenga majengo kwenye maeneo yaliyopangwa bila kufuata taratibu.

Mheshimiwa Spika, mambo yote manne niliyotaja hapo juu na mengine yanayofanana na hayo yanasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 na Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, bila kuathiri maana iliyopo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya 2004, Kifungu cha 55 na 57 cha Sheria hii, vimeeleza wazi na kutoa katazo la kutoruhusu mtu yeyote kufanya shughuli zozote za kibinadamu za kudumu ndani ya mita 60 ambazo zinaharibu au kwa asili yake inaweza kuathiri ulinzi wa mazingira ya bahari au kingo za mito, mabwawa au miamba ya asili ya ziwa.

Aidha, Sheria hii pamoja na mambo mengine, imekataza shughuli zozote zinazohusisha kuchepusha au kuzuia mto, ukingo wa mto, ziwa au mwambao wa ziwa, ufukwe au ardhi oevu kutoka mkondo wake wa asili au kukausha mto au ziwa. Vile vile imeeleza wazi kuwa mtu yeyote anayekiuka masharti hayo anakuwa ametenda kosa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria tajwa hapo juu, Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 inaeleza na kufafanua kwa upana namna bora ya kusimamia ardhi yote ya Mijini kuwa, "Sheria itaweka utaratibu wa maendeleo endelevu ya ardhi katika maeneo ya Mijini, kulinda na kuboresha huduma pamoja na kutoa vibali vya uendelezaji wa ardhi na kudhibiti matumizi ya ardhi katika masuala yanayohusiana na hayo."

Mheshimiwa Spika, wananchi wote watakaovunjiwa nyumba zao kwa sababu ya kutofuata sheria au kuvunja sheria au sababu nilizozitaja awali, hawatalipwa fidia. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma, hee, watu mbona mmesimama wengi, kuna nini? Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, swali la nyongeza!

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa Serikali kuwaacha wananchi mpaka wamejenga na baadaye Serikali utakuta inachukuwa hatua sasa ya kubomoa nyumba za wananchi ambao tayari wamekaa pale kwa muda mrefu.

Je, haionekani kwamba sasa inaweza kupelekea matatizo kwa wananchi na kushindwa kujiweza na kujimudu kutafuta makazi mengine? (Makofi)

Swali la pili; je, ni lini sasa Serikali itasimamia Mipango Miji yake kama sheria inavyotaka kama ambavyo amekuwa akizungumza Mheshimiwa Waziri ili kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Angeline Mabula, majibu mafupi sana, muda hauko upande wetu kabisa! (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza naomba kujibu kwamba, siyo kweli kwamba tunawaacha wananchi wanaendelea na kazi za kujenga bila kuwazuia. Tatizo lililoko ni katika Halmashauri zetu ambazo mara nyingi katika kutoa katazo mtu anapokuwa amekiuka wanaweka pengine alama ya X, lakini wakati huo huo pia wanaendelea na shughuli za maeneo mengine pasipo kufuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua hiyo, Wizara kama Wizara, sasa hivi imechukua hatua na tumeanza na Mkoa wa Dar es Salaam. Tunapeleka usimamizi kwa viongozi wa maeneo hayo na ndiyo maana tumetoa pengine Ramani kwa Wenyevidi wa Mitaa ili aweze kutambua maeneo yake na mpango

uliopo katika yale maeneo ili kuweza kujua lipi ni eneo la wazi, lipi ni eneo ambalo halitakiwi kujengwa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna imani kwamba kama watatoa ushirikiano watakuwa ni sehemu ya usimamizi na hapatakuwa na mwananchi yeyote ambaye atakuwa amejenga kinyume cha sheria kwa sababu usimamizi tayari utakuwa chini ya viongozi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nadhani limejibiwa pamoja na la kwanza kwamba ni lini tutafanya hivyo? Tayari hatua tumeshazianza. Natoa rai tu kwa sasa kupitia Bunge hili kwamba, tuombe Halmashauri zetu, kwa sababu maeneo mengi ambayo watu wanajenga kiholela; wapo wanaoona, wapo ambao wanakaa kimya na hawafuatilii.

Tuombe tu sasa kwamba popote pale ambapo mtu atajenga kinyume na utaratibu, halafu na uongozi wa pale upo unamwona mpaka anamaliza, atakapovunjiwa nyumba yake, kiongozi husika wa eneo lile atawajibishwa ikiwa ni pamoja na kulipa fidia kwa yule ambaye amekiuka taratibu na yeye akiwa anashuhudia. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Muda wetu kwa kweli hauko nasi. Tuanze kurekebisha ratiba sasa hivi, twende vizuri zaidi. Sasa tuna wageni waliofika asubuhi hii Bungeni, niwataje kwa haraka haraka!

Wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria, ambao ni Watendaji wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Profesa Sifuni Mchome na mke wa Mheshimiwa Waziri, Mama Linah Mwakyembe. Karibuni sana wote, karibuni sana Bungeni. Mama Mwakyembe peke yako simama, Karibu sana Shemeji yetu! (Makofi)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, pale mlipo hao wageni wawili; ahsante sana, wako upande ule kule. (Makofi)

Wageni 23 wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; karibuni sana! Hamkutajwa mnatoka wapi, sijui ni Wanyamwezi ninyi au vipi! Karibuni sana! (Makofi)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Jimbo la Bukoba Vijijini, ambao ni viongozi wa Chama cha Wamiliki wa shule binafsi TAPIE. Karibuni sana, tunashukuru sana wamiliki wa Shule Binafsi mmekuja. Wabunge wanalalamikia ada tu kwamba ni kubwa sana, punguzeni! (Makofi)

Wageni 22 wa Mheshimiwa Ahmed Shabiby; hawa wanatoka Jimbo la Gairo. Karibuni sana wale ndugu zangu wote kutoka Gairo. Majirani zetu wa Kongwa hao, karibuni sana! (Makofi)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum. Pale mlipo simameni, karibuni sana, karibuni sana! (Makofi)

Mheshimiwa Joseph George Kakunda ana wageni 30; wako wapi? Ahsante, ahsante sana. Miongoni mwao wako Wenyevidi wa CCM wa Kata 13, lakini pia wako wana-CCM 17 miongoni mwao. (Makofi)

Mgeni mmoja wa Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, karibu sana pale ulipo! (Makofi)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea kutoka Jimbo la Temeke. Karibuni sana! (Makofi)

Wageni Tisa wa Mheshimiwa Salum Rehani, Mbunge wa Jimbo la Uzini ambao wanatoka katika Taasisi nne, NGO zifuatazo:-

UNSAF, Action A, Policy Forum, TGMP, Oxform, karibuni sana, karibuni sana! Wageni wawili wa Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, sijui ni Mura hawa au vipi? (Makofi)

Wanafunzi waliokuja kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 100 toka Chuo cha Utumishi wa Umma, Dar es Salaam. Nafikiri hawa watakuwa wako njiani mahali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wa wageni tumemaliza. Sasa ni matangazo ya kazi. Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, anaomba niwatangazieni Wabunge wa Kamati hiyo kwenye saa 7.40, mkutane chumba namba 229, jengo la Utawala. Sheria Ndogo Utawala saa saba na dakika 40 mkutane, Mwenyekiti wenu Mheshimiwa Anderew Chenge anawaomba!

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, anaomba saa 7.00 mchana Wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii mkutane, chumba Na. 229 mtaelewana na Mheshimiwa Chenge, naona hivi vyumba vimegongana. Mtagawana vyumba huko huko 229.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazieni kwamba Ofisi yetu ya Bunge imepata msiba wa Mtumishi wetu aitwaye Bibi Betty Saro aliyekuwa anafanya kazi katika Idara ya Maktaba na Utafiti kama Katibu Mahsus. Marehemu Betty Saro alikuwa amelazwa katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma

kwa matibabu na amefariki leo asubuhi. Taratibu mbalimbali zinaendelea. Mtumishi huyu Betty Saro asili yake ni Mkoa wa Mbeya. Bwana alitoa, Bwana ametwaa!

Mheshimiwa Godfrey Mgimwa anawaomba Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa saa 7.00 mkutane pale *Canteen* kuna mambo kidogo ya kuzungumza yenye maslahi ya mkoa. Mheshimiwa Mgimwa anawaomba Wabunge wa Mkoa wa Iringa mkutane pale *Canteen*.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo langu la mwisho ni kwamba tarehe 29, Aprili nilishiriki kwa niaba yenu kwenye Mkutano wa Maspika wa Afrika Mashariki uliofanyika Arusha, ambao unaitwa *East African Speakers' Bureau*. Katika mkutano huo, yapo mambo mengi tulijadiliana na Maspika wenzangu lakini kwa leo yatosha nikiwajulisha kuhusu mambo mawili ambayo tumekubaliana.

Kwa kawaida kila mwaka kuna michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki, natumaini Dkt. Kigwangallah na timu yake wananisikia. Katika michezo hii ya Mabunge ya Afrika Mashariki inayoitwa *East African Interparliamentary Games*, mwaka huu itafanyika Desemba Nairobi.

Kwa kawaida huko awali michezo ilikuwa ni miwili tu ambayo inachezwa katika mashindano hayo, yaani mpira wa miguu na mpira wa pete (*netball*). Sasa tumekubaliana kuanzia michezo itakayoanza Nairobi, Kenya hiyo Desemba mwaka huu, tumeongeza wigo wa michezo; tutahusisha na michezo mingine.

Michezo iliyoongezeka ni *golf*, kuogelea, mpira wa wavu (*volleyball*), kutakuwa na kuvuta kamba na michezo mingine pia itaongezeka. Kwa hiyo, Waheshimiwa hata kuvuta kamba kutakushinda jamani! Kwa hiyo, naomba *Bunge Sports Club* sasa muwachagize Wabunge ili Desemba hiyo twende tukachukue makombe yote haya ambayo tumeyaainisha hapa. (*Makofi*)

Cha pili, *boxing* bado tunatafakari kama... (*Kicheko*)

La pili tulikubaliana na Maspika wenzangu kwamba itaanzishwa taasisi ya Kibunge inayoitwa *East African Parliamentary Institute*. Hii *institute* itakuwa inasaidia kutoa mafunzo maalum kabisa kwa Wabunge, kwa sababu tunakuwa Wabunge bila kupata mafunzo yoyote. Kwa hiyo, katika Kanda ya Afrika Mashariki, wenzetu wa Kenya wako tayari kutoa majengo na kila kitu ili chuo hiki kianze. Kwa hiyo, kitakapoanza, tutapeana taarifa ili kidogo kidogo kwa kadri hali itakavyoruhusu baadhi ya Wabunge tuwe tunahudhuria huko wakati kwa wakati katika mafunzo. (*Makofi*)

Katibu!



**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, mwongozo! Mwongozo wa Spika!

**KATIBU MEZANI - NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH:** Hoja ya Serikali, Hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Katiba na Sheria**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Naomba Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Tajeni majina yenu mnaotaka Mwongozo!

**MHE. JOSEPH. O. MBILINYI:** Joseph Mbilinyi!

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Dkt. Macha! Mheshimiwa Spika naomba mwongozo wako!

**SPIKA:** Dkt. Elly!

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Ndiyo!

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Dkt. Dalaly Peter Kafumu!

**SPIKA:** Dkt. Kafumu eh!

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Ndiyo!

**SPIKA:** Ahsante!

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mwalimu Bilago!

**SPIKA:** Naam! Si ni hawa watatu, eeh!

**MBUNGE FULANI:** Mwalimu Bilago hujamwandika!

**SPIKA:** Aaah, Mwalimu!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Ahsante sana. Tuanze na Dkt. Elly.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Spika, leo katika kipindi cha maswali, Naibu Waziri wa TAMISEMI amekuwa akizungumzia kuhusu suala la mikopo kwa wanawake na vijana. Suala la watu wenye ulemavu kuwepo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ni katika kuhakikisha kwamba masuala ya walemavu kwa masuala ya kiseri, Ofisi ya Waziri Mkuu inatoa mwongozo na kuzishauri Wizara nyingine zinazohusika. Haina maana kwamba watu wenye ulemavu masuala yao yasahaulike katika jamii. Wao ni sehemu ya jamii, wanahitaji kupata haki sawa kama wanavyopata vijana na wanawake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni *discrimination* kama Naibu Waziri wa TAMISEMI anaendelea ku-refer kutoa mikopo katika Halmashauri kuwakumbuka wanawake na vijana na kuwasahau watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (Makofi)

**SPIKA:** Naamini kabisa Mheshimiwa Dkt. Elly ulichotoa ni ushauri na Serikali imeupokea wala sidhani kama kuna ugomvi wowote katika hilo. Ni ushauri wa msingi sana, tunakushukuru sana. Serikali imesikia, naomba tuzingatie.

Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, jana tulikuwa tumepitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo, Wizara muhimu sana, lakini bajeti ile tumeipitisha kwa haraka haraka sana ili Wabunge wa CCM wawahi kikao cha chama chao; mabasi yaliwafuata hapa. Kwa hiyo, kilichopo ni kwamba shughuli za Vyama zimeingilia Bunge au Bunge limeingiliwa na shughuli za Vyama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wako, kama je, sisi CHADEMA au UKAWA tukiwa na *caucus*, tutembelewe na Mheshimiwa Lowassa au Waziri Mkuu Mstaafu mwingine, mzee Sumaye, atake kuzungumza na sisi; je, Bunge linaweza likaahirishwa ili na sisi twende tukazungumze na viongozi wetu? (Makofi)

**SPIKA:** Hapa leo kazi ipo!

Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishieni kabisa kwamba katika utaratibu wa Mabunge ya Jumuiya zote za Madola, pamoja na hili la kwetu, *caucus* za Vyama zinatambulika rasmi kabisa! Ndiyo maana mkiwa na vikao vya *caucus* tunavitangaza hapa na Katibu wangu ana jukumu kabisa la kuhakikisha kwamba kama mna *caucus* anawapa ukumbi kama mnahitaji au *facilities* nyingine zozote kadri mnavyohitaji. Ila tukumbuke, ni *caucus* za Vyama. Hiki kitu kinaitwa UKAWA, sijui kama ni Chama au ni nini! (Kicheko/Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Hakipo! (Kicheko)

**SPIKA:** Dkt. Kafumu! (Kicheko)

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, jana wakati Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi anajibu swali langu namba 103 alisema, nanukuu:

"Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 imezingatia matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Hivyo kwa sasa hakuna sababu ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi ili iendane na Sheria ya Madini."

Mheshimiwa Spika, majibu hayo hayakuwa kweli. Ukweli ni huu hapa; naomba ninukuu Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, inasema hivi:-

Kifungu Na. 97(1) "Where the rights conferred by a mineral right cannot reasonably be exercised without affecting injuriously the interest of any owner or occupier of the land over which those rights extend as required under section 96, the mineral right holder shall –

Mheshimiwa Spika, Kifungu (b) kinasema: *"submit a proposed plan on compensation, relocation and resettlement of the owner or occupier of the land as per the Land Act."*

Mheshimiwa Spika, sasa ukienda kwenye Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, inazungumzia fidia kulingana na soko, haizungumzii *relocation* wala *resettlement*. Maana yake wananchi wetu wanapohamishwa kwenye maeneo ya madini wanatakiwa wafanyiwe *compensation* kulingana na soko lakini pia wajengewe makazi na kuhamishiwa kwenye makazi mapya. Sasa hivi wanafanya kwa *goodwill* tu kwa sababu Sheria ya Ardhi haina Kifungu hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, kwamba Serikali iko tayari kuifanyia Sheria ya Ardhi marekebisho ili wananchi wetu wapate makazi mapya?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, mko tayari kufanya marekebisho ya hiyo sheria?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue ushauri ambao umetolewa na Mheshimiwa Mbunge na kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameshauri jambo jema, sisi kama Serikali tuko tayari kupokea ushauri huo na kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Vile vile kwa kuwa Wizara ya Ardhi bado itakuja na hotuba yake, basi tutaendelea wakati wa kipindi cha hotuba ya Wizara inayoshughulika na masuala ya ardhi. Waheshimiwa Wabunge wataendelea kutushauri na kutupa maeneo ambayo yanatakiwa yapewe kipaumbele kwetu kama Serikali ili kuweza kuyafanyia kazi kwenye Sekta hiyo ya Ardhi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwalimu Bilago!

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mwongozo wangu nauomba kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni namba 46, sina haja ya kuzisoma.

Mheshimiwa Spika, jana wakati wa kipindi cha maswali na majibu, asubuhi, swali la Mheshimiwa Joyce Mukya, linalohusu upungufu wa maji Arusha, alitaka kujua shida ya maji inayotokea Arusha na utatuzi wake. Baadaye ikaonekana kuna tatizo la umeme linalosababisha upungufu wa maji hayo. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Muhongo akajibu swali hilo kwa kejeli kubwa na kejeli hii imekuwa ni mazoea ya Mheshimiwa Muhongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge la Kumi, amekuwa akijibu majibu ya watu kwa kejeli, aliwahi kumwambia Mengi wawekeze kwenye vijuisi juisi, hawana uwezo wa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilago...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Nakwenda vizuri Mheshimiwa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilago, tusikilizane kidogo.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Naomba mwongozo sasa, naomba...

**SPIKA:** Eeh, tusikilizane lakini Mwalimu, maana wewe ni Mwalimu.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Ndiyo!

**SPIKA:** Sasa Walimu wana misingi yao. Naomba sana, usilete mambo ambayo wala hukuwepo kwenye Bunge la Kumi na nini; kwa hiyo, hebu wewe jikite tu kwa yale yaliyotokea, usiende nje ya mstari huo. Tafadhali Mwalimu. Endelea! *(Makofi)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilikuwa najenga hoja tu ili ieleweke vizuri. Majibu aliyoyatoa kwenye swali lile, alimwomba Mheshimiwa Mbunge aende akalinde watu wanaoiba umeme ili maji yapatikane Arusha.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua mwongozo wako, Wabunge wamekuwa ndio walinzi wa wizi wa umeme? Wabunge wamegeuka kuwa Mgambo? Wabunge wanatakiwa wawe Polisi wanaolinda umeme?

Je, Serikali imeshindwa kulinda wezi wa umeme mpaka inakabidhi Wabunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mwalimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Kwanza nikiri kwamba sikuwepo, kwa hiyo, sina uzito wa jambo lenyewe na mazingira yake, kwa hiyo, ni vigumu sana mimi kulizungumzia kwa sasa. Kwa hiyo, uniachie kwa wakati muafaka nitakuja kusema ikoje.

Kuhusu suala la ulinzi na usalama, siyo tu wa miundombinu ya umeme, lakini ulinzi na usalama wa kila kitu katika nchi hii tulikubaliana nchi hii kwamba ni jukumu la wananchi wote na sisi Wabunge tukiwa *included* pia. *(Makofi)*

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ili atoe hotuba yake.

Mheshimiwa Waziri, Dkt. Harrison Mwakyembe, tafadhali! *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA DKT. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, hotuba nitakayoisoma ni muhtasari tu wa hotuba kamili ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa au watagawiwa punde. Naomba hotuba yote kama ilivyo pamoja na majedwali yake iingie kwenye kumbukumbu za Bunge, yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aidha, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa heshima kubwa aliyonipa kuiteua kushika nafasi hii ya uongozi. Vile vile napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyela kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu nikupongeze wewe mwenyewe, Naibu wako na Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano na kwa kazi nzuri mnayofanya. Kwa dhati kabisa, napenda vile vile kumpongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuongoza wananchi wa Jimbo la Ruangwa na kuteuliwa kushika nafasi hii ya juu katika uongozi wa nchi yetu. Hakika kwa muda mfupi tangu ashike nafasi hiyo ya juu ya uongozi, ameweza kudhihirisha kuwa kiongozi makini na mchapakazi hodari. Vile vile nampongeza kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera kwa shughuli za Serikali kwa mwaka 2016/2017. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza vile vile Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Wajumbe wenzake wa Kamati, kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha mapendekezo ya mpango wa makadirio ya bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka wa fedha 2016/2017. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha taasisi, ofisi na idara mbalimbali zinazofanya kazi chini ya mwavuli wake ambazo ni Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Wizara ni kusimamia masuala ya Katiba; kusimamia utoaji haki; kuandaa Miswada ya Sheria; kuendesha mashtaka; kutoa ushauri wa kisheria na kuendesha mashairi ya madai; kukuza na kuhifadhi haki za binadamu; kushughulikia usajili, ufilisi na udhamini; kushirikiana Kimataifa katika kubadilishana wahalifu; kutoa mafunzo ya Uanasheria na kusimamia ustawi na maendeleo ya watumishi wake. Wizara imejipanga vilivyo kuhakikisha majukumu yake haya yanatekelezwa kwa weledi na ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu kufanya mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016. Katika kipindi hicho, Wizara ilielekeza nguvukazi na rasilimali nyingi ilizonazo katika kushughulikia masuala ya Katiba na Sheria ikiwa ni pamoja na kusimamia mchakato wa mabadiliko ya Katiba; kuimarisha mfumo wa sheria na utoaji haki; hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora; usajili na utunzaji wa kumbukumbu za matukio muhimu ya kibinadamu; ushauri wa kisheria na usimamizi wa mashauri ya madai na kuimarisha mindombinu na mifumo ya utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu nitoe maelezo ya kina kuhusu utekelezaji majukumu ya Wizara kwa kuzingatia mambo muhimu na ya kipaumbele kama ambavyo nimeweza kubainisha hivi punde.

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya Katiba. Kufuatia kukamilika kwa mchakato wa kupitisha Katiba inayopendekezwa ndani ya Bunge Maalum la Katiba na baadaye tarehe 8, Oktoba, 2014 Katiba Inayopendekezwa kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa mujibu wa Kifungu cha 28(1) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya 2011, maandalizi ya kufanyika kwa kura ya maoni ili kumpa mwananchi kauli ya mwisho kuikubali au kuikataa Katiba inayopendekezwa, yalianza na kulenga tarehe 3, Aprili 2015 kuwa siku ya kupiga kura hiyo nchini.



Mheshimiwa Spika, kwa matarajio ya Katiba inayopendekezwa kupitishwa kwa kura ya maoni na kuzaa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 2014, Wizara ilijipanga kuratibu uundaji na uendeshaji wa Kamati ya Utekelezaji wa Katiba katika muda wa mpito kwa mujibu wa Ibara ya 295 ya Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kujitokeza kwa changamoto za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu hususan kutokamilika kwa zoezi la kuandikisha wapiga kura kwa wakati, katika kipindi hicho hicho cha maandalizi ya kura ya maoni na ukweli kwamba siyo rahisi kuendesha kura ya maoni na Uchaguzi Mkuu kwa pamoja kifedha na *ki-logistic*, kulipelekea mamlaka husika, yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kuahirisha zoezi la kura ya maoni ili kujiandaa vyema na mchakato wa Uchaguzi Mkuu. Ni dhahiri kwamba kura ya maoni ingeweza kusubiri lakini Uchaguzi Mkuu usingeweza, kwani uko kikatiba, usingeweza kuahirishwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Katiba ni moja ya vipaumbele vya kufanyiwa kazi na Serikali ya Awamu ya Tano, kama Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alivyolieleza Bunge lako Tukufu tarehe 20 Novemba, 2015. Wizara imeimarisha mawasiliano yake na NEC, ZEC na Ofisi ya Waziri Mkuu ili muda muafaka ukiwadia tuwe tayari na mazingira stahiki ya kufanikisha zoezi hilo la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu kumekuwa na kilio kikubwa nchini cha ucheleweshaji wa mashauri Mahakamani, kilio ambacho kime lazimu hatua zifuatazo za makusudi kuchukuliwa:-

Kwanza kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri chini ya kauli mbiu ya mlundikano sifuri wa mashauri au *zero case backlog* kwa kuweka idadi mahsusi ya kesi anazotakiwa Hakimumu au Jaji kumaliza kwa mwaka. Chini ya utaratibu huu mpya wa kupima tija na ufanisi wa uendeshaji wa Mahakama, Hakimumu wa Mahakama ya Mwanzo anatakiwa kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri 260 kwa mwaka. Hakimumu wa Mahakama wa Wilaya na Hakimumu Mkazi mashauri 250 kwa mwaka na Jaji wa Mahakama Kuu anapaswa kusikiliza na kuhitimisha mashauri 220 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu haukushinikizwa na mamlaka za juu za Mahakama, bali ni matokeo ya makubaliano yaliyofikiwa na Mahakimu na Majaji wenyewe ili kupunguza mlundikano mkubwa wa kesi. Ni katika muktadha huo Mahakama imejiwekea utaratibu wa kumaliza mashauri yote katika kipindi cha mwaka 2016/2017 yenye umri wa zaidi ya miezi 24 kwa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani; miezi 12 kwa Mahakama za Wilaya na Hakimumu Mkazi na miezi sita kwa Mahakama za Mwanzo.

Utaratibu huu mpya wa Mahakama, umeanza kuonyesha matokeo chanya ambapo jumla ya Mahakama za Mwanzo 128 kati ya 906 zilizoko nchini zimesikiliza na kutolea uamuzi mashauri yote yaliyofunguliwa katika Mahakama hizo kati ya Januari na Desemba, 2015. Aidha, yapo mafanikio katika kesi za uchaguzi ambapo kesi 28 zimehitimishwa na kwa kiwango idadi ya mashauri ya zamani imepungua hadi kufikia asilimia 15 kama inavyoonekana katika hotuba yangu.

Pili, kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, *The Judiciary Administration Act* ya mwaka 2011, ambayo inaunda Kamati za Maadili za Mahakimu na Majaji kwa lengo la kuimarisha maadili na nidhamu ya kazi katika huduma ya utoaji haki. Kamati hizo ni Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama ya Wilaya, Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama ya Mkoa, Kamati ya Maadili ya Maafisa wa Mahakama na Kamati ya Maadili ya Majaji. Ni matumaini ya Wizara kuwa kuanza kwa shughuli kwa Kamati hizi kutaimarisha maadili, nidhamu ya kazi na uwajibikaji na hivyo kuondoa ucheleweshaji wa kesi bila sababu za msingi na kuongeza ufanisi wa Mahakama zetu. (Makofi)

Tatu, kuendelea kusogeza karibu na wananchi huduma ya utoaji haki kwa kukarabati majengo ya Mahakama yaliyobomoka au kuharibika na hivyo kulazimu shughuli za Mahakama kusitishwa.

Aidha, kujenga Mahakama kwenye maeneo yaliyokosa huduma hiyo katika kuhakikisha kwamba huduma ya utoaji haki inafikiwa na wananchi wetu kwa urahisi. Serikali ilifanya uamuzi wa kiseru kwa kuhakikisha kuwa kila Kata inakuwa na Mahakama ya Mwanzo. Ni katika hali hiyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kutolewa kwa fedha zote za bajeti ya Maendeleo katika Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ili kuimarisha miundombinu ya Mahakama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia fedha hizo za Maendeleo zilizotolewa zitawezesha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo nane; ujenzi wa Mahakama za Wilaya 12; na kuendelea na ukarabati wa Mahakama nyingine na Mahakama Kuu Shinyanga, Mtwara, Tanga na Mbeya. Aidha, maandalizi ya awali ya ujenzi wa Mahakama Kuu Kigoma na Mara yanaendelea. Maeneo ya ujenzi wa Mahakama hizo yameelezwa kwa kina katika hotuba yangu aya ya 13. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uhitimishaji wa kesi Mahakamani unategemea sana upatikanaji na ubora wa huduma za uendeshaji wa mashtaka na uratibu wa shughuli za upelelezi zinazotolewa na Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka (NPSA). Hivi sasa huduma hizo zinapatikana katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia

Ofisi za Mikoa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa Mkoa mpya wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa ni miaka minane sasa toka Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka nchini itungwe (*The National Prosecution and Service Act*) ya mwaka 2008 ambayo ilitenganisha kazi za upelelezi na mashtaka kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza uwajibikaji katika majukumu hayo mawili makubwa ya haki jinai.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya kuviondoa vyombo vya uchunguzi kwenye uendeshaji wa mashtaka na kuvibakiza kwenye upelelezi wa makosa (*civilianization of prosecution*) bado haijafikia malengo yake kwani Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka imeweza mpaka sasa kubeba jukumu hilo kwenye Makao Makuu ya Mikoa tu, ambapo inaendesha kesi za jinai katika Mahakama zote za Hakimu Mkazi na za Wilaya za Makao Makuu ya Mikoa, isipokuwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Monduli tu.

Mheshimiwa Spika, ni azima ya Wizara kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka au Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya (*DPP*), inapanua huduma zake kwenda Wilaya nyingi zaidi na hatimaye kuzifikia hata Mahakama za Mwanzo. Uwepo wa Ofisi ya *DPP* katika ngazi ya Mikoa na Wilaya una umuhimu mkubwa katika kuimarisha haki jinai nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto ya mamlaka ya Taifa ya mashtaka kupanuka kwa kasi ndogo, upungufu wa Mawakili na mapokezi yasiyoridhisha ya fedha ya matumizi, bado chombo hiki adhimu cha Umma kimeteteleza majukumu yake kwa ufanisi, weledi na uzalendo wa hali ya juu hasa katika uendeshaji wa mashauri makubwa (*high profile cases*) yanayohusu dawa za kulevya, uwindaji haramu, misitu na wanyamapori, watakatishaji fedha haramu na kadhalika.

Mfano kwa sasa, Ofisi hiyo ya *DPP* inaendesha kesi 161 za dawa za kulevya ambazo thamani yake inazidi shilingi milioni 10 kwa kila kesi zilizopo katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Ufafanuzi zaidi kuhusu mashauri ya madawa ya kulevya yapo katika hotuba yangu aya ya 18.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuwa chombo cha kuaminika cha Serikali, pamoja na mambo mengine, katika kutoa ushauri wa kisheria katika masuala ya madai, haki za binadamu, Katiba na mikataba na kuiwakilisha Serikali Mahakamani na Mabaraza ya usuluhishi na upatanishi. Pamoja na changamoto za uchache wa Mawakili wa Serikali, ufinyu wa Ofisi na mapokezi madogo ya fedha ya matumizi ya kawaida, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliwakilisha vyema Serikali katika mashauri

mbalimbali yaliyofunguliwa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mahakama ya Rufaa, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Mahakama ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi hii iliendesha kesi za Ubunge 52 na kesi 198 za Udiwani zilizofunguliwa baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015. Hadi kufikia mwezi uliopita wa Aprili, 2016 jumla ya kesi 28 za Ubunge zilihitimishwa na 24 zinaendelea kusikilizwa kwa hatua mbalimbali. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishinda katika mashauri yote hayo hatua ambayo imewawezesha Waheshimiwa Wabunge wote waliohusika na kesi hizo kuendela na Ubunge wao.

Vile vile Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliwakilisha Serikali katika mashauri ya madai 818 ambapo kati ya hayo, 38 yalihitimishwa na 780 yanaendelea kusikilizwa. Pia kulikuwa na maombi ya madai 350 na rufaa za madai 59 ambapo maombi ya madai 64 yamehitimishwa na rufaa zote zinaendelea kusikilizwa. Aidha, mashauri kuhusu haki za binadamu yameelezwa kwa kina katika aya ya 20 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kupokea, kuchambua na kufuatilia malalamiko kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu. Kuanzia mwaka 2010 hadi Aprili, 2016, Tume ilipokea na kuyachunguza jumla ya malalamiko 13,709. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 6,169 yalihitimishwa na malalamiko 7,540 yanaendelea kuchunguzwa.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi ambayo Tume inapokea yanahusu migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wawekezaji, wakulima na wafugaji, wananchi na maeneo ya hifadhi, matumizi mabaya ya madaraka kwa watendaji, ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ucheleweshaji wa haki kwa mahabusu na wafungwa na matumizi ya nguvu kwa upande wa vyombo vya dola.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeshirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (*National Human Right Action Plan*) wa mwaka 2013 hadi 2017, mpango ambao ulibuniwa na Serikali na kulivutia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) ambalo linachangia kifedha katika utekelezaji wake. Lengo kuu la mpango kazi huu ni kuongeza uelewa wa haki za binadamu na utawala bora nchini na nafasi yake katika mfumo wetu wa utawala. Kati ya Julai, 2015 na Januari, 2016 Tume imeendesha Semina za Walimu wa Sekondari na Wakurugenzi wa Halmashauri katika Mikoa tisa ya Tanzania Bara na semina hizo zinaendelea kwa Mikoa iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea na tafiti mbalimbali za sheria ili kubaini upungufu uliopo na kutoa mapendekezo kulingana na mahitaji ya sasa kwa ustawi wa jamii na Maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kwa mwaka 2015/2016 Tume imeendelea na utafiti kuhusu mfumo wa sheria zinazosimamia haki za walaji na watumiaji wa bidhaa, huduma za kijamii kwa wazee, haki za jinai, mfumo wa sheria ya ushahidi, usuluhishi na Sheria ya Ununuzi wa Umma. Tafiti hizo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ninavyoelezea ukurasa wa 20 na 21 wa hotuba yangu. Aidha, maelezo ya kina kuhusu tafiti za sheria mbalimbali yameoneshwa kwenye kiambatisho Na.1.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea na shughuli za usajili wa vizazi na vifo katika Wilaya mbalimbali Tanzania Bara katika mkakati wa kuongeza kiwango cha usajili wa vizazi na vifo nchini. Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*) imeanzisha kampeni ya usajili inayoambatana na uboreshaji wa mfumo wa usajili kwa kuweka mfumo wa *computer* katika kila Wilaya ambapo kampeni itafanyika.

Kwa kuanzia, kampeni hizi zimefanyika katika Wilaya ya Arusha na Arumeru ambapo jumla ya watu 49,548 walisajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa. Zoezi hili linaendelea katika Wilaya ya Kahama na baadaye kuendelea katika Wilaya 16 za Bariadi, Chato, Dodoma, Igunga, Kilombero, Kilosa, Lushoto, Maswa, Mbinga, Misungwi, Mtwara, Muleba, Nzega, Shinyanga, Sumbawanga na Tunduru. Wizara imekadiriya kusajili zaidi ya watu 500,000 katika maeneo hayo na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, *RITA* imeanza kukusanya ada zote zitokanazo na huduma inazozitoa kwa njia ya *ki-electronic* kwa wadau kufanya malipo yao kupitia simu za mkononi au Benki. Tayari jumla ya Wilaya 114 kati ya Wilaya 139, zinakusanya maduhuli kwa njia ya *ki-electronic* na kwamba ifikapo mwezi Juni, 2016 Wilaya zote za Tanzania Bara zitakuwa zikitumia njia za *ki-electronic* kukusanya maduhuli.

Vile vile Wizara inaendelea na mkakati wa usajili wa watoto chini ya miaka mitano na imeandaa mkakati wa Taifa wa Usajili na Ukusanyaji wa Takwimu Muhimu (*Civil Registration and Vital Statistic - CRVS*), ambao maandalizi ya rasimu ya kwanza yamekamiliwa, tayari kuwasilishwa Serikalini kwa maamuzi kama inavyoonekana katika hotuba yangu aya ya 26 na 27.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha shughuli za ufilisi, Wizara imeanzisha mchakato wa kutunga sheria moja ya ufilisi, tofauti na ilivyo sasa ambapo shughuli hizo zinasimamiwa na sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge lako Tukufu. Masuala mengine kuhusu usajili wa asasi za kidini na kijamii, masuala ya usimamizi wa mirathi, naelezea kwa kina ukurasa wa 21 mpaka 25 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kuboresha mfumo wa sheria nchini ili kuwezesha wananchi wote kuifikia haki wanapoitafuta bila kujali uwezo wa mtu katika jamii hasa wa maeneo ya vijijini. Hii ni hatua moja muhimu katika vita dhidi ya umaskini kwa kuwaunganisha wananchi wengi zaidi na mfumo wa kawaida wa utoaji haki. Hivyo, Wizara imewasilisha Serikalini rasimu ya waraka wenye mapendekezo ya kutunga upya Sheria ya Msaada wa Kisheria ambao unasubiri uamuzi wa Baraza la Mawaziri.

Matarajio ya Wizara ni kuwasilisha Muswada wa sheria hiyo Bungeni kabla ya kumalizika kwa mwaka 2016. Pia Wizara inaendelea kuratibu utoaji wa msaada wa kisheria kupitia Sekretarieti ya Msaada wa Kisheria ambayo ilianzishwa kama chombo cha mpito wakati Taifa likisubiri kukamilika kwa mchakato wa kutunga sheria mahususi ya kusimamia eneo hilo la huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ni moja ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika kuimarisha mfumo wa sheria nchini. Katika kuhakikisha hilo, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo imefanikiwa kuongeza uwezo wake wa kudahili wanafunzi kufikia wanafunzi 1,800 kwa mwaka, ambayo sasa imefanyika mwaka huu, pamoja na kushughulikia maombi ya kujiunga na Taasisi hiyo kwa njia ya mtandao (*online application*) ili kuwafikia wadau wengi zaidi na kupunguza gharama za kujiunga. Taasisi hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuziba pengo la mahitaji ya Mawakili na Wanasheria wanaojiunga na Sekta ya Umma na Binafsi kwa kuajiriwa au kwa kujitolea kutoa msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, dhamana ya Serikali kuhusu uboreshaji wa huduma za kisheria kwa umma, ndiyo kiini cha maboresho ya Sekta ya Sheria ambayo yamekuwepo nchini tangu mwaka 2007 kupitia *program* ya maboresho ya Sekta ya Sheria na mikakati yake. Kupitia maboresho hayo, Serikali imefanya mageuzi makubwa katika mfumo wa sharia, kuimarisha miundombinu ya utoaji huduma na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na ununuzi wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imefanya maboresho katika mfumo wa *ki-electronic* kuwawezesha wananchi kufikisha malalamiko yao kwa njia ya simu za mikononi. Aidha, Wizara inafanya maandalizi ya awali ya mradi mkubwa zaidi wa kuanzisha mfumo wa *ki-electronic* wa utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya kazi kwa karibu na Tume ya Utumishi wa Mahakama, taasisi huru iliyoungwa kwa mujibu wa Ibara ya 112 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kusimamia uendeshaji wa Mahakama za Tanzania. Majukumu Makuu ya Tume ni kushauri kuhusu teuzi za ngazi za juu ya



Mahakama na kusimamia masuala ya ajira na nidhamu ya Watumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika katika kipindi tunachokiaga Tume ya Utumishi wa Mahakama iliajiri jumla ya Watumishi 989. Kati yao Mahakimu Wakazi 248 na Watumishi wasio Mahakimu 741. Pia Tume ilishughulikia jumla ya mashauri 14 ya nidhamu kwa Watumishi wa Mahakama na kuyatolea uamuzi. Katika mashauri hayo, Watumishi 10 walifukuzwa kazi baada ya kupatikana na hatia ya utovu wa nidhamu na mengine manne yanaendelea kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya sh. 196,087,197,000/=; kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, sh. 68,819,125,000/= ni za mishahara; sh. 111,886,746,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na sh. 15,381,326,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za maendeleo za ndani sh. 13,319,000,000/=; na fedha za nje sh. 2,062,326,000/=.

Mheshimiwa Spika, katika mwezi wa Aprili, 2016, Wizara ilipokea jumla ya sh. 119,784,602,272/= sawa na asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo sh. 54,772,582,835/= ni mishahara ya Watumishi na sh. 51,802,552,437/= ni kwa matumizi mengineyo. Fedha za Maendeleo ni sh. 13,209,467,000/= ambapo fedha za ndani, ni sh. 12,644,744,000/= na fedha za nje ni sh. 564,727,000/=;

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya sh. 17,023,633,750,000/= kama Maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Aprili, mwaka huu, 2016 Wizara ilikusanya jumla ya sh. 11,116,849,811/= kama Maduhuli ya Serikali, kama ilivyochanganuliwa ukurasa wa tatu wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali zilizochangia kurudisha nyuma juhudi za Serikali za kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria. Kati ya hizo, ni changamoto ya ufinyu wa bajeti ambapo bajeti inayotengwa imekuwa haiakisi mahitaji halisi ya kuwezesha kutoa huduma bora na kwa wakati. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu taarifa ya kibajeti, angalia kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati ya kukabiliwa na changamoto zilizopo kwa kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayohusiana na uhaba wa Watumishi wenye ujuzi, ilikuwa ni pamoja na upatikanaji wa vibali vya ajira, kujaza nafasi zilizoachwa wazi, maslahi ya watumishi, kubainisha vyanzo vipya vya mapato na namna bora ya kuvitumia kama vile kutayarisha maandiko ya miradi na kuanzisha ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo.



Mheshimiwa Spika, vile vile Wizara imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo, ikiwa ni pamoja na kujiepusha na matumizi yasiyo ya lazima na kufanya marekebisho ya namna ya kupangilia utekelezaji wa majukumu yake kwa kuanzisha utaratibu wa kutumia vigezo vya watendaji kazi kwa watumishi na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma sanjari na kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Taasisi za Mashirika mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa yakiwemo nchi wahisani, Balozi zinazowakilisha nchi zao hapa nchini, Mashirika yaliyopo chini ya Umoja wa Mataifa, Asasi za Kijamii na Kiraia, Washirika wa Kimaendeleo, Vyuo Vikuu, Vyama vya Kitaaluma na Taasisi za Utafiti kwa michango yao mikubwa wanayoitoa katika utendaji kazi wa Wizara na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru wasaidizi wangu wakuu, Profesa Sifuni Mchome, Katibu Mkuu na Amon Mpanju, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

Aidha, nawashukuru Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakuu wa Idara na Vitengo kwa jitihada na ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu itaendelea na uimarishaji wa Mfumo wa Sheria ya Nchi na pia juhudi za kuongeza ubora na kuimarisha upatikanaji wa huduma za Kisheria na Kikatiba sanjari na dhima ya Wizara. Hivyo Wizara imeainisha maeneo muhimu ya kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake na katika mgawanyo wa rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Wizara itachukua hatua madhubuti kuimarisha usimamizi na utendaji wa mfumo wa Sheria, kukamilisha taratibu za Divisheni ya Rushwa ya Ufisadi ili ianze kazi tarehe 1 Julai, 2016 kama Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu ilivyobainisha na kusimamia mambo ya Katiba na Sheria kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kuimarisha miundombinu ya huduma za kisheria na kuboresha mazingira ya utendaji kazi; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kuimarisha utafiti na uandishi wa sheria ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Sheria za Usafirishaji, Uwekezaji, zinazosimamia eneo la ustawi wa jamii kama zilivyoainishwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara itachukua hatua kuimarisha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo, kuimarisha utunzaji wa

kumbukumbu na takwimu, kuwaendeleza watumishi kitaaluma, kuimarisha taasisi ya mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, kwa kuanzisha masomo ya jioni (*part time programs*) na kuanzisha Vituo vya Kanda ili kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 1,800 hadi wanafunzi 3,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendeleza ushirikiano wa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo Taasisi zake; Polisi na Magereza ni vyombo muhimu katika mfumo mzima wa haki jinai. Aidha, Wizara italitumia kwa karibu zaidi Jukwaa la Haki Jinai, chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambalo linajumuisha Wakuu wa vyombo vyote vya haki jinai katika kutatua kero zifuatazo zinazocheleweshwa au kukwamisha upatikanaji wa haki sawa kwa wote na kwa wakati:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mazoea ya kila kesi ya jinai, iwe ndogo au kubwa, kuchukua muda mrefu wa upelelezi hata kwa kesi ambayo mtuhumiwa kakiri kosa, au mashahidi wapo walioshuhudia kosa likitendeka. Wizara itataka maelekezo ya kisheria yawepo ya muda mahususi wa kumaliza kesi kama hizi bila kisingizio cha upelelezi. (*Makofi*)

Pili, upotevu wa mafaili ya kesi. Pamoja na Mahakama kuchukua hatua stahili za kiutendaji na kinidhamu, kila upotevu wa mafaili ukitokea, tatizo linazidi kujirudia na kuwa moja ya sababu ya mlundikano wa kesi Mahakamani. Wizara itataka hatua kali zaidi zichukuliwe dhidi ya wale wote wanaohusika na upotevu huo ili usirudiwe.

Tatu, ucheleweshwaji wa nakala za hukumu na mwenendo wa mashauri. Pamoja na jitihada bayana zinazofanywa na Mahakama kuongeza kasi katika utoaji wa nyaraka hizo, Wizara inaona tatizo kuwa kubwa linalohitaji Mahakama kuongezewa Kada ya Wachapaji na vitendea kazi.

Nne, ubambikizwaji kesi katika Vituo vya Polisi. Tuhuma hii imerudia mara nyingi mno kiasi ambacho haina budi kuangaliwa kwa jicho kali ili kudhibiti hali hiyo. Wizara itatafuta njia muafaka ya kisheria kuhakikisha kwamba hali hiyo hajitokezi katika mfumo wetu wa jinai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi na majukumu yanayoambatana na hayo Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa kiasi cha sh. 35,785,416,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kama ifuatavyo:-

- (a) Mishahara ya Watumishi Sh. 22,391,694,000/=
- (b) Matumizi mengineyo Sh. 10,616,234,000/=
- (c) Miradi ya Maendeleo Sh. 2,774,488,000/=

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zimegawanyika katika mafungu sita ya Wizara kama inavyoonekana kwenye jedwali lililoko kwenye ukurasa 38 ambapo tuna:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama; Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Fungu 35 - Divisheni ya Mashtaka; Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria; Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila Fungu nimeelezea kwa kina ukurasa 39 na 40 wa hotuba yangu fungu kwa fungu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha sh. 18,400,150,435/= ikiwa ni maduhuli ya Serikali kama inavyoonekana kwenye jedwali ukurasa wa 41.

Mheshimiwa Spika, mchanguo wa maombi ya fedha ya bajeti ya kila fungu, umeainishwa kwenye vitabu vya kasma za mafungu husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa kusoma hotuba yako kwa ufasaha mkubwa sana. (Makofi)

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA DKT. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2016/2017.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu

kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, napenda kutoa shukurani nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa heshima kubwa aliyonipa kuiteua kushika nafasi hii ya uongozi. Vilevile, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyela kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kuwa mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Binafsi ninaahidi kuzitumikia vema nafasi zote hizi kwa hekima, akili na nguvu alizonijalia Mwenyezi Mungu ili kuharakisha maendeleo ya jimbo langu na nchi yetu kwa ujumla.

3. **Mheshimiwa Spika**, niruhusu nikupongeze wewe, Mheshimiwa, kwa kuchaguliwa kulingoza Bunge la Jamhuri ya Muungano, ambalo ni moja ya mihimili mitatu ya dola la Tanzania. Hii inadhihirisha imani waliyonayo wabunge wa Bunge lako tukufu kutokana na uwezo ulionao, uzoefu na umahiri uliounesha wakati wa kulitumikia Bunge la Kumi katika nafasi ya Naibu Spika. Hakika hii ni heshima kubwa siyo kwako tu bali na kwa wananchi wa Jimbo la Kongwa waliotumia haki yao ya kidemokrasia kukuchagua kuwa mwakilishi wao. Pia, nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na wenyeviti wote wa Bunge kwa kuchaguliwa kwenye nafasi walizonazo na kwa uongozi mahiri wa Bunge letu tukufu.
4. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwaongoza wananchi wa Jimbo la Ruangwa na kuteuliwa kushika nafasi hiyo ya juu katika uongozi wa nchi yetu. Hakika kwa muda mfupi tangu ashike nafasi hiyo ya juu ya uongozi ameweza kudhihirisha kuwa kiongozi makini na mchapa kazi hodari. Vilevile, nampongeza kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kiseru kwa shughuli za Serikali kwa mwaka 2016/2017.
5. **Mheshimiwa Spika**, aidha nampongeza Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kwa kuchaguliwa kuingoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Wizara yangu ina imani kubwa na yeye binafsi na Kamati anayoingiza. Pia, natoa shukurani nyingi kwa Kamati yake kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha mapendekezo ya Mpango na Makadirio ya bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Ninaahidi kwa dhati kabisa kwamba tutaendelea kushirikiana na Kamati hii ili kuimarisha utawala wa sheria na upatikanaji haki katika jamii na hatimaye kutoa mchango unaostahili katika kukuza uchumi wa viwanda nchini. Hali kadhalika nafurahi kuwapongeza waheshimiwa wabunge wenzagu wote kwa kuchaguliwa kuwa wabunge wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ninawatakia kheri na mafanikio katika kuitekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha kuelekea mwaka 2020, kwa maendeleo ya nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha taasisi, ofisi na idara mbalimbali zinazofanya kazi chini ya mwavuli wake ambazo ni Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini; Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; na Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto.
7. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaongozwa na Dira mpya ya kuwa taasisi ya mfano wa kuigwa katika usimamizi wa masuala ya katiba na sheria na Dhima ya kutoa huduma bora katika masuala ya katiba na sheria kwa kujenga mifumo madhubuti kiseria na kisheria. Majukumu ya msingi ya Wizara ni kusimamia masuala ya katiba; kusimamia utoaji haki; kuandaa miswada ya sheria; kuendesha mashtaka; kutoa ushauri wa kisheria na kuendesha mashauri ya madai; kukuza na kuhifadhi haki za binadamu; kushughulikia usajili, ufilisi na udhamini; kushirikiana kimataifa katika kubadilishana wahalifu; kutoa mafunzo ya uanasheria na kusimamia ustawi na maendeleo ya watumishi wake. Wizara imejipanga vilivyo kuhakikisha majukumu yake haya yanatekelezwa kwa weledi na ubora wa hali ya juu.

## **B. MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016**

8. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa uniruhusu kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016. Katika kipindi hicho, Wizara ilielekeza nguvu kazi na rasilimali nyingine ilizonazo katika kushughulikia masuala ya katiba na sheria ikiwa ni pamoja na kusimamia mchakato wa mabadiliko ya katiba; kuimarisha mfumo wa sheria na utoaji haki; hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora; usajili na utunzaji wa kumbukumbu za matukio muhimu ya binadamu; ushauri wa kisheria na usimamizi wa mashauri ya madai; na kuimarisha miundombinu na mifumo ya utoaji huduma. Naomba sasa uniruhusu nitoe maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kuzingatia mambo muhimu na ya kipaumbele kama ambapo nimeweza kubainisha hapo juu.

### **I. MABADILIKO YA KATIBA**

9. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kukamilika kwa mchakato wa kupitisha Katiba Inayopendekezwa ndani ya Bunge Maalum la Katiba na baadaye tarehe 8 Oktoba, 2014 Katiba Inayopendekezwa kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar

kwa mujibu wa kifungu cha 28(I) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya 2011, maandalizi ya kufanyika kwa Kura ya Maoni ili kumpa mwananchi kauli ya mwisho kuikubali au kuikataa Katiba Inayopendekezwa yalianza na kulenga tarehe 3 Aprili, 2015 kuwa siku ya kupiga kura hiyo nchini. Kwa matarajio ya Katiba Inayopendekezwa kupitishwa kwa Kura ya Maoni na kuzaa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 2014, Wizara ilijipanga kuratibu uundaji na uendeshaji wa Kamati ya Utekelezaji wa Katiba katika muda wa mpito kwa mujibu wa Ibara ya 295 ya Katiba Inayopendekezwa.

- 10. Mheshimiwa Spika**, kujitokeza kwa changamoto za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu hususan kutokamilika kwa zoezi la kuandikisha wapiga kura kwa wakati (katika kipindi hicho hicho cha maandalizi ya Kura ya Maoni), na ukweli kwamba si rahisi kuendesha Kura ya Maoni na Uchaguzi Mkuu kwa pamoja, kifedha na kilojistiki, kulipelekea mamlaka husika yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kuahirisha zoezi la Kura ya Maoni ili kujiandaa vema na mchakato wa Uchaguzi Mkuu. Ni dhahiri kwamba Kura ya Maoni ingeweza kusubiri lakini Uchaguzi Mkuu ambao upo Kikatiba usingeweza kuahirishwa.
- 11. Mheshimiwa Spika**, suala la Katiba ni moja ya vipaumbele vya kufanyiwa kazi vya Serikali ya Awamu ya Tano kama Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyoeelekeza Bunge lako Tukufu tarehe 20 Novemba, 2015. Wizara imeimarisha mawasiliano na NEC, ZEC na Ofisi ya Waziri Mkuu ili muda muafaka ukiwadia, tuwe tayari na mazingira stahiki ya kufanikisha zoezi hilo la kitaifa.

## **II. MIFUMO YA UTOAJI HAKI NA UTAWALA WA SHERIA**

- 12. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi kirefu kumekuwa na kilio kikubwa nchini cha ucheleweshaji wa mashauri mahakamani, kilio ambacho kimejazimu hatua zifuatazo za makusudi kuchukuliwa:

(i) Kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri chini ya kauli mbiu ya “mrundikano sifuri wa mashauri” au “zero case backlog” kwa kuweka idadi mahsusi ya kesi anazotakiwa hakimu au jaji kumaliza kwa mwaka. Chini ya utaratibu huu mpya wa kupima tija na ufanisi wa hakimu au jaji mmoja mmoja, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo anatakiwa kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri 260 kwa mwaka; Hakimu wa Mahakama ya Wilaya na Hakimu Mkazi mashauri 250 kwa mwaka; na Jaji wa Mahakama Kuu anapaswa kusikiliza na kuhitimisha mashauri 220 kwa mwaka. Utaratibu huu haukushinikizwa na mamlaka za juu za mahakama bali ni matokeo ya makubaliano yaliyofikiwa na mahakimu na majaji wenyewe ili kupunguza mrundikano mkubwa wa kesi unaosababisha ucheleweshwaji wa mashauri

na hivyo kukiuka kanuni ya msingi ya utoaji haki ya, “haki iliyocheleweshwa, ni haki iliypotea” au “*justice delayed is justice denied*”.

Ni katika muktadha huo, mahakama imejiwekea utaratibu wa kumaliza mashauri yote katika kipindi cha mwaka 2016/17 yenye umri wa zaidi ya miezi 24 kwa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani; miezi 12 kwa Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi; na miezi 6 kwa Mahakama za Mwanzo.

Utaratibu huu mpya wa Mahakama umeanza kuonesha matokeo chanya ambapo jumla ya mahakama za mwanzo 128 kati ya 906 zilizoko nchini zimesikiliza na kutolea uamuzi mashauri yote yaliyofunguliwa katika mahakama hizo kati ya Januari na Desemba, 2015. Mafanikio kama hayo yameendelea kupatikana hata kwenye mashauri yanayohusu matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ambapo mashauri 250 ya kupinga matokeo ya uchaguzi katika majimbo na kata anuwai yalifunguliwa mahakamani. Mashauri 52 kati ya hayo ni ya kupinga matokeo ya ubunge na mashauri 198 ni ya kupinga matokeo ya udiwani; na kufikia mwezi Aprili, 2016 jumla ya mashauri 28 yalihitimishwa.

Kwa ujumla, idadi ya mashauri ya zamani (*backlog cases*), kwa Mahakama zote, ni chini ya wastani wa asilimia 15 ya mashauri yote yaliyopo mahakamani ikilinganishwa na hali ya miaka 2012/13 ambapo zaidi ya asilimia 60 ya mashauri yote mahakamani yalikuwa ya zamani.

(ii) Kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama (*The Judiciary Administration Act*) ya 2011 ambayo inaunda Kamati za Maadili za Mahakimu na Majaji kwa lengo la kuimarisha maadili na nidhamu ya kazi katika huduma ya utoaji haki. Kamati hizo ni: Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama ya Wilaya (*District Judicial Ethics Committee*); Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama ya Mkoa (*Regional Judicial Ethics Committee*); Kamati ya Maadili ya Maafisa wa Mahakama (*Judicial Officers Ethics Committee*); na Kamati ya Maadili ya Majaji (*Judges Ethics Committee*). Ni matumaini ya Wizara kuwa kuanza kwa shughuli kwa kamati hizi kutaimarisha maadili, nidhamu ya kazi na uwajibikaji na hivyo kuondoa ucheleweshaji wa kesi bila sababu za msingi na kuongeza ufanisi wa mahakama zetu.

(iii) Kuendelea kusogeza karibu na wananchi huduma ya utoaji haki kwa kukarabati majengo ya mahakama yaliyobomoka au kuharibika na hivyo kulazimu shughuli za mahakama kusitishwa. Aidha, kujenga mahakama kwenye maeneo yaliyokosa huduma hiyo. Katika kuhakikisha kwamba huduma ya utoaji haki inafikiwa na wananchi wetu kwa urahisi, Serikali ilifanya uamuzi wa kiseru kwa kuhakikisha kila kata inakuwa na mahakama



ya mwanzo. Ni katika hali hiyo, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kutolewa kwa fedha zote za bajeti ya maendeleo katika mfuko wa mahakama kwa mwaka wa fedha 2015/16 ili kuimarisha miundombinu ya Mahakama.

13. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuanzia fedha hizo za maendeleo zilizotolewa zitawezesha ujenzi wa mahakama za mwanzo 8 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.96, ambazo ni Iguguno (Iramba), Magoma (Korogwe), Totowe (Songwe), Wasso (Loliondo), Msanzi (Sumbawanga), Bereko (Kondoa), Karatu (Manyara) na Robanda (Serengeti). Aidha, maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mahakama zingine mpya 10 za mwanzo kwa gharama ya sh. bilioni 4.502 yameanza: Longido (Manyara), Terati (Simanjiro-Manyara), Machame (Hai), Makongolosi (Chunya-Mbeya), Ulyankulu (Urambo-Tabora), Sangabuye (Ilemela-Mwanza), Mtowisa (Sumbawanga), Njombe Mjini, Gairo (Morogoro) na Mangaka (Mtwara). Vilevile, fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa mahakama za wilaya 12 kwa gharama ya sh. bilioni 6.54, ambazo ni Kilindi, Nkasi, Bukombe, Makete, Nyasa, Chato, Bunda, Namtumbo, Bariadi, Kasulu, Kondoa na Sikonge. Aidha, mradi wa ukamilishaji wa Mahakama Kilwa Masoko utaanza mara tu mchakato wa zabuni utakapokamilika. Halikadhalika, ukarabati wa Mahakama Kuu Shinyanga, Mtwara, Tanga na Mbeya uko katika hatua mbali mbali za utekelezaji na maandalizi ya awali ya ujenzi wa Mahakama Kuu Kigoma na Mara yanaendelea.
14. **Mheshimiwa Spika**, uhitimishaji wa kesi mahakamani unategemea sana upatikanaji na ubora wa huduma za uendeshaji wa mashtaka na uratibu wa shughuli za upelelezi zinazotolewa na Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka (NPSA). Hivi sasa huduma hizo zinapatikana katika mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia ofisi za mikoa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, isipokuwa Mkoa wa mpya wa Songwe.
15. **Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa ni miaka 8 sasa toka Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka nchini itungwe (*The National Prosecutions Service Act, 2008*) ambayo ilitenganisha kazi za upelelezi na mashtaka kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza uwajibikaji katika majukumu hayo mawili makubwa ya haki jinai. Hatua hii ya kuviondoa vyombo vya uchunguzi kwenye uendeshaji wa mashtaka na kuvibakiza kwenye upelelezi wa makosa (*civilianisation of prosecution*) bado haijafikia malengo yake kwani Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka imeweza mpaka sasa kubeba jukumu hilo kwenye makao makuu ya mikoa tu ambapo inaendesha kesi za jinai katika Mahakama zote za Hakimku Mkuu na za Wilaya za makao makuu ya mikoa, isipokuwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

16. **Mheshimiwa Spika**, mkoani Dar es Salaam, Mawakili wa Serikali wanaendesha kesi za jinai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Mahakama ya Jiji, Mahakama ya Wilaya Ilala na Mahakama ya Wilaya Temeke. Aidha, Mamlaka hiyo inaendesha kesi katika wilaya ya Monduli ikiwa ni wilaya pekee ya nje ya makao makuu ya mkoa; Wilaya zingine nchini zinahudumiwa na waendesha mashtaka wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya uchunguzi. Ni azma ya Wizara kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka inapanua huduma zake kwenda kwenye Wilaya nyingi zaidi na hatimaye kuzifikia Mahakama za Mwanzo. Uwepo wa Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka katika ngazi ya mikoa na wilaya una umuhimu mkubwa katika kuimarisha haki jinai nchini kwani mbali na uendesha kesi za jinai, taasisi hii ya sheria ina jukumu la kukagua magereza na mahabusu za Polisi kujiridhisha na hali ya mahabusu na wafungwa kuendana na matakwa ya sheria.
17. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto ya Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka kupanuka kwa kasi ndogo, upungufu wa mawakili na mapokezi yasiyoridhisha ya fedha ya matumizi, bado chombo hiki adhimu cha umma kimetekeleza majukumu yake kwa ufanisi, weledi na uzalendo wa hali ya juu hasa katika uendesha mashauri makubwa (*high profile cases*) yanayohusu dawa za kulevya, uwindaji haramu, misitu na wanyama pori, utakasishaji fedha haramu, n.k. Mfano kwa sasa, Mamlaka ya Taifa ya Mashtaka inaendesha kesi 161 za dawa za kulevya ambazo thamani yake inazidi shilingi milioni 10 kwa kila kesi zilizopo katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.
18. **Mheshimiwa Spika**, kati ya mashauri hayo mashauri 4 yapo katika Mahakama ya Rufaa yakitokea Mahakama Kuu za Kilimanjaro na Dar es Salaam; mashauri 9 yamehitimishwa katika Mahakama Kuu za: Tanga (shauri 1), Kilimanjaro (mashauri 3) na Dar es Salaam (mashauri 5) katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016. Kutokana na kuhitimishwa kwa mashauri hayo, washtakiwa 13 walitiwa hatiani na kupewa kifungo kati ya miaka 20 hadi maisha. Vile vile dawa za kulevya aina ya cocaine na heroine zenye uzito wa kilo 278.9 na kilo 21 za mirungi zilitokezwa baada ya amri kutolewa mahamakani. Mashauri mengine yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za kusikilizwa mahakamani.
19. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuwa chombo cha kuaminika cha Serikali pamoja na mambo mengine, kutoa ushauri wa kisheria katika masuala ya madai, haki za binadamu, katiba na mikataba na kuiwakilisha Serikali Mahakamani na Mabaraza ya Usuluhishi na Upatanishi. Pamoja na changamoto za uchache wa Mawakili wa Serikali, ufinyu wa ofisi na mapokezi madogo ya fedha ya matumizi ya kawaida, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliwakilisha vema Serikali katika mashauri

mbalimbali yaliyofunguliwa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mahakama ya Rufaa, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Mahakama ya Afrika Mashariki. Aidha, Ofisi hii iliendesha kesi za Ubunge 52 na kesi 198 za udiwani zilizofunguliwa baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 jumla ya kesi 28 za ubunge zilihitimishwa na 24 zinaendelea kusikilizwa kwa hatua mbalimbali. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishinda katika mashauri yote hayo, hatua ambayo imewawezesha Waheshimiwa Wabunge wote waliohusika na kesi hizo kuendelea na ubunge wao. Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliiwakilisha Serikali katika mashauri ya madai 818 ambapo kati ya hayo 38 yalihitimishwa na 780 yanaendelea kusikilizwa. Pia, kulikuwa na maombi ya madai 350 na rufaa za madai 59 ambapo maombi ya madai 64 yamehitimishwa na rufaa zote zinaendelea kusikilizwa.

- 20. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilipokea mashauri mapya 20 ya haki za binadamu yaliyofunguliwa katika Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu na kufanya idadi ya mashauri hayo kufikia 33 ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, lilifunguliwa shauri moja jipya kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu katika Mahakama ya Afrika Mashariki na kufanya mashauri yaliyoko mahakamani hapo, dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa mawili. Mashauri ya kikatiba yalikuwa 151 kati ya hayo 7 yalihitimishwa na 144 yanaendelea kusikilizwa.

### **III. HIFADHI YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

- 21. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kupokea, kuchambua na kufuatilia malalamiko kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu. Kuanzia mwaka 2010 hadi Aprili 2016, Tume ilipokea na kuyachunguza jumla ya malalamiko 13,709; kati ya malalamiko hayo malalamiko 6,169 yalihitimishwa na malalamiko 7,540 yanaendelea kuchunguzwa. Malalamiko mengi ambayo Tume inapokea yanahusu migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wawekezaji, wakulima na wafugaji, wananchi na maeneo ya hifadhi; matumizi mabaya ya madaraka kwa watendaji; ukatili dhidi ya wanawake na watoto; ucheleweshaji wa haki kwa mahabusu na wafungwa; na matumizi ya nguvu kwa upande wa vyombo vya dola.
- 22. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (*National Human Rights Action Plan*) wa mwaka 2013 hadi 2017, mpango ambao ulibuniwa na Serikali na kulivutia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ambalo lina changia kifedha katika utekelezaji wake. Lengo kuu la mpango kazi huu ni kuongeza

uelewa wa haki za binadamu na utawala bora nchini na nafasi yake katika mfumo wetu wa utawala. Kati ya Julai, 2015 na Januari, 2016 Tume imeendesha semina za walimu wa sekondari na wakurugenzi wa halmashauri katika mikoa tisa (9) ya Tanzania Bara na semina hizo zitaendelea kwa mikoa iliyobaki. Aidha, Tume iliratibu maadhimisho ya siku ya Haki za Binadamu Afrika na siku ya Haki za Binadamu Kimataifa, maadhimisho ambayo yanatumika kuelimisha umma kuhusu haki za watu walio katika makundi maalum. Pia, katika mwaka wa fedha 2015/16, Tume ilirusha hewani jumla ya vipindi 10 vya redio na televisheni vinavyohusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora; na hivi sasa inashirikiana na Shirika la *“Under the Same Sun”* kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na ukatili na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*) hapa nchini.

#### IV. UTAFITI NA UREKEBU WA SHERIA

**23. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea na tafiti mbalimbali za sheria ili kubaini upungufu uliopo na kutoa mapendekezo kulingana na mahitaji ya sasa kwa ustawi wa jamii na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Maeneo ya sheria zinazoendelea kufanyiwa utafiti ni mfumo wa sheria zinazosimamia haki za walaji na watumiaji wa bidhaa, mfumo wa sheria zinazohusiana na huduma za kijamii kwa wazee, mfumo wa sheria zinazosimamia haki za jinai, mfumo wa Sheria ya Ushahidi, mfumo wa Sheria ya Usuluhishi na Sheria ya Ununuzi wa Umma. Tafiti hizo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo utafiti kuhusu mfumo wa sheria zinazohusiana na huduma za wazee unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/16 na kujumuisha jumla ya sheria 15. Aidha, utafiti wa Mfumo wa Sheria unaosimamia haki jinai utamalizika katika mwaka wa fedha 2016/2017 na kuhusisha sheria zipatazo 21; utafiti kuhusu mfumo wa sheria za haki jinai utamalizika katika mwaka wa fedha 2016/17. Utafiti kuhusu sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 umekamilika na utafiti kuhusu Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 na Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 5 upo katika hatua za awali. Maelezo ya kina kuhusu tafiti za sheria mbalimbali yameoneshwa kwenye **kiambatisho Na.1.**

#### V. USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU

**24. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea na shughuli za usajili wa vizazi na vifo katika wilaya mbalimbali Tanzania Bara. Katika mkakati wa kuongeza kiwango cha usajili wa vizazi na vifo nchini, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini (RITA) imeanzisha kampeni ya usajili inayoambatana na uboreshaji wa mfumo wa usajili kwa kuweka mfumo wa kompyuta katika kila wilaya ambapo kampeni itafanyika. Kwa kuanzia, kampeni hizi zimefanyika katika wilaya za Arusha na Arumeru ambapo jumla ya watu 49,548 walisajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa. Zoezi hili linaendelea katika wilaya ya Kahama

na baadaye kuendelea katika wilaya 16 za Bariadi, Chato, Dodoma, Igunga, Kilombero, Kilosa, Lushoto, Maswa, Mbinga, Misungwi, Mtwara, Muleba, Nzega, Shinyanga, Sumbawanga na Tunduru. Wizara imekadiria kusajili zaidi ya watu 500,000 katika maeneo hayo na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

- 25. Mheshimiwa Spika:** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, RITA imeanza kukusanya ada zote zitokanazo na huduma inazozitoa kwa njia ya kielektroniki kwa wadau kufanya malipo yao kupitia simu za mkononi au benki. Tayari, jumla ya wilaya 114 kati ya wilaya 139 zinakusanya maduhuli kwa njia za kielektroniki na kwamba ifikapo mwezi Juni, 2016 wilaya zote za Tanzania Bara zitakuwa zikitumia njia za kielektroniki kukusanya maduhuli.
- 26. Mheshimiwa Spika,** utafiti wa afya uliofanyika mwaka 2010 (the 2010 Tanzania Demographic and Health Survey) ulionesha kuwa ni asilimia 16 tu ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) ndio wenye usajili na vyeti vya kuzaliwa Tanzania Bara, ikilinganishwa na Tanzania Zanzibar ambapo usajili na vyeti vya kuzaliwa ulikuwa ni asilimia 79. Ili kubadilisha hali hiyo duni, RITA kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) wamebuni mradi wa kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano ambao ulifanyiwa majaribio Temeke mwaka 2012 na baadaye mwaka 2014 mradi huo kuzinduliwa Mbeya. Mradi huo unaonekana una tija kwani ulipoingia Mbeya usajili ulikuwa asilimia 8.7 tu na sasa umepanda hadi asilimia 58. Baada ya Mbeya kampeni hiyo imehamia Mwanza na baadaye itakwenda mikoa ya Mara, Shinyanga, Simiyu, Geita, Iringa, Njombe, Tabora, Kagera na Dodoma.
- 27. Mheshimiwa Spika,** hali kadhalika, Wizara iliimarisha ushirikiano kati yake na wadau na kufanikiwa kuandaa mkakati wa taifa wa usajili na ukusanyaji wa takwimu muhimu (Civil Registration & Vital Statistics - CRVS) ambao maandalizi ya rasimu ya kwanza yamekamiliika tayari kuwasilishwa Serikalini kwa maamuzi. Kutokana na mchango mkubwa waliutoa katika kufanikisha kazi hiyo, naomba kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa taasisi zote tulizoshirikiana nazo katika kubuni na kuandaa rasimu ya mkakati huu: Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (kwa wakati huo ikijulikana kama PMORALG); Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (kwa wakati huo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na wadau wengine wa maenndeleo.
- 28. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia uendeshaji wa shughuli za ufilisi na udhamini hapa nchini ili kuhakikisha kunakuwepo tija na ufanisi. Katika kuimarisha shughuli za ufilisi Wizara imeanzisha mchakato wa kutunga sheria moja ya ufilisi tofauti na ilivyo sasa ambapo shughuli hizo zinasimamiwa

na sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge lako tukufu. Katika masuala ya udhamini wa taasisi/asasi za kidini na kijamii Wizara imeanza kufanya mapitio ya taarifa zao ili kubaini taasisi hai na zinazoendeshwa kulingana na katiba zao na kuhakikisha kwamba zinatimiza malengo ya kuanzishwa kwake na kuzingatia sheria za nchi. Hali kadhalika, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za usimamizi wa mirathi na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuandika wosia ili kupunguza migogoro ambayo imekuwa ikitokea miongoni mwa ndugu wa jamaa aliyefariki bila kuacha wosia.

## **VI. ELIMU NA MSAADA WA KISHERIA KWA UMMU**

- 29. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na juhudi za kuboresha mfumo wa sheria nchini ili kuwezesha wananchi wote kuifikia haki wanapoitafuta, bila kujali uwezo wa mtu katika jamii, hasa wa maeneo ya vijijini. Hii ni hatua moja muhimu katika vita dhidi ya umaskini kwa kuwaunganisha wananchi wengi zaidi na mfumo wa kawaida wa utoaji haki. Hivyo, Wizara imewasilisha Serikalini rasimu ya waraka wenye mapendekezo ya kutunga upya sheria ya msaada wa kisheria ambao unasubiri uamuzi wa Baraza la Mawaziri. Matarajio ya Wizara ni kuwasilisha muswada wa sheria hiyo bungeni kabla ya kumalizika kwa mwaka 2016. Pia, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa msaada wa kisheria kupitia sekretarieti ya msaada wa kisheria, ambayo ilianzishwa kama chombo cha mpito wakati taifa likisubiri kukamilika kwa mchakato wa kutunga Sheria mahususi ya kusimamia eneo hilo la huduma.
- 30. Mheshimiwa Spika**, mafunzo ya uanasheria kwa vitendo ni moja ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika kuimarisha mfumo wa sheria nchini. Katika kuhakikisha hilo, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo imefanikiwa kuongeza uwezo wake wa kudahili wanafunzi kufikia wanafunzi 1,800 mwaka huu pamoja na kushughulikia maombi ya kujiunga na taasisi hiyo kwa njia ya mtandao (*online application*) ili kuwafikia wadau wengi zaidi na kupunguza gharama za kujiunga. Taasisi hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuziba pengo la mahitaji ya mawakili na wanasheria wanaojiunga na sekta ya umma na binafsi, kwa kuajiriwa na/au kwa kujitolea kutoa msaada wa kisheria. Maelezo ya kina kuhusu udahili wa wanafunzi yameoneshwa kwenye **kiambatisho Na. 2(a) na 2(b)**.
- 31.** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria na haki za kisheria kwa njia ya machapisho, vipindi vya redio na televisheni, mikutano ya hadhara, vijarida na vipeperushi pamoja na kushiriki katika maonesho ya kitaifa, ya Saba Saba, Wiki ya Utumishi wa Umma na wiki ya kuelekea Siku ya Sheria. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ilirusha hewani vipindi 16 vya redio na vipindi 3 vya televisheni vilivyolenga kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu sheria na huduma za kisheria zinazotolewa. Vilevile, iliendesha programu za elimu kwa umma, mahususi kwa wananchi wa mikoa



ya kati, kupitia kituo cha redio cha *Mwangaza FM*, Dodoma na *Voice of Tabora* ambapo wananchi walipata fursa ya kujifunza kuhusu maboresho ya mfumo wa mashtaka nchini na mafanikio yaliyopatikana, hususan kuharakisha usikilizaji wa mashauri. Hakika, matumizi ya redio yamedhihirika kuwa ni nyenzo muhimu ya kuwafikia wananchi na kuwawezesha kuzifahamu vema sheria za nchi, kuzishika na kuzitumia kufuatilia haki zao kwenye vyombo husika.

## **VII. UBORESHAJI WA HUDUMA ZA KISHERIA NA MAZINGIRA YA KAZI**

- 32. Mheshimiwa Spika**, dhamira ya Serikali kuhusu uboreshaji wa huduma za kisheria kwa umma ndiyo kiini cha maboresho ya sekta ya sheria ambayo yamekuwepo nchini tangu mwaka 2007 kupitia programu ya maboresho ya sekta ya sheria na mikakati yake. Kupitia maboresho hayo Serikali imefanya mageuzi makubwa katika mfumo wa sheria, kuimarisha miundombinu ya utoaji huduma na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), na ununuzi wa vitendea kazi.
- 33. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 Wizara imefanya maboresho katika mfumo wa kielektroniki kuwezesha wananchi kufikisha malalamiko yao kwa njia ya simu za mkononi. Aidha, Wizara inafanya maandalizi ya awali ya mradi mkubwa zaidi wa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji haki.
- 34. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kufanya kazi kwa karibu na Tume ya Utumishi wa Mahakama, taasisi huru iliyoungwa kwa mujibu wa ibara ya 112 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kusimamia uendeshaji wa Mahakama ya Tanzania. Majukumu makuu ya Tume ni kushauri kuhusu teuzi za ngazi za juu za Mahakama na kusimamia masuala ya ajira na nidhamu ya watumishi wa Mahakama.
- 35. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi tunachokiaga, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliajiri jumla ya watumishi 989, kati yao Mahakimu Wakazi 248 na watumishi wasio mahakimu 741. Pia, Tume ilishughulikia jumla ya mashauri 14 ya nidhamu kwa watumishi wa mahakama na kuyatolea uamuzi. Katika mashauri hayo, watumishi 10 walifukuzwa kazi baada ya kupatikana na hatia ya utovu wa nidhamu na mengine 4 yanaendelea kufanyiwa uchunguzi zaidi.



### C. MTIRIRIKO WA MAPATO NA MAKUSANYO YA MADUHULI

#### (i) *Mapato ya Bajeti*

**36. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya Shilingi 196,087,197,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi 68,819,125,000 ni za mishahara, Shilingi 111,886,746,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 15,381,326,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za maendeleo za ndani ni Shilingi 13,319,000,000 na fedha za nje ni Shilingi 2,062,326,000.

**37. Mheshimiwa Spika**, kufikia mwezi Aprili, 2016 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 119,784,602,272 sawa na asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi 54,772,582,835 ni mishahara ya watumishi na Shilingi 51,802,552,437 ni kwa matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo ni Shilingi 13,209,467,000 ambapo fedha za ndani ni Shilingi 12,644,740,000 na fedha za nje ni Shilingi 564,727,000.

#### (ii) *Makusanyo ya Maduhuli*

**38. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 17,023,933,750 kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 11,116,849,811 kama maduhuli ya Serikali, kama ilivyochanganuliwa hapa chini:

FUNGU			MAKADIRIO	MAKUSANYO	%
12	-	Sh.	0	0	0
16	-	Sh.	1,002,000	3,255,000	325
35	-	Sh.	13,002,000	12,000,000	92
40	-	Sh.	5,203,298,719	5,789,939,272	111
41	-	Sh.	11,801,400,000	5,890,822,355	50
55	-	Sh.	5,131,000	0	0
59	-	Sh.	100,000	0	0
<b>JUMLA</b>		<b>Sh.</b>	<b>17,023,933,719</b>	<b>11,696,016,627</b>	<b>65</b>

## A. CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO

### (i) *Changamoto*

1. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali zilizochangia kurudisha nyuma juhudi za Serikali za kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria. Kati ya hizo, ni changamoto ya ufinyu wa bajeti ambapo bajeti inayotengwa imekuwa haiakisi mahitaji halisi ya kuiwezesha kutoa huduma bora na kwa wakati. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu taarifa za kibajeti angalia **kiambatisho Na.3(a), 3(b) na 3(c)**.

### (ii) *Mikakati ya Wizara*

2. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwa kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, katika kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayohusiana na uhaba wa watumishi wenye ujuzi, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vibali vya ajira, kujaza nafasi zilizoachwa wazi na maslahi ya watumishi; kubainisha vyanzo vipya vya mapato na namna bora ya kuvitumia kama vile kutayarisha maandiko ya miradi na kuanzisha ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo. Vilevile, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na

changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kujiepusha na matumizi yasiyo ya lazima na kufanya marekebisho ya namna ya kupangilia utekelezaji wa majukumu yake kwa kuanzisha utaratibu wa kutumia vigezo vya utendaji kazi kwa watumishi; na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma sanjari na kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji.

## **B. SHUKRANI**

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa taasisi na mashirika mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa yakiwemo: nchi wahisani, balozi zinazowakilisha nchi zao hapa nchini, mashirika yaliyochini ya Umoja wa Mataifa, Asasi za Kijamii na Kiraia, Washirika wa Kimaendeleo, Vyuo Vikuu, Vyama vya Kitaaluma na Taasisi za Utafiti kwa michango yao mikubwa wanayotoa katika utendaji kazi wa Wizara na nchi yetu kwa ujumla. Taasisi na Mashirika hayo yamesaidia maeneo mbalimbali ya utendaji na hivyo kutuwezesha kufikia malengo yetu ya Wizara.
4. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, nawashukuru wasaidizi wangu Profesa Sifuni Mchome, Katibu Mkuu na Amoni Mpanju Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Taasisi zilizochini ya Wizara, Wakuu wa Idara na Vitengo kwa jitihada na ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.
5. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara nyingine, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kutupatia ushirikiano adhimu kwa nyakati mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

## **C. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2016/2017**

6. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu itaendelea na utaratibu na uimarishaji wa mfumo wa Sheria wan chi na pia juhudi za kuongeza ubora na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria na kikatiba sanjari na Dhima ya Wizara. Hivyo, Wizara imeainisha maeneo muhimu ya kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake na katika mgawanyo wa rasilimali zilizopo. Kwa muktadha huo Wizara itachukua hatua madhubuti kuimarisha usimamizi na utendaji wa mfumo wa sheria; kukamilisha taratibu za divisheni ya Rushwa na ufasadi ili ianze kazi tarehe 1 Julai 2016 kama hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu ilivyobainisha na kusimamia mambo ya Katiba na Sheria kwa ujumla. Hali kadhalika, kuimarisha miundombinu ya huduma za kisheria na kuboresha mazingira ya utendaji kazi; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kuimarisha utafiti na uandishi wa sheria

- ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya sheria za usafirishaji, uwekezaji, sheria zinazosimamia eneo la ustawi wa jamii linalojumuisha sheria zipatazo tano ambazo ni: Sheria ya maadili ya viongozi wa umma Na. 13 ya 1995, Sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa, Sheria ya Bima ya Afya, Sheria inayosimamia hifadhi ya jamii, na mfumo wa sheria zinazosimamia elimu, na Mapitio ya Sheria zinazosimamia biashara na uchumi.

7. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itachukua hatua kuimarisha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo, kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na takwimu, kuwaendeleza watumishi kitaaluma, kuimarisha taasisi ya mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa kuanzisha masomo ya jioni (*part-time programmes*) na kuanzisha vituo vya kanda ili kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 1,800 hadi wanafunzi 3,000 kwa mwaka, ifikapo mwaka 2020.
8. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendeleza ushirikiano wa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo taasisi zake, Polisi na Magereza ni vyombo muhimu katika mfumo mzima wa haki jinai nchini. Aidha, Wizara italitumia kwa karibu zaidi jukwaa la Haki Jinai chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambalo linajumuisha Wakuu wa Vyombo vyote vya haki jinai katika kutatua kero zifuatazo zinazochelewesha au kukwamisha upatikanaji wa haki sawa kwa wote na wakati:
  - i. Mazoea ya kila kesi ya jinai, iwe ndogo au kubwa kuruhusiwa muda mrefu wa upelelezi, hata kwa kesi ambayo mtuhumiwa kakiri kosa au mashahidi wapo walioshuhudia kosa likitendeka. Wizara itataka maelekezo ya kisheria yawepo ya muda mahsusi wa kumaliza kesi kama hizo bila kisingizio cha upelelezi;
  - ii. Upotevu wa mafaili ya kesi. Pamoja na mahakama kuchukua hatua stahili za kiutendaji na kinidhamu kila upotevu wa mafaili ukitokea, tatizo linazidi kujirudia na kuwa moja ya sababu ya mrundikano wa kesi mahakamani. Wizara itataka hatua kali zaidi zichukuliwe dhidi ya wale wote waliohusika na upotevu huo ili usirudiwe.
  - iii. Ucheleweshaji wa nakala za hukumu na mwenendo wa mashauri. Pamoja na jitahada bayana zinazofanywa na mahakama kuongeza kasi katika utoaji wa nyaraka hizo, Wizara inaliona tatizo kuwa kubwa linalohitaji mahakama kuongezewa kada ya wachapaji na vitendea kazi.
  - iv. Ubambikizwaji kesi katika vituo vya Polisi. Tuhuma hii imerudiwa mara nyingi mno kiasi ambacho haina budi kuangaliwa kwa jicho kali ili

kudhibiti hali hiyo. Wizara itatafuta njia muafaka ya kisheria kuhakikisha kuwa hali hiyo haijitokezi katika mfumo wetu wa haki jinai.

- 9. Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi na majukumu yanayoambatana navyo, Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi **35,785,416,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kama ifuatavyo:

- a) Mishahara ya Watumishi - Sh. **22,391,694,000**
- b) Matumizi Mengineyo - Sh. **10,619,234,000**
- c) Miradi ya Maendeleo - Sh. **2,774,488,000**

- 10. Mheshimiwa Spika**, fedha hizo zimegawanyika katika mafungu sita (6) ya Wizara kama inavyoonekana hapa chini.

<b>Fungu 12</b>	- Tume ya Utumishi wa Mahakama	-	1,134,955,000
<b>Fungu 16</b>	- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	-	6,997,324,000
<b>Fungu 35</b>	- Divisheni ya Mashtaka	-	13,299,639,000
<b>Fungu 41</b>	- Wizara ya Katiba na Sheria	-	9,137,717,000
<b>Fungu 55</b>	- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	-	3,557,589,000
<b>Fungu 59</b>	- Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	-	1,658,192,000
<b>Jumla</b>			<b>35,785,416,000</b>

**(a) Muhtasari wa Matumizi**

- 49. Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Matumizi ya Mishahara	- Sh. 314,448,000
Matumizi Mengineyo	- Sh. 820,507,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	- Sh. -
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	- Sh. -
<b>Jumla</b>	<b>- Sh. 1,134,955,000</b>

**(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Matumizi ya Mishahara	-Sh. 3,741,264,000
Matumizi Mengineyo	- Sh. 2,256,060,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	- Sh. 1,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	- Sh. -
<b>Jumla</b>	<b>- Sh. 6,997,324,000</b>

**(iii) Fungu 35: Divisheni ya Mashtaka**

Matumizi ya Mishahara	- Sh. 9,551,292,000
Matumizi Mengineyo	- Sh. 3,546,327,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	- Sh. -
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	- Sh. 202,020,000
<b>Jumla</b>	<b>- Sh. 13,299,639,000</b>

**(iv) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria**

Matumizi ya Mishahara	- Sh. 5,481,216,000
Matumizi Mengineyo	- Sh. 2,263,992,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	- Sh. 1,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	- Sh. 392,509,000
<b>Jumla</b>	<b>- Sh. 9,137,717,000</b>

**(v) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Matumizi ya Mishahara	- Sh. 2,383,116,000
Matumizi Mengineyo	- Sh. 994,514,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	- Sh. -
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	- Sh. 179,959,000
<b>Jumla</b>	<b>- Sh. 3,557,589,000</b>

**(vi) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria**

Matumizi ya Mishahara	- Sh. 920,358,000
Matumizi Mengineyo	- Sh. 737,834,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	- Sh. -
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	- Sh. -
<b>Jumla</b>	<b>- Sh. 1,658,192,000</b>

**(b) Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali**

**50. Mheshimwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **18,400,152,435** ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

Fungu 12	- Sh.	-
Fungu 16	- Sh.	1,002,000
Fungu 35	- Sh.	13,002,000
Fungu 40	- Sh.	6,504,132,435
Fungu 41	- Sh.	11,882,012,000
Fungu 55	- Sh.	-
Fungu 59	- Sh.	4,000

**51. Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya KASMA za mafungu husika.

**52. Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua masuala yanayohusu Wizara hii, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ili aje awasilishe taarifa ya Kamati. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Najma Giga, Makamu Mwenyekiti. (Makofi)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. NAJMA M. GIGA - (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijalia kuwa Mwakilishi wa Umoja wa Wazazi Tanzania katika Bunge hili. Pia, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mzima wa afya na leo hii kuja kupata fursa ya kuwasilisha mbele yako Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifuNgu cha 6(2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake.



Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ina mafungu sita ya bajeti ambayo ni:-

Kwanza ni Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria; Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria; Fungu 35 - Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka; Fungu 16 - Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa matano yafuatayo:-

(i) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;

(ii) Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2015/2016;

(iii) Utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016;

(iv) Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii na mwisho ni;

(v) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupokea taarifa kuhusu mradi unaohusu ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vile vile Kamati ilipata taarifa kuhusu miradi ya maendeleo iliyoko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Katiba na Sheria ilitengewa sh. 2,959,719,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo sh. 2,000,000,000/= ni fedha za ndani na sh. 959,719,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2016; Wizara ilipokea na kutumia sh. 33,630,000/= ambazo ni fedha za nje, kupitia mradi wa *UNICEF Multi-sectoral Support*. Ofisi haikupokea fedha yoyote ya ndani kama ilivyoidhinishwa na Bunge ambazo zingesaaidia katika utekelezaji wa mradi huu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishwa sh. 648,740,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha

hizo sh. 344,740,000/= ni fedha za ndani na sh. 300,000,000/= ni fedha za nje kutoka UNDP.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo zilikuwa ni kwa ajili ya kujengea uwezo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kusimamia masuala ya mikataba mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mikataba ya Sekta ya Nishati na Madini, kupitia mradi wa *Capacity Development in the Energy Sector and Extractive Industries*.

Mheshimiwa Spika, mradi huu haukuweza kutekelezwa ipasavyo kwa sababu ya kukosekana kwa fedha za nje kutoka *United Nation Development Program*; ambayo iliahidi kutoa sh. 300,000,000 na hazikutolewa. Fedha iliyotolewa ni sh. 344,740,000/= tu kwa mradi huu, ambazo ni fedha za ndani. Vile vile Ofisi hii imeshindwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa ukarabari wa majengo yake kwa sababu ya kukosekana fedha.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu la 55. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitengewa sh. 246,122,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa *National Human Rights Action Plan*. Mradi huu unahusu utekelezaji wa Mpango wa Mkakati wa Kitaifa wa Haki za Binadamu Nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2016 kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya mradi huu ni sh. 188,212,000/= sawa na asilimia 76 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Hivyo, mradi huu haukutekelezeka kikamilifu kutokana na kutotolewa fedha zote zinazokidhi mahitaji ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya ujumla kuhusu utekelezaji wa mradi wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016:-

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na kasi ya utoaji wa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kwani karibu miradi yote imepokea sehemu tu ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Kamati vile vile inasikitishwa na hatua ya Serikali kutotoa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi mingi ya maendeleo imekuwa inategemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje. Mfano katika Fungu 16, Ofisi ilipokea fedha za nje tu kupitia *UNICEF - Multi-sectoral Support Program* na haikupokea fedha yoyote kutoka ndani.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kufanya maendeleo, kuna umuhimu wa kila Taasisi ya Serikali, kubuni vyanzo vya mapato vitakavyosaidia kuongeza fedha za ndani ili kuepuka utegemezi wa fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni uchambuzi wa taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria, kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge mwezi Mei, 2015 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi, 2016. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa mpango wa bajeti ya mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2015/2016 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Katiba na Sheria kwa ujumla iliidhinishwa sh. 191,450,901,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, Wizara ilipokea jumla ya sh. 97,255,506,289/= sawa na asilimia 49 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, fedha inayoombwa na Wizara ya Sheria na Katiba kwa mafungu yote katika mwaka huu wa fedha ni sh. 35,785,416,000/=. Fedha hii ni mara tano pungufu ya fedha iliyotengwa kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu unatokana na kiasi kikubwa cha fedha iliyokuwa inatengwa chini ya Fungu 41 kuhamishiwa katika Fungu 40, yaani Mahakama, kutokana na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Pia upungufu huu unatokana na kupungua kwa fedha ya matumizi mengineyo kwa Wizara na Sekta zote ambazo ni mwenendo wa Bajeti katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara mpaka sasa imepokea asilimia 49 ya fedha iliyoidhinishwa. Kukosekana kwa kiasi hicho kikubwa cha fedha katika Wizara hii, kutakuwa kumeathiri utekelezaji wa majukumu muhimu na ya msingi na Kamati inaona kuwa kuna umuhimu wa kusisitiza Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati ili majukumu ya Wizara yaweze kutekelezeka kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kufikia Machi 2016, katika Mafungu sita yaliyosimamiwa na Wizara, yaani Fungu 41, 16, 35, 59, 55 na 12, umeidhinishwa kwenye majedwali hapa chini kama ambavyo mnaona.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa upokeaji wa fedha kwa ujumla unaonesha kwamba fedha inayopokelewa ni ndogo sana ukilinganisha na kiasi kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hii inaonesha kwamba Taasisi nyingi

zinashindwa kumudu majukumu yao kwa wakati na ufanisi kutokana na fedha kuchelewa kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Katiba na Sheria kwa pamoja na Taasisi zake ilitarajia kukusanya kiasi cha sh. 17,023,933,750/= kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Februari, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha sh. 11,116,849,811/= ikiwa ni sawa na asilimia 65 ya makusanyo yaliyotarajiwa kama ilivyochanganuliwa hapo chini mnaona.

Mheshimiwa Spika, makusanyo haya ni kutokana na ada za usajili wa matukio, ada za wanafunzi, uuzaji wa vitabu vya zabuni na huduma nyingine mbalimbali zinazotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria - Fungu 41 imeongoza katika ukusanyaji wa maduhuli kwa kukusanya sh. 5,890,822,000/= ikifuatiwa na Idara ya Mahakama iliyokusanya sh. 5,210,772,457/= na Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Fungu 16 ilikusanya sh. 3,225,000/=.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha uliopita haukuendana na matarajio ya Wizara. Matarajio ya Wizara yalikuwa makubwa lakini kilichopatikana ni kidogo. Hivyo kuna umuhimu wa kuweka vyanzo vingine vya ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa kwa zile Taasisi zilizokosa mapato kabisa. Hii ni changamoto ambapo Wizara na Taasisi zote zenye vyanzo vya mapato zinabidi kuliangalia kwa umakini kwani matarajio siyo mapato.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uwasilishwaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo 27 kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa mapendekezo yote yametokelezwa isipokuwa moja ambalo linahusu deni la RITA.

Katika mwaka 2015/2016, Kamati iliishauri Serikali kulipa fedha inazodaiwa na RITA ili RITA iweze kutekeleza majukumu yake katika mkataba wa ubia wa jengo la RITA tower ili kuepukana na ongezeko la riba. Kamati imeelezwa kuwa

kutokana na changamoto za kibajeti, Serikali imeshindwa kulipa deni hilo na inafanya jitihada ili fedha hizo zipatikane.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazidi kuisisitiza Serikali kulipa deni hilo mapema ili kupunguza ongezeko la riba kutokana na kutolipwa kwa deni hilo.  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni mpango wa Makadirio na Mapato ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Katiba na Sheria imejiwekea malengo 11 ya utekelezaji ili kuongeza ufanisi na ubora katika kutoa huduma za kisheria na masuala ya Katiba na malengo hayo ni haya yafuatayo:-

- (1) Kuimarisha usimamizi na utaratibu wa mfumo wa sheria;
- (2) Kuratibu uanzishwaji na uendeshwaji wa *Division* ya Mahakama ya Rushwa na Ufisadi ili kuharakisha usikilizaji wa mashauri;
- (3) Kuratibu uundaji na uendeshaji wa Kamati ya kusimamia utekelezaji wa masharti yatokanayo na masharti ya mpito kwenye Katiba inayopendekezwa;
- (4) Kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya huduma za Mahakama na Taasisi zake;
- (5) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma mbalimbali na kutunza kumbukumbu muhimu;
- (6) Kuimarisha shughuli za utafiti wa sheria na kufanya marekebisho ya sheria zilizopitwa na wakati;
- (7) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuendeleza watumishi kitaaluma;
- (8) Kuimarisha huduma za Taasisi ya mafunzo ya Wanasheria kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi na kupanua wigo wa huduma kwa walengwa;
- (9) Kuweka wigo mpana wa sheria na upatikanaji wa msaada wa kisheria (*legally aid services*) kwa watu wasio na uwezo;
- (10) Kuimarisha mfumo wa utunzaji wa nyaraka, kumbukumbu na takwimu; na

(11) Kuimarisha shughuli za usajili na utunzaji wa kumbukumbu (*civilian registration and vital statistics*).

Mheshimiwa Spika, malengo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii yameongezeka ukilinganisha na malengo waliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2015/2016. Kamati imeridhishwa na malengo ya Wizara kwa ujumla, kwani yanalenga katika kuboresha utekelezaji wa majukumu na kuleta ufanisi zaidi katika suala zima la utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni makadirio ya mapato ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha sh. 11,896,20,000/= ikiwa ni maduhuli ya Serikali kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini ambalo mnaliona.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa makadirio ya mapato hayaendani na hali halisi ya makusanyo. Hivyo Kamati inashauri kuwa ni vizuri Serikali ikaweka makadirio madogo yenye uhakika kuliko kuweka matarajio makubwa ambayo mwisho wa siku hayakusanywi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama hayana matarajio yoyote ya kukusanya maduhuli kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imeomba kuidhinishiwa kiasi cha sh. 35,785,416,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Mishahara ya watumishi sh. 22,391,694,000/=, matumizi mengineyo ni sh. 10,619,234,000/= na miradi ya maendeleo ni sh. 2,774,488,000 na jumla ya yote ni 35,785,416,000/.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoombwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ni sawa na asilimia 0.1 ya Bajeti Kuu ya Taifa ya mwaka wa fedha 2016 ambayo ni trilioni 29.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria katika mafungu sita unaonesha jumla ya fedha zitakazotumika katika mwaka wa fedha ujao, ikijumuisha matumizi ya mishahara, matumizi mengineyo pamoja na matumizi ya fedha za maendeleo za nje na ndani kwa ujumla katika kila fungu kama inavyoonekana katika jedwali hilo hapo chini.

Mheshimiwa Spika, *Division* ya Mashtaka, Fungu 35 lina Makadirio ya Matumizi ya juu zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine. Bajeti inayooombwa kwa ajili ya fungu hili ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12 lina makadirio ya matumizi madogo zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine ikiwa ni sawa na asilimia 3.2 ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55 inaombewa sh. 3,555,589,000/=. Wakati Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ikiwakilisha taarifa yake kwenye Kamati tarehe 8 Aprili, 2016 ilibainisha kuwa fedha zilizotengwa zinakidhi mishahara, malipo ya pango la ofisi na malipo mengine madogo madogo. Hivyo kwa bajeti inayooombwa, haiwezeshi Tume kutekeleza majukumu yake ya msingi yaliyowekwa kikatiba kama vile kuhamasisha haki za binadamu nchini, kufanya uchunguzi juu ya uvunjwaji wa haki za binadamu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kusisitiza umuhimu wa Tume hii kuongezewa fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, tarehe 4 Mei, 2016 Mwenyekiti wa Kamati hii ya Katiba na Sheria aliwasilisha maombi yake ya Kamati ya Bajeti ya nyongeza ya shilingi bilioni mbili katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala katika mwaka 2016/2017 inaombewa kiasi cha sh. 3,555,589,000/=. Kati ya fedha hizo sh. 2,383,116,000/= ni kwa ajili ya mishahara na sh. 994,514,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizi za matumizi mengineyo, sh. 320,000,000/= zimetengwa na kuzuiwa kwa ajili ya kulipa pango. Hivyo Tume inabakiwa na sh. 674,514,000/= za utekelezaji wa majukumu yake. Kiasi hiki hakitaweza kukidhi hata mahitaji ya uendeshaji ofisi ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa hapo chini katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Kamati inashauri Serikali kuiongezea Tume kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa bajeti hii ndogo inayooombwa, Watumishi wa Tume watapokea mishahara tu bila kufanya kazi yoyote kwa mwaka mzima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele kwa Tume yenye kugusa moja kwa moja haki za binadamu ambayo hayakutengewa fedha yoyote ni kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatilia haki za makundi maalum katika jamii, kama watoto, watu wenye ulemavu, wazee na kutoa elimu kwa umma;



- (b) Kufuatilia na kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu;
- (c) Kuimarisha mahusiano na wadau wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
- (d) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; na
- (e) Nyongeza ya gharama za utendaji na kuendesha ofisi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo hayakutengewa fedha hapo juu ni kati ya majukumu ya msingi ya Tume ambayo yalipaswa kupewa kipaumbele. Hivyo, kwa msingi huu Kamati inaona kuwa fedha inayoombwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni ndogo na haitaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati. Kwa upande wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55, Kamati inashauri Serikali itoe fedha za kutosha kwa Tume ili iweze kutimiza majukumu yake ya Kikatiba kwa ufanisi. Pia Serikali iongeze Ofisi za Tume katika mikoa mingi zaidi Tanzania Bara na Zanzibar na hasa Pemba ambapo Tume bado haijaweza kuanza kufanya kazi kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa upande wa Tanzania Bara, Tume iongeze ofisi zaidi katika Kanda ya Ziwa ambapo kumekuwa na matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za binadamu hasa maeneo ya migodini. Serikali pia ihakikishe kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya Tume inatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati pia inashauri Serikali kufuata sheria zilizowekwa katika kutekeleza majukumu yake kwa sababu kuna sheria ambazo inaonekana utekelezaji wake ni mgumu, kwa mfano adhabu ya kifo. Hivyo Kamati inashauri kama kuna sheria ambazo utekelezaji wake ni mgumu zifanyiwe marekebisho. Hii itaendana na Itifaki ya Pili ya Mkataba wa Kimataifa wa haki za kiraia na kisiasa wa mwaka 1966 unazozitaka nchi wanachama wa mkataba huu kuondoa adhabu ya kifo.

Mheshimiwa Spika, ingawa Tanzania bado haijaridhia itifaki hii ya mwaka 1986, Kamati inaishauri Serikali kuridhia itifaki hii na kutunga sheria ambayo itaondoa adhabu ya kifo. Hatua hii ni muhimu kwa sababu Tanzania tayari imeridhia mkataba huu wa mwaka 1966 na Kamati inashauri Serikali kuridhia itifaki hii ya mwaka 1989 iliyo chini ya mkataba huu wa mwaka 1966.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fungu la 16, Kamati inaishauri Serikali ianzishe mapema iwezekanavyo mchakato wa kujenga Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na wawekezaji wengine kama vile NSSF.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itenge bajeti ya kutosha itakayoweza kuwajengea uwezo na ujuzi watumishi wa ofisi hii na kuwapatia mafunzo ya kisasa katika nyanja mbalimbali ili waendane na mabadiliko ya teknolojia kulingana na taaluma zao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kuwa sasa nchi inaingia katika uchumi wa gesi, Kamati inashauri Serikali kujenga uwezo wa Wanasheria wa Serikali ili wabobee katika Sheria za Mafuta na Gesi hasa eneo la mikataba ya sekta hii. Hii itaongeza uwezo wa Serikali katika kujadili na kusimamia maslahi ya Taifa na kupunguza uwezekano wa kuhujumiwa na makampuni makubwa yaliyowekeza katika Sekta ya Gesi na Mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya Kurekebisha Sheria - Fungu 59; kutokana na ufinyu wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti kwa Tume ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Serikali pia iendele kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Tume kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa ili kuboresha sheria za nchi.

Aidha, Tume iendele kufanya tafiti kuhusu sheria mbalimbali ambazo kutokana na mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi, zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziweze kuendana na wakati wa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Serikali kufanyia kazi kwa haraka taarifa za utafiti za Tume hasa kuhusu Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambayo inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 kuhusu umri wa mtoto ili kulinda haki zote za mtoto (*birth interest of the child*) na hasa haki ya kila mtoto kupata elimu, kuwa na afya njema na kutoolewa mapema. Pia Kamati inaishauri Serikali kupitia na kuifanyia kazi taarifa na sheria zote zilizowasilishwa na Tume, zinazohitaji maboresho ili kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *Division* ya Mashtaka - Fungu 35, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuajiri Mawakili wa Serikali wa kutosha ili kukabiliana na wingi wa kesi kutokana na ongezeko la uhalifu. Aidha, maslahi ya watumishi hao yaboreshwe ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Vile vile Kamati inasisitiza juu ya ujenzi wa nyumba za Mawakili wa Serikali ili waweze kuishi kwenye makazi salama ukizingatia kuwa wanashughulikia kesi mbalimbali ambazo zinahusisha matukio makubwa ya uhalifu kama mauaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12, Kamati ina mashauri nane kwa Serikali. La kwanza, ni Serikali ione umuhimu wa kuiongezea Tume hii fedha kwa kulingana na majukumu yake; pili, kutokana na kutokamilika kwa matengenezo ya vyumba vya ofisi katika jengo la *RITA* ambao unasababisha Mwenyekiti wa Tume, Wajumbe na Makamishna

kukosa ofisi mahususi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili ofisi zilizopo kwenye jengo la RITA zikamilike kwa haraka.

Tatu, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili Tume hii iweze kushughulikia kikamilifu malalamiko ya ukiukwaji wa maadili na nidhamu kwa watumishi wa Mahakama. Nne, Kamati inaishauri Serikali kufuata Sheria za NACTE za Uanzishwaji wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na aidha Kamati inashauri Serikali kuboresha Chuo hicho cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kiweze kutoa wahitimu mahiri katika fani ya sheria katika kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo hili, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba Mkuu wa Chuo na Wahadhiri wengine wana viwango vya elimu vinavyokubalika katika kufundisha Vyuo Vikuu Tanzania hasa kiwango cha uzamivu na uzamili. Tano, kusimamia haki katika ubora unaotakiwa.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba idadi ya kesi walizopangiwa Mahakimu na Majaji kwa mwaka hakuathiri ubora na hukumu wanazozitoa na usimamizi wa haki Mahakamani. Kamati inatambua kwamba dhana ya *justice delayed is justice denied* ni muhimu katika utoaji wa haki; lakini ni muhimu pia kwa utendaji wa Mahakama kuzingatia dhana ya *justice hurried is justice buried* katika kusimamia haki. Hivyo, Kamati inashauri Mahakimu, Majaji na Watendaji wa Mahakama kuhakikisha kwamba haki inasimamiwa katika ubora wake na siyo katika wingi wa kesi zinazoamuliwa na Mahakama.

Sita, Kamati inashauri Serikali kuboresha miundombinu ya Mahakama hasa Mahakama ya mwanzo na Wilaya ili kuboresha mazingira ya ufanisi na utoaji wa haki nchini; na pia saba, Kamati inashauri Serikali kulipia gharama za nyumba na posho ya kutofanya shughuli binafsi za sheria (*rent assistance and non-practicing allowance*) kwa Mahakimu 1,224 walioajiriwa na Mahakama kama ilivyo kwa Wanasheria wa Serikali.

Mwisho, Kamati inashauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuendelea kuchukua hatua kali ya kinidhamu kwa Watumishi wa Mahakama wasiozingatia maadili ya kazi na kuhakikisha kwamba watumishi hao wanawajibishwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni Wizara ya Katiba na Sheria ambapo kwanza Kamati inashauri Wizara ya Katiba na sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhuisha mchakato wa kupata Katiba mpya kutokana na mapendekezo yaliyotolewa katika mchakato wa kupata Katiba uliosimama mwaka 2014 Oktoba.

Aidha, inasisitiza kwamba ni muhimu kwa Serikali kutenga fedha au kuongeza fedha ya nyongeza katika mwaka huu wa fedha ili kukamilisha mchakato na Tanzania kupata Katiba mpya.

Pili, kwa kuzingatia majukumu muhimu ya Wizara hii, Kamati inaishauri Serikali kuwezesha Wizara kuitengea bajeti ya kutosha ili kuhakikisha kuwa fedha hiyo inatolewa kwa wakati. Tatu, kwa kuwa Taasisi nyingi za Wizara hii Ofisi zake zipo katika majengo ya kupanga, hali inayosababisha Wizara kutumia fedha nyingi, hiyo, Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga majengo yake ili kuepuka gharama za upangaji.

Nne, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kujikita katika mfumo wa kielektroniki ili kubadilisha ufanisi katika Sekta ya Sheria na Miundombinu ya utoaji haki.

Mwisho, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake kuwa wabunifu katika kubuni miradi mbalimbali katika Sekta za Sheria itakayoongeza ufanisi katika sekta hii na ambayo itaongeza maduhuli ya Wizara kuliko kuendelea kutegemea wahisani katika bajeti zao za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, napenda kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati hii, lakini pia hatuna budi kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu na Wenyeviti wote kwa kuliongoza Bunge letu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa.

Napenda nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Harisson Mwakyembe; Katibu Mkuu, Profesa Sifuni Arnest Mchome; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Amon Mpanju; na watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa waliutoa wakati Kamati hii ilipojadili Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya, sina haja ya kuwataja, naomba waingie wote kwenye *Hansard*. Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kasilillah, Katibu wa Bunge, pamoja na Makatibu wote katika Kamati hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa nia njema na kwa maslahi ya Taifa letu. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Najma Giga. Tunakushukuru sana kwa taarifa hiyo ya Kamati ambayo imeunga mkono kabisa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu,

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kifungu 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria ina mafungu 6 ya bajeti ambayo ni;

- I. Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria
- II. Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
- III. Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria
- IV. Fungu 35** - Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka
- V. Fungu 16** - Mwanasheria Mkuu wa Serikali
- VI. Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama

**Mhehimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa matano yafuatayo:

- I. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.
- II. Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.
- III. Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.
- IV. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.
- V. Maoni na Ushauri wa Kamati

## **2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tarehe 30 Machi, 2016 na kupokea Taarifa kuhusu Mradi unaohusu Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vile vile Kamati ilipata Taarifa kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:

### **i) Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41)**

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Katiba na Sheria ilitengewa Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Hamsini na Tisa, Laki Saba Kumi na Tisa Efu (2,959,719,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Mbili (2,000,000,000) ni fedha za ndani na Shilingi Milioni Mia Tisa Hamsini na Tisa, Laki Saba Kumi na Tisa Efu (959,719,000) ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2016 Wizara ilipokea na kutumia Shilingi Milioni Thelathini na Tatu, Laki Sita na Thelathini Efu (33,630,000) ambayo ni fedha za nje kupia Mradi wa **UNICEF Multi-sectoral Support**. Ofisi haikupokea fedha yoyote ya ndani kama ilivyoidhinishwa na Bunge ambazo zingesainia katika utekelezaji wa mradi huu kikamilifu.

### **ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ( Fungu 16)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishwa Shilingi Milioni Mia Sita Arobaini na Nne, Laki Saba na Arobaini Efu (644,740,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha

hizo Shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini na Nne, Laki Saba na Arobaini Elfu (344,740,000) ni Fedha za Ndani na Shilingi Milioni Mia Tatu (300,000,000) ni Fedha za Nje kutoka UNDP

**Mheshimiwa Spika**, fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Maendeleo zilikuwa ni kwa ajili ya kujengea uwezo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kusimamia masuala ya Mikataba mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mikataba ya Sekta ya Nishati na Madini kupitia **Mradi wa Capacity Development in The Energy Sector and Extractive Industries** (CADESE)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu haukuweza kutekelezwa ipasavyo kwa sababu ya kukosekana kwa Fedha za nje kutoka **United Nations Development Programme** ambayo iliahidi kutoa Shilingi Milioni Mia Tatu (300,000,000) na hazikutolewa. Fedha liyotolewa ni Shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini na Nne Elfu, Laki Saba Arobaini Elfu (344,740,000) tu kwa Mradi huu ambazo ni Fedha za ndani. Vile vile Ofisi hii imeshindwa kutekeleza Mradi wa ujenzi na Ukarabati wa Majengo yake kwa sababu ya kukosekana fedha.

### iii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ( Fungu 55)

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha 2015/2016 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitengewa Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Sita, Laki Moja na Ishirini na Mbili Elfu (246,122,000) kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa **National Human Rights Action Plan** (NHRAP). Mradi huu unahusu Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Haki za Binadamu Nchini.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2016 kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya Mradi huu ni Shilingi Milioni Mia Moja Themanini na Nane, Laki Mbili na Elfu Kumi na Mbili (188,212,000) sawa na asilimia 76 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Hivyo Mradi huu haukutekelezeka kikamilifu kutokana na kutotolewa fedha zote zinazokidhi mahitaji ya utekelezaji wa mradi.

## 2.1 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na kasi ya utoaji wa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwani karibu miradi yote imepokea sehemu tu ya fedha iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kamati vilevile inasikitishwa na hatua ya Serikali kutotoa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Miradi mingi ya maendeleo imekua inategemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje. Mfano, katika Fungu 16 Ofisi ilipokea fedha za nje tu kupitia UNICEF Multi-Sectoral Support program na haikupokea fedha yoyote kutoka ndani.



**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kufanya Maendeleo, kuna umuhimu wa kila Taasisi ya Serikali kubuni vyanzo vya mapato vitakavyosadia kuongeza fedha za ndani ili kuepuka utegemezi wa fedha za nje.

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ilikutana Jijini Dar es Salaam Tarehe 8 na 9 Aprili, 2016 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mwezi Mei 2015 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika Mwaka wa Fedha Ujao.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Katiba na Sheria kwa ujumla ilidhiinishwa Shilingi Bilioni Mia Moja Tisini na Moja, Milioni Mia Nne Hamsini, Laki Tisa na Moja (191,450,900,001) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Mwezi Machi 2016, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Tisini na Saba, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tano, Laki Tano na Sita Elfu, Mia Mbili Thelathini na Tisa (97,255,506,239) sawa na asilimia 49 ya fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, fedha inayoombwa na Wizara ya Sheria na Katiba kwa Mafungu yote katika mwaka huu wa fedha ni Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Saba Themanini na Tano, Mia Nne Kumi na Sita Elfu (35,785,416,000/=). Fedha hii ni mara tano pungufu ya fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, Upungufu huu unatokana na kiasi kikubwa cha fedha iliyokua inatengwa chini ya Fungu 41 kuhamishiwa katika Fungu 40 (Mahakama) kutokana na Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015. Pia Upungufu huu unatokana na kupungua kwa fedha ya matumizi mengineyo kwa wizara na sekta zote ambao ni mwenendo wa bajeti katika mwaka huu wa fedha.

**Jedwali 01: Mlinganisho wa Fedha Iliyotengwa na Kupokelewa Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Chini ya Fungu 41**

<b>Fungu</b>	<b>Fedha Iliyoidhinishwa Sh.</b>	<b>Fedha Iliyopatikana Sh.</b>	<b>Tofauti Sh.</b>	<b>Asilimia Sh.</b>
41	Sh.191,450,900,001	Sh.97,255,506,239	Sh.94,195,393,762	49

Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara mpaka sasa imepokea Asilimia 49 ya fedha iliyoidhinishwa. Kukosekana kwa kiasi hicho kikubwa cha fedha katika Wizara hii kutakuwa kumeathiri utekelezaji wa majukumu muhimu na ya msingi. Kamati inaona kuwa kuna umuhimu wa kuisisitiza Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati ili majukumu ya Wizara hii yaweze kutekelezeka kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi kufikia Machi 2016 katika mafungu sita yanayosimamiwa na Wizara yaani Fungu 41, 16, 35, 59,55 na 12 umeainishwa kwenye majedwali hapa chini kwa kila Fungu

**1) Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41)(Jedwali 02)**

	<b>Fedha Zilizoidhinishwa</b>	<b>Fedha Zilizopokelewa</b>	<b>Asilimia</b>
Kawaida	Sh. 4,182,321,000	Sh. 1,159,151,385	28
Mishahara	Sh. 5,268,767,000	Sh. 3,051,795,520	58
Maendeleo	Sh. 2,959,719,000	Sh. 118,276,750	3.9
Jumla	Sh.12,410,807,000	Sh.4,329,223,655	35

**2) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16)(Jedwali 03)**

	<b>Fedha Zilizoidhinishwa</b>	<b>Fedha Zilizopokelewa</b>	<b>Asilimia</b>
<b>Kawaida</b>	Sh.4,784,217,000	Sh.2,045,921,885	Sh.43
<b>Mishahara</b>	Sh.3,759,244,500	Sh.2,506,163,000	Sh.66
<b>Maendeleo</b>	Sh.300,000,000	Sh.344,740,000	Sh.115
<b>Jumla</b>	Sh.8,843,461,500	Sh.4,896,824,885	Sh. 55

**3) Divisheni ya Mashitaka (Fungu 35)(Jedwali 04)**

	<b>Fedha Zilizoidhinishwa</b>	<b>Fedha Zilizopokelewa</b>	<b>Asilimia</b>
<b>Kawaida</b>	Sh. 7,160,742,000	Sh. 2,584,486,151	36
<b>Mishahara</b>	Sh.922,251,800	Sh.6,148,345,545	666.7
<b>Maendeleo</b>	Sh. 342,884,000	Sh. 342,884,000	100
<b>Jumla</b>	8,425,877,800	Sh. 9,075,715,696	107

**4) Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) (Jedwali 05)**

	<b>Fedha Zilizoidhinishwa</b>	<b>Fedha Zilizopokelewa</b>	<b>Asilimia</b>
<b>Kawaida</b>	Sh. 2,017,276,000	Sh. 322,050,463	16
<b>Mishahara</b>	Sh. 668,916,000	Sh. 67,134,000	10
<b>Maendeleo</b>	0	0	0
<b>Jumla</b>	Sh. 2,686,192,000	Sh. 389,184,463	14.58

**5) Tume ya Kurekebisha Sheria (Fungu 59) (Jedwali 06)**

	<b>Fedha Zilizoidhinishwa</b>	<b>Fedha Zilizopokelewa</b>	<b>Asilimia</b>
<b>Kawaida</b>	Sh. 1,755,874,961	Sh. 430,474,863	25
<b>Mishahara</b>	Sh. 1,229,817,000	Sh. 2,985,691,961	242
<b>Maendeleo</b>	0	0	0
<b>Jumla</b>	Sh. 2,985,691,961	Sh. 828,362,938	28

**6) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) (Jedwali 07)**

	<b>Fedha Zilizoidhinishwa</b>	<b>Fedha Zilizopokelewa</b>	<b>Asilimia</b>
<b>Kawaida</b>	Sh. 2,226,368,000	Sh. 740,962,701	33
<b>Mishahara</b>	Sh. 2,779,581,000	Sh. 1,536,418,700	55
<b>Maendeleo</b>	Sh. 572,389,000	Sh. 294,506,000	51
<b>Jumla</b>	Sh. 5,578,338,000	Sh. 2,571,887,401	46.1

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo huu wa upokeaji fedha kwa ujumla unaonyesha kwamba fedha inayopokelewa ni ndogo sana ukilinganisha na kiasi kinachoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Hii inaonyesha kwamba Taasisi nyingi zinashindwa kumudu majukumu yao kwa wakati na ufanisi kutokana na fedha kuchelewa kutoka Hazina.

### 3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA KUHUSU UKUSANYAJI MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Katiba na Sheria kwa pamoja na Taasisi zake ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Ishirini na Tatu, Laki Tisa Thelathini na Tatu, Mia Saba Hamsini (17,023,933,750) kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Februari, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Moja Kumi na Sita, Laki Nane Arobaini na Tisa Elfu, Mia Nane Kumi na Moja (11,116,849,811) ikiwa ni sawa na asilimia 65 ya makusanyo yaliyotarajiwa kama ilivyochanganuliwa hapa chini:

#### Jedwali 08: Mlinganisho wa Makadirio, Makusanyo na Asilimia Kwa Mafungu Yaliyo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Fungu	Makadirio	Makusanyo	Asilimia
12	Sh. 0	0	0
16	Sh. 1,002,000	Sh. 3,255,000	325
35	Sh. 13,002,000	Sh. 12,000,000	92
40	Sh. 5,203,298,719	Sh. 5,789,939,272	111
41	Sh. 11,801,400,000	Sh. 5,890,822,355	50
55	Sh. 5,131,000	0	0
59	Sh. 100,000	0	0
Jumla	Sh. 17,023,933,719	Sh. 11,696,016,627	65

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo haya ni kutokana na ada za Usajili wa Matukio, Ada za wanafunzi, uuzaji wa vitabu vya zabuni na huduma nyingine mbalimbali zinzotolewa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 41 imeongoza katika ukusanyaji wa Maduhuli kwa kukusanya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nane Tisini, Laki Nane Ishirini na Mbili Elfu (5,890,822,355) ikifuatiwa na Idara ya Mahakama iliyokusanya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili na Kumi, Laki Saba Sabini na Saba na Mbili, Mia Nne Hamsini na Saba (5,210,772,457). Iliyofuatia katika kukusanya maduhuli ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fungu 16 iliyokusanya Shilingi Milioni Tatu, Laki Mbili Ishirini na Tano Elfu (3,255,000).

**Mheshimiwa Spika**, Mafungu mengine yalikuwa na matarajio ya kukusanya maduhuli lakini matarajio hayakuwa kama yalivyopangwa. Hii ni changamoto ambayo Wizara na Taasisi zote zenye vyanzo vya mapato zinabidi kuiangalia kwa umakini kwani matarajio sio mapato.

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha uliopita haukuendana na matarajio ya Wizara. Matarajio ya Wizara yalikuwa makubwa lakini kilichopatikana ni kidogo. Hivyo kuna umuhimu wa kuweka vyanzo vingine vya ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa kwa zile Taasisi zilizokosa mapato kabisa.

### 3.1.1 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uwasilishaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo ishirini na saba (27) kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa mapendekezo yote yametekelezwa isipokuwa moja ambalo linahusu deni la RITA. Katika Mwaka 2015/2016 Kamati iliishauri Serikali kulipa fedha inazodaiwa na RITA ili RITA iweze kutekeleza majukumu yake katika Mkataba wa Ubia wa jengo la RITA TOWER ili kuepukana na ongezeko la riba. Kamati imeelezwa kuwa kutokana na changamoto za kibajeti Serikali imeshindwa kulipa deni hilo na inafanya jitihada ili fedha hizo zipatikane.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazidi kuisisitiza Serikali kulipa deni hilo mapema ili kupunguza ongezeko la riba kutokana na kutolipwa kwa deni hili.

## 4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria imejiwekea malengo kumi na moja (11) ya utekelezaji ili kuongeza ufanisi na ubora katika kutoa huduma za kisheria na masuala ya Katiba. Malengo hayo ni:-

- i) Kuimarisha usimamizi na uratibu wa mfumo wa Sheria;
- ii) Kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa Divisheni ya Mahakama ya Rushwa na Ufisadi ili kuharakisha usikilizaji wa Mashauri;
- iii) Kuratibu uundaji na uendeshaji wa Kamati ya kusimamia utekelezaji wa masharti yatokanayo na masharti ya mpito kwenye katiba inayopendekezwa;
- iv) Kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundobinu ya huduma za mahakama na Taasisi zake;

v) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma mbalimbali na kutunza kumbukumbu muhimu;

vi) Kuimarisha shughuli za utafiti wa sheria na kufanya marekebisha ya sheria zilizopitwa na wakati;

vii) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuendeleza watumishi kitaaluma;

viii) Kuimarisha huduma za Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi na kupanua wigo wa huduma kwa walengwa;

ix) Kuweka wigo mpana wa sheria na upatikanaji wa msaada wa kisheria (Legal Aid Services) kwa watu wasio na uwezo;

x) Kuimarisha mifumo ya utunzaji nyaraka , kumbukumbu na takwimu; na

xi) Kuimarisha shughuli za usajili na utunzaji wa kumbukumbu (Civil Registration and Vital Statistics).

**Mheshimiwa Spika**, malengo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii yameongezeka ukilinganisha na malengo waliyojiwekea katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na malengo ya Wizara kwa ujumla kwani yanalenga katika kuboresha utekelezaji wa majukumu na kuleta ufanisi zaidi katika suala zima la utoaji haki nchini.

#### **4.1 MAKADIRIO YA MAPATO YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane, Tisini na Sita, na Ishirini Efu, **(11,896,020,000/=)** ikiwa na Maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

Fungu	Matarajio ya Maduhuli (Sh.)
12	0
16	1,002,000
35	13,002,000
41	11,882,012,000
55	0
59	4,000
<b>Jumla</b>	<b>11,896,020,000/=</b>

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Makadirio ya Mapato hayaendani na hali halisi ya makusanyo. Hivyo Kamati inashauri kuwa ni vizuri Serikali ikaweka makadirio madogo yenye uhakika kuliko kuweka matarajio makubwa ambayo mwisho wa siku hayakusanywi.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu 55 (Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora) na Fungu 12 (Tume ya Utumishi wa Mahakama) hayana matarajio yoyote ya kukusanya maduhuli kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo vya mapato.

#### **4.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara imeomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Saba Themanini na Tano, Mia Nne Kumi na Sita Elfu (35,785,416,000) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo:

i)	Mishahara ya Watumishi	Sh.	22,391,694,000
ii)	Matumizi Mengineyo	Sh.	10,619,234,000
iii)	Miradi ya Maendeleo	Sh.	2,774,488,000
	<b>Jumla</b>	<b>Sh.</b>	<b>35,785,416,000</b>

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazombwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni sawa na asilimia 0.1 ya Bajeti Kuu ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambayo ni Trilioni 29.

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria katika mafungu sita (6) unaonyesha jumla ya fedha zitakazotumika katika Mwaka wa Fedha ujao ikijumuisha Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo pamoja na Matumizi ya Fedha za Maendeleo za Nje na Ndani kwa ujumla katika kila Fungu kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.



**JEDWALI 09: MCHANGANUO WA MATUMIZI KWA KILA FUNGU**

<b>Fungu</b>	<b>Jumla Ya Matumizi</b>
12	Sh. 1,134,955,000
16	Sh. 6,997,324,000
35	Sh. 13,299,639,000
41	Sh. 9,137,717,000
55	Sh. 3,557,589,000
59	Sh. 1,658,192,000
<b>Jumla</b>	<b>Sh. 35,785,416,000</b>

**Mheshimiwa Spika**, Divisheni ya Mashitaka (Fungu 35) lina makadirio ya matumizi ya juu zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine. Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Fungu hili ni sawa na asilimia 37% ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) lina Makadirio ya Matumizi madogo zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine ikiwa ni sawa na asilimia 3.2% ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) inaombewa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Mia Tano Themanini na Tisa Efu (3,557,589,000). Wakati Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inawasilisha Taarifa kwenye Kamati Tarehe 8 Aprili, 2016 ilibainika kuwa fedha zilizotengwa zinakidhi Mishahara, Malipo ya Pango la Ofisi na malipo mengine madogo madogo. Hivyo kwa Bajeti inayoombwa haiwezeshi Tume kutekeleza majukumu yake ya Msingi yaliyowekwa Kikatiba, kama vile kuhamasisha haki za Binadamu nchini, kufanya uchunguzi juu ya uvunjwaji wa Haki za Binadamu na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekutana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mara tatu kati ya Februari na Aprili 2016 na kujadili kwa kina uwezo wa kifedha wa Tume katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Baada ya kuwa imejiridhisha vya kutosha kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika mwaka huu wa fedha kuwa ni ndogo sana ukilinganisha mahitaji halisi ya Tume, Kamati iliamua kupeleka Ombi maalumu katika Kamati ya Bajeti ya Bunge ili bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu katika mwaka huu wa fedha iongezwe kwa Sh. Bilioni Mbili zaidi kutoka Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Saba, Mia Tano Themanini na Tisa Efu.(3,557,589,000).

**Mheshimiwa Spika**, katika kuisistiza umuhimu wa Tume hii kuongezewa fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, tarehe 4 Mei, 2016 Mwenyekiti wa Kamati hii ya Katiba na Sheria aliwasilisha maombi mbele ya Kamati ya Bajeti ya

nyongeza ya Shilingi Bilioni Mbili (2,000,000,000,000) katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017. Suala hili lilijadiliwa kwa kirefu kwenye Kamati ya Bajeti na Waziri wa Katiba na Sheria, watendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria na Kamishna wa Fedha walihudhuria. Baada ya majadiliano ya kina Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliahidi kulijadili kwa undani suala hili na kuahidi kutoa maamuzi baadae.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala katika mwaka 2016/2017 inaombewa kiasi cha Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Mia Tano Themanini na Tisa Efu ( **3,557,589,000**). Kati ya fedha hizo shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tatu Themanini na Tatu, Mia Moja Kumi na Sita Efu (**2,383,116,000**) ni kwa ajili ya mishahara (PE) na shilingi **994,514,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Kati ya fedha hizi za matumizi mengineyo shilingi Milioni Miatatu Ishirini (**320,000,000.00**) zimetengwa na kuzuiwa kwa ajili ya kulipa pango, hivyo Tume inabakiwa na Shilingi Milioni Mia Sita Sabani na Nne, Mia Tano Kumi na Nne Efu (674,514,000) za utekelezaji wa majukumu yake. Kiasi hiki hakitaweza kukidhi hata mahitaji ya uendeshaji wa ofisi. Ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa hapo chini, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Kamati inashauri Serikali kuiongezea Tume kiasi cha Shilingi Bilioni Mbili (**2,000,000,000.00**) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa bajeti hii ndogo iliyoombwa Watumishi wa Tume watapokea mishahara tu bila kufanya kazi yoyote kwa mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika**, maeneo ya kipaumbele kwa Tume yenye kugusa moja kwa moja haki za binadamu ambayo hayakutengewa fedha yoyote ni kama ifuatavyo;

- i) Kufuatilia haki za makundi maalum katika jamii kama watoto, watu wenye ulemavu, wazee na kutoa elimu kwa Umma;
- ii) Kufuatilia na Kushughulikia Malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu;
- iii) Kuimarisha Mahusiano na Wadau wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
- iv) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi;
- v) Nyongeza ya gharama za utendaji na kuendesha ofisi;

**Mheshimiwa Spika**, maeneo ambayo hayajatengewa fedha hapo juu ni kati ya majukumu ya msingi ya Tume ambayo yalipaswa kupewa kipaumbele. Hivyo, kwa msingi huu, Kamati inaona kuwa fedha inayoombwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni ndogo na haitaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi kwa manufaa ya Taifa.

### 5.1 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55)

- Serikali itoe fedha za kutosha kwa Tume ili iweze kutimiza majukumu yake ya Kikatiba kwa ufanisi
- Serikali iongeze Ofisi za Tume katika Mikoa mingi zaidi Tanzania Bara na Zanzibar na hasa Pemba ambapo Tume bado haijaweza kuanza kufanya kazi kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa upande wa Tanzania Bara Tume iongeze ofisi zaidi katika Kanda ya Ziwa ambapo kumekua na matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za Binadamu hasa maeneo ya migodini.
- Serikali ihakikishe kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya Tume inatolewa kwa wakati.
- Kamati inaishauri Serikali kufuata sheria zilizowekwa katika kutekeleza majukumu yake kwa sababu kuna sheria ambazo inaonekana utekelezaji wake ni mgumu kwa mfano adhabu ya kifo Hivyo Kamati inashauri kama kuna sheria ambazo utekelezaji wake ni mgumu zifanyiwe marekebisho. Hii itaendana na Itifaki ya Pili ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966 unaozitaka nchi wanachama wa Mkataba huu kuondoa adhabu ya kifo. Ingawa Tanzania bado haijaridhia Itifaki hii ya Mwaka 1989, Kamati inaishauri Serikali kuridhia Itifaki hii na kutunga sheria ambayo itaondoa adhabu ya Kifo. Hatua hii ni muhimu kwa sababu Tanzania tayari imeridhia Mkataba huu wa mwaka 1966 na Kamati inashauri Serikali kuridhia Itifaki hii ya mwaka 1989 iliyo chini ya Mkataba huu wa mwaka 1966.

### 5.2 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16)

- Serikali ianzishe mapema iwezekanavyo mchakato wa kujenga Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na Wawekezaji wengine kama NSSF
- Serikali itenge bajeti ya kutosha itakayowezesha kuwajengea uwezo na ujuzi watumishi wa ofisi hii na kuwapatia mafunzo ya kisasa katika Nyanja mbalimbali ili waendane na mabadiliko ya teknolojia kulingana na Taaluma zao.

- Kwa kuwa sasa nchi inaingia katika uchumi wa gesi Kamati inaishauri Serikali kujenga uwezo wa Wanasheria wa Serikali ili wabobee katika Sheria za Mafuta na Gesi na hasa eneo la mikataba ya sekta hii. Hii itaongeza uwezo wa serikali katika kujadili na kusimamia maslahi ya taifa na kupunguza uwezekano wa kuhujumiwa na makampuni makubwa yaliyowekeza katika sekta ya gesi na mafuta.

### **5.3 Tume ya Kurekebisha Sheria (Fungu 59)**

- kutokana na ufinyu wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti kwa Tume ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

- Serikali lendelee kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Tume kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa ili kuboresha sheria za nchi. Aidha, Tume iendelee kufanya Tafiti kuhusu sheria mbalimbali ambazo kutokana na mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi zinahitaji kufanyiwa marekebisha ili ziweze kuendana na wakati wa sasa.

- Kamati inashauri Serikali kufanyia kazi kwa haraka taarifa za utafiti za Tume hasa kuhusu Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 kuhusu umri wa mtoto ili kulinda haki zote za mtoto (**Best Interests of the Child**) na hasa haki ya kila mtoto kupata elimu, kuwa na afya njema na kutokuolewa mapema. Lakini pia, kamati inaishauri serikali kupitia na kufanyia kazi taarifa na sheria zote zilizowasilishwa na Tume zinazohitaji maboresho ili kuendana na wakati.

### **5.4 Divisheni ya Mashitaka (Fungu 35)**

- Serikali kuendelea kuajiri Mawakili wa Serikali wa kutosha ili kukabiliana na wingi wa kesi kutokana na ongezeko la uhalifu. Aidha, maslahi ya watumishi hao yaboreshwe ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Vilevile, kamati inasisitiza juu ya ujenzi wa nyumba za Mawakili wa Serikali ili waweze kuishi kwenye makazi salama ukizingatia kuwa wanashughulikia kesi za mbalimbali ambazo zinahusisha matukio makubwa ya uhalifu kama mauaji na kadhalika.

### **5.5 Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12)**

- Serikali ione umuhimu wa kuiongezea Tume hii fedha kwa kulingana na majukumu yake.

- Kutokana na kutokukamilika kwa matengenezo ya vyumba vya ofisi katika jengo la RITA ambao unasababisha Mwenyekiti wa Tume, Wajumbe na

Makamishna kukosa Ofisi mahsusi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao, Kamati inaishuri Serikali kutenga fedha za kutosha ili Ofisi zilizopo kwenye Jengo la RITA zikamilike kwa haraka.

- Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili Tume hii iweze kushughulikia kikamilifau malalamiko ya ukiukwaji wa maadili na nidhamu kwa Watumishi wa Mahakama.

- Kamati inaishauri Serikali kufuata Sheria za NACTE za uanzishwaji wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), ambazo zinataka Mkuu wa Chuo na Msaidizi wake kuwa na Shahada ya Uzamivu. (Ph. D )

- Kamati inaishauri Serikali kukiboresha Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kiweze kutoa wahitimu mahiri katika fani ya Sheria katika kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada. Ili kufikia lengo hili Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mkuu wa chuo na wahadhiri wengine wana viwango vya elimu vinavyokubalika katika kufundisha vyuo vikuu Tanzania hasa kiwango cha Uzamivu na Uzamili.

- Ili kusimamia Haki katika ubora unaotakiwa Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba idadi ya kesi walizopangiwa mahakimu na majaji kwa mwaka hakuathiri ubora wa hukumu wanazotoa na usimamizi wa haki mahakamani. Kamati inatambua kwamba Dhana ya **“Justice Delayed is Justice Denied”** ni muhimu katika utoaji haki lakini ni muhimu pia kwa watendaji wa Mahakama kuzingatia dhana ya **“Justice Hurried is Justice Buried”** katika kusimamia Haki. Hivyo kamati inashauri mahakimu, majaji na watendaji wa mahakama kuhakikisha kwamba haki inasimamiwa katika ubora wake na siyo katika wingi wa kesi zinazoamuliwa na mahakama.

- Kamati inaishauri Serikali Kuboresha Miundo Mbinu ya Mahakama Hasa mahakama za Mwanzo na Wilaya ili kuboresha mazingira na ufanisi wa utoaji Haki nchini.

- Kamati inaishauri serikali kulipia gharama za nyumba na posho ya kutokufanya shughuli binafsi za Sheria (Rent Assistance and Non-practising Allowance) kwa Mahakimu 1224 walioajiriwa na Mahakama kama ilivyo kwa wanasheria wa Serikali.

- Kamati inaishauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watumishi wa Mahakama wasiozingatia Maadili ya Kazi na kuhakikisha kwamba watumishi hao wanawajibishwa kwa mujibu wa Sheria.

## 5.6 Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41)

- Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhuisha mchakato wa kupata Katiba mpya kutokana na mapendekezo yaliyotolewa katika mchakato wa kupata katiba uliosimama mwaka 2014 Oktoba. Kamati inasisitiza kwamba ni muhimu kwa Serikali kutenga fedha au kuongeza fedha ya nyongeza katika mwaka huu wa fedha ili kumalizia mchakato wa Tanzania Kupata Katiba mpya.
- Kwa kuzingatia majukumu muhimu ya Wizara hii, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Wizara kwa kuitengea bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatolewa kwa wakati.
- Kwa kuwa Taasisi nyingi za Wizara hii Ofisi zake ziko katika majengo ya kupanga hali inayosababisha Wizara kutumia fedha nyingi kwa ajili hiyo, Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga majengo yake ili kuepuka gharama za upangaji.
- Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na Sheria kujikita katika mifumo ya kieletroniki ili kuboresha ufanisi katika sekta ya Sheria na miundo mbinu ya utoaji haki.
- Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake kuwa wabunifu katika kubuni miradi mbalimbali katika sekta ya Sheria itakayoongeza ufanisi katika sekta hii na ambayo itaongeza maduhuli ya wizara kuliko kuendelea kutegemea wahisani katika bajeti zao za maendeleo

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, hatuna budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa. Napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Dr.Harrison Mwakyembe, Mb, Katibu Mkuu Prof.Sifuni Ernest Mchome,Naibu Katibu Mkuu Ndugu Amon Mpanju na Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Matumizi Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa

Taarifa hii kwa wakati. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

- (i) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb, Mwenyekiti
- (ii) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb, Makamu Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb, Mjumbe
- (iv) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb, Mjumbe
- (v) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb, Mjumbe
- (vi) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb, Mjumbe
- (vii) Mhe. Makame Mashaka Fom, Mb, Mjumbe
- (viii) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb, Mjumbe
- (ix) Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb, Mjumbe
- (x) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb, Mjumbe
- (xi) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb, Mjumbe
- (xii) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb, Mjumbe
- (xiii) Mhe. Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Mb, Mjumbe
- (xiv) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, Mjumbe
- (xv) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb, Mjumbe
- (xvi) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb, Mjumbe
- (xvii) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, Mjumbe
- (xviii) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb, Mjumbe
- (xix) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb, Mjumbe
- (xx) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb, Mjumbe
- (xxi) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb, Mjumbe
- (xxii) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb, Mjumbe
- (xxiii) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb, Mjumbe
- (xxiv) Mhe. Dkt Mathayo David Mathayo, Mb, Mjumbe

Aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt Thomas D. Kashillah, Katibu wa Bunge, kwa kusaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza Majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Angelina Sanga, Stella Bwimbo, Dunford Mpelumbe na Gaitana Chima kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Sheria na Katiba.



Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

**MWENYEKITI,  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

**05 Mei, 2016**

**SPIKA:** Sasa naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Lissu! (Makofi)

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA TUNDU A. M. LISSU (MB) KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA 2016/2017  
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanyakazi ambayo ninatakiwa kuifanya kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu na ambayo umeniitia, naomba kwa ridhaa yako niseme maneno machache juu ya jambo binafsi linalonihusu mimi na familia yangu.

Tarehe 7 Aprili, 2016 aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Singida katika Bunge la Kumi, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, alifariki dunia katika Hospitali ya Agha Khan, Dar es Salaam. Marehemu alikuwa dada yangu na mdogo wangu wa kuzaliwa. Kufuatia kifo chake, licha ya kuwa hakuwa Mbunge tena, Uongozi wa Bunge lako Tukufu ulichukua jukumu la kuhakikisha kwamba, Marehemu Christina Mughwai anazikwa kwa heshima zote zinazostahili Mbunge. Waheshimiwa Wabunge kwa namna mbalimbali walishiriki katika kuhakikisha mpendwa wetu anapata mazishi ya heshima kubwa. Baadhi yenu hata mlifunga safari ya kumsindikiza Marehemu hadi nyumbani kwetu Kijiji cha Mahambe, Wilaya ya Ikungi ambapo mazishi yalifanyika tarehe 13 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Spika, siyo Bunge na Waheshimiwa Wabunge tu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano mwenyewe, Dkt. John Pombe Magufuli ilishiriki moja kwa moja katika mazishi hayo. Licha ya shughuli zake nyingi, Rais mwenyewe alikuja kuupokea mwili wa Marehemu na kutoa heshima zake katika Ukumbi wa kihistoria wa Karimjee na baadaye kwenye mazishi nyumbani kwetu Mahambe, Rais alimtuma Waziri wake, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, kuja kuiwakilisha Serikali katika mazishi hayo.

Tulipata kila aina ya msaada tuliohitaji kutoka kwa Bunge, Serikali na Waheshimiwa Wabunge. Hatukuwa wapweke. Hamkutuacha peke yetu katika majonzi yetu. Mlilia na sisi na mlitufuta machozi. Mlitufaraji sana katika kipindi chote cha kilio chetu. Mliufanya msiba wetu kuwa msiba wenu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu zote hizi, nimetumwa na waliomzaa na kumlea Marehemu Christina Mughwai, nimeagizwa na ndugu zake na marafiki zake na jirani zake, kutoa shukrani zao za dhati kabisa kwa Uongozi wa Bunge lako Tukufu, kwa Waheshimiwa Wabunge wote na kwa Rais na Mama John Pombe Magufuli na Serikali yake yote, kwa ajili ya wema na upendo na heshima mliyotupatia wakati wa mazishi ya mpendwa wetu Christina Lissu Mughwai. Mwenyezi Mungu awazidishie pale mlikopungukiwa na awabariki sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naomba nitimize wajibu wangu wa Kibunge kama Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu kuhusu hoja iliyoko mezani. Naomba niweke wazi mapema kabisa kwamba, nitakayoyasema hapa hayatawafurahisha wengi ndani na nje ya ukumbi huu wa Bunge lako Tukufu. (Makofi)

Hata hivyo, kama alivyosema Frederick Douglass, Babu wa harakati za kudai haki za watu weusi wa Marekani ya wakati wa utumwa wa Waafrika zaidi ya miaka 150 iliyopita; *“He is a lover of his country who rebukes its sins rather than justify them”* yaani ni mpenzi wa nchi yake yule anayekemea madhambi yake, badala ya kuyahalalisha.’ (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Aprili, 1980, Bunge hili lilitunga Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri, Sheria Na. 10 ya 1980. Sheria hiyo ilipata ridhaa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kuanza kutumika Mei Mosi ya mwaka 1980. Pamoja na mambo mengine, Kifungu cha 5(1) cha Sheria hiyo kilimpatia Rais mamlaka ya kuainisha idara, shughuli na mambo mengine ambayo kwayo kazi na majukumu yake amebaki nayo yeye mwenyewe au ameyakasimu kwa Mawaziri na tarehe ya kuanza kutekeleza majukumu hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tangu wakati huo, imekuwa ni sheria, na sehemu ya mila na desturi za Kikatiba ya nchi yetu, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuainisha kwa kupitia Tangazo lililochapishwa katika Gazeti la Serikali, Wizara, Idara, shughuli na mambo mengine ambayo Rais amejibakizia mwenyewe na yale ambayo amekasimu majukumu yake kwa Mawaziri. Utafiti wetu unaonyesha mambo yafuatayo katika miaka 36 na ya utekelezaji wa Sheria hii:

(i) Mwaka 1981, Rais Nyerere alitoa Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 1981 ambalo lilichapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 16 la tarehe 6 Februari, 1981.

(ii) Mwaka 1986, Rais Ali Hassan Mwinyi alitoa Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 1986 ambalo lilichapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 29 la 1986.

(iii) Mwaka 2000, Rais Benjamin William Mkapa alitoa Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2000 ambalo pia lilichapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 468 la 2000.

(iv) Mwaka 2006, Rais Jakaya Mrisho Kikwete naye alitoa Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2006 nalo pia lilichapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 2 la tarehe 13 Januari, 2006. Tangazo hilo lilifuta Matangazo mengine yote ya miaka ya nyuma.

(v) Mwaka 2010 Rais Kikwete alitoa Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2010 ambalo pia lilichapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 494(A) la tarehe 17 Disemba, 2010. Kama ilivyokuwa kwa Tangazo la mwaka 2006, Tangazo la 2010 lilifuta Matangazo mengine yote yaliyotolewa kabla ya tarehe 17 Disemba, 2010. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katikati ya Matangazo haya, Marais wa nchi yetu waliomtangulia Rais Magufuli, katika vipindi tofauti, wamekuwa wakitumia mamlaka yao chini ya kifungu cha 5 (1) cha Sheria kufanya marekebisho katika majukumu ya kiuwaziri ambayo yalikuwa chini ya Rais mwenyewe au aliyakasimisha kwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa mfano, mwaka 1982, Mwalimu Nyerere alitoa Tangazo la Serikali Na. 133 la 1982 kwa ajili hiyo. Mwaka 1984, Mwalimu Nyerere alifanya marekebisho mengine kupitia Tangazo la Serikali Na. 210 la 1984. Aidha, mwaka 1987, Rais Mwinyi alifanya marekebisho katika Tangazo la Serikali Na. 206 la tarehe 17 Aprili, 1987. Mwaka uliofuata, Rais Mwinyi alifanya marekebisho mengine kupitia Tangazo la Serikali Na. 42 la tarehe 26 Februari, 1988.

Mheshimiwa Spika, vile vile mwaka 2003, Rais Mkapa alitoa Tangazo la Serikali Na. 142 la tarehe 16 Mei, 2003. Mwaka huo huo Rais Mkapa alifanya marekebisho mengine kupitia Tangazo la Serikali Na. 413 la tarehe 19 Disemba, 2003. Aidha, mwaka uliofuata Rais Mkapa alifanya marekebisho mara mbili kupitia Tangazo la Serikali Na. 79 la tarehe 12 Machi, 2004 na Tangazo la Serikali Na. 523 la tarehe 3 Disemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, tumeelezea jambo hili kwa kirefu kiasi hiki kwa sababu lina umuhimu mkubwa Kikatiba na kisheria. Rais hatakiwi kugawa Wizara, Idara za Serikali na Majukumu ya Kiuwaziri kiholela. Haya ni majukumu ya umma na kwa sababu hiyo, ni lazima yafanywe kwa kufuata taratibu za kisheria zilizopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wao, Mawaziri wanatakiwa kutekeleza majukumu waliyokasimiwa na Rais kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri. Majukumu hayo lazima kwanza yatamkwe, yafafanuliwe na kuainishwa katika Tangazo lililochapishwa kwa ajili hiyo katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria hiyo, ushahidi pekee na wa mwisho juu ya suala kama Waziri ana mamlaka katika jambo fulani ni Tangazo la Serikali lililochapishwa chini ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inapenda Bunge hili lizifahamu, licha ya mabadiliko makubwa katika idadi, muundo na majukumu ya Wizara mbalimbali, hadi tunapoandika maoni haya Rais Magufuli hajatoa Tangazo lolote juu ya majukumu ya Kiuwaziri ambayo yeye mwenyewe amejibakishia au yale ambayo ameyakasimu kwa Mawaziri aliowateua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tofauti na alivyofanya Rais Kikwete na Serikali yake mwaka 2010, hakuna Mbunge hata mmoja ndani ya ukumbi huu ambaye amepatiwa nakala ya Tangazo lolote lililochapishwa kwa mujibu wa sheria. Licha ya madai ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu katika hotuba yake Bungeni ya tarehe 22 Aprili ya mwezi uliopita, Bunge lako Tukufu halijapatiwa nakala hata moja inayothibitisha kwamba Mawaziri walioteuliwa na Rais Magufuli, na ambao wamekuwa wakifanya mambo mbalimbali kwa kofia za Kiuwaziri, wanatekeleza majukumu waliyokasimishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hata Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, amekiri kwamba, Serikali inaendeshwa bila kuwa na alichokiita *instrument*. Kwa maneno yake mwenyewe, wakati akifanya majumuisho ya hoja za Wabunge kwa ofisi yake tarehe 27 Aprili, Waziri Mkuu amesema kwamba na nanukuu; "*Instrument* za Wizara zote zimeshakamilika na zimesainiwa tarehe 20/04/2016 sasa tunasubiri kutangaza wakati wowote Mheshimiwa Rais atakapoamua kutangaza zitakuwa zimetoka." Maana ya kauli hii ni kwamba hakuna *instrument* yoyote iliyotangazwa kama inavyotakiwa na Kifungu cha 5(1) cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, maana na athari ya kisheria ya kutokuwepo kwa Tangazo la ukasimishaji wa majukumu ya Kiuwaziri ni kubwa sana. Wengi wa Mawaziri wa Serikali hii waliteuliwa na Rais Magufuli tarehe 10 Disemba, 2015. Viporo vilivyobakia kwenye Baraza la Mawaziri vilikamilishwa tarehe 23 Disemba, 2015. Tangu wakati huo hadi sasa, Mawaziri wamefanya mambo mengi. Wametumbua majipu katika Wizara zao na taasisi zilizo chini yake kwa kufukuza, kuachisha, kusimamisha kazi au kuhamisha watendaji na watumishi mbalimbali wa Wizara au Taasisi hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wamefanya maamuzi juu ya matumizi ya fedha na rasilimali nyingine za umma, yote waliyoyafanya wameyafanya kinyume cha sheria. Hawakuwa na mamlaka ya kufanya waliyoyafanya kwa sababu Mawaziri hawa hawajakasimishwa mamlaka ya utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, watendaji na watumishi wote ambao wametumbuliwa majipu na Mawaziri hawa, wana haki na uwezo wa kwenda mahakamani na kuomba mahakama zetu zitengue utumbuaji wa majipu waliofanyiwa na Mawaziri wasiokuwa na mamlaka hayo kinyume cha sheria hii.

Ushauri wangu wa bure kwa watendaji na watumishi hao ni kwamba wakafungue mashauri Mahakama Kuu ya Tanzania kupinga kutumbuliwa kwao majipu na watu wanaojiita Mawaziri, lakini hawana hata *job description*! Kwenda kwao mahakamani siyo kutawasaidia kupata haki zao, bali pia kutakomesha vitendo vya kuendesha nchi kienyeji kienyeji na bila kufuata sheria, vinavyoelekea kushamiri chini ya utawala huu wa Rais John Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kila mtu anafahamu kwamba Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli siyo mwanasheria. Hata hivyo, pamoja na kutokuwa mwanasheria, Mheshimiwa Rais Magufuli naye anatakiwa kufuata sheria za nchi. Hayuko juu ya sheria. Kiapo chake kinamtaka kuilinda, kuitetea na kuihifadhi Katiba ya nchi yetu na Sheria zake. Aidha, mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika, kama inavyotamka Ibara ya 9(b) ya Katiba kwamba kuhakikisha sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Rais Magufuli siyo mwanasheria, ameteua Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye kwa maneno ya Ibara ya 59(3) ya Katiba ndiye mashauri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya sheria na atawajibika kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo yote ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo hiyo, Mheshimiwa Rais Magufuli ameteua Waziri wa Katiba na Sheria ili, kama inavyotakiwa na Ibara ya 54(3), awe Mshauri na Msaidizi wake Mkuu katika utekelezaji wa madaraka yake katika masuala ya Kikatiba na kisheria. Kwa bahati nzuri, Rais Magufuli amemteua Dkt. Harrison George Mwakyembe mmoja wa wasomi wa juu kabisa wa sheria katika nchi yetu kuwa Waziri wake wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rais Magufuli amemteua Dkt. Sifuni Ernest Mchome, samahani ni Profesa Sifuni Ernest Mchome msomi mwingine wa juu kabisa wa sheria kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria na Bwana Amon Anastazi Mpanju, mwanasheria mwingine tena kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo.

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inataka kupatiwa majibu sahihi ni kwa nini wanasheria wabobezi wote hawa wameshindwa kumshauri Mheshimiwa Rais Magufuli kutoa Tangazo la kukasimisha majukumu ya Kiuwaziri kwa Mawaziri mbalimbali aliowateua karibu miezi sita iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendeshwa kama mali binafsi ya Mheshimiwa Rais Magufuli, bila kufuata wala kuheshimu sheria, siyo tu kwa sababu Mheshimiwa Rais Magufuli ana viashiria vyote vya utawala wa kiimla, bali pia kwa sababu anaelekea kutokuwa na washauri katika masuala ya Katiba na Sheria za nchi. Kwa kuangalia mifano ya Matangazo mbalimbali ambayo yametolewa na watangulizi wa Rais Magufuli tangu Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri ilipotungwa mwaka 1980, hata mwanafunzi wa sheria wa mwaka wa kwanza angeweza kumtengenezea Rais Magufuli *draft* ya Tangazo la aina hiyo. Iweje watu wenye Shahada za Uzamivu na Uzamili katika sheria washindwe kufanya hivyo kwa karibu nusu mwaka tangu wateuliwe! Kama ni majipu ya kutumbuliwa na Rais Magufuli, basi wasomi hawa wa sheria ni majipu na wanastahili kutumbuliwa. Itatushangaza sana endapo Rais Magufuli atayafumbia macho majipu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie masuala ya Kikatiba yanayohusu Muungano wetu. Kwa wasiofahamu Katiba yetu na wanaoweza kuhoji kwa nini tunazungumzia masuala ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar katika hoja iliyoko mezani, Sura ya Nne yote ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano inahusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Aidha, Ibara ya 104 ya Katiba yetu imewekwa mahsusi kwa ajili ya Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa sababu hizi ni halali kabisa kuzungumzia yaliyotokea Zanzibar katika hoja iliyoko mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Maoni yake juu ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa



fedha 2014/2015, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu baada ya uchambuzi wa kina wa masuala ya fedha za Muungano ilisema yafuatayo kuhusu mahusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar tangu Muungano wetu uzaliwe tarehe 26 Aprili, 1964; "kwa vyovyote vile, takwimu hizi zinaonyesha kwamba, kwa sababu ya Muungano huu, uhusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar ni uhusiano wa kinyonyaji. Kwa sababu hiyo, huu ni uhusiano wa kikoloni. Ni uhusiano kati ya himaya ya Tanganyika na 'koloni' lake la Zanzibar. Himaya za kikoloni huwa zinadhibiti masuala yote ya ulinzi na usalama, mambo ya nje na uhusiano wa kimataifa, uraia, kodi, fedha, sarafu na benki kuu ya makoloni yao. Na himaya za kikoloni huwa zinatumia nguvu na udhibiti wao wa masuala haya kuyanyonya makoloni yao kiuchumi, kuyadidimiza kijamii na kuyatawala kisiasa." Hivi ndivyo ambavyo imekuwa kwa mahusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar tangu kuzaliwa kwa Muungano huu tarehe 26 Aprili, 1964. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964 hadi leo hii Tanganyika imeidhibiti Zanzibar kijeshi na kisiasa. Ukweli ni kwamba kama ambavyo Ndugu Harith Ghassany ameonyesha katika kitabu chake Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru! Zanzibar na Mapinduzi ya Afrabia Serikali ya Tanganyika ilishiriki kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya Mapinduzi ikiwemo kutoa silaha na mafunzo ya kijeshi katika mashamba ya mkonge ya *Sakura Estates*, Pangani - Tanga, kwa walioipindua Serikali ya Waziri Mkuu Mohamed Shamte na Sultan Jamshid bin Abdullah. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, siku tatu tu baada ya Mapinduzi hayo, Serikali ya Tanganyika kupitia Waziri wake wa Mambo ya Nje na Ulinzi Oscar Salatiel Kambona ilipeleka vikosi vya *Tanganyika Rifles* (Jeshi la Tanganyika) ili kuidhibiti Zanzibar Kijeshi. Mambo yote haya yamejulikana kwa miaka mingi na wasomi na wanazuoni wa Muungano huu na yamechapishwa katika vitabu na machapisho mengine rasmi ya kitaaluma ndani na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia udhibiti wake wa kijeshi, Tanganyika imedhibiti pia siasa za Zanzibar. Watawala wa Tanganyika ndiyo wanaoamua nani awe mtawala wa Zanzibar na wamefanya hivyo tangu mwaka 1964. Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi asingekuwa Rais wa Zanzibar baada ya kuuawa kwa Sheikh Abeid Amani Karume mwaka 1972 bila ushawishi wa Mwalimu Nyerere na Serikali ya Tanganyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wanazuoni wa Muungano huu, kama vile Profesa Issa G. Shivji wameonyesha, Jumbe asingeng'olewa madarakani mwaka 1984 bila shinikizo la Mwalimu Nyerere na watu wake hapa Dodoma. Aidha, Rais Mwinyi na Marais wengine wote wa Zanzibar waliomfuatia wametengenezewa Dodoma na siyo Zanzibar. (Makofi)



Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Aprili, 1968 Mwalimu Nyerere alisema yafuatayo wakati akihojiwa na gazeti la *The Observer* la London, Uingereza: *"If the mass of the people of Zanzibar should, without external manipulation, and for some reason of their own, decide that the Union was prejudicial to their existence, I could not bomb them into submission. The Union would have ceased to exist when the consent of its constituent members was withdrawn."* Ikiwa na maana kuwa endapo umma wa wananchi wa Zanzibar wataamua bila kurubuniwa kutoka nje na kwa sababu zao wenyewe kwamba Muungano unaathiri kuendelea kuwepo kwao sitaweza kuwalazimisha kwa kuwapiga mabomu. Muungano hautaendelea kuwepo pale ridhaa ya Washirika wake itakapoondolewa.

Mheshimiwa Spika, alichokisema Baba wa Taifa kwamba hata kifanya, Serikali ya Tanganyika imekifanya kwa zaidi ya miaka 20 sasa. Kabla ya Mfumo wa Vyama vingi kuruhusiwa mwaka 1992 udhibiti wa Tanganyika kwa siasa za Zanzibar ulifanyika kwa kutumia dhana ya vhama kushika hatamu.

Mheshimiwa Spika, katika zama za vyama vingi, Wananchi wa Zanzibar wamekuwa wapinzani wa ukoloni wa Tanganyika kwa nchi yao, kwa sababu hiyo, tangu uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, Serikali ya Tanganyika imetumia mabavu ya kijeshi ya wazi wazi ili kuwaweka madarakani vibaraka wake na kuendelea kuitawala Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kilele cha matumizi haya ya mabavu ya kijeshi ni Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana ambako vibaraka wa Tanganyika katika Zanzibar walikataliwa kabisa na wananchi wa Zanzibar katika uchaguzi wa Rais, Wawakilishi na Madiwani. Ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania tu ndilo ambalo limehakikisha kwamba vibaraka hawa waliokataliwa na wananchi wao wanaendelea kubakia madarakani.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yetu, katika mazingira haya, tatizo la msingi la Zanzibar siyo Mheshimiwa Jecha Salim Jecha, wala ZEC wala Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, hawa ni vibaraka tu wasiokuwa na nguvu wala uhalali wowote. Bila nguvu ya Tanganyika, vibaraka hawa hawawezi kudumu madarakani kwa muda mrefu. Tatizo la msingi ni ukoloni wa Tanganyika kwa Zanzibar ambao umevikwa joho la Muungano. Bila kulivua joho hili na kushona lingine badala yake, Zanzibar haitakuwa huru na itaendelea kutawaliwa na Tanganyika kisiasa, kiuchumi na kijeshi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwanaharakati mmoja wa haki za binadamu wa karne ya 19 aliwahi kuandika kwamba, *once a government is committed to the principle of silencing the opposition, it has only one way to go, and that is down the path of increasing the oppressive measures until it becomes a source of terror to all its citizens and create the country where everyone lives in fear yaani*

pale Serikali inapoamua kunyamazisha upinzani, inakuwa na njia moja tu ya kupita, nayo ni njia ya kuongezeka kwa vitendo vya kikandamizaji mpaka Serikali hiyo inakuwa chanzo cha hofu kwa wananchi wake wote na inatengeneza nchi ambapo kila mmoja anaishi kwa hofu.

Maneno haya yametimia katika nchi yetu, kwasababu ya kubaka demokrasia kwa kutumia nguvu za kijeshi Zanzibar ili kukipokonya Chama cha Wananchi (CUF) ushindi wake halali, Serikali hii ya hapa kazi tu imeingia katika njia ya kuongezeka kwa vitendo vya kikandamizaji kila mahali katika nchi yetu. Katika Jiji la Tanga ambako CCM ilikataliwa na wananchi, Serikali hii ilitumia ghilba na mabavu ya kila aina kuhakikisha CCM inanyakua Umeya wa Jiji hilo. Leo viongozi wa vyama vya UKAWA na Madiwani waliochaguliwa na wananchi wanakabiliwa na mashtaka ya jinai ya kutengeneza kwa sababu tu ya kukataa kwao kutawaliwa na watu ambao hawakupata ridhaa ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo ndiyo ilivyotokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ambako ilibidi Mbunge wa Jimbo la Kilombero na Mjumbe halali wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali atolewe kwa nguvu na polisi ili kuiwezesha CCM iliyokataliwa na wananchi kwenye kura kushinda nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero. Sasa Mbunge huyo naye anakabiliwa na mashtaka ya jinai mahakamani kwa kosa la kutetea demokrasia na utawala wa sheria na kukataa utawala wa mabavu na udikteta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri zake, licha ya nguvu kubwa na hila nyingi zilizotumiwa na Serikali hii, wananchi wa Dar es salaam na viongozi wao wa UKAWA walifanikiwa kutetea maamuzi ya wapiga kura na kuzuia jaribio la kubaka demokrasia kwa kuweka Meya wa chama kilichokataliwa na wananchi kwenye uchaguzi.

Hata hivyo, badala ya kuchukua hatua za kijinai dhidi ya Mkurugenzi wa Jiji, Mwanasheria wa Jiji na Katibu Tawala wa Mkoa waliodiriki hata kughushi hati ya amri ya Mahakama kwa lengo la kuzuia uchaguzi halali wa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, leo wanaokabiliwa na mashtaka ya jinai ni Wabunge Halima James Mdee, Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara waliohakikisha kwamba uhuni huu wa kisiasa haufanikiwi katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo Vyama vya Siasa na wanasiasa tu ambao wameangukiwa na adha hii ya Serikali kuingia katika njia ya ukandamizaji. Kwa sababu Rais anatumbua majipu hadharani na hasa kwenye vyombo vya habari, sasa Mawaziri nao wanatumbua majipu ya Wizara zao hadharani. Haijalishi kwamba Mawaziri hawa siyo mamlaka za kinidhamu za utumishi wa umma na kama tulivyoonyesha wala hawajakasimishwa majukumu yoyote

kisheria, sasa Mawaziri wanafukuza au kusimamisha au kuhamisha watumishi wa umma walio chini yao. Wakuu wa Mikoa nao sasa wanatumbua majipu Mikoani, wanasimamisha Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa na watumishi wengine wa Serikali za Mitaa bila kujali kwamba hawana mamlaka yoyote kisheria ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, siku hizi haipiti wiki hata moja bila kusikia kwenye vyombo vya habari kwamba Mkuu wa Mkoa au Wilaya fulani ameamuru Afisa huyu ama yule wa Halmashauri au Diwani huyu au yule, akamatwe kwa sababu hii au ile. Wote hawa wanafanya hivyo ili wajionyeshe kwamba wanafanya kazi ya bwana mkubwa ili asije akawatumbua majipu wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hofu ya kutumbuliwa majipu ama na Mheshimiwa Rais mwenyewe ama na Mawaziri ama na Wakuu wake wa Mikoa na Wilaya sasa imetanda kila mahali katika utumishi wa umma. Hofu hii inatokana na ukweli kwamba katika kutumbua majipu haya, hakuna tena kufuata utaratibu wa kinidhamu uliowekwa na sheria za nchi yetu. Sasa hatua hizo zinachukuliwa na wasio na mamlaka kisheria katika majukwaa ya kisiasa au kwenye mikutano ya waandishi habari. Hakuna aliye salama, kuanzia Katibu Mkuu Kiongozi hadi nesi wa hospitalini na mfagizi wa ofisini. Nchi yetu imeingia katika mteremko wenye utelezi mwingi kuelekea kwenye dola la kidikteta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali hii ya Rais Magufuli imekumbatia dhana ya kunyamazisha upinzani dhidi yake, uhuru wa vyombo vya habari umewekwa rehani. Kwa kuwa Bunge hili lilijitokeza katika miaka kumi ya utawala wa Mheshimiwa Rais Kikwete, kama chombo chenye nguvu ya kuiwajibisha Serikali na watendaji wake, Serikali ya hapa kazi tu imeamua kulinyamazisha Bunge na kulifanya kama lilivyokuwa wakati wa miaka ya chama kushika hatamu, yaani chombo cha kupiga muhuri na kuhalalisha maamuzi ya watawala.

Mheshimiwa Spika, wala siyo siri tena kwamba Kamati za Kudumu za Bunge hili zimepangiwa nje ya Bunge na mamlaka ambazo siyo za Kikatiba wala Kikanuni, na wala siyo siri tena kwamba sasa Bunge hili linaongozwa kwa maagizo ya Ikulu, ndiyo maana kila Kiongozi wa Bunge sasa anajipendekeza Ikulu kwa vitendo ambavyo mara nyingine vinafedhehesha, kama vile kumpelekea Mheshimiwa Rais Magufuli fedha zilizoidhinishwa na Bunge hili kwa ajili ya matumizi yake ili zikanunue madawati ya mashule. Kufuta matangazo ya moja kwa moja ya televisheni ni sehemu tu ya mkakati wa kulinyamazisha Bunge ili lisiendeleo kuwa chombo cha kuiwajibisha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wenyewe ni kunyamazisha upinzani dhidi ya utawala huu. Mkakati huu umelenga vilevile kunyamazisha vyombo binafsi vya

habari ambavyo kwa wakati mwingine vimekuwa ni sauti ya Upinzani kwa watawala wa nchi hii. Ndiyo maana hata nusu ya mwaka haikupita tangu iingie madarakani na Serikali hii ikaanza kufuta siyo kufungia, magazeti binafsi yanayotoa habari zisizowapendeza watawala na kutishia hatua hiyo hiyo kwa magazeti mengine.

Mheshimiwa Spika, hata Mahakama ya Tanzania haijapona wimbi hili la kuongezeka kwa vitendo vya kikandamizaji. Ibara ya 107(a)(1) ya Katiba ya nchi yetu inatamka wazi kwamba mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni mahakama. Aidha, Ibara ya 107(b) ya Katiba hiyo imeweka wazi kwamba katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, mahakama zote zitakuwa huru na zitatakiwa kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi."

Mheshimiwa Spika, licha ya msimamo huu wa Kikatiba, Serikali hii ya hapa kazi tu imeanza kuingilia uhuru wa mahakama kwa njia za ajabu kama siyo za kutisha. Kwa mfano, wakati wa sherehe za ufunguzi wa mwaka wa Kimahakama mwanzoni mwa mwezi Februari mwaka huu, Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Ndugu Charles Rwechungura alitoa mfano wa Mkuu wa Wilaya ya Babati, Mheshimiwa Crispin Meela aliyeamuru Hakimu mmoja wa Mahakama ya Mwanzo akamatwe na kuwekwa mahabusu baada ya Hakimu huyo kutoa hukumu ambayo haikumfurahisha Mkuu wa Wilaya. Kitendo kama hicho kiliwahi kutokea katika miaka ya 1970 wakati Mkuu wa Mkoa wa Mara alipoamuru watuhumiwa waliopewa dhamana na mahakama.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzunguzaji)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, yaliyobaki yaingie katika record Rasmi za Bunge lako. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja!

**SPIKA:** Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Lissu tunakushukuru kwa hotuba yako. Waheshimiwa mbona mnapiga makofi sana, kuna nini?

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA TUNDU A. M. LISSU (MB) KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016)*

UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kufanya kazi ambayo ninatakiwa kuifanya kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge lako tukufu na ambayo umeniitia, naomba – kwa ridhaa yako – niseme maneno machache juu ya jambo binafsi linalonihusu mimi na familia yangu. Tarehe 7 Aprili, 2016, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Singida katika Bunge la Kumi, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, alifariki dunia katika Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam. Marehemu alikuwa dada yangu na mdogo wangu wa kuzaliwa.

Kufuatia kifo chake, na licha ya kuwa hakuwa Mbunge tena, uongozi wa Bunge lako tukufu ulichukua jukumu la kuhakikisha Marehemu Christina Mughwai anazikwa kwa heshima zote zinazostahili Mbunge. Waheshimiwa Wabunge – kwa namna mbali mbali – walishiriki katika kuhakikisha mpendwa wetu anapata mazishi ya heshima kubwa. Baadhi yenu hata mlifunga safari ya kumsindikiza Marehemu hadi nyumbani kwetu Kijiji cha Mahambe, Wilaya ya Ikungi ambapo mazishi yalifanyika tarehe 13 Aprili, 2016.

Na sio Bunge na Waheshimiwa Wabunge tu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano mwenyewe, Dkt. John Pombe Magufuli, ilishiriki moja kwa moja katika mazishi hayo. Licha ya shughuli zake nyingi, Rais mwenyewe alikuja kuupokea mwili wa Marehemu na kutoa heshima zake katika Ukumbi wa kihistoria wa Karimjee. Na baadae kwenye mazishi nyumbani kwetu Mahambe, Rais alimtuma Waziri wake, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, kuja kuiwakilisha Serikali katika mazishi hayo. Tulipata kila aina ya msaada tuliohitaji kutoka kwa Bunge, Serikali na Waheshimiwa Wabunge. Hatukuwa wapweke. Hamkutuacha peke yetu katika majonzi yetu. Milia na sisi, na mlitufuta machozi. Mlitufariji sana katika kipindi chote cha kilio chetu. Mliufanya msiba wetu kuwa msiba wenu.

Kwa sababu zote hizi, Mheshimiwa Spika, nimetumwa na waliomzaa na kumlea Marehemu Christina Mughwai; nimeagizwa na ndugu zake na marafiki zake na jirani zake, kutoa shukrani zao za dhati kabisa kwa uongozi wa Bunge lako tukufu, kwa Waheshimiwa Wabunge wote na kwa Rais na Mama John Pombe Magufuli na Serikali yake yote, kwa ajili ya wema na upendo na heshima

mliyotupatia wakati wa mazishi ya mpendwa wetu Christina Lissu Mughwai. Mwenyezi Mungu awazidishie pale mlipokungukiwa na awabariki sana.

Baada ya kusema haya, Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitimize wajibu wangu wa kibunge kama Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu kuhusu hoja iliyoko mezani. Na naomba niweke wazi mapema kwamba nitakayoyasema hapa hayatawafurahisha wengi, ndani na nje ya Ukumbi huu wa Bunge lako tukufu. Hata hivyo, kama alivyosema Frederick Douglass, babu wa harakati za kudai haki za watu weusi wa Marekani ya wakati wa utumwa wa Waafrika zaidi ya miaka mia moja na hamsini iliyopita, *“he is a lover of his country who rebukes its sins rather than justify them”*, yaani, *“ni mpenzi wa nchi yake yule anayekemea madhambi yake badala ya kuyahalalisha.”*

## UTAWALA BILA SHERIA!

### **Mheshimiwa Spika,**

Tarehe 15 Aprili, 1980, Bunge hili lilitunga Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri, Sheria Na. 10 ya 1980.<sup>1</sup> Sheria hiyo ilipata ridhaa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na kuanza kutumika Mei Mosi ya 1980. Pamoja na mambo mengine, Sheria hiyo ilimpatia mamlaka ya kuainisha idara, shughuli na mambo mengine ambayo kwayo kazi na majukumu yake amebaki nayo yeye mwenyewe au ameyakasimu kwa Mawaziri na tarehe ya kuanza kutekeleza majukumu hayo.<sup>2</sup>

Tangu wakati huo, imekuwa ni sheria, na sehemu ya mila na desturi ya kikatiba ya nchi yetu, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuainisha – kwa kupitia Tangazo lililochapishwa katika Gazeti la Serikali – Wizara, idara, shughuli na mambo mengine ambayo Rais amejibakizia mwenyewe, na yale ambayo amekasimu majukumu yake kwa Mawaziri. Utafiti wetu unaonyesha mambo yafuatayo katika miaka 36 na ya utekelezaji wa Sheria hii:

1. Mwaka 1981, Rais Nyerere alitoa *Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 1981 (The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice, 1981*, ambalo lilichapishwa katika *Gazeti la Serikali* kama *Tangazo la Serikali Na. 16 la tarehe 6 Februari, 1981*;
2. Mwaka 1986, Rais Ali Hassan Mwinyi alitoa *Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 1986 (The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice, 1986)*, ambalo lilichapishwa katika *Gazeti la Serikali* kama *Tangazo la Serikali Na. 29 la 1986*;

<sup>1</sup>Sura ya 299 ya Marejeo ya Sheria za Tanzania, 2002

<sup>2</sup> Kifungu cha 5(1)



3. Mwaka 2000, Rais Benjamin William Mkapa alitoa *Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2000 (The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice, 2000)*, ambalo lilichapishwa katika *Gazeti la Serikali* kama *Tangazo la Serikali Na. 468 la 2000*;
4. Mwaka 2006 Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitoa *Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2006 (The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice, 2006)*, ambalo lilichapishwa katika *Gazeti la Serikali* kama *Tangazo la Serikali Na. 2 la tarehe 13 Januari, 2006*. Tangazo hilo lilifuta Matangazo mengine yote ya miaka ya nyuma;
5. Mwaka 2010 Rais Kikwete alitoa *Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2010 (The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice, 2010)*. Tangazo hilo lilichapishwa katika *Gazeti la Serikali* kama *Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Disemba, 2010*. Kama ilivyokuwa kwa Tangazo la mwaka 2006, Tangazo la 2010 lilifuta Matangazo mengine yote yaliyotolewa kabla ya tarehe 17 Disemba, 2010.

### **Mheshimiwa Spika,**

Katikati ya Matangazo haya, Marais waliomtangulia wa nchi yetu Rais Magufuli, katika vipindi tofauti tofauti, wamekuwa wakitumia mamlaka yao chini ya kifungu cha 5(1) cha Sheria, kufanya marekebisho katika majukumu ya kiuwaziri ambayo yalikuwa chini ya Rais mwenyewe, au aliyakasimisha kwa Mawaziri. Hivyo, kwa mfano, mwaka 1982, Mwalimu Nyerere alitoa *Tangazo la Serikali Na. 133 la 1982* kwa ajili hiyo. Mwaka 1984, Mwalimu Nyerere alifanya marekebisho mengine kupitia *Tangazo la Serikali Na. 210 la 1984*.

Aidha, mwaka 1987, Rais Mwinyi alifanya marekebisho kupitia *Tangazo la Serikali Na. 206 la tarehe 17 Aprili, 1987*. Mwaka uliofuata, Rais Mwinyi alifanya marekebisho mengine kupitia *Tangazo la Serikali Na. 42 la tarehe 26 Februari, 1988*. Vile vile, mwaka 2003, Rais Mkapa alitoa *Tangazo la Serikali Na. 142 la tarehe 16 Mei, 2003*. Mwaka huo huo, Rais Mkapa alifanya marekebisho mengine kupitia *Tangazo la Serikali Na. 413 la tarehe 19 Disemba, 2003*. Aidha, mwaka uliofuata Rais Mkapa alifanya marekebisho mara mbili kupitia *Tangazo la Serikali Na. 79 la tarehe 12 Machi, 2004*, na *Tangazo la Serikali Na. 523 la tarehe 3 Disemba, 2004*.

### **Mheshimiwa Spika,**

Tumeelezea jambo hili kwa kirefu kiasi kwa sababu lina umuhimu mkubwa kikatiba na kisheria. Rais hatakiwi kugawa wizara, idara za serikali na majukumu ya kiuwaziri kiholela. Haya ni majukumu ya umma na, kwa sababu hiyo, ni lazima yafanywe kwa kufuata taratibu za kisheria zilizopo. Kwa upande wao,



Mawaziri wanatakiwa kutekeleza majukumu waliyokasimiwa na Rais kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri. Majukumu hayo lazima kwanza yatamkwe, yafafanuliwe na kuainishwa katika Tangazo lililochapishwa kwa ajili hiyo katika *Gazeti la Serikali*. Ndio maana, kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria hiyo, ushahidi pekee na wa mwisho juu ya suala kama Waziri ana mamlaka katika jambo fulani, ni Tangazo la Rais lililochapishwa chini ya kifungu hicho.

### **Mheshimiwa Spika,**

Kwa sababu ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inapenda Bunge hili lizifahamu, licha ya mabadiliko makubwa katika, idadi, muundo na majukumu ya Wizara mbali mbali, hadi tunapoandika Maoni haya, Rais Magufuli hajatoa Tangazo lolote juu ya majukumu ya kiuwaziri ambayo yeye mwenyewe amejibakishia na/au yale ambayo ameyakasimu kwa Mawaziri aliowateua. Tofauti na alivyofanya Rais Kikwete na Serikali yake mwaka 2010, hakuna Mbunge hata mmoja ndani ya Ukumbi huu ambaye amepatiwa nakala ya Tangazo lolote lililochapishwa kwa mujibu wa Sheria.

Licha ya madai ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu katika hotuba yake Bungeni ya tarehe 22 Aprili ya mwezi uliopita, Bunge lako tukufu halijapatiwa nakala hata moja inayothibitisha kwamba Mawaziri walioteuliwa na Rais Magufuli, na ambao wamekuwa wakifanya mambo mbali mbali kwa kofia za kiuwaziri, wanatekeleza majukumu waliyokasimishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri.

Ukweli ni kwamba hata Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, amekiri kwamba Serikali inaendeshwa bila kuwa na alichokiita 'instrument.' Kwa maneno yake mwenyewe, wakati akifanya majumuisho ya hoja za Wabunge kwa Ofisi yake tarehe 27 Aprili, Waziri Mkuu amesema kwamba "*instrument za Wizara zote zimeshakamilika na zimesainiwa (tarehe) 20/04; sasa tunasubiri kutangaza, wakati wowote Mheshimiwa Rais atakapoamua kutangaza zitakuwa zimetoka.*" Maana ya kauli hii ni kwamba hakuna instrument yoyote iliyotangazwa kama inavyotakiwa na kifungu cha 5(1) cha Sheria.

### **Mheshimiwa Spika,**

Maana na athari ya kisheria ya kutokuwepo kwa Tangazo la ukasimishaji wa majukumu ya kiuwaziri ni kubwa sana. Wengi wa Mawaziri wa Serikali hii waliteuliwa na Rais Magufuli tarehe 10 Disemba, 2015. 'Viporo' vilivyobakia kwenye Baraza la Mawaziri vilikamilishwa tarehe 23 Disemba, 2015. Tangu wakati huo hadi sasa, Mawaziri wamefanya mambo mengi. 'Wametumbua majipu' katika Wizara zao na taasisi zilizo chini yake kwa kufukuza, kuachisha, kusimamisha kazi au kuhamisha watendaji na watumishi mbali mbali wa Wizara

au taasisi hizo. Wamefanya maamuzi juu ya matumizi ya fedha na rasilmali nyingine za umma.

Yote waliyoyafanya wameyafanya kinyume cha sheria. Hawakuwa na mamlaka ya kufanya waliyoyafanya kwa sababu Mawaziri hawa hawajakasimishwa mamlaka ya utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri. Watendaji na watumishi wote ambao wametumbuliwa majipu na mawaziri hawa wana haki na uwezo wa kwenda mahakamani na kuomba Mahakama zetu zitengue utumbuaji wa majipu waliofanyiwa na Mawaziri wasiokuwa na mamlaka hayo kinyume cha Sheria hii.

Ushauri wangu wa bure kwa watendaji na watumishi hao ni kwamba wakafungue mashauri Mahakama Kuu ya Tanzania kupinga kutumbuliwa kwao majipu na watu wanaojiita Mawaziri lakini hawana hata *job description*! Kwenda kwao mahakamani sio kutawasaidia kupata haki zao, bali pia kutakomesha vitendo vya kuendesha nchi kienyeji enyeji na bila kufuata sheria, vinavyoelekea kushamiri chini ya utawala huu wa Rais John Pombe Magufuli.

### **Mheshimiwa Spika,**

Kila mtu anafahamu kwamba Rais John Pombe Magufuli sio mwanasheria. Hata hivyo, pamoja na kutokuwa mwanasheria, Rais Magufuli naye anatakiwa kufuata sheria za nchi. Hayuko juu ya sheria. Kiapo chake kinamtaka 'kuilinda, kuitetea na kuihifadhi' Katiba ya nchi yetu na sheria zake. Aidha, Mamlaka ya Nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika, kama inavyotamka ibara ya 9(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, "... kuhakikisha ... kwamba sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa."

Kwa sababu Rais Magufuli sio mwanasheria, ameteua Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye – kwa maneno ya ibara ya 59(3) ya Katiba – *"ndiye mashauri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya sheria na ... atawajibika kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo yote ya kisheria...."* Aidha, kwa sababu hiyo hiyo, Rais Magufuli ameteua Waziri wa Katiba na Sheria ili, kama inavyotakiwa na ibara ya 54(3), awe mshauri wake mkuu katika utekelezaji wa madaraka yake katika masuala ya kikatiba na kisheria.

Kwa bahati nzuri, Rais Magufuli amemteua pia Dkt. Harrison George Mwakyembe – mmoja wa wasomi wa juu kabisa wa sheria katika nchi yetu – kuwa Waziri wake wa Katiba na Sheria. Vile vile, Rais Magufuli amemteua Dkt. Sifuni Ernest Mchome – msomi mwingine wa juu kabisa wa sheria – kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria; na Bwana Amon Anastazi Mpanju, mwanasheria mwingine tena, kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Kambi

Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka kupatiwa majibu sahihi ni kwa nini wanasheria wabobezi wote hawa wameshindwa kumshauri Rais Magufuli kutoa Tangazo la kukasimisha majukumu ya kiuwaziri kwa Mawaziri mbali mbali aliowateua karibu miezi sita iliyopita. Serikali inaendeshwa kama mali binafsi ya Rais Magufuli, bila kufuata wala kuheshimu sheria, sio tu kwa sababu Rais Magufuli ana viashiria vyote vya utawala wa kiimla, bali pia kwa sababu anaelekea kutokuwa na washauri katika masuala ya katiba na sheria za nchi.

Kwa kuangalia mifano ya Matangazo mbali mbali ambayo yametolewa na watangulizi wa Rais Magufuli tangu Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kiuwaziri ilipotungwa mwaka 1980, hata mwanafunzi wa sheria wa mwaka wa kwanza angeweza kumtengenezea Rais Magufuli *draft* ya Tangazo la aina hiyo. Iweje watu wenye shahada za uzamivu na uzamili katika sheria washindwe kufanya hivyo kwa karibu nusu mwaka tangu wateuliwe? Kama ni majipu ya kutumbuliwa na Rais Magufuli, basi wasomi hawa wa sheria ni majipu na wanastahili kutumbuliwa. Itatushangaza sana endapo Rais Magufuli atayafumbia macho majipu haya.

## **UCHAGUZI WA ZANZIBAR NA UKOLONI WA TANGANYIKA**

**Mheshimiwa Spika,**

Sasa naomba nizungumzie masuala ya kikatiba yanayohusu Muungano wetu. Kwa wasiofahamu Katiba yetu na wanaoweza kuhoji kwa nini tunazungumzia masuala ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar katika hoja iliyoko mezani, Sura ya Nne yote ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano inahusu 'Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (na Rais wa Zanzibar), Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.' Aidha, ibara ya 104 ya Katiba yetu imewekwa mahsusi kwa ajili ya 'Uchaguzi wa Kiongozi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.' Kwa sababu hizi, ni halali kabisa kuzungumzia yaliyotokea Zanzibar katika hoja iliyoko mezani.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Maoni yake juu ya *Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015*, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu – baada ya uchambuzi wa kina wa masuala ya fedha za Muungano - ilisema yafuatayo kuhusu mahusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar tangu Muungano wetu uzaliwe tarehe 26 Aprili, 1964:

*"Kwa vyovyote vile, takwimu hizi zinaonyesha kwamba, kwa sababu ya Muungano huu, uhusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar ni uhusiano wa kinyonyaji. Kwa sababu hiyo, huu ni uhusiano wa kikoloni. Ni uhusiano kati ya 'himaya' ya Tanganyika na 'koloni' lake la Zanzibar. Himaya za kikoloni huwa*

zinadhibiti masuala yote ya ulinzi na usalama, mambo ya nje na uhusiano wa kimataifa, uraia, kodi, fedha, sarafu na benki kuu ya makoloni yao. Na himaya za kikoloni huwa zinatumiwa nguvu na udhibiti wao wa masuala haya kuyanyonya makoloni yao kiuchumi, kuyadidimiza kijamii na kuyatawala kisiasa. Hivi ndivyo ambavyo imekuwa kwa mahusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar tangu kuzaliwa kwa Muungano huu tarehe 26 Aprili, 1964."

### **Mheshimiwa Spika,**

Tangu mara baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964, hadi leo hii, Tanganyika imeidhibiti Zanzibar kijeshi na kisiasa. Ukweli ni kwamba – kama ambavyo Harith Ghassany ameonyesha katika kitabu chake *Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru! Zanzibar na Mapinduzi ya Afrabia* – Serikali ya Tanganyika ilishiriki kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya Mapinduzi, ikiwemo kutoa silaha na mafunzo ya kijeshi katika mashamba ya mkonge ya Sakura Estates, Pangani, Tanga, kwa walioipindua Serikali ya Waziri Mkuu Mohamed Shamte na Sultan Jamshid bin Abdullah.

Aidha, siku tatu tu baada ya Mapinduzi hayo, Serikali ya Tanganyika – kupitia Waziri wake wa Mambo ya Nje na Ulinzi Oscar Salatiel Kambona – ilipeleka vikosi vya *Tanganyika Rifles*, Jeshi la Tanganyika, ili kuidhibiti Zanzibar kijeshi. Mambo yote haya yamejulikana kwa miaka mingi na wasomi na wanazuoni wa Muungano huu, na yamechapishwa katika vitabu na machapisho mengine rasmi ya kitaaluma ndani na nje ya Tanzania.

Kwa kutumia udhibiti wake wa kijeshi, Tanganyika imedhibiti pia siasa za Zanzibar. Watawala wa Tanganyika ndio wanaoamua nani awe mtawala wa Zanzibar na wamefanya hivyo tangu mwaka 1964. Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi asingekuwa Rais wa Zanzibar baada ya kuuawa kwa Sheikh Abeid Amani Karume mwaka 1972 bila 'ushawishi' wa Mwalimu Nyerere na Serikali ya Tanganyika. Na kama ambavyo wanazuoni wa Muungano huu, kama vile Profesa Issa G. Shivji wameonyesha, Jumbe asingeng'olewa madarakani mwaka 1984 bila shinikizo la Mwalimu Nyerere na watu wake hapa Dodoma. Aidha, Rais Mwinyi na Marais wengine wote wa Zanzibar waliomfuatia, 'wametengenezewa' Dodoma na sio Zanzibar.

### **Mheshimiwa Spika,**

Tarehe 20 Aprili, 1968, Mwalimu Nyerere alisema yafuatayo wakati akihojiwa na gazeti la *The Observer* la London, Uingereza: "*If the mass of the people of Zanzibar should, without external manipulation, and for some reason of their own, decide that the Union was prejudicial to their existence, I could not bomb them into submission.... The Union would have ceased to exist when the consent of its constituent members was withdrawn.*" Yaani, "endapo umma wa

wananchi wa Zanzibar wataamua, bila kurubuniwa kutoka nje na kwa sababu zao wenyewe, kwamba Muungano unaathiri kuendelea kuwepo kwao, sitaweza kuwalazimisha kwa kuwapiga mabomu.... Muungano hautaendelea kuwepo pale ridhaa ya washirika wake itakapoondolewa."

Alichokisema Baba wa Taifa kwamba hatakifanya, Serikali ya Tanganyika imekifanya kwa zaidi ya miaka ishirini sasa. Kabla ya mfumo wa vyama vingi kuruhusiwa mwaka 1992, udhibiti wa Tanganyika kwa siasa za Zanzibar ulifanyika kwa kutumia dhana ya 'chama kushika hatamu.' Katika zama za vyama vingi, wananchi wa Zanzibar wamekuwa wapinzani wakubwa wa ukoloni wa Tanganyika kwa nchi yao. Kwa sababu hiyo, tangu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, Serikali ya Tanganyika imetumia mabavu ya kijeshi ya wazi wazi ili kuwaweka madarakani vibaraka wake na kuendelea kuitawala Zanzibar.

Kilele cha matumizi haya ya mabavu ya kijeshi ni Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, ambako vibaraka wa Tanganyika katika Zanzibar walikataliwa kabisa na wananchi wa Zanzibar katika Uchaguzi wa Rais, Wawakilishi na Madiwani. Ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) tu ndilo ambalo limehakikisha kwamba vibaraka hawa waliokataliwa na wananchi wao, wanaendelea kubakia madarakani.

Kwa maoni yetu, Mheshimiwa Spika, katika mazingira haya, tatizo la msingi la Zanzibar sio Jecha Salim Jecha wala ZEC wala Ali Mohamed Shein. Hawa ni vibaraka tu wasiokuwa na nguvu wala uhalali wowote. Bila nguvu ya Tanganyika vibaraka hawa hawawezi kudumu madarakani kwa muda mrefu. Tatizo la msingi ni ukoloni wa Tanganyika kwa Zanzibar ambao umevikwa joho la Muungano. Bila kulivua joho hili na kushona lingine badala yake, Zanzibar haitakuwa huru na itaendelea kutawaliwa na Tanganyika kisiasa, kiuchumi na kijeshi.

### **KUNYAMAZISHA UPINZANI NI KUKARIBISHA UDIKTETA!**

#### **Mheshimiwa Spika,**

Mwanaharakati mmoja wa haki za binadamu wa karne ya 19 aliwahi kuandika kwamba: *"Once a government is committed to the principle of silencing the opposition, it has only one way to go, and that is down the path of increasingly repressive measures, until it becomes a source of terror to all its citizens and creates a country where everyone lives in fear"*, yaani *"pale serikali inapoamua kunyamazisha upinzani, inakuwa na njia moja tu ya kupita, nayo ni njia ya kuongezeka kwa vitendo vya kikandamizaji, mpaka serikali hiyo inakuwa chanzo cha hofu kwa wananchi wake wote na inatengeneza nchi ambapo kila mmoja anaishi kwa hofu."*

Maneno haya yametimia katika nchi yetu. Kwa sababu ya kubaka demokrasia kwa kutumia nguvu za kijeshi Zanzibar ili kukipokonya Chama cha Wananchi (CUF) ushindi wake halali, Serikali hii ya hapa kazi tu imeingia katika njia ya kuongezeka kwa vitendo vya kikandamizaji kila mahali katika nchi yetu. Katika Jiji la Tanga ambako CCM ilikataliwa na wananchi, Serikali hii ilitumia ghibla na mabavu ya kila aina kuhakikisha CCM inanyakua Umeya wa Jiji hilo. Leo viongozi wa vyama vya UKAWA na madiwani waliochaguliwa na wananchi wanakabiliwa na mashtaka ya kutengeneza kwa sababu tu ya kukataa kwao kutawaliwa na watu ambao hawakupata ridhaa ya wananchi.

Hivyo ndivyo ilivyotokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, ambako ilibidi Mbunge wa Jimbo la Kilombero na mjumbe halali wa Halmashauri hiyo atolewe kwa nguvu na mapolisi ili kuiwezesha CCM, iliyokataliwa na wananchi kwenye kura, kushinda nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya. Sasa Mbunge huyo naye anakabiliwa na mashtaka ya jinai mahakamani kwa kosa la kutetea demokrasia na utawala wa sheria na kukataa utawala wa mabavu na udikteta.

Katika Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri zake, licha ya nguvu kubwa na hila nyingi zilizotumiwa na Serikali hii, wananchi wa Dar es Salaam na viongozi wao wa UKAWA walifanikiwa kutetea maamuzi ya wapiga kura na kuzuia jaribio la kubaka demokrasia kwa kuweka Mameya wa chama kilichokataliwa na wananchi kwenye uchaguzi. Hata hivyo, badala ya kuchukua hatua za kijinai dhidi ya Mkurugenzi wa Jiji, Mwanasheria wa Jiji na Katibu Tawala wa Mkoa waliodiriki hata kugushi hati ya amri ya Mahakama kwa lengo la kuzuia uchaguzi halali wa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, leo wanaokabiliwa na mashtaka ya jinai ni Wabunge Halima James Mdee, Saed Ahmed Kubenea na Mwitwa Mwikwabe Waitara waliohakikisha kwamba uhuni huu wa kisiasa haufanikiwi katika Jiji la Dar es Salaam.

Na sio vyama vya siasa na wanasiasa tu ambao wameangukiwa na adha hii ya Serikali kuingia katika njia ya ukandamizaji. Kwa sababu Rais anatumbua majipu hadharani na, hasa, kwenye vyombo vya habari, sasa Mawaziri nao wanatumbua majipu ya Wizara zao hadharani. Haijalishi kwamba Waziri hawa sio mamlaka ya kinidhamu ya utumishi wa umma na, kama tulivyoonyesha, wala hawajakasimishwa majukumu yoyote kisheria, sasa Mawaziri wanafukuza au kusimamisha au kuhamisha watumishi wa umma walio chini yao.

Wakuu wa Mikoa nao sasa wanatumbua majipu mikoani; wanasimamisha Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa na watumishi wengine wa serikali za mitaa bila kujali kwamba hawana mamlaka yoyote kisheria ya kufanya hivyo. Na siku hizi haipiti wiki moja bila kusikia kwenye vyombo vya habari kwamba Mkuu wa Mkoa au Wilaya fulani ameamuru ameamuru afisa



huyu ama yule wa Halmashauri, au diwani huyu au yule, akamatwe kwa sababu hii au ile.

Wote hawa wanafanya hivyo ili wajionyeshe kwamba wanafanya kazi ya Bwana Mkubwa ili asije akawatumbua majipu wao wenyewe. Hofu ya kutumbuliwa majipu ama na Rais mwenyewe ama na Mawaziri ama na Wakuu wake wa Mikoa na Wilaya wake sasa imetanda kila mahali katika utumishi wa umma. Hofu hii inatokana na ukweli kwamba katika kutumbua majipu huku, hakuna tena kufuata utaratibu wa kinidhamu uliowekwa na sheria za nchi yetu. Sasa hatua hizo zinachukuliwa na wasio na mamlaka kisheria katika majukwaa ya kisiasa au kwenye mikutano ya waandishi habari. Na hakuna aliye salama, kuanzia Katibu Mkuu Kiongozi hadi nesi wa hospitalini na mfagizi wa ofisini. Nchi yetu imeingia katika mteremko wenye utelezi mwingi kuelekea kwenye dola la kidikteta.

### **Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Serikali hii ya Rais Magufuli imekumbatia dhana ya kunyamazisha upinzani dhidi yake, uhuru wa vyombo vya habari umewekwa rehani. Kwa kuwa Bunge hili lilijitokeza, katika miaka kumi ya utawala wa Rais Kikwete, kama chombo chenye nguvu ya kuiwajibisha Serikali na watendaji wake, Serikali ya hapa kazi tu imeamua kulinyamazisha na kulifanya kama lilivyokuwa wakati wa miaka ya 'chama kushika hatamu', yaani chombo cha kupiga muhuri na kuhalalisha maamuzi ya watawala.

Wala sio siri tena kwamba Kamati za Kudumu za Bunge hili zimepangiwa nje ya Bunge na mamlaka ambazo sio za kikatiba wala kikanuni. Na wala sio siri tena kwamba sasa Bunge hili linaongozwa kwa maagizo ya Ikulu. Ndio maana kila kiongozi wa Bunge sasa anajipendekeza Ikulu kwa vitendo ambavyo mara nyingine vinafedhehesha, kama vile kumpelekea Rais Magufuli fedha zilizoidhinishwa na Bunge hili kwa ajili ya matumizi yake ili zikanunue madawati ya mashule. Kufuta matangazo ya moja kwa moja ya televisheni ni sehemu tu ya mkakati wa kulinyamazisha Bunge ili lisiendelee kuwa chombo cha kuiwajibisha Serikali.

Mkakati wenyewe ni kunyamazisha upinzani dhidi ya utawala huu. Mkakati huu umelenga vile vile kunyamazisha vyombo binafsi vya habari ambavyo wakati mwingine vimekuwa ni sauti ya upinzani kwa watawala wa nchi hii. Ndio maana hata nusu mwaka haikupita na Serikali hii ikaanza kufuta – sio kufungia! - magazeti binafsi yanayotoa habari zisizowapendeza watawala, na kutishia hatua hiyo hiyo kwa magazeti mengine.



**Mheshimiwa Spika,**

Hata Mahakama ya Tanzania haijapona wimbi hili la ‘kuongezeka kwa vitendo vya kikandamizaji.’ Ibara ya 107A(1) ya Katiba ya nchi yetu inatamka wazi kwamba “mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama.” Aidha, ibara ya 107B ya Katiba hiyo imeweka wazi kwamba “katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi.”

Licha ya msimamo huu wa kikatiba, Serikali hii ya hapa kazi tu imeanza kuingilia uhuru wa mahakama kwa njia za ajabu, kama sio za kutisha. Kwa mfano, wakati wa sherehe za ufunguzi wa mwaka wa kimahakama mwanzoni mwa mwezi Februari ya mwaka huu, Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Bwana Charles Rwechungura alitoa mfano wa Mkuu wa Wilaya ya Babati, Crispin TP Meela (mwenyewe mwanasheria na mwanachama wa (TLS) aliyeamuru hakimumu mmoja wa Mahakama ya Mwanzo akamatwe na kuwekwa mahabusu baada ya hakimumu huyo kutoa hukumu ambayo haikumfurahisha Mkuu wa Wilaya.

Kitendo kama hicho kiliwahi kutokea katika miaka ya 1970 wakati Mkuu wa Mkoa wa Mara alipoamuru watuhumiwa waliopewa dhamana na Mahakama ya Hakimumu Mkazi ya Musoma wakamatwe na kurudishwa rumande. Hakimumu Mkazi aliyewapa watuhumiwa hao dhamana alichukua hatua ya kumjulisha Jaji Mkuu, wakati huo Marehemu Francis Lucas Nyalali juu ya kitendo hicho cha Mkuu wa Mkoa. Siku hiyo hiyo taarifa hizo zilimfikia Rais Nyerere na wiki mbili baadae Mkuu wa Mkoa alihamishwa kutoka Mkoa wa Mara. Leo hakimumu anakamatwa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya lakini kwa sababu ya hofu iliyotanda ya kutumbuliwa majipu, Jaji Mkuu na Mahakama nzima inenyamaza kimya.

**MAJIPU YA MAHAKAMA!****Mheshimiwa Spika,**

Sasa naomba nizungumzie masuala ya Mahakama ya Tanzania ambayo, kwa sababu ya utamaduni uliojengeka kwa miaka mingi wa kulindana, hayazungumzwi. Tarehe 30 Novemba, 2014, Bunge hili lilipitisha kwa kauli moja Maazimio ya Bunge Kuhusu Hoja ya Taarifa Maalum ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalum Kuhusiana na Miamala Iliyofanyika Katika Akaunti ya ‘Escrow’ ya Tegeta Pamoja na Umiliki wa Kampuni ya IPTL, maarufu kama Maazimio ya Tegeta Escrow Account.

Azimio la 4 la Maazimio ya Tegeta Escrow Escrow lilisema yafuatayo: “KWA KUWA, Taarifa Maalum ya Kamati imeonesha kwamba katika watu waliotajwa

*kuhusika kwa namna moja au nyingine katika kashfa ya miamala ya Akaunti ya Escrow wapo pia Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania; KWA KUWA, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ... imeweka utaratibu mahsusi wa kushughulikia nidhamu ya Majaji; KWA KUWA, utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji kwa mujibu wa Katiba unamtaka Rais kuunda Tume ya Uchunguzi wa Kijaji kuchunguza tuhuma za utovu wa maadili dhidi ya Majaji; NA KWA KUWA, utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji unamruhusu Rais kumsimamisha kazi Jaji au Majaji husika wakati uchunguzi wa tuhuma dhidi yake unaendelea; HIVYO BASI, BUNGE LINAAZIMIA KWAMBA, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aunde Tume ya Kijaji ya Uchunguzi kuchunguza tuhuma za utovu wa maadili dhidi ya Jaji Aloysius Mujulizi na Jaji Profesa Eudes Ruhangisa wa Mahakama Kuu ya Tanzania."*

### **Mheshimiwa Spika,**

Baada ya Bunge lako tukufu kupitisha maazimio haya, tarehe 22 Disemba, 2014, Rais Jakaya Kikwete aliwahutubia 'Wazee wa Dar es Salaam' ambako alisema yafuatayo kuhusu Azimio la Majaji wa Tegeta Escrow: *"Azimio hili nimelipokea, (na) tumelijadili. Hata hivyo, itabidi tufuate utaratibu wa kikatiba na kisheria wa kushughulikia masuala ya namna hiyo. Inatakiwa suala kama hili lianzie kwenye Mhimili wa Mahakama yenyewe na siyo kwa Rais au Bunge. Tume ya (Utumishi wa) Mahakama ndiyo yenye mamlaka ya kumtaka Rais aunde Tume ya Kijaji ya kumchukulia hatua Jaji yeyote pale inapodhihirika kuwa amepoteza sifa za kuendelea kufanya kazi hiyo. Nashauri suala hili tumuachie Jaji Mkuu wa Tanzania alishughulikie atakavyoona inafaa."*

### **Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa taarifa zilizochapishwa na vyombo vya habari mwaka jana, baada ya maelezo hayo ya Rais Kikwete, Jaji Mkuu, Mheshimiwa Mohamed Chande Othman aliunda jopo la Majaji watatu, chini ya Mwenyekiti wake, Jaji Mbarouk Salim Mbarouk wa Mahakama ya Rufani ya Tangania. Aidha, mwishoni mwa mwaka jana, Jaji Mkuu Othman aliwaambia waandishi habari kuwa taarifa ya uchunguzi ya Tume ya Jaji Mbarouk ilikuwa 'imeiva.' Cha kushangaza, Mheshimiwa Spika, tangu kuiva kwa taarifa hiyo, Jaji Mkuu Othman, na Serikali hii ya CCM, wamepata kigugumizi kikubwa cha 'kuipakua' ili Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla 'waile'! Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inamtaka mtoa hoja alieleze Bunge lako tukufu iliko taarifa ya uchunguzi wa Majaji wa Tegeta Escrow na kwa nini haijaletwa mbele ya Bunge lako tukufu kwa taarifa au kwa mjadala.

## SOMO KUTOKA KENYA

**Mheshimiwa Spika,**

Hatuna budi kujifunza namna ya kushughulikia masuala ya maadili ya Majaji wetu kutoka kwa jirani zetu. Naomba, katika hili, kutoa mfano wa hivi karibuni kutoka nchini Kenya. Mapema mwaka huu, Jaji Phillip Tunoi wa Mahakama ya Juu (Supreme Court) ya Kenya alituhumiwa katika kashfa inayofanana na kashfa ya Majaji wa Tegeta Escrow. Mara baada ya tuhuma dhidi ya Jaji Tunoi kutolewa hadharani, Jaji Mkuu wa Kenya, Dkt. Willy Mutunga, aliunda Tume ya Uchunguzi ya Kijaji kuchunguza tuhuma hizo. Mnamo tarehe 5 Februari ya mwaka huu, ndani ya kipindi cha wiki mbili, Jaji Mkuu Mutunga alimkabidhi Rais Uhuru Kenyatta taarifa ya uchunguzi wa tuhuma dhidi ya Jaji Tunoi. Kwetu Tanzania ni zaidi ya mwaka na nusu tangu Bunge lako tukufu lipitisha azimio la kuunda Tume ya kuwachunguza Majaji wa Tegeta Escrow na Jaji Mkuu wetu anaelekea kuwa amekalia taarifa ya uchunguzi huo, kama kweli ulifanyika.

Tarehe 12 Februari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Fedha za Serikali (PAC) ya Bunge la Kenya ilitoa taarifa iliyomtuhumu Jaji Mkuu Mutunga kuwa hachukui hatua zozote dhidi ya vitendo vya rushwa vinavyofanywa na Majaji, Wasajili na Mahakimu wa Kenya. PAC ya Kenya ilimtaka Jaji Mkuu Mutunga kuwajibika ama kuwajibishwa, ikiwa ni pamoja na kuondolewa kwenye nafasi ya Jaji Mkuu wa Kenya kwa kushindwa kudhibiti maadili ya maafisa hao wa Mahakama ya Kenya.

Siku moja baadae, Jaji Mkuu Mutunga alijibu PAC kwa kutoa takwimu zilizothibitisha jitihada za Mahakama ya Kenya katika kukabiliana na rushwa na ufisadi ndani ya Mahakama hiyo. Kwa maelezo ya Jaji Mkuu Mutunga, *"... three judges have been referred to a tribunal ... on allegations of corruption, a few others are under consideration in the Judicial Service Commission, a Chief Registrar and five Directors have been dismissed, 9 magistrates and 65 Judicial Staff are facing disciplinary proceedings, some have been dismissed or retired in the public interests...."*

Kwetu Tanzania, kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (MB), Akiwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara Kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 mwezi uliopita: *"Tume (ya Utumishi wa Mahakama) ilishughulikia jumla ya mashauri 14 ya nidhamu kwa watumishi wa mahakama na kutolewa uamuzi. Katika hayo watumishi 10 walifukuzwa kazi baada ya kupatikana na hatia ya utovu wa nidhamu na mengine 4 yanafanyiwa uchunguzi zaidi."*

Na kwa kadri ya ufahamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, mara ya mwisho Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania aliwahi kuchukuliwa hatua

za kinidhamu kwa utovu wa maadili ilikuwa ni mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1990, wakati Jaji Mwakibete alipoondolewa na Rais Ali Hassan Mwinyi kwa tuhuma za rushwa na baada ya kuundiwa Tume ya Uchunguzi ya Kijaji. Tangu wakati huo, inaelekea Majaji wa Tanzania wamekuwa malaika na watakatifu wasiokula kula rushwa wala kufanya makosa mengine ya utovu wa maadili, maana hakuna hata mmoja ambaye ameundiwa Tume ya Uchunguzi ya Kijaji au kuchukuliwa hatua stahiki za kinidhamu.

Hii, Mheshimiwa Spika, haiwezi kuwa kweli. Kwa jinsi ambavyo tuhuma za rushwa na ufisadi katika ngazi zote za Mahakama ya Tanzania zimekuwa kubwa na kwa miaka mingi, ni wazi hatuna malaika wala watakatifu katika Mahakama ya Tanzania. Na kwa ushahidi wa *Addendum Juu ya Uteuzi wa Majaji* niliyoitoa kufuatia Maoni yangu mbele ya Bunge lako tukufu ya tarehe 13 Julai, 2012, matatizo ya utovu wa maadili katika Mahakama zetu za juu ni makubwa sana.

Kwa sababu hiyo, ni lazima sisi kama Bunge na kama taifa tutumbue majibu makubwa na mengi ya Mahakama ya Tanzania. Bunge lako tukufu lisinyamaze kwa hofu ya kuwaudhi Majaji na Mahakimu wetu. Kukosekana kwa haki katika Mahakama zetu kutapelekea machafuko katika nchi yetu. Kama kiongozi maarufu wa Mapinduzi ya Mexico ya 1910, Emiliano Zapata, alivyowahi kusema: *"If there is no justice for the people, let there be no peace for the government"*, yaani *"kama hakuna haki kwa wananchi, basi kusiwe na amani kwa serikali."*

---

Tundu Antiphas Mughwai Lissu

**MSEMAJI & WAZIRI KIVULI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

MEI 5, 2016

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Naomba tutoe nafasi sasa kwa uchangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, na mimi sina budi kwanza kabisa kuungana na Bunge zima kumpa pole sana familia ya Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kufiwa na Marehemu Christina ambaye alikuwa ni mwanafunzi wangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ilikuwa ni pigo sana, poleni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpogeze sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe kwa hotuba yake ambapo ametuelezea kabisa hatua kubwa ambazo zimeshafanyika na zinazoendelea kufanyika katika kuboresha hali ya utawala wa sheria na Katiba katika Nchi hii. Nashangaa sana na naomba niongee kwa mtazamo wangu kama mchumi, mtu ambaye naelewa hali halisi inayokabili utawala wa sheria. Mwanamapinduzi Karl Marx alisema nanukuu

kwamba *economics drives politics* na akasema Karl Marx kwamba *power makes law*, maana yake ni kwamba uchumi unaendesha siasa na akasema mamlaka, madaraka pia hutengeneza sheria, mwisho wa kunukuu, huyo ni Karl Marx siyo Anna Tibaijuka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa hivi nilisema awali na narudia tena, nchi yetu imebahatika, Watanzania wamekaa wakamchagua Rais ambaye ni kiongozi wa nchi naomba tumpe *support*, Waheshimiwa wenzetu ambao kazi yao ni kuja kutusimamia sisi, wana haki ya kusema wanayoyasema, pia tuna haki ya kuyawekea *context* yake kusudi yaeleweke. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa uelewa wangu wa mambo, nchi yetu sasa hivi ina nafasi ya kurekebisha yale ambayo yalikuwa yametushinda kusudi twende mbele. Kwa hiyo, Upinzani ukifilisika ukabaki sasa kukemea kwa sababu lazima useme kitu, Bunge linageuka kijiwe. Bungeni hapa hatulefi hoja za vijiwani. Kwa mfano kusema kwamba Tanganyika inainyonya Zanzibar inainyonya katika lipi? Hili ni jambo la kujiuliza! Nimejiuliza kama mchumi tena mchumi kazi yangu ya kwanza ninyi mnanijua nilikuwa kwenye Shirika la Makazi Duniani, hamjui kwamba nilikuwa kwenye Shirika la Biashara la Dunia (UNCTAD) nikisimamia..... (Makofi)

*(Hapa baadhi Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namlinda mzungumzaji, muwe na uvumilivu. Mheshimiwa Profesa endelea.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, linda muda wangu, kwanza kabisa kwa wale wanaosema nimeiba hapa mtaisoma namba, mimi siyo mtu wa kutishwa na vitu vya hovy hovy! (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Wapee!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, kama kuna mtu anafikiria kwamba mimi naweza nikatishwa hoja za hovy hovy huyo asome namba. Soma namba nasimama hapa nataka nitetee vitu ambavyo kwa kawaida watu tunanyamaza lakini sasa mtu anapopotosha hoja inaweza ikaleta hatari.

Mheshimiwa Spika, Tanganyika kwa mtazamo wa kiuchumi, haiwezi kuinyonya Zanzibar kwa mtazamo wa kiuchumi wa haraka. Nimeona niseme hili kwa sababu sheria na Katiba ya nchi yetu nimeona Mheshimiwa amezungumzia Katiba mpya mambo ambayo nilitaka kuyaainisha hapa, kuna

suala la Katiba Mpya, Katiba Mpya tuliifanyia kazi wote tukawa tumekwama na Waziri amesainisha.

Mheshimiwa Spika, tunapoleta hoja zetu, tuzilete kwenye mantiki ambayo sasa haipotoshi umma wa Watanzania na kuleta vurugu katika nchi hii. Kisiwa cha Zanzibar nilisema wakati wa Bunge la Katiba na narudia, Kisiwa cha Zanzibar huwezi kusimama ukasema itakuwa Singapore, itakuwa Singapore vipi haina bandari, Comoro ina hali gani?, Commoro ina hali gani?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, naendelea kuchangia. Katika dunia ya ustaarabu unasikia hoja, Mheshimiwa Lissu amesoma hapa angeweza kuzomewa lakini wastaarabu wakamsikiliza wamekomaa kisiasa. Sasa ninyi mkianza kupiga kelele ilimradi kelele zote naomba muda wangu ulindwe.(Makofi)

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa ongea na mimi, usisikilize kelele zao.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, suala la Zanzibar tulijadili kwa umakini, tulijadili kwa ukweli, tulijadili kwa haki lakini siyo kwa hoja za vijiwani hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, inapokuja suala la uhuru wa mahakama, wananchi wangu wa Muleba Kusini wa Kata ya Mgunda na Kata ya Karami wako katika hali ngumu. Hakimu pale anakula rushwa ya waziwazi, hatuwezi kusema kwamba Mkuu wa Wilaya ambaye anasimamia maadili ya Mahakimu au Mkuu wa Mkoa ambaye anaangalia aache mambo yaende kama yanavyokwenda. Uhuru wa mhimili wa mahakama haumaanishi kwamba wafanye wanavyotaka na wenyewe wanapofanya kosa lazima sheria itafuata mkondo wake.

Hivyo, suala hili naomba niliweke mbele na Mheshimiwa Waziri utakaposimama kwa sababu tunakutegemea wewe kwamba uwajibishwaji wa mawakili, mahakimu katika sehemu nyingi hasa Mahakama za Mwanzo imekuwa ni mgogoro na shida kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Muleba Kusini hali yetu siyo nzuri, tumeshahangaika, hatujui mahali pa kwenda naomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama utuambie unavyoweza na jinsi mhimili huu utakavyoweza kusimamia utendaji na uadilifu wa Mahakimu hasa wa Mahakama za Mwanzo. Wamejifanya miungu watu, wanashirikiana wakati mwingine na polisi ambao siyo waaminifu kubambikiza watu kesi na mtu yoyote anayekubali kubambikizwa kesi au



kubambikizwa hivi vitu vya hovyho hovyho, mtu dhaifu lazima tusimamie wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, hilo nimelisema naomba kabisa lishughulikiwe na kwa upande wa Muleba Kusini tuko katika hali ngumu, tunahitaji Mheshimiwa Waziri uwasiliane na mahakama utusaidie.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka niliseme, tunapozungumzia sheria na Katiba, utawala wa sheria pia, hauondoi mamlaka ya watendaji wa Serikali kufanya kazi yao kama Mheshimiwa Rais anavyofanya kazi yake kwa *speed* kusudi twende mbele. Kwa sababu sasa *you can not have your cake and eat it*, hapa naona kuna hoja za mtu kula keki yake na anataka abaki na keki yake. Serikali ilipofanya kazi polepole wakasema Serikali ni dhaifu, nikasikia kauli kwamba Rais huyu ni dhaifu, Rais anapofanyakazi anasimama mtu anasema Rais anakwenda kiimla, *please*, mbona tunapingana? Nataka kusema kwamba tunapozungumzia sheria tusiwa-*confuse* wananchi wetu kwa kusema kwamba Serikali inaendesha kiimla, hakuna Serikali inayokwenda kiimla. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nichangie kwa kusema kwamba, hali za mahakama hususani Muleba na Kagera nyingi zipo katika hali mbaya. Majengo yamechakaa, majengo hayatoshi yanatakiwa yafanyiwe ukarabati. Kwa hiyo, tunapogawa fedha sasa, tunapoimarisha sheria, *justice delayed, justice denied* kama hakuna vifaa vya kutosha katika Mahakama haiwezekani! Nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ambaye tayari ameshawawezesha muhimili huu wa mahakama ili kusudi waweze kupata fedha wanazozihitaji na kesi ziende haraka.

Kwa hiyo, nataka kusema kwamba kwa upande wa mtizamo wa muhimili huu wa sheria inatulinda wote, hayo tunayoyasema hapa Bungeni ni kwa sababu tunalindwa na sharia, unapotuhumiwa unasimamia haki yako! Hizi kelele za chura haziwezi kumzuia ng'ombe kunywa maji! Hiyo naomba niseme kabisa. Haziwezi kumzuia ng'ombe kunywa maji (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nifafanue kwa sababu naelewa mambo mengi. Nilipokuwa Kenya nilishuhudia Rais Mheshimiwa Mwai Kibaki alisimamisha Majaji 23 kwa siku moja, kwa hiyo lazima watu wawajibishwe, lazima kuwe na unautaratibu wa kuwawajibisha watendaji wa Mahakama. Hivyo, msiwa-*confuse* wananchi, msiwadanganye, mlete hoja, wengi wetu tunazipenda tutazisikiliza lakini ziwe na mashiko. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)



**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru tumeanza mjadala vizuri, lakini naomba kitu kimoja, kwa sababu sisi ni Wabunge, hapa vikitoka vidonge vizuri, wewe tulia tu, kama unapigwa sindano, tulia tu! Ukitaka unaomba hapa, utapata nafasi ya kujibu. Ndiyo maana Mheshimiwa Tundu Lissu ameongea hapa mwanzo mwisho hakuna mtu hata aliyekohoa au siyo jamani? Sasa Profesa Tibaijuka pale, tena leo ame-beep tu maana yake siku nyingi hajaongea, tayari kelele moja kwa moja!

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo naomba tusikilizane kidogo, zamu yenu Mheshimiwa Ali Ngwali utaona hakuna mtu atakaekufanyia fujo, Ngwali karibu. Mheshimiwa Ahmed Ali Ngwali. (Makofi)

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, mimi jina langu naitwa Ahmed Juma Ngwali, siitwi Ahmed Ali Ngwali.

Mheshimiwa Spika, sihitaji makofi wala sihitaji vijembe. Nimekuja hapa na nimesimama hapa nina jambo langu ambalo naiomba Serikali inisikilize kwa umakini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna Sheria ya Wakfu, (*Commission Ordinance*) ya mwaka 1953, Sheria hiyo ikafanyiwa marekebisho mwaka 1956. Ilikuwa Sheria namba 7 na ikafanyiwa marekebisho ikawa Sheria Namba 9. Jambo la kushangaza, sheria hiyo mpaka leo ipo, Sheria hiyo inahusu Wakfu ya Waislamu. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza Mwalimu Nyerere akaiacha hiyo *commission* hakuwahi kuiunda pia Mheshimiwa Rais Mwinyi akapita hiyo *commission* haikuundwa, akapita Rais wa Tatu Mheshimiwa Benjamin Mkapa pia hiyo *commission* haikuundwa na Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Jakaya Kikwete *commission* haijawahi kuundwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo mali za waislamu zimekuwa zikiibiwa. Hiyo *commission* ni muhimu sana kwa ajili ya maslahi ya waislamu na mali zao.

Kuna Sheria ya Mirathi ambayo ndani ya Sheria ya Mirathi sasa imeingizwa sehemu ya Sheria ya Wakfu ambayo imeeleza mambo mengi. Inashangaza sana! Sheria ya Wakfu ipo halafu ikatiwa ndani ya Sheria ya Mirathi.

Mheshimiwa Spika, mirathi na wakfu ni mambo mawili tofauti, hayafanani!

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngwali, neno moja dogo tu....

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Naam.

**SPIKA:** Umesema mali za waislam zinaibiwa tukashtuka, ni kitu gani? Unaweza ukafafanua kidogo?

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Tunakwenda, tulia...

**SPIKA:** Ni jambo kubwa hilo!

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, tulia!

Mheshimiwa Spika, nirudi hapo ambapo unapotaka sasa, kwasababu tu hii *commission* ya kusimamia mali za waislamu....

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimwa Ngwali pokea Taarifa.

### TAARIFA

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa kutumia Kanuni ya 68(8) ambayo inasema kamba "Vilevile Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake, akasema taarifa, na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au...

**SPIKA:** Ahsante Dkt. Suleiman, nenda moja kwa moja kwenye Taarifa.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Taarifa niliyotaka kumpa Mheshimiwa msemaji hapa ni kwamba maneno mawili haya Wakfu na Mirathi ni tofauti kama alivyofanya.

Sasa mimi namfafanulia kidogo tu! Ni kwamba ukienda katika Sheria ya Zanzibar, Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana, Sheria Na. 2 ya mwaka 2007, Kifungu cha 2 (1) kinafafanua vizuri sana mambo haya. Kinasema kwamba Wakfu ni ile mali iliyohamishwa kwa mmiliki wa mwanzo ikapelekwa kwa ajili ya kunufaisha au kusaidia mambo ya kiislamu au kusaidia malengo maalum au kufaidisha kundi la watu maalum....

**SPIKA:** Dkt. Taarifa yapaswa kuwa fupi sana.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika mirathi ni ule mchakato ambao unaangalia ni namna gani mali ya marehemu inaweza kugawiwa kwa wahusika wa kisheria wa marehemu yule.

Kwa hiyo, nilichotaka kusema ni kwamba mirathi katika Uislamu imegawiwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe ama mambo ya Wakfu ni ya

watu au binadamu wenyewe ndiyo ambao tunapanga, hapo ndipo tunapata tofauti. Naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, nimepokea vizuri sana.

**SPIKA:** Mmetuchanganya kabisa, nia yenu kumbe ni kuchangia kijanja (Kicheko)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ahmed Ngwali, *chap chap*, Katibu angalia hizo dakika.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika nimepokea vizuri na muda wangu nilindie.

Mheshimiwa Spika, tunachosema sasa ni kuiomba Serikali, hii *commission* ya Wakfu ianze kufanya kazi, kwa sababu sheria tayari ipo na kila kitu kipo, waislamu wengi wanapata shida na kuchelewa kwa Serikali kuanzisha wakfu hii kumesababisha mali za wakfu zilizowekwa waislamu hawajui ni kiasi gani zilikuwepo, kiasi gani zilizopo sasa, zilizouzwa na zilizofanyiwa mambo mengine. Kuna waislamu wengi wanataka kuweka mali lakini kwa sababu *commission* bado haijaundwa ni shida sana wanaogopa mali zao kupotea, hata mimi nataka kuweka wakfu.

Mheshimiwa Spika, katika hili tunaiomba Serikali kwa nia njema kwa sababu Serikali ina nia njema, hii sheria ipo, hawajaifuta, siyo tu kwamba hawajaifuta, wameitengenezea utaratibu mwingine mzuri ili kupitia katika Sheria ya Mirathi waislamu waweze kufaidika na hiyo Sheria ya Mirathi.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Wakoloni mwaka 1953 walikuwa na sheria hii, wala jambo hili siyo la dini, jambo hili ni la kisheria. Wakoloni ndiyo waliokuja na dini, wao ndiyo waliokuwa na dini, kwa nini waliweka utaratibu kwamba watu hawa waisalmu waishi hivi na watu hawa wa dini nyingine waishi hivi, hivyo tunaiomba Serikali kwamba kama Rais hajateua au kama kateua atuambie hao watu aliowateua katika hiyo *commission* ni akina nani na kwa mujibu wa ile sheria Rais anayo mamlaka ya kuchagua siyo chini ya watu nane na katika hao watu watano watakuwa waislamu, pia Rais atachagua Mwenyekiti atateua na Katibu. Vilevile Rais atachagua kwa mapenzi yake anayoyaona na Tume ile inaweza kukaa kwa muda ambao Rais atapenda. Katika hali hiyo tunaiomba Serikali hii Tume ianzishwe.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nataka kuzungumzia Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo. Sheria hii inafanya kazi vizuri sana kwa upande wa Tanzania Bara lakini kwa upande wa Zanzibar hii sheria ni tatizo.

Kwa mfano, fedha zikitoka Hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinakwenda katika Ofisi ya Makamu wa Rais, zikitoka Ofisi ya Makamu wa Rais zinakwenda Hazina Zanzibar, zikitoka Hazina Zanzibar zinakwenda kwa Makamu wa Pili wa Rais, zikitoka kwa Makamu wa Pili wa Rais zinakwenda kwenye ofisi ya Haji Omar Kheir, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, zikitoka hapo ndiyo ziingie katika Halmashauri za Majimbo. Sasa hii inashangaza sana, huo mlolongo hata hizo fedha zikifika inakuwa ni muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine baya zaidi ni kwamba pesa zile hazikaguliwi kwa sababu Mdhidhi na Mkaguzi wa Mahesabu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano hawezi ku-cross over akaenda kukagua Hazina ya Zanzibar. Kwa hiyo, kwa miaka mitano fedha zile au kama ushahidi kuna mtu alete ushahidi kama upo, miaka mitano fedha zile hazikaguliwa! Mwisho wa siku wanakuja watu kutoka katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na karatasi zao eti wanakagua fedha ambazo zinatoka katika Hazina ya Jamhuri ya Muungano na ni fedha za Muungano. Wala sheria haijasema mahali popote kwamba mwenye mamlaka ya kwenda kukagua zile fedha ni mtu fulani kwa hivyo zile fedha za Serikali zinapotea, Serikali yenyewe ipo na haina habari! Naomba Serikali kwenye jambo hilo walitazame vizuri na sisi tutaweka *input* zetu katika kuleta maerekebisho ya sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka kuuliza ambalo ni dogo tu, ile Mahakama ya Kadhi imefikia wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali tunataka mtuambie tu kwamba ile Mahakama ya Kadhi imeshindikana, haipo ama vipi kwa sababu ile mimi naithamini sana kwa sababu iliahidiwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015 ikasema kwamba ile ni moja katika mkakati wa Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba Mahakama ya Kadhi inasimama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (Makofi)

**SPIKA:** Huyo ni Ahmed Juma Ngwali. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Ally Hassan King. (Makofi)

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya Katiba na Sheria ili kuweza kuboresha mambo yetu ya kisheria katika nchi yetu ya Tanzania kwa maslahi ya wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, awali namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyingine kutujaalia kufika hapa kuja kuchangia mambo ya Watanzania. Watanzania hawa wana matumaini na sisi sana, kwa hiyo niwaombe

Waheshimiwa Wabunge tuchangie kwa mujibu wa mahitaji ya Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumesikiliza hotuba tofauti hapa, tumemsikia Mheshimiwa Waziri, tumesikia Kamati, tumewasikia na Wapinzani, siku zote sitegemei kwamba kutatoka jambo zuri upande wa Upinzani hata siku moja! Mheshimiwa Waziri angesema hapa kwamba jamani kuna Mungu aliyetuumba mimi naamini wangesema hakuna Mungu aliyetuumba, hicho ndicho kitu ambacho kwao wao ni cha msingi.

Katika hoja ambazo zinajadiliwa hapa, wengi wamejikita katika kuzungumza mahusiano haya katika Muungano, wako wanaosema kwamba Zanzibar ni koloni la Tanganyika, nilikuwa najiuliza huyu aliyesimama akasema yeye ni nyapara? Maana yake na yeye katokea Tanganyika sasa ikiwa kwamba Zanzibar ni koloni la Tanganyika ina maana kwamba yeye huyu ni nyapara. Ametumwa aseme hivyo. (Makofi/kicheko)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo huyu nyapara tunamwambia kwamba huu ni Muungano halali na Muungano unaojulikana, lakini kuna msemu husema kwamba nyapara huwa ana nguvu kuliko bwana na hao wanazungumza hivi maksudi kwa sababu nafikiri hawaelewi. Humu ndani tutatofautiana kwa mengi sana, hata tukiulizana uhuru umepatikana lini basi pia tutatofautiana humu kwa sababu tu ya kusema kwamba labda kuna upinzani na utawala, lakini tunachojadili hapa ni maslahi ya wananchi, kwa hiyo tujikite katika kuchangia vitu ambavyo vitafanya maslahi kwa wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna msemi mmoja pale kwetu Jang'ombe alisema hivi alitumia lugha moja; "kuendesha siyo lazima kupitia kwenye haja kubwa, inawezekana kuna wengine wanaendesha kwa mdomoni." Kwa hiyo tumewaona hao, kwa sababu leo tukitazama maneno ambayo yamezungumzwa, hiyo ni kuendesha kupitia mdomo au kwa jina la haraka haraka kuharisha. Kwa hiyo, tumepokea na tutamsafisha na atasafishika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la haki za binadamu. Suala hili la haki za binadamu na utawala bora kule kwetu iko Tume ingawa mwanzo ilikuwa Zanzibar, kuna tatizo kidogo lakini ikaja pakarekebishwa. Kwa hiyo, tunachoomba kwa sasa hivi ile Tume ya kule kwetu ifanye kazi vizuri sana, kwa sababu yako mambo ya kuzingatiwa na ni muhimu yafanyiwe kazi kwa haraka kwa sababu tunataka kuimarisha masuala ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tujue kwamba tumesaini Mikataba ya Kimataifa, hizo nazo zinahitajika kulindwa, hususan haki za watu ambao wanaishi katika Magereza, zimetajwa, kwa hiyo zifuatiliwe na zifanyiwe uchambuzi watu waweze kupewa haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ni cha muhimu sana kukizungumza hapa ni suala la Katiba Mpya. Mheshimiwa Waziri aligusia, amezungumzia katika kurasa za mwanzo kuhusiana na Katiba Mpya na ameeleza kwamba taratibu zimegusa sekta tofauti ikiwemo Tume zetu za Uchaguzi, tunaomba jambo hili lifanywe haraka ili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Rais alivyokuja kulihutubia Bunge hapa alizungumza kwamba atamalizia kiporo, kwa hiyo maana ya kiporo ni pale kilipofikia, kinapashwa moto tunamaliza. Nafikiri mchakato ulikwenda vizuri, palipobakia tuje tumalize kwa kuzihusisha Tume zetu hizo ili tuwe na Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie jambo lingine ambalo limezungumzwa hapa kuhusu vibaraka. Mimi nilishangaa sana kwamba kuna vibaraka kule Zanzibar ambao wameweka Serikali...

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Taarifa

### TAARIFA

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayeongea hapo. Amejaribu kutoa tafsiri ya neno kiporo kwa mujibu alivyomsikia Rais alivyozungumza, lakini tafsiri sahihi ya kiporo ni chakula kilichobakia asubuhi yake kinakuwa kimechacha na hicho hakifai kutumiwa tena kama ilivyo Katiba hii ambayo mliitayarisha imechacha na haifai Watanzania kuendelea na Katiba hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani, kiporo kina uhusiano gani na kuchacha? Mheshimiwa Ally King unapokea hiyo Taarifa? *(Kicheko)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika siipokei, hata ningesema kuna Mungu, yule angesema hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea. Alizungumzia habari ya vibaraka na akataja pande mbili kana kwamba hazina mahusiano kwamba je, tungewauliza na wao hawa ambao wamekuwa wana ndoa hii ya mkeka hii ambayo siyo rasmi watu wote wanaijua je, yeye anakuwa kama nani wakati anayasemea haya? Kwa sababu hata na yeye huyu mimi simkumbuki kama

labda ametokea katika Majimbo ya kule kwetu sijui atakuwa ni nani, lakini ndiyo wale niliosema kwamba nyapara siku zote huwa ana nguvu kuliko bwana. Amejariibu kulinganisha uhusiano, anakubali Mwafrika wa Tanzania kwamba ukoloni ulikuwa bora kuliko uhuru, huyu mtu sijui tumuite mtu wa aina gani? Lakini siku zote ukitaka kumjua mtu ambaye amezoea kulamba makombo ya sahani ya bwana siku zote atakuwa yuko chini yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hawa ni watu ambao wamezoea kulamba makombo ya sahani ya bwana, watakumbuka tu kwamba wao wanahitaji kulamba. Hakubali uhuru, mimi nashangaa sana tunamwita mtu kwamba utakuja kuwawakilisha wapinzani, unakuja kutoa hoja kama hizi, kwamba uhuru siyo bora kuliko ukoloni. Unauponda uhuru ambao umepatikana umerudi kwa watu wengi, Waafrika wenyewe una-support kwamba bora usingepatikana wewe ni mtu wa aina gani, kwa kutaja nukuu nyingi, kutaja nukuu nyingi siyo kujua, ni kwenda kusoma hata magazeti ukaja ukanukuu hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hicho tunajaribu kusema kwamba wajaribu kukiangalia na wakitathmini, upinzani siyo wa aina hiyo hapa tupo kwa ajili ya wananchi, tumeingia humu kwa sababu ya uhuru na tumo humu tunajadili kwa sababu ya uhuru. Uhuru na Muungano ndiyo uliotuleta hapa, utakapozungumza kinyume na hivi Watanzania watakushangaa, hawahitaji haya, ndiyo maana mnapokosa televisheni huumwa ninyi. Product kama hii ingerushwa kule kwenye televisheni watu wangeonaje kitu kama hicho? tujaribuni kufanya kwa ajili ya Watanzania wote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningelipenda kuchangia, tunajua kwamba zipo Tume, Haki za Binadamu, Tanzania tuna mahusiano ya Kimataifa, pia kuna masuala mengine ya kupata fedha pengine za kutoka nje katika kuhuisha masuala haya ya haki za binadamu. Tujaribu katika fedha zetu za maendeleo tuwe japo kidogo tunazipata ziwe zinatokana na sisi wenyewe, kuliko zaidi kutegemea kutoka kwa wafadhili. Bila ya hivyo tutakuja kujikuta kwamba wakati mwingine tunaweza tukaja tukakwama katika utekelezaji wa masuala ambayo tumejipangia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu, tumo humu katika Bunge kama chombo cha kutunga sheria, basi tujaribu tukubali ukweli kwamba Watanzania wanatutegemea na wanatukubali na ndiyo maana wametuchagua kwa hiyo tusiendeleze mambo ambayo yanaweza yakatuletea mfarakano ambao utakuwa hauna maana...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (Makofi)



**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali King, amenipa *vocabulary* mpya, anasema UKAWA ni ndoa ya mkeka, nimenukuu tu jamani. Sasa twendeni CHADEMA Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, tafadhali! (Kicheko)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kupongeza hotuba nzuri sana aliyotoa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambayo kusema kweli kama tuna Serikali sikivu, inapaswa itoke hapo kwamba imepata somo na iende iwatendee Watanzania haki. Imekuwa ni mazoea kuchukulia michango ya wapinzani kama mzaha, lakini mwisho wa yote tunaona *dublication* ya mambo yale yale ambayo tayari yamekuwa yametolewa tahadhari na upande wa Upinzani. (Makofi)

Mheshimiwa Wenje akiwa Bungeni hapa, aliitanabaisha Serikali madudu gani alikuwa anayafanya Ndugu Kabwe kule Mwanza, ninyi mkaona tu kwamba ni mchezo wa kuigiza, lakini juzi tu Makonda akampandia mtu yule yule na akalalamika kwa Rais na Rais akamfukuzia mtu kwenye jukwaa la shughuli nyingine kabisa ya kuzindua daraja. Jamani kuweni *serious* na hoja zinazotolewa na Upinzani.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, msomi Mwakyembe na AG, kweli mpo pale kwa ajili ya kumsaidia Rais kama wasomi wazuri wa sheria ambao Taifa hili limewaamini mmeteuliwa kwa usomi wenu, mnakaa katika Baraza la Mawaziri kumshauri Rais kwa mambo yanayohusiana na sheria? Inapokuja kutoka kitu ambacho amekizungumza kwa kina Mheshimiwa Lissu ni aibu! Huo ndiyo ukweli maana yake kuna mtu tumbo limemletea shida barabarani akachepuka aende pembeni akaanza kujisitiri kidogo ili tumbo liwe *released* kidogo, sasa kwa kuwa watu wanapita anajifunika uso anafikiri hawamwoni kumbe mwili wote uko nje.

Mheshimiwa Spika, mambo haya ninaamini ukweli mnaujua, lakini pamoja na usomi wenu mnapotosha mambo maksudi kwa sababu ya hulka za kisiasa. Matokeo yake Rais mnamuweka katika matatizo makubwa, mnamweka katika *tension* ya ajabu, mpaka juzi, kwenye sherehe za walimu anasema anajuta kwa nini alivuta fomu, matokeo ni haya! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama Serikali inaendeshwa, bila *instrument*, Rais anajikuta maskini anafanya kila kitu. Kuagiza sukari yeye, kuipanga sukari yeye, wakati kuna Waziri mhusika wa shughuli hii, ni kwa sababu watu aliowateua wote kama yeye amejikuta katika mfumo huo, anakwenda kwa *decree*, ikizungumzwa majipu, kuanzia juu kwa Rais, Waziri Mkuu nani wote, majipu kila mmoja yuko kwenye majipu. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, akisema sasa zoezi la kubaini watumishi hewa kila mtumishi kuanzia Waziri mpaka chini hakuna shughuli nyingine ni kutafuta watendaji hewa. Tutaendesha hii Serikali kwa *decree* mpaka lini? Hapa ndiyo umuhimu wa *instrument* unapokuja.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa Dar es Salaam katika ofisi ndogo za Bunge, wakaja wasomi ambao walikuwa wanajaribu kutupa *orientation* ya namna ya ku-*scrutinize* bajeti na namna ya kupanga bajeti, niliwauliza kitu kimoja, niliwaambia nchi hii uchumi wake unafanana na uchumi ulioanza kule kwenye nchi za Taiwan, Kuwait, Botswana, Vietnam, Rwanda, Singapore, Malaysia, Hong Kong na nchi nyingine, lakini leo hii hata Vietnam walikuja kuchukua mbegu ya korosho huku sasa hivi ni mzalishaji wa korosho dunia nzima. Nikawauliza hawa wasomi niambie muwe wakweli, hivi tatizo la mipango yenu tangu mwaka 1961 mpaka leo mwaka 2016, mipango yenu hakuna unaotekelezeka kutupa uchumi ambao ni endelevu wenye mashiko. Matatizo ni usomi wenu, vyuo mnavyosoma, walimu wanaowafundisha au matatizo ni yapi?

Mheshimiwa Spika, wale mabwana waliniambia Mheshimiwa Lwakatare wewe yaache tu hayo bwana. Lakini ninachofahamu tatizo ni mfumo, mfumo wa kiutawala hata angekuja malaika mwenye mipango mizuri ya uchumi ukamtumbukiza kwenye Chama cha Mapinduzi, *wallah* yote inakuwa mguu chini, mguu pande, mna matatizo! CCM ndiyo tatizo, mnawapotosha watu wa mipango yetu, mnawapotosha hata wanasheria.

Mheshimiwa Spika, najua huyu siyo Mwakyembe halali tunayemjua wa Chuo Kikuu, huyu ni wa kutengenezwa, amechongwa kutokana na mfumo uliopo, hawezi kutetea, huwezi kukurupuka, hawezi kuchomoka, hata AG hawezi, CCM *is a problem*, angekuwa bado babu yupo kule Loliondo tungewapeleka mkapate kikombe cha babu. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, si mnaona anavyobonyeza eeh, upande wa pili wanafanya fujo? Wamenyamaza wametulia na ninyi muwe hivyo hivyo.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Ahsante, nitunzie dakika zangu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lwakatare malizia.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikiridhia mikataba na tumekuwa tunaletewa mikataba ya kuridhia na najua itaendelea kuletwa, ningeomba basi tunapoletewa mikataba, tuwe na *political will*, tuwe na utashi ambao ni wa dhati, na ambao unanua kuwasaidia Watanzania pindi mikataba hiyo inaporidhiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikataba ambayo imewahi kuridhiwa, kuna Mkataba wa nchi za SADC wa Utawala Bora na Uchaguzi wa Kidemokrasia ambao kimsingi pamoja na kusainiwa na viongozi wetu haujawahi kuletwa hapa ndani ya Bunge kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri na AG anatoa ufafanuzi, ni lini mnaleta mkataba huu uridhiwe? Najua hamtaki huu mkataba unayozungumzia masuala ya utawala bora na kuchungana katika demokrasia kupiga kura na uchaguzi hamtaki, ndiyo maana mwendelezo wa kuiba kura umeendelea, ndiyo maana matendo yanayofanyika Zanzibar wala hamuoni haya, mnayafanya makusudi kwa sababu ya kisingizio kwamba hamjaridhia mikataba ya namna hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niwaeleze ukweli siyo kwamba Watanzania pamoja na kutowaonesha *live* nini tunachoongea siyo kwamba hawajui, ninawapongeza Wabunge wote ambao sasa wameamua kutafuta njia mbadala. Sasa hivi *ma-group* yote yanapata *live*, mambo yanayoendelea humu, hata CCM kuna *ma-group* ambayo tunaona na wao wana-*post* hotuba zao ili watu wajue wanasema nini, huo ndiyo unafiki uliopo humu.

Kwa hiyo, suala la kuzuia habari msifikiri kuzuia *live coverage* ya tv Watanzania hawapati taarifa! (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Hii ni kengele ya kwanza Mheshimiwa.

**SPIKA:** Ni kengele ya pili kaka tunakushukuru, umesahau kuunga mkono hoja, ahsante sana. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, karibu tafadhali.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kusema machache kutokana na hotuba hii ya Waziri inayohusu Katiba na Sheria. Ninampongeza Waziri kwa yale yote ambayo yameelezwa katika kitabu chake na mimi kama mmoja wa wadau wa kitabu hiki basi napenda nimshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kama kawaida atika Bunge letu siku hizi huwa kuna hotuba ya Waziri na ile ya Kambi ya Upinzani. Tunaziangalia na tunazisikiliza nilikuwa nikisikiliza sana hotuba ya Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani, na nimekwenda kwenye ukurasa wa nane wa kitabu chake, hali kadhalika nimesogea katika ukurasa wa tisa, yale ambayo yamezungumzwa humu, ni mambo ambayo tulikuwa tunakumbushana tu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ukiangalia ukurasa wa nane kuna suala kwamba limezungumzwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano kazumgumzwa Rais wa Zanzibar katika Jamhuri ya Muungano, sote tunafahamu hivyo na tumefahamu hivyo kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Katiba yake inasema wazi kwamba kutakuwa na Serikali mbili ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Moja ya Zanzibar na ile ya Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia Katiba hiyo inasema kutakuwa na Maraisi wawili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mmoja wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivyo ndivyo Katiba ilivyosema wala hatuna haja ya kukumbushana kwa sababu sote tunajua, wala sikuona faida ya kuandikwa kwenye kitabu hiki kwa sababu ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa tisa kuna mtu mmoja ametangazwa anaitwa Ghassany katika kitabu chake, amezungumzia kuhusu Kwaheri ukoloni, kwaheri uhuru wa Zanzibar na karibu Mapinduzi. Hatuna haja ya kukumbushana, kwa sababu aliyeandika kitabu hiki alijua kwamba baada ya Mapinduzi, ukoloni kwaheri, alikuwa anajua kwamba baada ya Mapinduzi, na wale waliotawala pia kwaheri, lakini yakakaribishwa Mapinduzi!

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya kawaida na mimi namshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba na haya anayafahamu. Lakini lingine ambalo limezungumzwa hapa na wenzetu wa Kambi ya Upinzani, wanasema kwamba Tanganyika, wametumia neno Tanganyika, siyo vibaya! wametumia neno Tanganyika kwamba ilishiriki kikamilifu katika Mapinduzi ya Zanzibar hakuna asiyejua katika ulimwengu huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wanzanzibar tunajua kwamba Mapinduzi ya Zanzibar yamechangiwa sana na ndugu zetu wa Tanganyika, yalichangiwa kwa sababu maalum, siyo kwa kubahatisha hapana! Juzi nilisema hapa mimi waliokwenda Zanzibar hawakutokea Dubai, walioanzisha Kisiwa cha Zanzibar hawakutoka Oman, walioanzisha Kisiwa cha Zanzibar hawakutoka Qatar, walioanzisha Zanzibar wametoka Bagamoyo, wametoka Tabora, wametoka Mtwara na sehemu nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hawa ndiyo walioanzisha Zanzibar, miongoni mwa hao walioanzisha Zanzibar wengine humu babu zao wamo, sasa mimi nashangaa sana kusema kwamba Tanganyika imesaidia kweli Tanganyika imesaidia Mapinduzi ya Zanzibar, itaendelea kusaidia Mapinduzi ya Zanzibar wakati huu Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wamesaidia tumeweka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wanaendelea kusaidia Zanzibar, wataendelea kusaidia Zanzibar kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na atakayejaribu kuigusa Zanzibar atajua Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tumepindua kuondoa ukoloni, na tunaendelea kulinda Mapinduzi makusudi wala hatuwezi kumpa nafasi, mtu ambaye ana uchu wa madaraka haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na viongozi wengi pale walafi wa madaraka wengi tu, lakini tumekuwa na viongozi wengi ambao wanatumwa siyo mara moja, siyo mara mbili kuna historia pale ya Mapinduzi yaliyokuwa yanataka kufanywa Zanzibar mara 23, majaribio ya Mapinduzi hayakufanikiwa! Hayakufanikiwa kwa sababu Muungano wetu uko imara na hatuwezi tukampa mtu madaraka mwenye ulafi.

Mheshimiwa Spika, nitawapa mfano hai tu, hapa wenzetu wanazungumza sana na juzi nimemsema Maalim, sawa Maalim lakini kwa Zanzibar Maalim ni Maalim tu na kwa sababu tumekaa naye Maalim tunajua Maalim yukoje.

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu leo bahati mbaya Mheshimiwa Ally Saleh hayupo hapa, Maalim alikuwa anasoma Lumumba, pale Lumumba palikuwa na timu ya mpira, palifanyika uchaguzi wa uongozi wa timu ya mpira Maalim aligombea ukapteni, lakini hachezi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani! Hiyo ndiyo dira iliyotunesha Maalim yukoje, utakuwaje kepteni wa mpira wewe mwenyewe huchezi? Haiwezekani, kwa sababu alitaka na yeye awemo akagombea ukepteni watu wakampa, watu wanakwenda Lumumba kucheza yeye amekaa nje, kepteni huyo? Hilo ni matatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, tunapokaa tukasema Mapinduzi tutayalinda, tutayalinda kweli na tutawapa watu wanamapinduzi.

**MBUNGE FULANI:** Kwa Jeshi?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Tatalinda kwa Jeshi, tatalinda kwa Polisi, tatalinda kwa chochote, hii ndiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninyi mmepata kuona wapi Mapinduzi yakalindwa kwa kanga, utalinda Mapinduzi kwa kanga? Mapinduzi tumepindua tumekwenda Jeshini tukachukua mashoka tukalinda na tutaendelea kulinda.

Mheshimiwa Spika, nabaki hapa kwenye kiongozi mlafi hatuwezi hata wale ndugu zangu Wapemba tukitembea kule huwa wanatuambia kwa lugha ile ya kwao kipemba. Hivi mwataka kumpa Urais mtu asiye nyumba kwao au ugenini? Umesikia lugha? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwa Rais kama huna mke haiwezekani, umepata kuona wapi? Unataka tukupe nchi huna nyumba, haiwezekani!

**MBUNGE FULANI:** Wewe unaye?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Kwa hiyo, tunachosema Mapinduzi ya Zanzibar yatalindwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tena yatalindwa kwa nguvu zote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa nazungumza suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa jinsi ilivyokuja Zanzibar, kila mtu Mzanzibar anajua, mpaka hawa ndugu zetu hawa wanajua, imekujaje Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama juzi nilivyotoa mfano nasema walikaa watu wawili wakazungumza peke yao, CUF wanashindwa kumuuliza Maalim Seif umezungumza nini na Mheshimiwa Amani mtoto wa Mama Fatma? Wanashindwa kumuuliza, waulize mpaka leo!

Mheshimiwa Spika, hiyo haitoshi imekuja Serikali ya Umoja wa Kitaifa wakati wa kampeni, unaleta posters zinasema Ally Hassan Mwinyi anasema ndiyo, Mkapa anasema ndiyo, wewe unasemaje, huyo Mheshimiwa Ally Hassan Mwinyi kaulizwa lini? Hajaulizwa wanasema Salmin anasema ndiyo kaulizwa lini na mwenyewe akasimama akasema hamjaniuliza, lakini Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu siyo Maalim juzi kawafanya kitendo hawa, kawafanya kitendo kibaya sana, kwa sababu kajua kama akienda hospitali atalipwa milioni 350, halafu atasema kwamba uchaguzi hawa wasiende, hawakuenda katika uchaguzi, mambo ya ajabu sana.....

**MBUNGE FULANI:** Semea wananchi wako!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Wanajutaa!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Umoja wa Kitaifa imekufa. Naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. Waheshimiwa Wabunge, naona Bunge limechemka kuna nini? (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho linatolewa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambaye ni Katibu wa TAPAFE (Chama cha Wanamazingira Wabunge Huru) anaomba wale wanachama wa TAPAFE muwe na kikao kifupi katika Ukumbi wa Msekwa, tutakapoahairisha shughuli za mchana huu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge uchangiaji utaendele jioni na tutaendelea na Wizara yetu kama kawaida jioni ya leo, kwa jinsi hiyo naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017, majadiliano yanaendelea.

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 - Wizara ya Katiba na Sheria**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala. Majina niliyonayo hapa nitayasoma kwenu. Tunaanza na Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Valentine Magige.

**MHE. OMAR M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikushukuru kwa kunipa fursa jioni ya leo niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Sheria. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri husika wa Wizara hii kwa bajeti nzuri sana ambayo ameiwasilisha kwa siku ya leo. Bajeti hii imechukua mambo mengi sana ambayo yalikuwa ni kilio cha wananchi, nikiamini kabisa kwamba imeweza kujibu kilio cha wananchi wa maeneo mbalimbali, hususan wa Jimbo la Kilindi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakililia Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua zake anazochukua za kutumbua majipu.



Vilevile nimpe moyo kwa changamoto anazozichukua kwa wale watendaji ambao kwa muda mrefu wamekuwa ni matatizo ya nchi hii, ninaamini kabisa Waheshimiwa Wabunge na hata wale wa upande mwingine wanajua Mheshimiwa Rais anachukua msimamo ulio sahihi kabisa. Mambo haya ni ya msingi tukiweza kuyazungumzia kwa mustakabali wa nchi yetu hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze moja kwa moja kuchangia hususan kwenye Mahakama zetu. Tanzania hii ina Mahakama za Mikoa, Mahakama za Rufaa na Mahakama za Mwanzo, lakini ninaamini kabisa changamoto za Mahakama hasa hizi za Mwanzo na Wilaya zimekuwa ni kubwa sana, kwa maana kwamba mahakama nyingi zimekuwa chakavu na hazijafanyiwa ukarabati wa muda mrefu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna maeneo ambayo yana Wilaya lakini hayana Mahakama za Wilaya. Mfano katika Jimbo langu la Wilaya ya Kilindi ni takribani miaka 13 toka tumepata Wilaya lakini hatuna Mahakama za Wilaya. Jambo hili limekuwa ni kero kubwa sana kwa sababu wakazi wa Jimbo la Kilindi wamekuwa wakifuata huduma hii ya Mahakama kwa takribani kilometa 200 au 190 kutoka Wilaya moja hadi Wilaya nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi kwa ujumla ina changamoto nyingi sana za migogoro hasa ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, unakuta kwamba, jambo hili limekuwa ni kero ya muda mrefu na hata Mbunge aliyepita alikuwa akilipigia kelele suala hili, lakini ninamshukuru Mheshimiwa Waziri husika kwenye bajeti yake ameweza kuliona hili na miongoni mwa Wilaya 12 ambazo zimetengewa hela kwa ajili ya kujengewa Mahakama ya Wilaya basi na Wilaya ya Kilindi imepata fursa hiyo. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni suala la Mahakama hizi za Wilaya kutokuwa na Mawakili wa Serikali. Mawakili wa Serikali wamekuwa ni msaada mkubwa sana kwa wananchi ambao hawana uelewa wa elimu ya sheria. Nashauri hususan kaka yangu Waziri, Mheshimiwa Mwakyembe kwamba muda umefika sasa hivi wa kuwa na Mawakili katika kila Mahakama ya Wilaya, kwa sababu watu hawa wanawasaidia wananchi wasiokuwa na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme jambo moja, Mawakili katika kitabu chako umeeleza hapa kwamba mna mpango wa kupunguza idadi ya mrundikano ya kesi, kwa maana ya kwamba *zero case backlog!* Mheshimiwa Waziri hebu nikuulize swali moja pengine utanipa maelezo wakati unajibu hoja hizi kwamba unatarajia Mahakama ya Wilaya *at least* iweze kujibu kesi 250 kwa mwaka, sasa Hakim wa Wilaya ambaye anabeba Wilaya mbili kwa maana ya Wilaya ya Kilindi na Wilaya ya Handeni anawezaje kutatua kesi hizi kwa kipindi cha mwaka mmoja? Haya ni mambo ya msingi kabisa na unaweza tu ukaenda

ukauliza pale Mahakama ya Wilaya ya Handeni kwamba, Hakimumu ana idadi kiasi gani ya kesi za kutoka Wilaya hizi mbili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba wakati tunasubiria kujenga Mahakama ya Wilaya, sisi tunayo majengo katika Jimbo la Kilindi tunaweza tukapewa Hakimumu wakati tunasubiri jengo likijengwa. Mimi nadhani fursa hii ni nzuri, ili tuweze kuwapa haki wananchi wa Wilaya ya Kilindi. Ninadhani changamoto hii haipo katika Jimbo langu tu, ipo katika Wilaya mbalimbali ambazo hazina Mahakama za Wilaya, nikiamini kwamba wananchi wanayo haki ya kuwa na huduma hizi za kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuchangia siku ya leo ni suala la Serikali kupoteza kesi. Serikali inapokuwa inawashtaki watu mbalimbali mara nyingi huwa inapoteza kesi! Sasa tunatakiwa tujiulize sababu za msingi ni kwa nini Serikali inapoteza kesi? Haya ni mambo ya msingi kwa sababu wakati mwingine Serikali inashtaki mambo ambayo watu wamehujumu nchi! Tuchukulie mfano wa kesi ya samaki wale, Serikali imepoteza na inatakiwa kulipa fidia. Sasa ni nini kilichosababisha Serikali ikapoteza kesi hiyo wakati Serikali inao wataalam, inao Waendesha Mashitaka wa kutosha na wenye elimu yakutosha! Nadhani imefika muda sasa tuangalie utaratibu mzuri wa namna gani tunaweza kupata watu ambao wamebobea wanaoweza kuishauri Serikali katika mambo ya kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulichangia ni juu ya bajeti ya Wizara hii. Mheshimiwa Waziri husika wa bajeti hii amezungumza sana kwamba ana changamoto ya bajeti, nadhani kwa sababu Wizara hii inahusika na mambo ya sheria na mambo ya mahakama ifike wakati kwamba, Wizara hii yenyewe tuiongezee hela ili tuweze kuondokana na changamoto mbalimbali kwa ajili ya kutatua kesi za wananchi na kutoa haki kwa wananchi wa Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuchangia katika upande wa Mahakama za Mwanzo. Nichukulie mfano katika Jimbo langu la Kilindi, Mahakama za Mwanzo ziko chache sana! Jimbo lenye Kata 21 na vijiji visivyopungua 102, Mahakama za Wilaya nadhani ziko kama tatu kama siyo nne! Maana yake ni kwamba wananchi wanakosa haki zao za kimsingi. Kwa hiyo, imefika wakati Mheshimiwa Waziri husika ahakikishe kwamba ule mpango wa kuwa na Mahakama za Mwanzo katika kila Kata, basi mpango huo Serikali kwa dhati ya moyo wake ihakikishe kwamba mahakama hizo zinaanzishwa na zinakuwa na Mahakimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ni juu ya idadi ya Mahakimu katika Mahakama zetu. Sehemu nyingi sana utakuta utakuta kwamba, hatuna Mahakimu, lakini tunacho Chuo cha Mahakama

Lushoto! Kwa nini Serikali isingetia nguvu pale tukahakikisha kwamba wataalam wengi wanapatikana, Mahakimu wanapatikana, ili Mahakama zetu ziweze kuwa na Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu kuna uanzishwaji wa Mahakama ya Mafisadi ambayo inatarajiwa kuanza mwaka wa fedha huu. Jambo hili nataka niipongeze sana Serikali hususan Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wa dhati wa kuanzisha Mahakama hii. Mimi naamini kabisa kwamba muda umefika sasa hivi wa kuwa na Mahakimu wa kutosha katika kila Wilaya, kila Kata, ili wananchi wetu waweze kupata haki za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuchangia juu ya ukusanyaji wa maduhuli katika mahakama zetu. Nadhani utaratibu uliopo sasa hivi ni mzuri lakini inabidi uboreshwe sana. Uboreshwe kwa sababu mahakama hizi zina mahitaji mengi sana, wakitegemea OC ya Serikali maana yake uendeshaji wa mahakama hizi hautakwenda vizuri. Mimi ni imani yangu kwamba Serikali imesikia haya na imesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali tukiamini kwamba muda umefika wa kuweza kutoa haki kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo machache, naomba kuunga mkono hoja ya bajeti hii. Ahsante. (Makofi)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, Mwongozo!

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambayo inampa mamlaka Mbunge yeyote kusimama kama hakuna Mbunge mwingine anayeongea kupata Mwongozo wako kutokana na maneno makali yaliyotolewa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, akizungumzia kwamba Zanzibar iko kwenye kutawaliwa leo hii na kwamba Serikali yetu inaongozwa kwa mujibu wa taratibu za kiimla na pia kuhusiana na uchochezi ambao amekuwa akiutumia katika hotuba yake yote kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kama hizi ndiyo taratibu za Bunge na vinginevyo namtaka Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani aweze kufuta maneno yote ya kichochezi aliyoyatoa katika hotuba yake. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo unaombwa ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo ambalo limetokea mapema linaruhusiwa au haliruhusiwi. Kwa hiyo, kimsingi ni Spika ndiye atakayeamua katika Mwongozo ulioutoa, naona umeenda mbele na kuanza kupendekeza nini cha kufanya!

Waheshimiwa Wabunge, nitatoa huo Mwongozo hapo baadaye. Tunaendelea!

Mheshimiwa Joseph Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Kiteto Koshuma, halafu Mheshimiwa Anna Joram Gidarya ajiandae!

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii ya Sheria na Katiba ninayo machache sana. La kwanza imenipa faraja sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuonesha kwamba fedha za ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Sikonge zipo na akataja na kiwango kabisa. Mimi namuomba Mheshimiwa Waziri asimamie kwa sababu fedha hizo ni za mwaka huu wa fedha wa 2015/2016 ili zifike haraka, ili kusudi hiyo Mahakama ianze kujengwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimejitolea kuruhusu ofisi ya zamani ya Mbunge iwe wazi kwa ajili ya matumizi ya Mahakama ya Wilaya ya dharura. Niliachia hiyo ofisi tangu mwezi wa 11 mwaka jana, lakini mpaka sasa hivi Hakimu wa Wilaya hajahamia! Wakati anafanya majumuisho Mheshimiwa Waziri naomba aniambie kwamba Hakimu wa Wilaya atahamia lini? Labda wiki hii au wiki ijayo? Ili kusudi wananchi wasiendeleo kutaabika! Wanatumia fedha nyingi kwenda Tabora kwa ajili ya kuhudhuria kesi zao au kesi za ndugu zao na hakuna sababu kwa nini waendeleo kupata shida namna hiyo wakati ambapo Mbunge wao nimejitolea ofisi iliyokuwa ya zamani ya Mbunge, itumike kwa ajili ya Hakimu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hata polisi wanatumia pesa nyingi sana, gharama kubwa kwenda kupeleka watuhumiwa Tabora wakati ambapo nimeachia ofisi! Ninaomba sana Wizara hii iweke msisitizo wa dharura kabisa ili Mahakama ya Wilaya ya Sikonge ianze kwa dharura hata wiki ijayo, wasisubiri mpaka majengo yakamilike! Najua majengo yatachukua muda mrefu, inawezekana wakianza ujenzi mwezi huu au mwezi ujao wanaweza wakachukua miaka miwili kukamilisha majengo, miaka miwili nadhani haitavumilika kuendelea kusubiri wakati maeneo ya kuanzia kwa dharura yapo, hilo lilikuwa jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili napenda kuzungumzia maeneo ambayo sheria zinakinzana. Ninajua sekta zinahusika lakini mratibu mkubwa wa

sheria katika nchi yetu ni Wizara hii. Ninaomba sana ichukue uongozi wa kusoma sheria zote, ili kusudi maeneo yote ambayo yanakinzana, unakuta sheria hii inakinzana na sheria nyingine, zifanyiwe *harmonization* mapema iwezekanavyo ili kuondoa utata wa aina yoyote ambao unaweza ukajitokeza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni masuala yanayohusiana na Sheria ya Ununuzi. Tuliahidiwa kwamba sheria ile itakuja ili kusudi tuifanyie marekebisho lakini bado mpaka sasa hivi naona haijaletwa! Sikuona vizuri kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri jambo hilo limeripotiwa! Kwa sababu sheria hiyo ni ya msingi sana na imekuwa ni sehemu kubwa ya malalamiko kwa watekelezaji wengi kuhusu kuchelewesha kazi na mambo mengine ninaomba sasa Wizara hii ichukue hatua za makusudi ili kusudi sheria hiyo ifanyiwe marekebisho haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya mambo ambayo kwenye sheria ile hayapo, kwa mfano, masuala yanayohusu miradi mikubwa ya miundombinu, *turnkey projects*. Kwa mfano, ujenzi wa Reli ya Kati, ujenzi wa barabara kuu kama kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma! Hizo ni *turnkey projects* ambazo unaweza ukakaribisha sekta binafsi zikaingia kwenye *investment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya masuala yanayohusu *turnkey projects* hayamo kwenye hii sheria na yamekuwa yakisababisha utata mkubwa wakati mwingine Wizara zimekuwa zinaambiwa hazijafuata taratibu za manunuzi, lakini unakuta ule utaratibu haujaelezwa vizuri kwenye hiyo sheria

Mheshimiwa Naibu Spika, Kimataifa baadhi ya taratibu za *turnkey projects* zinapingana na Sheria ya Ununuzi ya kwetu hapa Tanzania! Nilikuwa naomba mambo kama hayo yafanyiwe haraka utaratibu ili kusudi tusiachwe kama kisiwa Tanzania twende pamoja na nchi za wenzetu ambazo zimeingiza taratibu za *turnkey projects* kwenye sheria zao za manunuzi ili tuweze kufaidika na uwekezaji mkubwa wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kulizungumzia kwenye sekta hii ya sheria ni idadi ya watumishi katika Idara ya Mahakama. Maeneo mengi sana hata Mahakimu tu wa Mahakama za Mwanzo ni shida! Kule kwetu Sikonge tumejitolea Kata tano zianzishwe Mahakama za Mwanzo, lakini wanatuambia sijui kama watapatikana Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo!

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa tuna Tume ya Utumishi wa Mahakama na amepewa kazi bwana mkubwa mmoja ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa TAMISEMI, yuko pale! Nilikuwa ninadhani labda hawana fedha, lakini sijaona humu kama fedha imeombwa kwa ajili ya watumishi! Naomba sana

Serikali ichukue hatua za maksudi kuhakikisha kwamba Watumishi katika Idara ya Mahakama wanapatikana na wanakuwa wa kutosha. Hiyo ni pamoja na Majaji, pamoja na Mahakimu wa Mahakama za Wilaya, Wasajili, ile *schedule* yote ya utumishi katika Mahakama ikamilike ipasavyo ili kusudi kama kesi kusikilizwa zichukue muda mfupi, kusiwe na muda mrefu wananchi wanasumbuliwa kusubiri kesi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo tu na mimi naunga mkono, ahsante sana. (Makofi)

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Pili, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia fursa hii ili niweze pia kuendelea kuchangia katika Hotuba hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Ninawashukuru pia wanawake wa Mkoa wa Mwanza ambao waliniamini na kunipa kura nyingi na kuweza kuwakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba kuchangia kwa upande wa Sheria ya Ndoa. Katika Sheria ya Ndoa nimeangalia na kuona kwamba kuna upungufu ambao unafanya sheria hii kukandamiza haki za wanawake katika Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kuna *contradictions* ambazo zinatokea katika Sheria ya Ndoa. Mtoto wa kike katika sheria hii anaweza akaolewa akiwa na umri wa miaka 16 lakini ukija katika Sheria ya Watoto (*Children Act Law*) mtoto anajulikana ni mtoto mwenye umri wa kuanzia sifuri hadi miaka 18, lakini kuna sheria ya *Sexual Offensive Act*, sheria hii pia na yenyewe inakuambia kwamba mtu ambaye anafanya mapenzi na mtoto mwenye umri chini ya miaka 18 amefanya kosa la jinai. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata wakati mgumu sana kwamba hizi sheria tatu ambazo nimeziangalia zinaleta *contradictions* na zinamgusa mtoto wa kike, kwa sababu mimi ni mwakilishi wa wanawake siyo tu wa Mkoa wa Mwanza bali ni mwakilishi wa wanawake Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaniuma sana kuona kwamba mtoto mdogo, tayari umemuita ni mtoto katika *Children Act Law*, mtoto ni wa umri chini ya miaka 18 lakini kwenye Sheria ya Ndoa unampa mwanaume mamlaka ya kumchukua huyu mtoto asiyekuwa na hatia, ambaye *psychologically* akili yake bado haijaweza kufikiria lolote kuhusiana na suala zima la ndoa. Lakini umempa



mamlaka mwanaume aweze kumchukua mtoto huyu na kumweka unyumba kitu ambacho naona ni unyanyasaji kwa mtoto wa kike. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, ninaitaka Serikali itakapokuja kujibu hoja za hotuba yake basi ije na kauli moja, kwamba inasema nini kuhusiana na hizi *contradictions* ambazo zinatokea katika hizo sheria tatu ambazo nimeziainisha hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na kesi kurundikana katika mahakama zetu. Kesi zimekuwa ni nyingi sana zinarudikana kwenye mahakama na kufanya mahabusu kuwa wengi kwenye mahakama zetu. Lakini ukiangalia katika kesi hizo siyo wote wanaoenda kushtakiwa mahakamani wana makosa, wengi wao wamekuwa wakibambikwa kesi. Mfano mtu kaiba kuku lakini kwa sababu kuna fisadi mmoja ambaye amejificha *somewhere* anataka kumtumia huyu mtu ambaye ameiba kuku tu basi ahukumwiwe kwa kesi ya kuiba kuku, lakini mtu huyu anapewa kesi ya mauaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasikitisha sana unajiuliza Taifa letu la Tanzania tunaelekea wapi. Kwa uchungu mkubwa sana ninaiomba Serikali ianze kuangalia kesi hizi, japokuwa kwa juhudi za Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli amelikemea sana suala hili la kesi kurundikana mahakamani hadi akaweza kuwaongezea Majaji fedha kwa ajili ya kuweza kuendesha kesi, lakini bado kesi zinaendelea kurundikana mahakamani na kesi nyingi kwa kweli ni zile za kusakiziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naiomba Serikali itoe tamko kwa vyombo hivi vya kisheria ambavyo vinasimamia *reinforcement* ya sheria kwamba ni nini kinatakiwa kifanyike kwenye kesi ambazo ziko mahakamani ili kuweza kupunguza watuhumiwa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni kuhusiana na utoaji wa haki na utawala wa sheria. Kwa masikitiko makubwa sana na hata kama ni kulia ningeweza kulia mbele ya Bunge lako Tukufu, wanawake wamekuwa wakinyanyasika sana, mwanamke utakuta amepigwa na mume wake, anakwenda kushtaki polisi mwanaume anapelekwa mahakamani, lakini bado mwanamke huyu anaoneka kwamba ilikuwa ni halali kwa mwanaume kumpiga huyu mwanamke kana kwamba ni ngoma yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ijaribu kuangalia suala zima la wanawake kunyanyasika katika utoaji wa haki zao. Unakuta kwa mfano, hapa sijui ni sheria gani inahusika lakini unakuta mwanamke ameolewa na mume wake kwa ridhaa yake na wanaishi vizuri, baada ya muda mfupi mwanamke huyu na mwanaume wanaamua kutengana kwa sababu labda wametofautiana baadhi ya vitu. Katika utofauti huo basi unakuta mwanaume



anapofika Mahakamani kwa ajili ya kutoa talaka, mwanamke huyo anapopewa talaka anaambiwa nenda halafu mali zote anaachiwa mwanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasikitisha sana kwa sababu ni wanawake wengi sana afadhali hata wale ambao wamejaliwa basi hata kusoma wamepata elimu wanajua ni jinsi gani wataweza kujikwamua kuondokana na unyanyasaji huu ambao tunaupata kutoka kwa wanaume. Lakini vipi wale kundi kubwa la wanawake ambao hawajakwenda shule? Hawajui ni nini wafanye?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika waweze kuangalia dawati la kijinsia ambalo lipo lakini kiuhalisia halina kazi linayofanya. Ninaitaka Serikali sasa ianze kuangalia masuala ya kusaidia utoaji wa haki kwa wanawake na kuhakikisha kwamba wanawake wote wanapatiwa haki zao. Kwa sababu wanawake wengi wamekuwa wakinyimwa haki zao hata pale wanapofiwa na waume zao. Wajane wameteseka, wamenyang'anywa mali na kuondoka bila chochote, wanabaki wanahagaika mtaani wakati ndugu wamebeba mali zote wameondoka wanajisifia mtaani kwamba wanazo mali halafu mwanamke huyu anaanza kukanda maandazi, anauza karanga, anafunga ufuta ili mradi maisha yake yaweze kusogea. Inasikitisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea kuhusiana na kesi za Serikali. Inasikitisha kwamba Serikali inakuwa na kesi nyingi sana, inashitaki watu kwa kufanya makosa, lakini kesi zote *almost 99 percent* ya kesi za Serikali inapoteza ama Serikali inashindwa. Ninaitaka Wizara ije iseme, itoe tamko lake kwamba kwa nini Serikali inapoteza kesi nyingi? Ni kwa sababu gani kesi ziwe nyingi Serikali inashindwa? Kesi 1000 Serikali inashinda kesi mbili tu, inasikitisha sana! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumaliza kwa kuongelea kuhusiana na suala zima la majengo ya mahakama ambayo yamechakaa sana. Naomba Serikali katika bajeti yake iangalie ni namna gani itaweza kusaidia kufanya *renovation* ya majengo ya mahakama Tanzania nzima kwa sababu ya kuweza kuwasaidia wananchi kupata haki zao lakini pia kuongeza watumishi katika Mahakama zetu. Kwa sababu upungufu wa watumishi ume-deprive haki za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nimalizie kwa kukushukuru sana na kumshukuru Mungu kwa sababu ya kutoa *speech* hii ahsante sana. Naunga hoja mkono ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto takwimu zako hizo duuh! Nahisi AG hapo anataka kuzimia kabisa! Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mheshimiwa Tundu Lissu ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza kabisa naomba nipongeze hotuba ya Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na naomba nichangie maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Wizara yenyewe ya Katiba na Sheria. Wizara hii sasa imekuwa kubwa ina taasisi kama tano ndani yake ambazo zina uwezo wa kufanya kazi zake kwa kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume hii inafanya kazi nyingi, inaleta marekebisho mengi ya Katiba na Sheria, lakini Tume hii inaonekana kazi zake hazifanyiwi kazi kwa wakati.

Naomba niende kwenye Sheria ya Vijiji kuhusu ardhi sheria ya mwaka 1999 Na. 5. Sheria hii ya Ardhi ilipitisha Hati za Kimila lakini kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi katika maeneo yetu, tunaomba sheria hii irekebishwe hata ikiwezekana Wenyeviti wa Vijiji na Watendaji wapewe nakala halisi kwa kufanya mikutano ya hadhara kuwaelimisha wananchi ili kuondoa mgongano kati ya Wenyeviti wa Vijiji na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi imetumika vibaya. Tangu Vijiji kugawiwa kwa wananchi, Operesheni Vijiji wananchi walipewa maeneo, lakini inavyoonekana hao wawekezaji, wahifadhi walikuja baada ya vijiji kugawiwa, leo hii inaonekana wananchi katika maeneo yale hawatakiwi kukaa pale wanaoneka wamevamia maeneo. tunajiuliza, nani alikuwa mkaaji wa kwanza katika hii ardhi kati ya mwekezaji na mwananchi. Tunaomba sheria hii irekebishwe ili kuondoa mgongano, wananchi wetu waishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika eneo la tozo za kodi ya ardhi na nyumba. Kumekuwa na tabia mwananchi wa kawaida amejenga nyumba yake ya kawaida ya nyasi yuko kwenye Halmashauri ya Mji, hana elimu yoyote kuhusu kukuza Mji wala *plan* ya Mji, lakini mwananchi huyu pamoja na kuishi kwenye nyumba ya nyasi analipishwa shilingi 2,000 na kiwanja chake kama cha ardhi anakilipia, tunaomba hizi sheria zirekebishwe, zinatuletea matatizo, kumekuwa na manung'uniko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo la Mahakama. Mahakama nyingi za Mwanzo hazifanani na mahakama na hata wanaoingia humo hawafanani na majengo halisi. Miundombinu ya mahakama ni michafu, mahakama imekuwa ni mbovu, majengo yanataka kuanguka. Pia hata

miundombinu ya vyoo, hakuna vyoo kabisa, maeneo mengi wanahifadhi mahabusu zaidi ya 60 wanatumia choo kimoja, jinsia ya kiume na ya kike, hapa tunahifadhi maradhi na sisi tunasema adui mkubwa ni maradhi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende eneo la utawala. Kumekuwa na mgongano mkubwa sana hususani kwa *Babati TC*, mgongano huu unatokana na *DC* anaingilia mamlaka ya Kibunge, *DC* huyo amekuwa kero kwa Mbunge wa Babati Mjini. Tunaomba *DC* aelekezwe mipaka yake ya ki-*DC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Sheria ya Ndoa aliyozungumzia dada yangu Kiteto, lakini naomba niende kwenye magereza. Hali ya magereza yetu ni mbovu na ni mbaya. Kwanza kuna mrundikano wa mahabusu, pili hawapati lishe nzuri, hasa kwenye mahakama zenye vitengo vya watoto. Kumekuwa na vitendo vya kikatili wanafanyiwa wale watoto, tunaomba mahakama za watoto zitengewe eneo lake peke yake, sheria hii iwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo la ajira; Kumekuwa na matatizo mengi katika eneo la ajira, vijana wengi hawaajiriwi, wanamaliza vyuo lakini kumekuwa na dana dana nyingi. Tunaomba hizi sheria zote zirekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende katika eneo la Sheria ya Walaji na Watumiaji. Kumekuwa na matatizo ya hapa na pale katika matumizi ya vyakula tunavyokula hasa vinavyotoka nje ya nchi. Hata hivyo kumekuwa na tabia ya *TFDA* kwenda kwenye maduka ya wale wanaouza bidhaa za vyakula. Unakuta bidhaa ina- *expire* mwaka 2016 mwezi wa sita, lakini hilo kontena limepita wapi? Utashangaa *TFDA* wanakuja kuvamia maduka ya watu wanatoa vyombo, wanachoma na wanatoza faini. Lakini tunajiuliza hili kontena limepita wapi? Sheria hii haiko sawa tunaomba hawa wa *TFDA* watueleze na Waziri mwenye dhamana ashughulike na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo la uvunjaji wa sheria na haki za binadamu. Mwaka jana tumetoka kwenye uchaguzi, tumefanya uchaguzi vizuri lakini tarehe 26 kulitokea na tukio kwa upande wa Upinzani. Vijana wetu walikamatwa, kompyuta zao zilichukuliwa kisa tu wanakusanya matokeo. Huu ni uvunjaji wa haki za binadamu, halafu bado tunasema hii haki tunaitumia. Haki hapa haijatumika! Vijana hawa wamebambikiwa kesi, bado tunalia tunasema haki imetendeka!

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa kumalizia. Ni hatari sana kuanzisha familia ambayo uwezi kuitunza. Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, tumeona Bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu, bajeti hii hairidhishi hata kwa mtu wa kawaida unaona ni jinsi gani hii Tume haihitajiki katika Serikali hii. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri, Fungu namba 55 tunahaja ya kulishikilia, huwezi kubeba mzigo mzito ambao huwezi kuutekeleza! Tume hii inafanya kazi nyingi, Kazi nyingi zinaletwa kwenye Wizara husika lakini kazi hizi zinazimwa kwa sababu maalum. Sasa kwa nini hii Tume mmeiweka? Tume hii kwenye bajeti yake haina maeneo mengine zaidi ya OC, sasa kama ina OC na hawana jengo wanapangisha wana kazi gani ya kulipwa mishahara? Kwa kazi ipi wanayofanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema posho ya Wazee wa Mahakama. Wazee wa Mahakama wanalipwa shilingi 5,000; wanahudhuria mahakamani mwezi mzima halafu bado Serikali inawakopa! Tunaomba muwalipe hawa wazee na ikiwezekana wazee hawa wapandishiwe posho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia eneo lingine ni eneo la haki za wazee. Ahsante, siungi hoja mkono. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryamu Kisangi.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa sababu muda nitazungumzia masuala mawili tu na yote yanahusu mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza linahusu masuala ya kinidhamu ya Majaji. Tarehe 30 Novemba, 2014, Bunge hili lilipitisha Azimio kwamba Rais aunde Tume ya Uchunguzi ya Kijaji kuchunguza Majaji wa ESCROW. Majaji wawili ambao kwa ripoti maalum ya uchunguzi ya Kamati ya Kudumu ya Bunge hili iliwakuta wamechukua mamilioni ya fedha kutoka kwa yule bwana wa ESCROW James Rugemalira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majaji wawili Aloysius Mujulizi na Profesa Eudes Ruhangisa. Bunge lilipitisha Azimio, baadae Mheshimiwa Rais Kikwete alipozungumza na wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam, tarehe 12 Disemba mwaka huo alisema kwamba, suala la nidhamu ya uchunguzi wa Majaji hao linapelekwa kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama lianzie huko, halafu baadaye ndiyo liletwe kwa Rais kwa ajili ya hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka jana na baadaye mwishoni mwa mwaka jana Mheshimiwa Jaji Mkuu aliviambia vyombo vya habari kwamba uchunguzi wa Majaji hawa wawili ulikuwa umeisha kamilika! Leo ni mwaka mmoja na nusu, tangu Azimio la Bunge, kuhusu Majaji wa ESCROW pamoja na wengine litolewe, taarifa iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujumuisha, utuambie Majaji waliochukua shilingi milioni mia nne, mia nne kutoka kwa Rugemalira na Bunge hili likapitisha Azimio kwamba washughulikiwe kwa mujibu wa Katiba, kitu gani kinatokea na huu ukimya ni wa nini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la nidhamu ya Majaji ni suala muhimu sana, mahakama zetu zimechafuka, tunapenda kulalamika Mahakimu, Mahakimu, Mahakama zetu katika ngazi zote zimechafuka! Kitu cha ajabu kabisa ni kwamba tumekuwa tunachukua hatua dhidi ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo *once in a long while*, Majaji hawaguswi! Hatuna malaika wala watakatifu katika Mahakama Kuu, hatuna malaika wala watakatifu katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania, kitu cha ajabu ni kwamba mara ya mwisho na hii ni muhimu, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania amechukuliwa hatua ilikuwa mwaka 1991, Mheshimiwa Jaji Mwakibete alipoundiwa Tume ya Uchunguzi akaondolewa madarakani. Miaka zaidi ya 25 Mahakama ni rushwa tupu na kila mtu analalamika hapa! Lakini ikifika kuchukua hatua, kila mtu anaogopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hili ambalo liko wazi kabisa la waliokutwa wamechukua mamilioni ushahidi wa nyaraka upo, tuambiwe imekuwaje? Tusinyamaziwe tafadhali, mahakama zetu kama tunakubali kwamba kutumbua majipu ya muda mrefu ni kitu muhimu, haya ya wazi haya, tusiyaache hilo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili ambacho kinasemwa sana ni hiki kinachoitwa kuanzishwa kwa Mahakama ya Mafisadi. Mara nyingi ninapoona watu ambao wanaonekana onekana kama wana akili hivi, kama wamesoma hivi, kama wanajua sheria hivi, halafu wanazungumza vitu vya ajabu kabisa, nakuwa nafedheheka sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa na Mahakama ya Mafisadi tangu mwaka 1984; kwa miaka 32 leo tuna Mahakama ya Mafisadi. Sasa haiitwi jina hilo inaitwa kwa kiswahili maarufu inaitwa Mahakama ya Wahujumu Uchumi. Ilianizhwa wakati wa *crackdown* ya Sokoine wa wahujumu uchumi na walanguzi. Mahakama Kuu inaposikiliza kesi zote za rushwa, Mahakama Kuu inaposikiliza kesi zote za kutakatisha fedha haramu, Mahakama Kuu inaposikiliza kesi zote za hujuma ya uchumi, makosa kwa mfano yanayohusiana na Sheria za Wanyamapori, Sheria za Dawa za Kulevy *and so on and so forth*, inakaa kama Mahakama ya Mafisadi, imeanzishwa kwa mujibu wa sheria. Sasa unashangaa watu wanaonekana kama wanafahamu wanazungumza, tunampongeza Mheshimiwa Rais sana, ameamua kutuanzishia Mahakama ya Mafisadi *nonsense!* (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nani aliyewaambia hakuna Mahakama ya Mafisadi? Kama mnataka kuibatiza tu semeni, halafu ukiuliza eehe! huo Muswada uko wapi? Aah tutaianzisha tu kama *Division* ya Mahakama Kuu, *nonsense!* *Division* ya Mahakama Kuu inahitaji Sheria, kuna *Division* ya Mahakama Kuu ya Ardhi, imeundwa kwa sheria. *Division* ya Mahakama Kuu ya Ajira Kazi, imeundwa kwa Sheria, *Division* ya Mahakama Kuu ya Biashara, imeundwa kwa sheria, hii *Division* ya Mahakama Kuu ya Mafisadi, sheria yake iko wapi? Hii ambayo mnasema mtaianzisha sijui mwezi Julai!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mambo haya, ambayo tunaambiwa tuna wataalam wa sheria wanaofahamu fahamu, *why are they allowing these nonsense to go on.* Kwa nini watu wenye utaalum wa sheria, madaktari hapa na wengine maprofesa, kwa nini wanaacha ujinga huu unaendelea kusambaa? Nafahamu na kwa sababu nimeshughulikia haya masuala kwa miaka mitano Bunge lililopita, kwamba kuna matatizo makubwa kuhusiana na uendeshaji wa kesi za ufisadi, nayafahamu, lakini kusema kwamba hakuna mahakama ya kuyashughulikia ni kuthibitisha ujinga tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kupigana sawa sawa na tatizo la ufisadi, tuzungumze kuna tatizo gani katika Mahakama ya *Economic and Organized Crimes Court* iliyoanzishwa na Marehemu Sokoine mwaka 1984. Tusijifanye tunatengeneza mambo, hakuna kitu kipya hapa, Mahakama hii ipo *for the past 32 years*, ina matatizo yes, tuyazungumze hayo matatizo. Lakini tusizungumze *as if* hakuna kitu, tunaanzishiwa kitu kipya na Rais John Pombe Magufuli. Akizungumza Rais, namsamehe siyo mwanasheria, akizungumza Daktari wa Sheria nafedheheka sana kwa sababu anajua kama hajui anapaswa kujua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa vile muda hakuna, hivi umri wa kustaafu wa Jaji Mkuu ni miaka mingapi? Hivi huyu Jaji Mkuu wa kwetu hajafikisha huo umri wa kustaafu? Wenzake wote aliokuwa nao darasa moja, Jaji Msofe, Jaji Masati, Dkt. Steven Bwana, walishastaafu miaka mingi, Jaji Mkuu wetu umri wake wa kustaafu ni lini? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwa siku ya leo.

Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutumbua majipu na kuhakikisha kwamba itapofika Julai aanzishe hiyo Mahakama ya Mafisadi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli wanaweza wakasema kulikuwa na mahakama, Mahakama tunazoziona, mimi naishi Dar es salaam, naona kuna Mahakama Kuu, kuna Mahakama ya Rufaa na kuna Mahakama ya Kisutu sijaona Mahakama ya Mafisadi iliyo wazi, Mheshimiwa Rais ajitahidi kwa kila liwezekanalo alete sheria hapa ya kuanzisha Mahakama ya Mafisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kututeulia Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Waziri wetu mahiri, muelewa na anatosha kwa nafasi hiyo. Lakini pia nawapongeza Waheshimiwa Makatibu Wakuu. Waheshimiwa Makatibu Wakuu wamewekwa kulingana na elimu zao na taaluma zao katika Wizara hii na nina imani kabisa kwamba watafanya kazi nzuri sana kwa Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wangu hapa duniani kuna matatizo mengi, wewe ni mwalimu, umewafundisha wengi sana lakini kuna baadhi yao watakushukuru na baadhi yao watakubeza. Hayo yote ndiyo mzazi anayopata na ndivyo mzazi alivyo. Unapozaa unaweza ukazaa mtoto mwema na mtoto mbaya yapokee, lakini Mwenyezi Mungu atakulinda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie suala zima linalohusu utumbuaji wa majipu. Katika hotuba ya Upinzani wameeleza kwamba kuna baadhi ya Mawaziri, Wakuu wa Mkoa wanatumbua majipu wakati hawana mamlaka, hiyo siyo kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, utumbuaji majipu utaendelea kufanyika kwa yeyote yule ambaye atakwenda kinyume na maadili ya kazi yake, tena utaendelea utumbuaji huu kwa ngazi za aina mbalimbali. Kama kuna mtu ambaye anaona alitumbuliwa kinyume na taratibu au kinyume na sheria ndiyo maana mahakama zipo, mahakama zimewekwa ili mtu apeleke matatizo yake na hata yule ambaye anaona utumbuaji wake umekwenda kinyume ruhusa kwenda mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie kuhusu fedha za Bunge shilingi bilioni sita. Kwanza nilipongeze Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya, wananchi wetu wanakaa chini, mimi natoka Mkoa wa Dar es Salaam, sasa hivi tumeandikisha watoto wengi sana kuna limbikizo la watoto. Watoto wanasoma wakiwa wamekaa chini hivi leo kuna ubaya gani Bunge kutoa shilingi bilioni sita, kutusaidia Wabunge wote tulioko hapa katika Majimbo yetu tupate madawati.



Mheshimiwa Naibu Spika, nataka wananchi wawaone wenzetu hao wakati wanaomba kura walisema wao ni wazalendo kweli kweli, leo nashangaa uzalendo huu wa kukataa hata kupeleka pesa za madawati katika Majimbo yetu. Jamani hivi tunakokwenda tuko sahihi kweli, kuna mambo ya kubeza, lakini kuna mambo mengine tusifanye masihara kwa sababu wananchi wetu wanapata shida, watoto wetu wanahangaika, wanakaa chini wengine wanakalia vipande vya mawe au matofali. Leo Bunge hili, hivi zile shilingi bilioni sita tulitaka tuzifanyie nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalipongeza sana Bunge hili kwa kuamua, uamuzi wake ni wa busara na waendeleo kama kuna pesa ambayo inaonekana haina kazi watuletee tunahitaji bado vifaa zaidi katika afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nirudi katika Mkoa wangu. Katika mahakama za Mkoa wa Dar es Salaam kuna Mahakama ya Mbagala, mahakama hii ina hali mbaya sana, Mahakama ya Temeke, Mahakama ya Magomeni, Mahakama ya Mnazi Mmoja na Mahakama ya Buguruni. Mahakama hizi zote zina hali mbaya, zina zaidi ya miaka 50 toka zimejengwa, Dar es Salaam ni Jiji, Dar es Salaam ni kioo cha Tanzania, tunapokuwa na Mahakama za aina hii katikati ya Mji, inakuwa ni tatizo na wala haioneshi kwamba tunakwenda mbele kama Jiji la Dar es Salaam. Ninaomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi waangalie kwenye bajeti zao kuboresha Mahakama ukianzia zile zenye hali mbaya Mahakama za Buguruni, Mbagala, Magomeni na ile Mahakama ya Mnazi Mmoja, ziangaliwe kwa jicho la pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika ngazi ya Wilaya, kuna Mahakama ya Wilaya ya Temeke, Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni na Mahakama ya Wilaya ya Ilala. Hizo ni Mahakama za Wilaya lakini hazina hadhi ya Wilaya, niiombe Serikali iboreshe mazingira yale, kubwa zaidi ni zile selo zilizoko katika mahakama hizo. Mahabusu wanajaa mno katika selo zile vyumba ni vidogo, ninaomba Serikali iwapanulie hivyo vyumba na kuweka madirisha ambayo, yatakuwa yanawasaidia mahabusu katika kuvuta hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie juu ya sheria inayounda Jiji. Kambi ya Upinzani wamesema wamepata Jiji, ndiyo, mmepata Jiji, je, Jiji lile lina faida gani? Mimi ninaomba Serikali iangalie upya Sheria ya Jiji. Jiji lile ni Serikali ya tatu halina rasilimali yoyote, pale ni utata mtupu, sehemu ilipo Jiji ni eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. *Parking* ambazo ndiyo mapato ya Jiji zipo kwenye Halmashauri ya Temeke, Halmashauri ya Ilala, Jiji lile ni mgogoro halina rasilimali ya aina yoyote. Nawashangaa wenzangu niliwatarajia leo hapa walete hilo tuliangalie, wao wanafurahia kupata Meya, Meya huyo ataendeshaje wakati hana rasilimali? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niungane na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Kiteto kuzungumzia juu ya Sheria ya Mwanamke, sheria hii iangaliwe kwa mapana zaidi kwa sababu Sheria hii ya Ndoa inawamina sana watoto wa kike, lakini pia..

**NAIBU SPIKA.** Mheshimiwa Mariam naomba utulie kidogo. Mheshimiwa Gekul utaratibu, naomba kama unataka kuongea na mtu across umuandikie, Mheshimiwa Mariam naomba uendelee.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba dakika zangu unitunzie.

Ninaomba Sheria hii ya Ndoa iangaliwe tena upya. Kweli mtoto wa kike kwa dunia hii ya leo, Sheria ya Ndoa inasema mtoto wa kike ataolewa akiwa na umri wa miaka 16, bado ni mtoto mdogo sana, ninaiomba Serikali iiangalie kwa mapana yake Sheria hii na iifanyie marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fursa hii niitumie kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi, hususani Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi, kurudisha majina yenye dhana ya *fifty-fifty*, kweli Chama cha Mpinduzi ndiyo Chama ambacho kinaendeshwa kwa ukweli na uwazi. Imerudisha majina wanawake wawili na wanaume wawili kazi kwetu. Nakipongeza chama changu, kwa uamuzi wake wa busara ambao wameufanya na vyama vingine navyo viige mfano wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Mheshimiwa Wabunge walizungumza bila ya mpangilio)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mbona hawa wana vurugu! Tulieni ninyi!

Naomba nimpongeze kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Katibu wa CCM Bunge, amefanya kazi yake kwa ubora, kwa uzuri ameliendesha Bunge hili vizuri sana, anaachia gari hili na wengine tuje tufuate jinsi gani amefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia moja na kura Wabunge wa CCM....

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama makelele yangukuwa yanashinda kesi basi upande wa Upinzani wangukeshinda sana, lakini ndiyo wamepoteza kesi zote ambazo walishtaki kwa sababu ya kushindwa kura, licha ya makelele yote ambayo wanafanya humu ndani, mahakamani hatushindi kura kwa kupiga makelele. Pia niungane na mwenzangu Mheshimiwa Tundu Lissu, aliposema asubuhi kwamba tunaposema sisi sikilizeni msiumie, tuseme mtusikilize.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu hawa hawajielewi kwa nini hawapewi Serikali, hawapewi Serikali kwa sababu wananchi hawawaamini, hawa ni ving'ang'anizi hawa kwenye madaraka. Tawi lao la CUF la UKAWA la CUF, Kiongozi wake ana miaka 20 anagombea yeye peke yake, vilevile hawajielewi wenzetu hawa kwa nini hawapewi madaraka.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba ukae.

**MBUNGE FULANI:** Ahsante lakini asiseme hatujielewi.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa, Mheshimiwa Maige endelea.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema tukiumia tuvumiliane, neno la ufisadi lilikuwa ndiyo ajenda ya Upinzani kwa mwaka mzima mmetangaza ufisadi kwamba haufai. Imetokea nini?

Mimi nina orodha ya mafisadi ambayo mliitangaza ninyi UKAWA, lakini shemeji yangu huko umemchukua namba moja fisadi unaye wewe huko na jambo hili linafanya wananchi wasiwaamini. Mnawafanya watu waamini kwamba ninyi ni vinyonga, mnabadilika badilika, hatutaki sera ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchaguzi wa Zanzibar. Hakuna mtu aliyewakataza kushiriki uchaguzi uliorudiwa na hasa tawi lenu hilo la CUF, siyo kosa la Chama cha Mapinduzi kushinda kura zote kwa sababu ninyi mlitia mpira kwapani. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma tafadhali uwe mvumilivu, tuendeleo.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hawa UKAWA wanajua siri kwa nini hawakushiriki uchaguzi mbona hamuendi mahakamani? Mbona hamsemi kwa nini hamkushiriki? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mapinduzi ya Zanzibar ni kweli kwamba Tanzania Bara ilishiriki na kusaidia mapinduzi kwa nguvu yote na sababu kubwa

tulijua kwamba mapinduzi yale ni haki, yanaleta uhuru kwa Wanzanzibar. Wale ambao wanapinga Mapinduzi sasa ni mikia au vitukuu vya wale watawala waliotawala Zanzibar. Najua inawauma sana na itawauma sana, lakini tunaendelea kusema Mapinduzi daima. (Makofi)

Mheshimwa Naibu Spika, nirejee katika hoja iliyopo mbele yetu ya Katiba na Sheria na kwanza nianze kwa ku-*declare interest* kwamba mwaka 2014 Shirika la Kazi Duniani liliipa fursa Tanzania kuwa Kiongozi wa Vyama vya Waajiri Afrika na huyo Mtanzania ni mimi Mbunge mwenzenu. Vilevile mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri hapa Tanzania na mwishoni Serikali ya Jamhuri ya Muungano inafanya kazi vizuri katika kujenga barabara na kujenga majumba mazuri kama hili tulilomo ndani kwa kutumia wakandarasi. Naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni mkandarasi daraja la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nirejee kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais alipohutubia humu ndani, kwamba kulikuwa na sheria anazozifahamu yeye na wanasheria wote wanazifahamu ni mbaya kwa Watanzania na angependa sheria zifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Sheria ya Manunuzi ya Umma. Sheria hii ina kasoro haitoi upendeleo kwa wazawa wale wanunuzi wanapofanya manunuzi kwa mali na kazi inayopatikana pia kwa Watanzania. Ninashauri Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie lini sheria hii italetwa hapa kwa marekebisho ili iweze kutoa fursa kwa Watanzania. Vilevile inatoa uhuru mkubwa kwa wanunuzi kuchagua mzabuni wanayemtaka na hiyo inasababisha mirejesho ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ina mapungufu pia na ningependa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria anapokuja kuleta majumuisho yake hapa atuambie lini Serikali italetwa sheria hiyo hapa kurekebisha mambo yafuatayo; moja ni likizo ya uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la likizo ya uzazi limekuwa kero kubwa kwa waajiri. Waajiri wanapata taabu sana kuwahudumia akina mama wanaorudi baada ya kujifungua, kuna watu wanaenda kunyonyesha kwa muda wa masaa mawili, kwa mwaka mmoja, miaka mitatu mpaka miaka mitano, sheria haisemi mpaka wa muda wa kunyonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sheria hii inaleta machungu makubwa wakati wa kuachana na wafanyakazi wabaya, wafanyakazi wakikaribia kutimiza muda wa kustaafu wanafanya makosa makusudi, aidha wanaiba na ukiwapeleka mahakamani kesi ikianzishwa mahakamani mwajiri hawezi kumfukuza huyu mfanyakazi na kesi itaendelea na kama alikuwa anapata marupurupu ya nyumba, gari na wafanyakazi nyumbani ataendelea kulipwa

na mnavyojua sheria humu ndani na mahakama inachukua muda mrefu, mwajiri ataendelea kumlipa mfanyakazi huyu hata kama kesi itachukua miaka kumi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria utakapokuja ujaribu kutusaidia suala hili pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lipo suala lingine ambalo ni sekta ya ulinzi binafsi, sekta hii haina sheria huu mwaka wa 36 tangu ianzishe hapa na matokeo yake sekta hii inajiendesha hovyoyote, na kuleta matatizo kwa watu ambao wanaendesha biashara hii. Sheria hii ikitungwa italeti uhaba wa sekta ya ulinzi binafsi na kuwafanya watu hawa waweze kufanya kazi kama ambavyo Serikali itataka na kwa manufaa ya Watanzania. Watu wengi wameumizwa na makampuni ya ulinzi binafsi lakini hakuna sehemu ya kuyashitaki, napendekeza atakapokuja Mheshimiwa Waziri aje na majibu kwa nini asilete Bungeni humu Muswada wa kuanzisha sekta ya ulinzi binafsi, Sheria ya Ulinzi Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, anisaidie pia kule kwetu Upuge iko Mahakama ya Msingi ambayo ni nzuri ina majengo yote, mahakama yenyewe lakini na majengo ya kukaa wafanyakazi imetelekezwa huu mwaka wa 12, majengo yale sasa wanakaa panya, wanakaa wanyama hovyoyote. Ningependa pia anieleze itakuwaje kuhusu majengo yale yaliyopo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliff Makamba, halafu Mheshimiwa Abdallah Mtolea ajiandae.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapa pole Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wote ambao wametajwa ndani ya Bunge hili ambao hawawezi kufika ndani ya Bunge hili kujitetea. Kanuni zetu za kilatini Mheshimiwa Tundu Lissu atakuwa mwenyeji kwenye hili *right to be heard, rule of law* ambazo zinatuongoza anazifahamu vizuri, lakini nitambue mchango Jaji Mkuu Mheshimiwa Mohamed Othmani Chande, amefanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba mahakama zetu zinakwenda vizuri kupunguza kesi za mahakama ambazo zilikuwa msongamano kwa muda mrefu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Rufiji kwa kunielewa, wananifahamu kule Rufiji naitwa jembe, wengine wananiita sururu. Ninashindwa kutambua uwezo wa kisheria au uwezo wa kufahamu wa ndugu yangu Tundu Lissu, kwa muda mrefu sana nimekuwa nikifuatilia mchakato na namna ambavyo akiendesha Bunge kwa muda mrefu sana kwa zaidi ya miaka sita nimekuwa nikifuatilia. Mheshimiwa

Tundu Lissu namfananisha na mwandishi wa vitabu vya *movie*, aki-act mwaka 1940 ile *movie* ya Ndugu Charlie Chaplin. Kuna *movie* moja, *political satire*, hii ukiifuatilia vizuri inaendelea kiundani, Mheshimiwa Tundu Lissu ni mtaalam mzuri wa kuiga kisiasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielezee uteuzi wa Mawaziri. Tunaongozwa hapa na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, kama ambavyo imekuwa ikirekebishwa mara kwa mara. Lakini katika Katiba hii, Ibara ya 54 na 55 inazungumzia kwa uwazi uteuzi wa Mawaziri. Ibara ya 56 inazungumzia mchakato mzima wa nani anaweza ku-qualify kuwa Waziri yaani kwamba mchakato huu, mtu atakuwa Waziri baada tu ya kuapishwa na Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaongozwa na Sheria Na. 15 ya mwaka 1984 kama ambavyo Mheshimiwa Tundu Lissu ameizungumzia. Katika *instrument of appointment* ya Mawaziri ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu amekuwa akiikazania kwa muda mrefu, siyo yeye tu hata Mwenyekiti wa Chama chao amekuwa akizungumza sana kuhusiana na sheria hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge hili lipate fursa ya kutufundisha kizungu inaonekana kuna shida ya kufahamu kizungu. Kwa mujibu wa Sura ya 299 ya sheria inayompa mamlaka Mheshimiwa Rais ya kuwaapisha pamoja na kuunda *instrument* yaani sheria hii inaitwa *The Minister's (Discharge of Ministerial Functions) Act*, Sura ya 299. Ukisoma kifungu cha tano cha sheria hii kinasema hivi ninaomba wataalam wa *linguistic* watusaidie ili waweze kumueleweshwa huyu bwana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tano cha sheria hii kinasema hivi; “*The President may, may na shall* ina maana kubwa sana kwa kizungu. Wataalam wa *linguistic* watusaidie kumfahamisha *may* ina maana gani na *shall* ina maana gani. Siyo hivyo tu kifungu hiki kimekwenda moja kwa moja kuzungumzia kwamba *from time to time by notice published in the Gazette specify the departments, business and other matters responsibility for which he has retained himself or he has assigned under his direction to any Minister, and may in that notice specify the effective date of the assumption of that responsibility.* (Makofi)

Sheria hii inasema wazi ni wakati gani. Mheshimiwa Rais wakati wowote anaweza kutengeneza *instrument* kwa sababu sheria hii haija-specify ni wakati Mheshimiwa Rais anapaswa kutoa *gazette* la Rais. Sheria hii haitoi muda. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais hajavunja Katiba yoyote kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende mbele zaidi, amezungumzia suala zima la *ESCROW* kuna Majaji walishutumiwa *not* kushtakiwa. Naomba nimkumbushe



vifungu vya sharia vinasema *allegation however strong it may it cannot convict the accused person*, hata kama shutuma zitakuwa na uzito wa kiasi gani haziwezi kumtia hatiani mshitakiwa.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika taarifa...

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Kwa mujibu wa Katiba...

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha naomba ukae tafadhali. Mheshimiwa Maftaha naomba ukae tafadhali. Mheshimiwa Mchengerwa malizia.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 112 inazungumzia Tume ya Utumishi wa Mahakama. Tume hizi zimepewa uwezo mkubwa wa kujadili nidhamu za Majaji na Mahakimu. Ibara ya 113 inakazania kwenye suala hili zima. Bunge halina mamlaka juu ya Mahakama, hali kadhalika Serikali haina mamlaka dhidi ya Bunge na Mahakama. Kilichofanyika baada ya mapendekezo ya Bunge, Mheshimiwa Rais alikabidhiwa mapendekezo ya Bunge, kwa mujibu wa Ibara hii ya 113 Mheshimiwa Jaji Mkuu aliunda Tume, Tume ya Utumishi wa Mahakama ipo kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Tume Rais hana mamlaka ya kumfukuza Jaji isipokuwa tu Ibara ya 113 inampa mamlaka Mheshimiwa Rais iwapo itaonekana Jaji amefanya utovu wa nidhamu na maadali baada ya Tume ya Utumishi wa Mahakama kutoa mapendekezo yake. Jambo hili lilifanyika na Waheshimiwa Majaji hawa baada ya kupitia na jambo kubwa ambalo lilifanyika, Mheshimiwa Jaji Mkuu pamoja na Tume hii walitumia *the Code of Ethics for Judicial Officers*, pia kwa kuzingatia *the independence of the judiciary* walizingatia haya yote kimsingi na ilionekana kabisa wazi kwamba hakuna jambo lolote lililofanyika na taarifa hii ipo mbele ya Mheshimiwa Rais kwa tafiti zangu binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaenda kwa haraka. Kuhusu Mahakama ya Mafisadi imekuwa ikipigiwa kelele sana, sasa sijui kwa nini ndugu zetu hawa wanakuwa waoga, wanaogopa nini? Kwa mujibu wa taratibu na sheria kinachoweza kufanyika ni kufanya mabadiliko ya Sheria hii ya Uhujumu Uchumi ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu ameizungumza hapa, Sura ya 200 imezungumzia kiundani kabisa. *Division* hizi za Mahakama Kuu zipo nyingi Tundu Lissu anafahamu, tunayo *Division* ya Ardhi, tunayo *Division* ya Biashara, tunayo *Division* ya Kazi, kwa mujibu wa taratibu na sheria hii kwa kufanya mabadiliko Mheshimiwa Jaji Mkuu anaweza akaunda *special court* kwa kupitia muundo



huu ambao nimezungumzia hapa ambao inakua *division* ya Mahakama Kuu hakuna tatizo lolote wala Katiba haijavunjwa kutokana na hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka nizungumzie Muungano. Mheshimiwa Tundu Lissu anasahau kwamba Muungano wetu uliasisiwa na Waasisi hawa wawili, Mwenyezi Mungu azirehemu roho zao. Kupitia Sheria Na. 4 ya mwaka 1964 iliondoa haya matatizo yote ambayo anazungumzia Mheshimiwa Tundu Lissu. Hata Mwenyekiti wa Marais Afrika anatambua mchango wa Tanzania katika kukomboa Bara la Afrika, siyo kwenda kusababisha Mapinduzi ya Zanzibar, Tanzania ilifanya kazi kubwa Afrika nzima siyo huko. Mimi nilichotegemea ni kwamba kwa Wapinzani wanapaswa kuleta hoja ya kusaidia Wizara hii ya Katiba na Sheria. Siyo kuanza kuzungumza maneno ambayo ni ya uchochezi maneno ambayo hayafai. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea Mheshimiwa Tundu Lissu hapa angekuja na akatuambia ni namna gani tutaweza kulizungumzia Fungu Na. 40 ambalo Mheshimiwa Waziri hajalizungumzia, ni namna gani Mahakama itaweza kupatiwa fedha zake kwa mujibu wa taratibu na suala hili halijazungumzwa na Mheshimiwa Waziri. Lakini pia nilitegemea watu wa Upinzani wangezungumzia kuhusu Fungu Na. 55 la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili tume hii iweze kuongezewa fedha.

Ninaishauri Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuweza kuona mchakato wa kuongezea fedha Tume hii ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niongelee suala la Mahakimu. Mahakimu wetu wanafanya kazi ngumu, nawapongeza sana kwa kuchapa kazi Mahakimu na Majaji wote Tanzania. Ninaomba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kuona uwezekano wa kuwaongezea mishahara Mahakimu wetu, pia kuangalia kuwapatia *non- practicing allowance* pamoja na *rent assistance* kwa ajili ya kuwapunguza ukali wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya mishahara kati ya Mahakimu na Majaji ni kubwa sana, ninaomba Mheshimiwa Waziri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuweza kufikiria uwezekano wa kupunguza ukubwa wa tofauti ya mishahara kati ya Hakimumu na Jaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka Tundu Lissu pia amezungumzia kuhusiana na Mkuu wa Wilaya kutoa maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Wycliff Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Mtolea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Pia ningependa kuchukua fursa hii kuipongeza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa hotuba nzuri iliyoonesha weledi na uzamifu katika suala zima la Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeeleza yote watu watapiga makofi lakini mwenye macho na masikio atasikia neno hili ambalo watu wa Upinzani tumeeleza Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema inahitaji digrii ya ujinga kukubali kupewa kazi bila *job description* halafu useme huo ni uamuzi wa bosi wako kama anaweza akakupa au asikupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kushauri Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa kama Wabunge kazi yetu kubwa ni kuisimamia na kuishauri Serikali ili iweze kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutekeleza hayo ningependa kushauri na kuwaomba wanasheria waliopo humu na Mawaziri waliopewa dhamna hii waishauri Serikali itekeleze majukumu hayo kwa kumshauri Rais ipasavyo juu ya utekelezaji wa majukumu hayo kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafahamu wazi kwamba Urais ni taasisi na siyo mtu binafsi.

Mheshimiwa Rais tamko lolote atakalolitoa iwe ni kwa masihara au yupo anakunywa chai au anafanya kitu chochote kwetu sisi tunaiona kama ni agizo na tunaichukulia kama ni sheria, kwa hivyo, Mawaziri wahakikishe kwamba Rais wao anapotoa matamko basi yawe ni ya kujenga na siyo kubomoa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba suala la uendeshwaji wa nchi hii, tukiangalia suala la sukari, suala la vyombo vya habari, suala la utekelezaji wa haki za binadamu, uendeshwaji wa mahakama ni suala ambalo kimsingi Rais wa nchi hii alipaswa kukalishwa chini na kuelezwa ni lipi aliongee kwenye jamii ambalo mwisho wa siku litaleta matunda na siyo kuibomoa nchi hii na kuirudisha mwaka 1980 enzi za uhujumu uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara makubwa, leo asubuhi tumepata taarifa kwamba bei ya sukari imefika shilingi 3,200...

**MBUNGE FULANI:** Duh.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Na hii nayo inasababishwa na tamko ambalo Mheshimiwa Rais alilitoa, tunaamini matamko, sheria, kanuni na taratibu za nchi hii zinafanyika kwa kushirikisha wadau, endapo tatizo au suala la sukari na ukuzaji wa viwanda lingeshirikisha wadau ambao ni watumiaji wa sukari pamoja na wafanyabiashara wa sukari, huenda tusingefikia kwenye hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mahakama zetu tukubaliane mbali na itikadi zetu za kisiasa ni tatizo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa umakini wa hali ya juu. Tunakosa uhuru wa mahakama kwa sababu mahakama hizi kinyume na sheria mbalimbali zilizowekwa ikiwa ni pamoja na sheria za kimahakama na uendeshaji wa nchi hii zimekosa uwezo na uwezeshaji. Nimeshangaa sana Mheshimiwa Mbunge aliyepita aliposema kwamba tusiongelee kwa sababu hii ni mhimili inayojitegemea, lakini sisi kama Wabunge ndiyo tunaopitisha bajeti ambayo inakwenda kuiendesha hiyo mhimili mingine. Kwa hiyo, ni jukumu letu kuhakikisha tunatetea na tunasimamia maslahi ili mhimili hii iweze kuwa *independent* na iweze kufanya kazi kwa ufanisi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahakama zetu zimekuwa zikikabiliwa na changamoto za miundombinu, malipo ya wafanyakazi na madaraja ya mahakimu; mahakimu wawili wana cheo kimoja, wana daraja moja lakini wanalipwa mishahara tofauti. Suala hili linapaswa kuzungumziwa humu kinyume na mjumbe aliyetoka kuongea anasema kwamba huo ni mhimili unaojitegemea sijui kama yeye ana mfuko wa kuwapelekea mahakama pesa hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mahakama inakabiliwa na changamoto kubwa ya rasilimali. Mwaka wa fedha uliopita Wizara ya Katiba na Sheria ilipangiwa fungu lakini pesa hazikupelekwa ndiyo tunaona inazidi kudorora siku hadi siku. Tumeshuhudia kwenye kesi za uchaguzi, Majaji wanakosa *impartiality* katika *decisions* zao, ni kwa sababu ya umaskini wa hali ya juu ulioko katika ngazi ya mahakama. Mahakimu wanapewa baiskeli kwa ajili ya kwenda kazini, wanakosa nyumba, hawawezi kujikimu na hii inapelekea kushindwa kusimamia majukumu yao wakiwa kama mhimili wa Serikali unaojitegemea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoka kwenye suala la mahakama mwaka 2012 ulitolewa waraka ambao ulikuwa unaongelea kada ya Mtendaji wa Mahakama. Lengo la kuwa na kada ya Mtendaji wa Mahakama ilikuwa ni

kuboresha utendaji kazi wa kiutawala katika ngazi ya Mahakama. Kinyume na mategemeo, kada hii imeshindwa kutekeleza majukumu yake badala yake hali imezidi kuwa mbaya lakini watu hawa wanalipwa na Serikali. Ningeomba Waziri wa Katiba na Sheria aliangalie suala hili kwa umakini sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba niongelee suala la *Law School*. Tanzania tumekuwa na mfumo ambapo mwanafunzi anapomaliza shahada yake ya sheria analazimishwa kwenda kusoma *Law School*, lakini *Law School* imekuwa tofauti na shahada ya sheria. Tanzania vyuo vinavyotoa shahada ya sheria viko Mwanza, Mbeya, Arusha na maeneo mbalimbali na *Law School* ya Tanzania iko Dar es Salaam. Wanafunzi wanalazimishwa kusafiri kutoka huko wanakosomea ambako walichagua mpaka Dar es Salaam kwa ajili ya *Law School*. Usipofanya hivyo, pamoja na miaka minne aliyoipoteza wakati unasoma shahada yako ya sheria mwanafunzi yule hawezi kutambulika kama ni mwanasheria kamili na hawezi kupata ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na tatizo hilo, wanafunzi hao walio wengi walikuwa wanasomeshwa kwa kutumia mkopo. Cha kusikitisha ni kwamba anapokwenda *Law School* suala la mkopo inabidi lifanyiwe *pre-assessment* tena na wanafunzi hawa hawapewi mkopo. Kwa taarifa tu, sasa hivi ada ya *Law School* ni shilingi milioni moja laki tano na zaidi. Watoto waliokuwa wanasoma shahada ya sheria walikuwa wanalipiwa mkopo na Serikali lakini linapofikia suala la kwenda *Law School* linakuwa ni jukumu la mzazi kujua yule mtoto atafikiaje kwenye hatua hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili inabidi liangaliwe kwa umakini. Tunayo majengo yako *UDOM* pale wanakaa buibui, tunayo majengo na watu ambao wanaweza kutekeleza suala hili, lakini leo watu wachache wamejirasimisha zoezi hili wameweka *Law School* Dar es Salaam. Watu wanalazimishwa kusafiri mpaka Dar es Salaam, hawana makazi, wengine hawajawahi hata siku moja kufika Dar es Salaam, wanalazimishwa wakakae pale wasome *Law School* kwa sababu kuna maprofesa wachache au watu wachache wanaotaka kunufaika na mfumo huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda suala la *Law School* lishirikishe wadau hasa wanafunzi wanaokwenda kwenye shule hiyo. Pia ifahamike kuna watu ambao hawakusoma *Law School* zamani lakini leo kila gazeti utakalolishika linatangaza kazi lazima uwe umepitia *Law School*. Kwa yule ndugu yangu ambaye hafahamu kiingereza kama alivyoomba afundishwe *Law School* ni ile shule ya sheria ambayo ni lazima uende kusoma ili uweze kuwa Wakili kwa mujibu wa *Law School Act* ya mwaka 2007. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Ameelewa.

**MHE. SALOME. W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namuone huruma sana Mheshimiwa anayesimama na kusema kwamba anakaa Dar es Salaam lakini hajawahi kuona mahakama. Mahakama si kama tangazo la Vodacom au la Tigo linalobandikwa kwenye jukwaa.

**MBUNGE FULANI:** Waeleze mama.

**MHE. SALOME. W. MAKAMBA:** Mahakama ni *institution* ambayo iko kwa mujibu wa sheria na anachoelezwa ni *fact* kwa mujibu wa sheria. Unaweza ukakaa Dar es Salaam ukafahamu ratiba ya vigodoro Dar es Salaam nzima lakini usijue ziko mahakama ngapi. (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Waeleze, waeleze.

**MHE. SALOME. W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia kidogo katika bajeti ya Wizara hii ya Katiba na Sheria kwa niaba ya wananchi wa Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nioneshe masikitiko yangu makubwa kwa Bunge lenyewe kwa sababu Bunge limeunda Kamati na miongoni mwa Kamati ambazo limeziunda limeunda Kamati ya Sheria Ndogo. Kwa uelewa wa kawaida, Kamati ya Sheria Ndogo ilikuwa iwe Kamati pacha ya Katiba na Sheria. Kwa hiyo, ilikuwa tutegemee hapa wakati Kamati ya Katiba na Sheria inawasilisha pia kungekuwa na wasilisho kutoka Kamati ya Sheria Ndogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Kamati ya Sheria na Katiba imejikita katika sheria mama ambapo utekelezaji wa hizi sheria mama upo chini ya sheria ndogo ndogo ambazo ziko nyingi na hizo ndizo zinazowagusa Watanzania. Kwa kukosa nafasi ya kuzisemea sheria ndogo hizo katika Bunge hili si jambo zuri. Mwishoni unajiuliza hivi hii Kamati ya Sheria Ndogo yenyewe ikasemee wapi maana Kamati zote zimekuwa *connected* na Wizara na zinapata nafasi ya kuwasilisha hapa isipokuwa Kamati ya Sheria Ndogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza kwamba tunataka tutengeneze Taifa la kijani kwamba mwanamama Mtanzania aache kutumia mkaa atumie gesi unazungumzia sheria ndogo ndogo zitakazosimamia uagizaji wa gesi hiyo ili ipatikane kwa bei nafuu. Usipopata nafasi ya kuzisemea hapa

unakwenda kuzisemea wapi ili uhakikishe kwamba hilo Taifa la kijani linakuja? Unaposema kwamba gharama ya ndege hapa nchini imekuwa kubwa unazungumzia uagizaji mbovu wa mafuta ya ndege ambapo waagizaji wanajiwekea bei zao wenyewe. Hapo unahitaji sheria ndogo kwa ajili ya kusimamia haya ili Mtanzania aweze kusafiri hapa ndani ya nchi kwa tiketi za bei nafuu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Land Registration Act* inampa mamlaka Waziri kuweka kanuni na sheria ndogo ndogo za kusimamia vibali vya makazi. Katika hili, pale Dar es Salaam pana changamoto sana na hasa jimboni kwangu. Vile vibali vya makazi vimeainisha kwamba watu wanaokaa mita 60 kutoka kwenye reli ya TAZARA hawastahili kupewa hivyo vibali vya makazi. Hapa wanasimamia Sheria Ndogo ya mwaka 1995 inayoongeza eneo la kuachwa wazi kutoka kwenye reli lakini hao watu ambao wananyimwa vibali hivyo wamekuwepo hapo kabla ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wakazi pale kwenye Kata za Mtoni, Azimio, Tandika, Kilakala, Yombo Vituka na Sandali ambao toka mwaka 2002 nyumba zao zimewekwa alama ya "X" na watu wa TAZARA wakisimamia hiyo sheria ya mwaka 1995 inayowataka wahame bila kulipwa wakati watu hao walikuwepo pale kwa muda mrefu. Tunapoacha kuzijadili hizi sheria ndogo tunawaacha Watanzania walio wengi kwenye matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri mkalitazama hili kwa kushirikiana na Wizara hii ili tuone haya mambo tunakwenda kuyashughulikia kwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee kabisa nimpungeze sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa namna ambavyo amewasilisha hotuba yake yenye mashiko, iliyojaa *facts* na imedhihirisha kama kweli imewasilishwa na Wakili msomi. Suala la watu wanaipokeaje, hilo si jukumu lake, yeye amewasilisha na ni ukweli utaendelea kubaki kuwa ukweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na hili suala mnaliita kiporo, suala la Katiba Mpya. Mchakato huu wa Katiba Mpya wakati unaanza kwanza harakati zake hazikuwa za muda mfupi, zilianza muda mrefu na hazikufanywa tu na wanasiasa zilifanywa na taasisi mbalimbali. Baadaye Serikali ya Awamu ya Nne iliona kwamba kweli kuna umuhimu wa kupata Katiba Mpya kwa sababu jambo hili mnakuwa mnatafuta muafaka wa kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato ulianza vizuri lakini ulikuja kuharibika kwenye Bunge la Katiba. Hatua za awali za ukusanyaji wa maoni zilikuwa ni nzuri kweli kweli lakini ilipofika kwenye Bunge la Katiba mchakato ule uliharibika pale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Taifa hili na Serikali hii ya Awamu ya Tano inatamani kuendeleza muafaka huo wa kitaifa kwamba hili Taifa lipate Katiba Mpya, ni vizuri mchakato huo ukarejewa kuanzia pale kwenye Bunge la Katiba na Mheshimiwa Rais ana mamlaka hayo. Kwa mujibu wa kifungu cha 28(2) cha Sheria Na. 83 ya 2011 maarufu kama Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inampa mamlaka hayo Mheshimiwa Rais kuweza kuliita tena Bunge la Katiba na kujadili mapendekezo yaliyopendekezwa na Tume ya Jaji Warioba. Kama kweli wote nia yetu ni moja tunakwama wapi? Ndugu zangu wana CCM jambo hili litawajenga ninyi. Mnapoanzisha mchakato, mkausimamia na ukafika mwisho mnajitengenezea heshima ninyi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo likiishia kati mnawapa wasiwasi sana Watanzania. Jana tumepitisha hapa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi alisema anataka kulitoa jembe la mkono na kuliweka makumbusho, watu wanahoji, mmeshindwa kulitoa jembe la mkono kwenye bendera ya Chama cha Mapinduzi unawezaje kulitoa shambani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nia ni hiyo, watu waliofanya *marketing* wanajua, kile kinachopepea kwenye bendera kinapeleka ujumbe mzuri sana kwa wananchi. Kumbe tunganze kwenye bendera ya Chama cha Mapinduzi kuondoa nyundo na jembe la mkono tukaweka *computer* na treka ili kuonyesha kwamba kile tunachokihubiri ndicho tunachokisimamia. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ishauri Serikali hii iuanzishe mchakato wa Katiba Mpya kuanzia kwenye Bunge la Katiba. Kuupeleka mbio mbio kweli tutafanikisha tutaileta Katiba lakini itakuwa si Katiba ambayo wananchi walikuwa wakiitarajia na hili haliwezi kutusaidia, tutakuwa tukiendelea kuimba Katiba Mpya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni huu mrundikano wa kesi. Mrundikano wa kesi mahakamani umekuwa ni mkubwa sana na *work load* kwa Majaji na Mahakimu ni mkubwa. Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba ni kesi 200 kwa Jaji, huo si mzigo mdogo, huo ni mzigo mkubwa sana. Inafika mahali labda shahidi hajatokea siku moja Jaji anakuambia mimi nina kesi nyingi msinisumbue, mimi ninaendelea tu. Sasa haya mambo ya kutafuta haki za watu huwezi kuyapeleka namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tuone katika bajeti hii kwamba kuna vifungu vya kutosha kuweza kuongeza Majaji na Mahakimu ili kesi hizi ziweze kuisha. Kusema tu kwamba tunahitaji twende kwenye zero case bila kuwa na Mahakimu na Majaji wa kutosha maana yake utakwenda kulazimisha Majaji na



Mahakimu waliopo wazimalize hizo kesi kwa namna yoyote ile na *justice* haitaki namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni uchakavu wa majengo. Majengo ya mahakama yanatia aibu kweli kweli. Kibaya zaidi *nature* ya hao wanaofanya kazi kwenye hayo majengo mabovu ni kuwa watu nadhifu. Tunawafedhehesha sana kuwarundika Majaji na Mahakimu kwenye vijumba vya hovyoy, vyenye joto la ajabu na kwa unadhifu wao wamevaa tai na suti kubwa, kwa nini tunawatesa watu hawa?

**MBUNGE FULANI:** Tunawadhalilisha sana.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Wizara hii ikajipanga, iombe fedha ya kutosha kuhakikisha kwamba wanawatengenezea Majaji na Mahakimu majengo yenye heshima ya kuwa ofisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Ya kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Ni ya pili Mheshimiwa.

**WABUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Sekretarieti hapa mbele ndiyo inayotunza muda. Mheshimiwa Goodluck Mlinga atafutiwa na Mheshimiwa Augustine Vuma Holle.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, naomba niwape pole wananchi wangu wa Ulanga kwa hii hali ya mvua inayoendelea, barabara hazipitiki, mafuriko kila kona. Pia naomba niwapongeze wafanyakazi wa Halmashauri kwa kukubali kufanya kazi katika mazingira magumu kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakyembe kaka yangu, Wilayani kwangu hakuna jengo la Mahakama ya Wilaya, wanatumia jengo la Mkuu wa Wilaya, naomba unijengee. Hakuna nyumba za watumishi wa mahakama, wananchi wangu wanatembea umbali mrefu kufuata hizi huduma za mahakama. Kwa hiyo, naomba nisaidie hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho wakati nachangia tarehe 25 ilitokea tafrani ya kutoeleweka kwa lugha ambayo niliitumia, nilisema Mheshimiwa Pinda ametokea dirishani. Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana

na mimi kuwa kiswahili kilianza maeneo ya Pwani kwa hiyo sisi kwetu Upogoroni maneno ya kiswahili yalichelewa kufika, matokeo yake tuna umaskini kidogo wa maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu ilikuwa kusema hivi, sisi Chama cha Mapinduzi hatuna msalie Mtume katika maslahi ya wananchi. Inapotokea sintofahamu mahali tunakuita tunakuhoji, ukituridhisha tunakuruhusu uendelee. Kwa hiyo, wapinzani naomba mtuige na ndiyo maana tunaendelea kutawala nchi hii kwa sababu ya mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemu usemao mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Naomba nimpe hongera baba mkwe wangu Mheshimiwa Mbowe kwa kuwaruhusu wapinzani kuendelea kuchangia Bungeni kutokana na ushauri niliomba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Mbunge atakayepinga ni mimi niliyeleta semina humu Bungeni ya Mwenyekiti kasema ndiyo iliyopelekea Wabunge wa Upinzani kuruhusiwa kuchangia. Nilisema kuwa nina umbo dogo lakini nina mambo makubwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lissu pamoja na kujinadi amebobea sheria alishindwa kumshauri Mbowe ili waendeleo kuchangia. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa pamoja na uchungaji wake alishindwa kumshawishi Mheshimiwa Mbowe waendeleo kuchangia humu Bungeni. Mheshimiwa Sugu pamoja na kuzaliwa mjini kashindwa kumshawishi Mheshimiwa Mbowe kuendelea kuchangia humu Bungeni, ni Mlinga pekee ndiye aliyemshawishi Mheshimiwa Mbowe mpaka Kambi Rasmi ya Upinzani wakaendelea kuchangia humu Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakuwa funzo kwa Wabunge wa Upinzani, bila ya mimi mngokuwa mabubu mpaka Bunge hili linaisha. Naomba mpelekeeni salamu baba mkwe wangu, najua haingii Bungeni ananiogopa, aingie mimi ni mtoto wa mjini, nimeshasahau. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote ni mashahidi, hakuna Mbunge aliyekuwa anaikashifu Zanzibar kama Mheshimiwa Tundu Lissu. Wanasema hivi, ukitaka umuamize adui zaidi jifanye kuwa rafiki yako. Mheshimiwa Tundu Lissu alitumia njia ile akaona hailipi, akawageuza Wazanzibar kuwa rafiki yao matokeo yake akawashawishi wasiingie kwenye uchaguzi, CUF kwisha Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa mara ya kwanza wakati ninamsikia Mheshimiwa Tundu Lissu kuwa ni mwanasheria nilishtuka lakini nilipoingia Bungeni nilisikitika baada ya kuhakikisha kweli ni Mwanasheria na Wakili. Hofu yangu, kama ni Mwanasheria na Wakili

ambao tunawategemea kutetea na kututunzia sheria mcharuko kiasi hiki hao waalifu wakoje? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia CHADEMA, upande wa sheria tunamzungumzia Tundu Lissu, katika hiyo hiyo CHADEMA kumekuwa na ukanyagaji mkubwa wa demokrasia. Tumeshuhudia uchaguzi wa Viti Maalum ukikanyagwakanyagwa, kila mwanamke wa CHADEMA aliyechaguliwa kwa Viti Maalum ameingia kwa sifa yake. Sifa kubwa ili uwe Mbunge wa Viti Maalum kupitia CHADEMA lazima uitwe baby. Ushahidi ninao! (Makofi/Kicheko) **[Maneno haya sio sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. Wewe ni teja, teja, teja. (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilindie muda wangu. Wote ni mashahidi...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mnatuletea mateja Bungeni eeh?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilindie muda wangu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Wote ni mashahidi, CHADEMA kuna wanachama wengi wa kike, iweje wachukuwe hadi kutoka CCM? (Makofi)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wote ni mashahidi wa ukanyagaji wa demokrasia unaofanywa na chama ambacho Tundu Lissu ndiyo anakitetea kwenye upande wa sheria. Tumeshuhudia Mheshimiwa Lowassa alivyoingia CHADEMA, ameingia siku hiyo hiyo, amepewa fomu ya Urais siku hiyo hiyo, ametangazwa siku hiyo hiyo. (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanachama wa CHADEMA Jimboni kwangu walikuwa wanasema mimi nimerithishwa, nikawauliza kati ya mimi na Lowassa ni nani aliyepata fursa ya kugombea kwa

kufuata taratibu za demokrasia? Nimepita kura za maoni, sawa, tulikuwa wagombea nane nikawapiga, nikaenda Uchaguzi Mkuu nikakutana na mgombea wa CHADEMA ana umri wa miaka 40 hana jino hata moja nikampiga. (Makofi/Kicheko)

*Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka na Tundu Lissu kwenye utetezi wa sheria anazifahamu sheria za nchi hii na anazifahamu vizuri, lakini kwenye chama chake kumekuwa na uvunjwaji mkubwa wa Katiba na sheria ya nchi. CHADEMA kuna Wabunge wenye mapenzi ya jinsia moja, kuna Wabunge wasagaji. Tundu Lissu analifahamu hilo, angeanza kutekeleza sheria kwenye chama chake ndiyo aje nje. (Makofi/Kicheko) [Maneno haya sio sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa, Taarifa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga, naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Tuzime hapa mpaka atupe nafasi tuongee.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Na bado.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Tukae Waheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Haya Waheshimiwa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Bunge lisiendelee humu ndani.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Bunge lisiendelee mpaka afute maneno yake, Bunge lisiendelee, kila mtu asimame.

**WABUNGE FULANI:** Afute kauli yake.

**MBUNGE FULANI:** Tutapigana ngumi humu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBUSPIKA:** Naomba mkae tusikilizane, naomba mkae tusikilizane, naomba mkae tusikilizane.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna kukaa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mtu asikae chini, wote simameni, Upinzani wote simameni.

**NAIBU SPIKA:** Naomba utulivu, naomba utulivu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, naomba utulivu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mtulie ili nimruhusu mmoja aongee sasa wote mkiniongelesha siwezi kuwaelewa, naomba mkae, tafadhali! Tafadhali, waruhusu watu wako wakae, Mheshimiwa Tundu Lissu, Chief Whip, naomba uwatulize watu wako ili tuendelee na utaratibu. Naomba watu wako wakae.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, Chief Whip wa Kambi ya Upinzani, naomba uwatulize watu wako ili niruhusu mmoja aongee.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Kaeni, kaeni.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Hatuwezi kudhalilishwa kiasi hiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, Utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Muache Mheshimiwa Lissu aongee.

**MBUNGE FULANI:** Pumbavu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Hatuwezi kudhalilishwa kiasi hicho.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Lissu ongea.

**MBUNGE FULANI:** Vigodoro hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul utaratibu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Namuachia *Chief Whip*.

**NAIBU SPIKA:** *Chief Whip*, endelea na utaratibu.

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(f) inakataza Mbunge kumsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote na (g) inakataza Mbunge kutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Vigodoro hivyo.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, maneno ambayo yamezungumzwa na msemaji aliyekaa ni maneno ya udhalilishaji sana wa wanawake. Ni maneno ya matusi, ni maneno ambayo kwa vyovyote vile yanakiuka Kanuni za Bunge ambazo nimezisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama msemaji anabisha hoja ambazo tumezungumza abishie hoja lakini kuzungumza maneno ambayo yako nje ya mjadala, nje kabisa, maneno ya mahusiano binafsi, masuala ya udhalilishaji namna hii ni kinyume cha Kanuni ...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu endelea, Waheshimiwa Wabunge, tumuache Mheshimiwa Tundu Lissu amalize.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tafadhali Kiti chako kichukue hatua stahiki, hii lugha ya aina hii, lugha ya mambo ambayo hayako kwenye mjadala kabisa, lugha ya udhalilishaji wa wanawake ikome.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu ni hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, nadhani tumekumbushwa hapo na Mheshimiwa Tundu Lissu, *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani, ametoa ushauri mzuri sana baada ya kutupeleka kwenye Kanuni ya 64 ambayo inahusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka asubuhi Mheshimiwa Spika, alitutahadharisha kuhusu matumizi ya maneno na kututaka ustahimilivu. Kwa sababu lugha zinazotumika humu ndani kwa pande zote mbili nyingi haziko sawasawa. Nasema hivyo kwa sababu mchana huu, ukiacha asubuhi, pengine upande mmoja haujayasema kwa wingi lakini pia umetumia maneno hata yale ambayo tulishatoa Mwongozo hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba tafadhali ili tuweze kutumia muda wetu vizuri wa kuishauri na kuisimamia Serikali tutumie lugha ya Kibunge. Maneno ya kuita watu wengine ni wajinga, maneno ya kuita watu wengine ni watu ambao wana tabia za aina fulani, tujikite kwenye hoja tuache kutumia maneno mabaya yanayodhalilisha utu wetu lakini pia utu wa wale waliotutuma humu ndani.

Mheshimiwa Goodluck endelea kwa kutumia lugha ya Kibunge. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Tunaomba afute...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimesema hivi, uzuri...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*



**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *Chief Whip* wenu ameshaongea, tusikilizane.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Afute.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maneno mabaya yaliyotumika upande huu hayajafutwa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Afute kauli yake yule.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Afute Kauli yake ya kuwadhalilisha Wabunge wa Viti Maalum, ndiyo achangeie.

**MBUNGE FULANI:** Na atuombe radhi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Hawezi akadhalilisha wanawake.

**MBUNGE FULANI:** Afute kauli, anadhalilisha wanawake.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Madam Spika na wewe ni mwanamke.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama naomba mkae chini.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama naomba mkae chini.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama naomba mkae chini.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, nimesema hivi, tangu asubuhi...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize *Chief Whip* wa upande wa pili, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MBUNGE FULANI:** Wanawake hatutakubali.

**MBUNGE FULANI:** Jenista na wewe ni mwanamke.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa kutumia Kanuni ileile alioisema Mheshimiwa Tundu Lissu ya 64 ambayo inaonyesha mambo ambayo hayaruhusiwi Bungeni. Mheshimiwa Tundu Lissu ameliweka vizuri sana, ameeleza yale masharti ya Kikanuni katika Kanuni hiyo ya 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulichokisema hapo ni jambo la msingi sana ukikubaliana na uongozi wa Kikanuni uliotolewa na *Chief Whip*. Naomba niendeleo kusisitiza kwamba hayo uliyoyatumia kama mamlaka ya Kiti ni mamlaka ambayo yanataka kuonyesha udhahiri wa Kiti chako kwa sababu zimetolewa hapa kauli kwa pande zote mbili. Zimetolewa kauli...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Si msikilize basi?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani, tusikilizane. *Chief Whip* wa upande wa Upinzani ameongea, naomba mumpae nafasi *Chief Whip* wa upande wa Serikali aongee.

**MBUNGE FULANI:** Aombe radhi.

**NAIBU SPIKA:** Naomba aendeleo kumaliza alichokuwa anasema.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge wenzangu kama tutakuwa tunaheshimiana itakuwa vizuri sana. Kwa sababu *Chief Whip* wa Upinzani amezungumza na Kambi ya Chama Tawala tumekuwa kimya sana, tulikuwa tunaheshimu kile kilichokuwa kinasemwa na *Chief Whip*. Kwa hiyo na mimi naomba Waheshimiwa Wabunge mtulie ili na mimi niweze kusema kwa niaba ya Kambi ya Chama Tawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno yaliyozungumzwa ndani ya Bunge leo kwa siku nzima yamekuwa ni maneno mazito na watu wote humu ndani leo wamepokea matusi mazito. Mchangiaji wa Chama cha Mapinduzi aliyemaliza, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge aliyefuata kuchangia mwanamke kutoka Kambi ya Upinzani amesema neno zito sana linalohusiana na tabia... (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya maneno yaliyosemwa na Mbunge aliyekuwa anachangia, tumetukanwa hapa Mawaziri kwamba ni wajinga lakini hakuna mtu aliyesema. (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naamini katika Kiti chako na maneno uliyoyasema wewe, ukifuta kauli zote ambazo zilikuwa na kebehi ndani ya Bunge leo unafanya jambo ambalo ni sahihi. Vinginevyo siyo haki upande mmoja wavumulie kutukanwa na upande mwingine waone matusi ya upande mmoja ni matusi sahihi lakini upande mwingine si matusi sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri hapa jambo la msingi ni kutumia mamlaka ya Kiti kufuta maneno yote ya matusi yaliyosemwa leo ndani ya Bunge toka asubuhi. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Jenista oyeee.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante *Chief Whip*.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumeshawasikia *Chief Whip* wa pande mbili na mimi nilikuwa nimeshatoa maelezo lakini ushauri uliotolewa kwa mujibu wa hiyo Kanuni ya 64, naagiza maneno ya udhalilishaji yaliyotumiwa na upande wa Kambi ya Upinzani na maneno yaliyotumiwa na upande wa Chama Tawala yafutwe katika record za Bunge. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tusianzishe tena mjadala huu kwa sababu tunalo jukumu kubwa mbele yetu, Mheshimiwa Goodluck malizia.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Jamani nilishasema Upogoroni maneno yamechelewa kufika, sijajua kuwa hilo neno lilikuwa zito kiasi hicho, nimelifuta. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangazwa na Kambi ya Upinzani kuhoji habari ya Escrow mpaka leo hii wakati baba mkwe wangu alichukua gari ya Serikali, mafuta ya Serikali, alienda kuchukua dola milioni moja Kenya, Nairobi, mbona Kambi ya Upinzani hamlizungumzii hilo? (Makofi/Kicheko)

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Sijamtaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba...

**MBUNGE FULANI:** Atoe ushahidi.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chief Whip, naomba tumuache Mheshimiwa Goodluck tuendeleo na mchangiaji mwingine, tumeshachoka sasa hivi. (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu yeye maneno yake nimeshayafuta, naomba tuendeleo. Naomba tuendeleo Mheshimiwa Tundu Lissu. Mheshimiwa Augustine Vuma Holle ndiyo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ya mimi kuweza kuchangia kwenye hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria, lakini pia na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kueleza masikitiko yangu kwa hali ambayo imejitokeza jioni ya leo. Ama kweli hii imedhihirisha kwamba mkuki kwa nguruwe lakini kwa binadamu ni mchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja, kwanza napenda kumshukuru Mzee wangu Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa kutuonyesha umahiri wake leo tena kwa kupitia hotuba yake ambayo ameitoa hapa. Napenda kulikumbusha Bunge hili kwamba umahiri wa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe haujaanza leo, huyu ndiye aliyeongoza Kamati ambayo ilimuondoa madarakani fisadi papa namba moja Ndugu Edward Ngoyai Lowassa. Mzee Mwakyembe tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe yako mambo machache ya kukushauri tu mzee wangu. Suala la kwanza ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya 2006...

**MBUNGE FULANI:** Anasoma.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Kifungu 32(1), nanukuu, kinasema; "Mfanyakazi atakuwa na haki ya likizo ya ugonjwa angalau siku 126 kwa kila mzunguko wa likizo."

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limeleta utata wakati mwingine kwa sababu wako wagonjwa ambao wameugua zaidi ya muda huu. Naomba sana kipengele hiki kiweze kurekebisha ili watu wapate nafasi ya kuweza kutibiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la wafanyakazi wa migodini. Watu hawa wamekuwa wakifanya kazi ngumu na wakati mwingine kulingana na mazingira duni ya migodini wamekuwa wakipata shida au matatizo ya kiafya na mara baada ya kupata matatizo ya kiafya huwa wanaachwa na waajiri wao na hatimaye wanakuwa maskini wakubwa sana. Kwa hiyo, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwenye majumuisho hili nalo alizungumzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejikita tena kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni...

**MBUNGE FULANI:** Wewe Waziri?

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 11, Mheshimiwa Tundu Lissu anasema kunyamazisha upinzani na kukaribisha udikteta. Labda niwakumbushe watu hawa kwamba upinzani umejiua wenyewe yaani wamejikaanga kwa mafuta yao wenyewe. Moja, wamejikaanga kwa unafiki wao uliopitiliza, nitasema hapa ambao hasa umeongozwa na huyu huyu ambaye ni Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria.

*Mheshimiwa Tundu Lissu ndugu yangu, nimekuwa nikifuatilia siasa zako kwa muda mrefu sana na wakati mwingine nimekuwa nikikaa chini na kutafakari sana lakini jioni ya leo nimefanya majumuisho yangu ikatosha kabisa kuamini haya maneno ambayo nakutana nayo mtaani kwamba unalo file Mirembe ni sahihi kabisa. (Makofi/Kicheko)* **[Maneno haya sio sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze, kitu cha kwanza...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Kwanza wakati anachangia hapa...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Taarifa.

**MHE TUNDU A. LISSU:** Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Holle naomba ukae, Mheshimiwa Tundu Lissu.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu na naomba nitumie Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inakataza Wabunge kusema uongo. Kwa sababu ukimtumumu Mbunge kusema uongo unatakiwa uthibitishe wewe kwanza halafu ndiyo yeye athibitishe, sasa naomba niseme yafuatayo kuhusu hilo linaloitwa *file* la Mirembe.

Mimi Mirembe nafahamu iko mahali fulani kwenye Mji wa Dodoma, sijawahi kuingia getini Mirembe, sijawahi kwa namna yoyote ile kuhusishwa,

sijawahi kuingia Hospitali ya Mirembe, sijawahi kuugua ugonjwa wa akili, sijawahi na haya sijui kama ni mambo ya kucheka sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sheria za Tanzania ukiwa mgonjwa wa akili mwenye *file* Mirembe, kwa mujibu wa Katiba ya nchi hii na sheria zake huruhusiwi kugombea nafasi yoyote ya uongozi. Huruhusiwi kuingia kwenye mikataba kwa sababu sheria inasema wanaoingia kwenye mikataba ni watu wenye *legal capacity*, kama una *file* Mirembe huwezi ukaingia mikataba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno ya uongo, huyo anayesema nina faili Mirembe ni vizuri alithibitishie Bunge lako kwa mujibu wa taratibu zilizopo kwenye Kanuni hizi. Athibitishie kwa mujibu wa Kanuni hizi na kama atashindwa kuthibitisha Kanuni hizi zimeweka utaratibu wa hatua za kuchukua.

Kwa hiyo, naomba tafadhali hii kauli ya *file* la Mirembe ithibitishwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (Makofi)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia, naomba ukae.

Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Kanuni ya 64(1)(a) inasema; “Mbunge, hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha (2), kwa sababu Mheshimiwa Tundu Lissu ameshatoa maelekezo haya, kinanitaka mimi nitoe maelekezo ama Mwongozo kwako. Kwa kutumia Kanuni ya 73(2) nakupa fursa urekebishe kauli hiyo ama kama hukurekebisha kauli hiyo kwa kufuta hayo maelezo basi hapo nitaendelea vingine, tafadhali!

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, ngoja nimalize Mwongozo huu kwanza.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Hapo hapo kwenye Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Holle endelea.



**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba kwa taarifa zilizozagaa na ambazo kila Mtanzania anazifahamu... (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba wagonjwa wa namna hii kwao wako wengi, mbona Mheshimiwa Mnyika yuko Muhimbili naye anatibiwa hivyo hivyo tu.

**MBUNGE FULANI:** Ooooooh.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa mujibu wa Kanuni nifute kauli hiyo ya Mirembe na naomba kuendelea na unilindie muda wangu. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Na ya Mnyika ifutwe.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilisema hayo kwamba nimejiridhisha na kauli hizo za mtaani kwa sababu moja ya unafiki...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Tulia, tulia. Ni kwa sababu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Holle, tafadhali, umeshafuta hiyo kauli, naomba uendelee kuchangia.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mtu huyu amekuwa ni mnafiki namba moja katika nchi hii. Nitathibitisha unafiki na uongo wake.

Kwanza wakati anachangia hapa amesema eti anashangaa kwa nini Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania hajastaafu wakati aliosoma nao wamestaafu, anashindwa kujua kwamba siyo kila unayesoma naye umri wake ni sawa. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Muda wa kufanya kazi siyo muda wa kuishi wewe.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Amesema aliosoma nao. Wakati mimi nasoma nimesoma na watu ambao wana umri wa baba yangu lakini mtu huyu ni msomi na anajua mambo yote haya anaamua kupotosha Taifa kupitia chombo kitakatifu cha Bunge kwa makusudi kabisa. Ndiyo maana nasema unafiki huu unanirejesha kwenye hizi *rumors* ambazo nimesikia mtaani.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, la pili...

**MBUNGE FULANI:** Hajafuta huyu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Holle, hii ni nafasi ya mwisho kuhusu jambo hilo.

**MBUNGE FULANI:** Huyu vipi huyu?

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo nimeshafuta na mimi naendelea na mchango wangu. Sasa kama unaniambia kwamba niache kuchangia kwa kumzungumzia mtu huyu...

**MBUNGE FULANI:** Acha.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Hapa nafanya hivyo ili kuweka *record clear*, kwa namna ambavyo amepotosha Bunge, kwa namna ambavyo ... (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Holle ongea na Kiti, endelea.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu. Wewe unataka nini?

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilindie muda wangu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, naomba urudi kwenye kiti chako.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, naomba urudi kwenye kiti chako.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** *Sergeant at arms*, naomba mumtoe Mheshimiwa Waitara nje. *Sergeant-at-Arms* mtoeni Mheshimiwa Waitara nje.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilindwe kwa mujibu wa Kanuni. Nimekuja hapa kwa mujibu wa Kanuni.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Inauma eeh?

**MBUNGE FULANI:** Inauma sana.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** *Sergeant at arms* mtoeni Mheshimiwa Waitara nje.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Ninyi muacheni achangeie.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Holle naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Holle naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Sergeant-at-Arms mtoeni Mheshimiwa Waitara nje tuweze kuendelea, tafadhali.

*(Hapa Mheshimiwa Mwita M. Waitara alitolewa Nje ya Ukumbi wa Bunge)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Katibu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Wewe endelea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza michango, tunaendelea na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ili wahitimishe hoja. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Muda wetu bado.

**MBUNGE FULANI:** Sasa Mnyika amefanya nini?

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Bunge ni mbaya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba uendelee.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Huku watu wanatu...

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii kwa mara nyingine niweze kuchangia hoja hii muhimu sana ya Waziri wa Katiba na Sheria. Nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa fursa hii na nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na niseme moja kwa moja kwamba naiunga mkono hoja hii.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, naomba sasa nijielekeze kutoa ufafanuzi na ushauri kwenye hoja mbalimbali ambazo zimeelezwa na Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze na yale ambayo nimeyasikia kutoka kwa Wabunge hapa. Waheshimiwa Wabunge wameleta mapendekezo, kwa mfano Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Maige wameleta mapendekezo ya kufanya mabadiliko kwenye Sheria hii ya Manunuzi ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba katika Mkutano huu wa Bunge Serikali italeta Muswada wa Marekebisho ya Sheria hii ya Manunuzi. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mjiandae wakati utakapofika mchangie kukosoa ubovu wa ile sheria iliyopo sasa hivi ili tuwe na sheria nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nichukue fursa hii kujibu hoja ambayo imezungumzwa na Mheshimiwa Makamba ambapo alikuwa anasisitiza juu ya umuhimu wa wanafunzi wanaosoma Shule ya Sheria kwa Vitendo ya Tanzania kupata mikopo. Niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Bunge hili mliswapitisha sheria, katika Bunge la mwezi wa kumi mpaka wa kumi na moja mwaka 2014 ambayo inawapa haki sasa wanafunzi wanaosoma Shule hii ya Sheria ya Tanzania kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Mtolea amezungumza akishauri kwamba pengine ingekuwa vizuri kwamba wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria basi Kamati ya Sheria Ndogo nayo ingekuwa inatoa taarifa. Naomba kushauri tu kwamba ile Kamati haiwezi kutoa taarifa kwa sababu sio Kamati ya Kisekta. Kwa hiyo, hii Kamati ina muda wake huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kulitolea ufafanuzi katika hoja ambazo nimesikia kwa Waheshimiwa hapa ni kuhusu

mapendekezo ambayo yameletwa na Mheshimiwa Holle kuhusu umuhimu wa kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba katika Mkutano huu wa Bunge hili pia Serikali italeta Muswada kwa ajili ya marekebisho ya sheria mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue fursa hii kuzungumza mambo ya msingi sana ambayo yamejitokeza ndani ya Bunge hili Tukufu.

Kwanza nianze kwa kuwatahadharisha na kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba Ibara ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa ile Ibara ndogo ya (2) inasema; "Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake."

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo msingi ambao pia umewekwa kwenye Kanuni ya 64 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni ya 64(1)(f) na (g) zinasema, Mbunge; "(f) hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote na (g) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo msingi ambao unapaswa utawale. Kwa sababu hizi Kanuni ambazo zina msingi wake kwenye Katiba, Ibara ya 12, zikitawala Bunge litaendeshwa kwa amani na Waheshimiwa Wabunge mtajikita tu kwenye hoja, mtawasaidia wananachi wenu ambao wanawasikiliza na ambao wamewatuma ili mje muwatete.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hizi nimeona mambo haya ya kudhalilishana yakijitokeza na mambo yameanzia kwenye hotuba rasmi ya Kambi ya Upinzani. Naomba kushauri kwamba hatupaswi kufikia hatua hiyo. Nianze na hili la kuwaita Majaji kama majipu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 30(2)(d) inalinda hadhi na uhuru wa mahakama na heshima yao. Ibara hii inasema hivi, naomba kunukuu yaani; "ni wajibu wa kila mtu na kila raia kulinda sifa, haki na uhuru wa watu wengine au maisha binafsi ya watu wanaohusika katika mashauri mahakamani; kuzuia kutoa habari za siri; kutunza heshima, mamlaka na uhuru wa mahakama."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona imezungumzwa vibaya hapa, Waheshimiwa Majaji wakiitwa majipu, hiyo ni kuwavunjia heshima yao. Pia ni kuudhalilisha mhimili wa Mahakama ambao tunapaswa tulinde heshima yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu fulani kwenye hotuba hii imezungumzwa kwamba sasa hivi Majaji hawa siyo watakatifu na kweli hakuna mtu ambaye ni mtakatifu lakini wanaishi kwa kuzingatia Katiba na sheria. Wao katika Ibara ya 107 Katiba inasema watakuwa huru wanapotekeleza majukumu yao isipokuwa tu watapaswa kuzingatia masharti ya Katiba hii na sheria za nchi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kushauri kwamba tunapokuwa tunazungumzia ama mtu au mihimili tutumie lugha fasaha ili kulinda hadhi na sifa za mihimili mingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hii haikuwa sahihi pia kumzungumzia Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa namna ambayo imezungumzwa, ni kinyume cha Ibara ya 12 ya Katiba na Kanuni kwa sababu Kanuni yenyewe ya 64(1)(c) inakataza hata unapojadili kutolitumia vibaya jina la Jaji, Rais na kumuongelea mtu ambaye hayupo.

**MBUNGE FULANI:** Anapotosha.

**MBUNGE FULANI:** Usimjibu yeye.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba mambo haya tuyazingatie sana tunapotekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa sababu ya kulinda hadhi na thamani ya utu ambao umewekwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sharti tuheshimu mamlaka ya viongozi wa Serikali walioko.

Sehemu fulani katika hotuba hii imezungumzwa kwamba Rais Shein ni kibaraka. Rais Shein kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar huyu ni Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, utamwitaje Rais wa nchi kwamba ni kibaraka. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Kibaraka.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Huku ni kumdhalilisha kitu ambacho kimekatazwa na Kanuni zetu za Bunge, ni kumvunjia hadhi, ni kuidharau mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hili halipaswi kusemwa na Wazanzibari wako hapa halafu wanashangilia *that is too much odd to me*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe tu kwamba sisi Wabunge tunapokuja hapa tunakula kiapo. Kwa mujibu wa Ibara 68 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatupasa tule Kiapo cha Uaminifu. Kanuni ya 24 ya Kanuni za Kudumu pale kuna kiapo cha utii na ambacho kinasisitiza kulinda na kuhifadhi Katiba, wote tumeapa hapa. Muungano huu upo kwenye Katiba na



ni kwa sababu ya Muungano huu ndiyo maana leo tuko hapa na ndiyo maana tunapata fursa ya kuzungumzia wananchi wetu na kutoa hoja mbalimbali za kuisaidia Serikali. Kwa hiyo, mimi naomba tuheshimu viapo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar haiwezi kuwa koloni. Ukisoma Ibara ya 1 ya Katiba ya Zanzibar inasema hiyo ni nchi ambayo kabla ya Muungano ilikuwa ikiitwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar. Ibara ya 2 inasema, Zanzibar ni mojawapo ya nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano Tanzania. Sasa leo Zanzibar itakuwaje tena koloni? Lazima muelewe haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, si kweli kwamba Zanzibar imekuwa koloni la Tanzania, Zanzibar ni mamlaka halali. Ibara hii ya 1 na ya 2, ukiacha tu makubaliano ya 1964 (*Articles of Union*) zimepitishwa baada ya kupigiwa kura ya maoni na Wazanzibari wote wakakubali ule Muungano. Kwa hiyo, si vizuri kutumia fursa hii kuwavuruga wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Ibara ya 28(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inataka kila raia pamoja na mambo mengine alinde, adumishe na kuhifadhi umoja wa Taifa letu. Ibara ya 23(4) ya Katiba ya Zanzibar nayo inawataka Wazanzibar kudumisha umoja wa Wazanzibar. Mimi naona kama tunakuwa salama sana tunapokuwa tunadumisha umoja kuliko kuja kutofautiana hapa kwa sababu ambazo wala hazina sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba Ibara ya 20(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inakataza vyama vya siasa kupigania kuvunjwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huwezi kuwa umekula kiapo cha kuitii Katiba ambayo ina masharti ya kutokusajili vyama vinavyopigania kuvunjwa kwa Muungano wa Tanzania halafu ukabaki Bungeni. Mimi nafikiri umefika wakati sasa mamlaka zinazohusika zichukue hatua. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nizungumzie hili la hati ya mgawanyo wa madaraka ya Rais. Nimesema sana hapa na naomba nirudie tena kwa sababu ni kazi yangu. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawakuwepo na nalazimika kuirudia hii ili niweke record sawa.

Moja, Mawaziri hawa wanateuliwa na Rais kwa mujibu wa Ibara ya 55 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanakabidhiwa majukumu yao chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mawaziri, Sura ya 299 halafu kuna hiyo hati inaweza ikatolewa na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mchengerwa amelifafanua vizuri hili, nilimuona Mheshimiwa Tundu akimpigia makofi na mimi nimeshalisema siku nyingi sana yaani hata kulisema naona kama nachoka. Kwa sababu neno linalozungumzwa pale katika ile kifungu cha 5 linasema, *the president 'may' from time to time* na matumizi ya neno 'may' limetafsiriwa vizuri kabisa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kifungu cha 53 kinaeleza nini maana ya maneno 'may' na 'shall' yanapotumika katika sheria. Neno 'may' linaashiria hiari na 'shall' inaashiria lazima, kwa hiyo, hili lisingekuwa ni tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hali ya kawaida hata Waheshimiwa wasomi wanafahamu kwamba sheria ndogo (*subsidiary legislation*) haiwezi ika-supersede sheria kuu, ile sheria yenyewe ya Utekelezaji wa Majukumu au Katiba. Rais alipokuwa anatangaza zile Wizara alisema kabisa, kwa mfano Wizara inaitwa Wizara ya Maliasili na Utalii...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa hiyo, unajua kwamba haya ni majukumu yao. Kwa hiyo, kutoitoa ile hati hakuwa amevunja Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze pia kwamba Sheria hii ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mawaziri inasema ikiwa kuna jambo lolote labda linachunguzwa Mahakamani au *is likely to be inquired in the court*, basi hawa watu wataenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakachosema ni kwamba suala hili linaangukia dhamana ya mtu fulani au Wizara fulani ndiyo mwisho wa hilo suala, kwa hiyo, sheria yenyewe haimlazimishi Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwaambieni Kanuni zinatukataza kusema uongo. Jana niliwaambia na wiki iliyopita nilisema mpaka nikawapa waandishi habari, gazeti la Sauti ya Watu Daima liliandika kwamba Rais alishatoa hiyo hati tangu tarehe 22/04/2016...

**MBUNGE FULANI:** Iko wapi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kupitia *government notice* ambayo ni *public notice*.

**MBUNGE FULANI:** Iko wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Mdee, naomba mumuache Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amalize.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili halipaswi kutusumbua sana. Ni suala ambalo linaletwa labda kwa namna ya kupotosha tu. Haiwezekani kwamba *subsidiary legislation* ika *supersede* sheria kuu na hata Katiba yenyewe.

**MBUNGE FULANI:** GN namba ngapi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ni GN namba 144...

**MBUNGE FULANI:** Iko wapi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ya tarehe 22 Aprili, 2016.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa AG naomba uongee na Kiti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Wewe ongea na Meza usiwasikilize hao.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kutakuwepo kwa hiyo, haisaidii kwa sababu Mawaziri na Serikali yote inafanya kazi kwa mujibu wa Katiba, sheria, sera na Ilani ya Uchaguzi ya chama kinachotawala. Mpaka sasa hivi hakuna mtu yeyote aliyekwenda mahakamani au aliyekuja kuniuliza mimi kwamba hivi suala hili linaangukia kwenye dhamana ya nani? Rais hakupewa muda kwamba ndani ya muda fulani awe ametekeleza suala hili. Kwa hiyo, mimi naomba kushauri hili suala labda sasa kama Kiti chako kinaweza kuamua kiamue kwa sababu tumelisemea mno halina tija kwa Watanzania. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Eeeh?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais huyu ambaye amezungumzwa hapa kwamba anatawala kiimla Rais huyu hatawali kiimla. Ibara ya 33 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema Rais ni Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Kama kiongozi wa Serikali katika mgawanyo wa madaraka, Serikali ina mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa sheria, anachokifanya sasa Rais ni kutukumbusha turejee kutekeleza sheria kwa ufanisi. Hata haya mambo yanayofanyika ya uwajibishaji ni katika kuturejesha katika uzingatiaji wa sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais mwenyewe ana mamlaka chini ya Ibara ya 36 ya Katiba kuwawajibisha hata wale ambao hakuwateua, lakini pia Mawaziri wana mamlaka ya kuwawajibisha wale ambao wanawateua, Makatibu Wakuu na Bodi zina mamlaka ya kuwawajibisha wale ambao

wanawateua. Mtu ambaye anadhani ameonewa Mahakama iko pale aende akatafute haki yake. Watanzania wengi sana ambao walidai wameonewa wameenda mahakamani wamepata haki zao. Kinachofanyika hawafukuzwi, wanachoambiwa ni kwamba wanawekwa pembeni ili wakachunguzwe na wakati wa kuchunguzwa wanapewa fursa ya kujitetea.

**MBUNGE FULANI:** Naam!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kama wana hatia basi wanawajibishwa, kama wengine wana makosa ya jinai wanashtakiwa. Kwa hiyo, hili sasa halipaswi kurudiwarudiwa hapa kila siku kana kwamba ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba kulizungumzia ni suala la kudai kwamba Bunge linaongozwa na Ikulu hii si kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ibara ya 62 ya Katiba inamtaja Rais kuwa sehemu ya Bunge hili na Ibara ya 63 ndiyo inasema Bunge ndicho chombo kwa niaba ya wananchi kina jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali. Rais huyu huyu ambaye ni sehemu ya Bunge hili ndiye anayelipa hata hizo posho kwa masharti yenu yale. Masharti ya posho zile mpaka ziidhinishwe na Rais.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ya matangazo ni mambo ambayo iliamuliwa na ikapitishwa humu kwamba matangazo sasa yafanywe na studio ya Bunge na Bunge likapitisha hapa Sheria ya Matumizi ya Fedha. Kwa hiyo, siyo sahihi kudai madai hayo. Halafu mnawachonganisha viongozi wa Bunge, Bunge ni mhimili ambao hauwezi kuingiliwa tu na Serikali itauingiliaje?

**MBUNGE FULANI:** Wewe siyo Msemaji wa Bunge.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mimi ni Msemaji wa Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Ongea na Kiti.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala hili mimi nashauri Kiti chako kilichukulie hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru kwa michango yote na ningeomba tu usikivu kwamba sijaja hapa kujibizana na mtu. Mimi sifanani kabisa na yule jamaa aliyekuwa anaoga, kichaa akaja akachukua nguo zake akaanza kumfukuza, kwa hiyo, mimi nabakia kwenye maji. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa George Masaju kwa kuungana na mimi katika kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile na kwa namna ya pekee kabisa niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa maoni na ushauri wao kwa kweli uliokwenda shule. Maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge na ya Kamati ya Kudumu ya Bunge tumeyachukua kama Wizara na tunaahidi kuyafanyia kazi na kuyatolea majibu kwa maandishi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa wengi wameongea na wengi wametuletea kwa maandishi hivyo nashindwa kupata idadi maana zinakuja karatasi mpaka sasa lakini kama nilivyosema majibu tutaleta kwa maandishi na muda nilionao ni mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya hoja zimeletwa hapa chache nitazijibu kwa haraka haraka. Hoja ya kwanza ya Kamati ni kuhusu deni la mkataba wa ubia wa jengo la *RITA*. Naomba kusema kwamba mazungumzo tayari yanaendelea kati ya taasisi zinazohusika na ubia huu wa jengo la *RITA*. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba tunaishauri Serikali kulitwaa deni hilo na kupunguza ongezeko la deni linaloendelea katika mradi huu wa ujenzi huu wa jengo la *RITA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kifuata sheria za *NACTE* na walimu wawe na sifa za shahada na uzamifu za kufundishia vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto tukumbuke wote kilianzishwa mwaka 1988 kwa ajili ya kutoa mafunzo endelevu kwa Majaji, Mahakimu na watumishi wa Mahakama. Kwa kweli chuo hiki kimefuata miundo kabisa ya vyuo vingine vilivyopo Kenya, Afrika Kusini na Canada vinavyotoa ujuzi wa kuboresha utendaji wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tunaweza kufika huko lakini kwa sasa tumejikita na lengo la awali la kutoa mafunzo endelevu kwa Majaji na Mahakimu na watumishi wa Mahakama lakini baadaye kama hali kwa kweli ita-demand tuanze kutoa mpaka degrees tutafanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya kufanya mapitio ya kisheria kuhusu adhabu ya kifo ili tuifute hapa Tanzania. Naomba tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba utafiti uliofanyika mwaka 2009 na Tume ya Kurekebisha Sheria ulionyesha kuwa Watanzania wengi bado wanataka adhabu ya kifo iendele. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema hivi kutokana na vitendo vya kikatili na vya kutisha kama vile kuwakata viungo wenzao hasa kwa mfano ndugu zetu wenye ualibino, kuua vikongwe, kuua watoto wachanga na huko nyuma kulikuwepo na mchezo wa kuchunana ngozi. Kutokana na hayo, Watanzania wengi wanaamini kwamba kuendelea na adhabu hii ni tishio zuri, *it is a deterrent* ambayo hatuwezi kuachana nayo haraka haraka hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja kwamba Mahakama ihakikishe ufanisi na ufasaha katika umaliziaji wa mashauri kwa kuzingatia kuwa *justice delayed, is justice denied* na kwamba *justice hurried is justice buried*. Nakubaliana kabisa na Kamati kwamba katika kuharakisha sana kumaliza hizi kesi tunaweza kujikuta kweli tunakanyaga baadhi ya haki za watu. Naomba tu Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba tulikuwa na mzigo mkubwa sana wa kesi (*backlog*). Mimi naipongeza sana timu ya uongozi wa Mahakama ya sasa kwa kuhakikisha kwamba tunaondokana na huu mzigo wa kesi na baada ya mwaka mmoja au miwili tutarudi sasa kukazania kuhusu *substance* na *quality* ya *judgements* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka kuzungumzia kuhusu mchakato wa Mahakama ya Kadhi. Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali anasema mchakato wa kuanzisha Mahakama ya Kadhi umeishia wapi?

Mimi niombe tu kusisitiza kwa Mheshimiwa Ngwali kwamba kimsingi Mahakama ya Kadhi ipo na inafanya kazi. Serikali ilichotaka kukifanya katika Bunge la Kumi kwa wale tuliokuwepo hapa ni kuyapa nguvu ya kisheria maamuzi yanayotokana na Mahakama hiyo kupitia sheria ya Bunge. Mliokuwepo mnakumbuka kwamba katika Bunge la Kumi Serikali ilipowasilisha Muswada huo wa Mabadiliko ya Sheria ulikabiliwa na upinzani mkubwa siyo tu ndani hata nje ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai mengi yalikuwa kwamba hatukulifanyia hili suala kazi ya kutosha kuwahoji Watanzania wengi inavyostahili. Vilevile nje ya Bunge kulikuwa na mhemko mkubwa wa mawazo kiasi cha wananchi wawili

kumfungulia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kesi mbili. Alikuwapo, wote mnamkumbuka, Marehemu Mchungaji Christopher Mtikila alimfungulia kesi Mwanasheria Mkuu Mkuu wa Serikali kuhusu hili hili suala, kesi namba 7 ya mwaka 2015. Vilevile alikuwapo Shehe Rajabu Katimba na wenzake nao wakamfungulia kesi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tukalazimika kuliondoa suala hili Bungeni kwa lengo la kulifanyia kazi zaidi na suala hilo tayari tumelipokea rasmi kutoka Serikali ya Awamu ya Nne na sasa tunalifanyia kazi. Si suala jepesi maana lengo ni kupata muafaka wa Watanzania tuweze kuishi vizuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ngwali vilevile naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana kwa kunikumbusha kuhusu *The Waqf Commission* na vilevile Dkt. Suleiman naye alituongezea elimu yake kuhusu suala hili na sheria yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ni kwamba sheria hiyo haipo ila vipengele vyake vimekuwa *incorporated* kwenye *Probate and Administration of Estate Act*, Sura ya 352 na ukiangalia kifungu cha 142 kinaongelea kuhusu hiyo *Waqf Commission*. Namuomba Mheshimiwa Ngwali aniamini, nitalifuatilia. Nimekushukuru *to bring it to my attention*. Tuna sehemu ya kujifunza, wenzetu Zanzibar Sheria yao ya *Waqf and Trust Commission* inaweza kutoa mafunzo mazuri kwetu lakini kama nilivyosema nimelichukua hilo, nakushukuru sana kwa kunikumbusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka amelalamika sana kuhusu Mahakama Wilaya ya Muleba hasa za Mwanzo, zinajisahau kama ni Mahakama. Anasema Mahakimu wamekuwa kama machifu wadogo wadogo kule. Vilevile Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu amelalamikia Mahakama za Mwanzo Wilayani Igunga kufikia mpaka kuwabambikizia wananchi kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme mawili, unapofikia mahali ambapo hujaridhika na uamuzi wa mahakama hizo za chini na ili tusiingilie uhuru wa mahakama, tafadhali Waheshimiwa Wabunge tuwatie moyo wale ambao wamesikitishwa wakate rufani. Siyo hivyo tu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusiwe sehemu ya watu wanaolalamika, tuwe sehemu ya watu ambao wanasaidia *kui-operationalise*, kuitekeleza Sheria ya mwaka 2011 ambayo inaunda *District Ethics Committees* za watumishi wa mahakama. Kila Wilaya inatakiwa iwe na Kamati ya Wilaya ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama. Sasa Wabunge tuhakikishe tunapofika Wilayani kwetu tumuulize Mkuu wa Wilaya kama tayari ameunda Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii itatusaidia sana kwa sababu Wajumbe wake ni Mkuu wa Wilaya ambaye anakuwa Mwenyekiti lakini wapo



walioonesha kwamba ni tatizo kubwa hilo kwa Wakuu wa Wilaya kuwemo humo. Tulilijadili vizuri hapa, litakwenda vizuri kama Waheshimiwa Wabunge mtasaidia katika kuhamasisha hizi Kamati ziundwe haraka na tuweze kurejesha nidhamu hasa kwenye Mahakama zetu za chini. Mbali na Mkuu wa Wilaya tunaye DAS pale ndiye anakuwa Katibu. Mkuu wa Wilaya anateua Wajumbe wawili mmoja kiongozi wa dini anayeheshimika anaweza kuwa muislamu au mkristo na mtu wa pili atakuwa ni mzee mwenye heshima katika jamii ambaye kila mtu ukisema ameteuliwa wanasema sawa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Jaji Mfawidhi katika eneo husika atateua wajumbe wawili ambao ni Wanasheria, wanaweza kuwa Mahakimu na Hakimu wa Wilaya vilevile anakuwa ni sehemu ya hiyo Kamati. Kwa hiyo, madudududu kama hayo yapelekwe moja kwa moja kwenye hiyo Kamati. Hiyo Kamati haina mamlaka ya mwisho itapeleka mapendekezo yake kwenye *Judicial Service Commission* ambacho ni chombo cha kikatiba. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tukifanya vizuri hapa, tunaweze tukaleta mabadiliko makubwa sana badala ya sisi kuwa tunalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa George Lubeleje ameongelea uhitaji wa miundombinu ya Mahakama katika Wilaya ya Mpwapwa. Mheshimiwa Omary ameongelea Wilaya ya Kilindi, nafikiri wengi wameongelea suala hili.

Waheshimiwa Wabunge, katika hotuba yangu nimeeleza kuwa tuna tatizo kubwa la miundombinu ya mahakama. Kama nilivyosema, *the ideal situation* tulitakiwa tuwe na mahakama zinazofanana angalau na kata tulizonazo maana tunaamini kuwa *proper access to justice* nchini kwetu inahitaji mahakama moja katika kila kata. Tuna kata 3,957 lakini tuna Mahakama za Mwanzo 976 tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naupongeza sana uongozi wa Mahakama chini ya Jaji Mkuu Othman Chande na Mtendaji Mkuu Katanga kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kipindi kifupi sana kwa kuanza kampeni ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Wilaya na kwa kweli hata Mahakama Kuu, hata jengo la Mahakama ya Rufani hatuna. Kwa hiyo, tulikuwa tumelala kidogo kipindi kirefu sasa hivi ndiyo tumeamka na hawa watu wanahitaji kutiwa moyo sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameliezea vizuri sana suala alilokuwa analalamikia mdogo wangu Mheshimiwa Tundu Lissu hapa kuhusu *instrument* ya mpangilio wa kazi za Mawaziri. Kaeleza vizuri kwamba mbona *instrument* ilishatoka? *Tt the same time, it is not such a big deal* mpaka Mheshimiwa Tundu Lissu unasahau kwamba sisi ni kaka zako, tumekusomesha sisi mpaka unaongea maneno

mazito kutuita wajinga lakini sasa walimu wako wakiwa wajinga wewe unafikiri utakuwa nani? *You could even be worse than that.* Kwa sababu sisi kwenye Wizara bahati mbaya ni kaka zako. Niko na Profesa Mchome pale, ni mwalimu wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais anapoteua Mawaziri anatumia Katiba, Ibara ya 55. Akishamteua Waziri kuna *condition* moja tu inakuwa imebaki ili Waziri aweze kufanya kazi siyo lazima iwepo *instrument!* Ibara ya 56 inasema; “Waziri au Naibu Waziri hatashika madaraka yake ila mpaka awe ameapa kwanza mbele ya Rais Kiapo cha Uaminifu na pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kinachowekwa kwa mujibu wa sheria inayotungwa na Bunge.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna *instrument* hapa ili uwe Waziri! Rais anaweza akaacha hata akakaa miaka mitatu bila *instrument* lakini Serikali ikaenda. Maana tumefika mahali pa kuona kuwa hata Waziri Mkuu alikuwa anafanya kazi bila uhalalai, hapana! Tusome vizuri Katiba Ibara ya 52 imempa kazi ya kufanya Waziri Mkuu. Inasema; “Waziri Mkuu atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.”

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema tu kwamba tusilitie chumvi sana hoja hii, tukafika mahali kusema kwamba tulikuwa tumepotea, hapana! Hii ni Serikali ya Awamu ya Tano, Rais anafanya mabadiliko makubwa katika mfumo wa Serikali ilibidi tumpe muda kuweza ku-come-up na hiyo *instrument* ambayo tayari alishaitoa. Watanzania bahati nzuri mimi nafurahi kwamba wame-*appreciate* kazi anayoifanya ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kakunda yeye anadai ameachia Ofisi ya Mbunge Sikonge ili iwe ya Mahakama. Dah! Sasa hapa ni kazi kwa sababu siyo kila ofisi inaweza ikatosha kuwa Mahakama na Ofisi ya Mahakimu. Mimi nashukuru tu kwamba umetupa hiyo ofisi, kwa heshima na taadhima tutafika kuiangalia. Nitaongea na Mtendaji Mkuu wa Mahakama aangalie kama miundombinu ya kuweza kufanya hiyo kazi ipo. Cha msingi ni kwamba Sikonge tumeiweka kwenye orodha ya Wilaya ambazo tutazijengea Mahakama, uwe na subira tu, usiende haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Manunuzi, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nakushukuru sana umelijibu, umelimaliza suala hili. Haikuwa kazi rahisi Waheshimiwa Wabunge kuipitia sheria hii. Wengi wanaisema tu hawajawahi kuona wala kuosoma. Mimi ningesema nipitisha mtihani hapa, sitaki kusema! Maana hii sheria ina vifungu 108, ina majedwali makubwa matatu na ina Kanuni zake 380 na majedwali ya Kanuni 19.

Watanzania hatupendi kusoma tunakimbilia tu magazeti ya Tanzania Daima na kadhalika, lakini hii *document* iko hivyo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu ni mfupi sana, Mheshimiwa Koshuma naye ameongelea kuhusu Sheria ya Ndoa. Tulishasema hili suala Serikali imelipa kipaumbele sana. Katika Mkutano huu huu nilishasema, hata hivi juzi nilisema tutaleta mapendekezo ya kubadilisha Sheria ya Elimu ili mtoto yeyote ambaye yuko shule ya msingi na sekondari ni marufuku kuoa au kuolewa na ni marufuku kupata mimba! Sasa hiyo marufuku tutaismamia namna ya kuifanya, tutaleta hapa ninyi wenyewe ndiyo wazazi mtaona hiyo marufuku ya kupata mimba tutaifanyafanyaje. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa anasema kwamba eti Serikali inashindwa kesi nyingi sana! Unachosema una uhakika nacho? Unajua hili Bunge linahitaji *facts*. Mimi sasa nafikiri nitakuja hapa niwaeleze jinsi ambavyo vijana wetu wanavyofanya kazi nzuri na ya ajabu sana katika mazingira magumu sana. Tuna Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanafanya kazi kubwa sana *under extremely difficult conditions* lakini wanashinda kesi dhidi ya matajiri, watu wenye kesi kubwa na Mawakili wanaolipwa sana, vijana wetu hata nyumba za kukaa hawana. Kwa hiyo, tusiwakatishe tamaa vijana wetu, kazi wanayoifanya ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu haraka haraka mambo mawili, matatu. La kwanza, Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa anauliza hivi Jaji Mkuu atastaafu lini? Mimi namwomba mdogo wangu awe anasomasoma hii Katiba kwani Ibara ya 120 ina majibu, sikutegemea wewe ulize swali hilo.

**MBUNGE FULANI:** Ana umri gani?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ana umri gani? Jibu lipo hapa kwenye Ibara ya 120(2) ambayo inasema kwamba; “Jaji yeyote wa Rufani aweza kustaafu Ujaji wa Rufani wakati wowote baada ya kutimiza umri wa miaka sitini, isipokuwa kama Rais ataagiza kwamba asistaafu, na iwapo Rais ataagiza hivyo basi, huyo Jaji wa Rufani atakayehusika na maagizo hayo ya Rais hatakuwa na haki ya kustaafu mpaka upite kwanza muda wowote utakaotajwa na Rais kwa ajili hiyo.” (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 120(3) inaendelea kusema kwamba; “Iwapo Rais ataona kuwa kwa ajili ya manufaa ya umma inafaa Jaji wa Rufani aliyetimiza umri wa miaka sitini na tano aendeleo kufanya kazi, na Jaji huyo wa Rufani anakubali kwa maandishi kuendelea kufanya kazi, basi Rais aweza kuagiza kwamba...”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukafika miaka sabini na zaidi, yote iko ndani ya Katiba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi mazito yameongelewa hapa. Mheshimiwa Maige anasema Jimboni kwake kuna majengo mazuri ya mahakama lakini hakuna Hakimu. Hili nalisikia na Ndugu yangu Katanga akisikia hivyo atashtuka sana kwamba kuna majengo mazuri Jimboni kwa Maige lakini hakuna Hakimu, tutalifuatilia hili kwa karibu sana tena sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Ulanga, Bwana Mdogo Mheshimiwa Goodluck Mlinga anasema kwake hakuna miundombinu ya Mahakama. Umenishtua sana, sisi hatupendi kusikia kitu kama hicho kwamba Wilaya ipo lakini hakuna kabisa miundombinu. Nitakaa na ndugu zangu upande wa Mahakama tuweze kutembelea Jimbo lako na mimi nakuhakikishia kuwa kama hali ni mbaya kiasi hicho hatuwezi kuliacha Jimbo lako la Ulanga kwenye mpango wa miaka mitano wa ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimeelewa masuala aliyoyalalamikia Mheshimiwa Augustine Holle ya sheria za kazi na hali ya migodini. Wakati wataalam wa Tume ya Kurekebisha Sheria bado wako hapa, hata kesho tunaweza tukapata muda kukusikiliza ulete yote unayofikiria ni muhimu tuyaangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi hapa yameongelewa, pengine niongelee la mwisho la Mheshimiwa Tindu Lissu kuhusu kuanzishwa Mahakama ya Mafisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na Mahakama ya Wahujumu Uchumi, ni kweli. Tulivyoanza, pengine huwezi kukumbuka ulikuwa bado mdogo pengine shule ya msingi, tulipoanza na hiyo Mahakama *it was a non-starter* kwa sababu *it was a tribunal* nje ya mfumo rasmi wa Mahakama. Kwa hiyo, hiyo *tribunal* sisi tukiwa *university* tuliipinga sana na ilibidi sasa ibadilishwe tena ikawa *appeal* zinakwenda kwa Rais. Sasa hiyo ndiyo ikawa mbaya zaidi na ikashindikana, ndipo marekebisho yakaja kwamba *High Court* yenyewe inaweza ikasikiliza hizo *economic crimes cases*. Kwa taarifa tu ni kwamba kuanzia mwaka 2011 mpaka leo mimi sijaona kesi pale, wewe mwenyewe ni Wakili hujaona Mahakama Kuu ikisikiliza kesi za namna hiyo kama Mahakama ya Uhujumu Uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo kubwa hapa ni kurekebisha hitilafu tulizokuwanazo katika msururu wa sheria zetu hizi tuje na kitu kizuri zaidi, tutakileta mbele yenu hapa si muda mrefu. Atakayeileta hapa ni yule yule Mwanasheria wetu Mkuu mahiri George Masaju ambaye mimi nimekaa naye

muda mrefu na mimi nawaambia hii ndiyo kamusi ya weledi upande wa sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Rais kuonekana ni dikteta! Mimi imenishangaza sana! Maneno yanayoongelewa hayafai, eti Mawaziri wanaogopa, Rais hashauriwi! Jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu dakika mbili hizi nimalizie, unajua hii mimi inanikumbusha kuhusu mchezo wa mpira. Ukienda kuangalia watu wanaangalia screen inacheza timu nzito kama Barcelona na Manchester, utaona sasa pale wanaoangalia wanajua zaidi mpira kuliko wanaocheza! Unamsikia mtu anasema aah Messi angedokoa tu pale kidogo kwa kisigino, wewe! Ukimwangukia mtu mwenyewe pengine ana miguu yote ya kushoto utadokoa vipi mpira pale? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hilo tatizo hapa! Tunajua zaidi kupita watu ambao wako jikoni! Sisi tuna uzoefu wa kuendesha Serikali. Unapomwona Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ametoa *directive*, hiyo *directive* imetolewa na *presidency*! Sisi kama Mawaziri, *we are part of that presidency*. Haiwezekani leo Rais amesema twende kushoto unafikiri ameamua mwenyewe? Ana *cabinet* yake ni sisi tuko sehemu yake. Kwa hiyo, siyo uwoga ndiyo utaratibu wa kuendesha Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu zangu mnajua mambo yalikuwa hayaendi vizuri sana, Rais amejitahidi kwa kweli kurekebisha mambo mengi sana. Amejitoa sana kiongozi wetu, kafanya mambo mengi ambayo hayajapata kutokea na dunia nzima inamuimba leo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kuondoa pesa za sherehe akanunulia vitanda Muhimbili ni udikteta? Kuondoa fedha za sherehe akajenga barabara ni udikteta? Ndugu zangu itakuwa tunayoongea hapa ni tofauti kabisa na *thinking* ya *public* huko nje. Hicho kitu kinampa Mheshimiwa Rais *comfort* kubwa ndani ya moyo kwa sababu wananchi wanachakisema kinamtia moyo sana. Sisi wenyewe hapa tulikuwa tunalalamika ooh, uongozi huu legelege, dhaifu, limekuja tingatinga, malalamiko tena eee, nini tena? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele ikilia, kwa mara nyingine tena mimi nakushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vyema katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika mjadala huu...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** (Hakutumia kipaza sauti).

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Napenda kuahidi...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Hakutumia kipaza sauti).*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaongea halafu kuna vichaa humu ndani wanaongeaongea...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mimi nashindwa kuelewa sijui wanakula yale majani yale, sielewi? *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Majani ya Msukuma.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Haya!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda tu kurudia kuahidi kwamba maoni na ushauri ambao Waheshimiwa Wabunge mmeutoa tuta-compile na tutawaletea majibu yake yote. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, nitawahoji baada ya kumaliza utaratibu unaofuata, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Kif. 1001 Administration and HR Mgt.....Sh.1,033,855,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi napenda kupata ufafanuzi kwenye *subvote* 1001, *item* 220700, *rental expenses*. Kifungu hicho kwa mwaka 2015/2016 kulikuwa na Sh.478,180,000 mwaka huu kuna ongezeko la shilingi 122,000,000 na imefikia shilingi 600,000,000.

Utetezi wa hoja kwenye randama inasema kwamba ni fedha za kulipia kodi za pango za ofisi za Tume. Mwaka huu wa fedha kuna shilingi 600,000,000, mwaka wa fedha wa 2015/2016 kulikuwa kuna shilingi 478,180,000 na mwaka 2014/2015 kulikuwa na shilingi 267,908,000 jumla ya fedha hizi ni shilingi bilioni 1.3 ndani ya ndani ya miaka mitatu, ni kulipia kodi za Ofisi za Tume. Sasa najiuliza hili nalo si jipu au ni upele, ongezeko la shilingi 122,000,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi wa kina juu ya ongezeko hili la pango la ofisi ya Tume ni kwa jambo gani zaidi, mbona mnaongeza fedha kiasi hiki? Naomba nipate maelezo ya kina sana juu ya tatizo hili kubwa ambapo wanaongeza fedha hizi nyingi wakati mnasema mwaka huu ni wa kubana matumizi, tatizo nini kwenu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo. Hili ongezeko unaloliona hapa ni kutokana na sehemu ya Tume kuhamia katika ofisi mpya na kubwa zaidi zilizopo katika jengo la RITA, jengo la kisasa kabisa lililopo katikati ya mji.

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri ni...

**MWENYEKITI:** Hatujafika bado.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002	Finance and Account.....	Sh.10,900,000
Kif. 1003	Procurement Mgt. Unit.....	Sh. 6,750,000
Kif. 1004	Internal Audit Unit .....	Sh.3,700,000
Kif. 1005	Recruit., Appoint. & Confirmation.....	Sh. 71,750,000
Kif. 1006	Ethics and Discipline Section.....	Sh.800,000,000



(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 *Administration and HR Mgt*.....Sh.1,093,191,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika subvote ya 1001, item 221400, *hospitality supplies and services*. Kwa mwaka 2015/2016 kulikuwa na shilingi 18,200,000, mwaka huu wa fedha wa 2016/2017 kuna shilingi 29,015,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utetezi unasema fedha hizi zimetengwa kukirimu vikao vya kikazi vitakavyopitishwa kwa malipo na zawadi ya mfanyakazi bora, takrima, vinywaji, viburudisho, mnaongeza shilingi 11,000,000!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnabana matumizi mnaongeza fedha za takrima, vinywaji, viburudisho vitamu vitamu, vikeki keki, mnaongeza shilingi 11,000,000 wakati Serikali hii mnasema mnabana matumizi! Miongoni mwa fedha hizo mnasema pia kuna fedha za mfanyakazi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la shilingi 11,000,000 tatizo ni nini, hebu tuambieni hali halisi Serikali hii ya Chama cha Mpinduzi, tuambieni uhalisia sasa wa ongezeko hili kwamba ninyi mna mfanyakazi bora mnataka kumpa zawadi lakini mnataka kukirimu viongozi, mnataka kupata viburudisho, vinywaji vitamu vitamu, jamani, kazi ipo kweli. Naomba ufafanuzi wa kina. (Kicheko)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna vikao vingine ambavyo kwenye kanuni vina posho lakini pia na ofisi zetu zimeongezeka. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu ya ongezeko hilo. Kwa hiyo, utaona kwamba hiyo shilingi 11,000,000/= siyo ongezeko kubwa sana. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 *Finance and Accounts Unit*.....Sh.386,944,000  
Kif.1003 *Planning Division*.....Sh.404, 066,000  
Kif.1004 *Internal Audit Unit* .....Sh.241,140,000  
Kif.1005 *Gvt. Communication Unit*.....Sh.65,720,000  
Kif. 1006 *Legal Registry Unity* .....Sh.106,004,000  
Kif.1007 *Procurement Management* .....Sh.201,220,000  
Kif. 1008 *Research and Library Service Unit*.....Sh.71,148,000

Kif.1009 *Information & Comm. Technology*.....Sh.196,480,000  
Kif. 2003 *Legislature Drafting*.....Sh.937,766,000  
Kif. 3001 *Civil Litigation & Arbitration Div.* .....Sh.921,446,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3002 *Treaties and Contracts Division*.....Sh. 852,775,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nipate ufafanuzi kwenye kifungu kidogo cha 221000, *travel out of country*, imeongezeka kutoka shilingi 100,000,000 mpaka shilingi 154,000,000 kwa ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 50 na ukizingatia kwamba tuna *discourage* safari hizi za nje. Kama suala ni mikataba, kuna wenzetu wa G7 na *Great Lake Zones* wanatoa *support* hata kwa mikataba ya *gas and oil* kama wataalam wetu wanapungukiwa. Ni kwa nini tunatenga fedha nyingi kiasi hiki za safari za nje ilhali mkituaminisha kwamba hizi safari mnazi-*discourage*? Naomba nipate ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba siyo ya gesi tu lakini hata kama ingekuwa ni hiyo ya gesi hatuwezi kutegemea wafadhili. Ofisi ile ndiyo inahusika kwenye *negotiation* zote ziwe ni zile za kikanda au za kimataifa na mikataba mingine ya uwekezaji. Kwa hiyo, kimsingi sehemu kubwa ya fedha hizi zinatumiwa kwa shughuli kama hizo. Kwa hiyo, utaona kwamba hilo ongezeko ambalo Mheshimiwa Gekul amelizungumzia pale siyo kubwa sana. Kwa hiyo, naomba kutoa ufafanuzi huo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 - *Constitutional Affairs & Human Rights* .....Sh.519,424,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 35 - Divisheni ya Mashtaka**

Kif. 2002 *Public Prosecution Division*.....Sh.2,874,611,000  
Kif. 2004 *Zonal Office Arusha*.....Sh.923,052,000

Kif. 2005 Zonal Office Dodoma.....Sh.464,380,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2006 Zonal Office Dar Es Salaam.....Sh. 2,155,754,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mimi langu ni kwenye *rental expenses* zimeongezeka kutoka shilingi milioni 314 mpaka shilingi milioni 430. Ni kwa nini sasa Serikali isione kwamba tunapoteza pesa nyingi sana kukodi ofisi za Serikali? Miaka zaidi ya 50 ya Uhuru bado ofisi zetu tunakodi na kwa kiasi hiki cha shilingi milioni 430 ilhali Mahakimu wetu hawana ofisi. Ni kwa nini Waziri asione kwamba hili ni tatizo na hizi pesa zikahamishwa?

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni ongezeko la kawaida tu hatuwezi tukabakia *static*. Ni ongezeko kutokana na kuongezeka kwa gharama za kulipia pango la ofisi na tuna *expand* sasa na tunafungua ofisi nyingine. Tumepata *directive* juzi, tumefurahi sana, kutoka kwa Mheshimiwa Rais kwamba sasa tuanze kutafuta viwanja na tuanze kujenga. Kwa hiyo, hatujaenda mbali sana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge pia.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kulipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2007 Zonal Office Iringa .....Sh.360,566,000  
 Kif. 2008 Zonal Office Moshi.....Sh.345,495,000  
 Kif. 2009 Zonal Office Kagera .....Sh.245,726,000  
 Kif. 2010 Zonal Office Mbeya .....Sh.499,721,000  
 Kif.2011 Zonal Office Mtwara .....Sh.317,474,000  
 Kif. 2012 Zonal Office Mwanza.....Sh.866,637,000  
 Kif. 2013 Zonal Office Ruvuma.....Sh.255,755,000  
 Kif. 2014 Zonal Office Sumbawanga .....Sh.274,880,000  
 Kif. 2015 Zonal Office Tabora.....Sh.481,902,000  
 Kif.2016 Zonal Office Tanga .....Sh.522,875,000  
 Kif.2017 Zonal Office Shinyanga.....Sh.410,909,000  
 Kif. 2018 Zonal Office Singida.....Sh.231,904,000  
 Kif. 2019 Zonal Office Lindi.....Sh.205,124,000  
 Kif. 2020 Zonal Office Mara.....Sh.298,922,000  
 Kif. 2021 Zonal Office Manyara.....Sh.104,203,000  
 Kif. 2021 Zonal Office Kigoma.....Sh.186,989,000

Kif. 2023 Zonal Office Pwani .....	Sh.272,645,000
Kif. 2024 Zonal Office Njombe.....	Sh.159,711,000
Kif. 2025 Morogoro.....	Sh.220,094,000
Kif. 2026 Zonal Office Geita.....	Sh.144,789,000
Kif. 2027 Zonal Office Simiyu.....	Sh.124,675,000
Kif. 2028 Zonal Office Katavi.....	Sh.148,826,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **Fungu 41 - Wizara ya Sheria na Katiba**

Kif. 1001 Administration &HR Mgt.....	Sh. 6,207,700,000
---------------------------------------	-------------------

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, mshahara wa Waziri, hapa tunayo majina ya wachangiaji na tutaanza na Mheshimiwa Kanyasu Costantine.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka tu kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba Mkoa mpya wa Geita ulipoanzishwa ulitumia *facilities* nyingi ambazo zilikuwa za Wilaya na mpaka sasa hivi wanaonekana wanahangaika sana. Ni kwa kiwango gani katika mwaka huu wa fedha Wizara hii imejipanga kushughulikia matatizo ya majengo ya Mahakama? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia concern ya Mheshimiwa Kanyasu. Mimi toka nianze kuongoza Wizara hii nimetembelea mikoa michache sana, lakini kati ya michache niliyotembelea wiki tatu zilizopita ni Mkoa wa Geita kutokana na *special condition* za Geita. Lengo langu kubwa pale ni kuangalia pia kuhusu miundombinu ya Mahakama na *facilities* nyingine. Vilevile tumepanga na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuangalia maendeleo ya ujenzi wa gereza Chato, kwa sababu mkoa huu una shida kubwa sana ya gereza. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Geita sisi tumeuchukulia kama ni mkoa maalum wa kuangalia kwa sababu ni mpya na una changamoto nyingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu naona ameridhika. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**MHE. RIDHIWANI J.KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri, Halmashauri ya Chalinze ni mpya lakini katika Halmashauri ile kuna wenzetu wanaoishi Tarafa ya Kwaruhombo, kwa kipindi kirefu sana imekuwa ni kilio chao juu ya kukosekana kwa Mahakama lakini

umbali mrefu ambao wanatembea kutoka katika vijiji kama vya Kibindu na maeneo mengine ya Kwakonje kwenda kutafuta haki yao. Mara nyingi kinachotokea, wanapokwenda katika Mahakama pamoja na umbali wanaotembea na umaskini mkubwa walionao watu wangu wanakwenda kule wanakuta Mahakama zile hazifanyi kazi.

Naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuambie ni mpango gani walionao mwaka huu juu ya kujenga Mahakama ya mwanzo ya Tarafa ya Kwaruhombo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Meshimiwa Mwenyekiti, pengine nitumie fursa hii ya kumjibu Mheshimiwa Kikwete pia kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba ni azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kwamba tunatatua hili tatizo la *access to justice* kwa wananchi wetu. Tatizo ni kubwa kama nilivyolieleza wakati naeleza hapa kwamba tuna kata zaidi ya 3,900 ambazo zote zinatakiwa ziwe na Mahakama za Mwanzo lakini tuna Mahakama 970 tu. Hiyo ni *crisis* na ndiyo maana simung'unyi maneno kuupongeza sana uongozi wa Mahakama sasa hivi kwa kuanzisha mradi mkubwa wa miaka mitano. Ni mpango wa miaka mitano kuhakikisha tunajenga na kukaratabati majengo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huo wa miaka mitano, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote ambao mnadhani mna matatizo makubwa mtuambie, *ofcourse* siyo kutuambia tu na sisi tutakuja ku-cross check kama kweli *distance* ni kubwa kiasi hicho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kikwete tafadhali tunaomba uwasilishe hayo mahitaji ya jimbo lako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani ameridhika.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Bado Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba maswali au ufafanuzi unaoweza kuombwa kwenye kifungu hiki ni ufafanuzi wa mambo ya jumla. Naomba tafadhali tuzingatie Kanuni ya 101(3). Mheshimiwa Ridhiwani.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mpango mzuri wa Serikali juu ya kuhakikisha ile *access to justice* inapatikana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Waziri mimi naomba unapokuwa unaanza kutekeleza mpango wako huo uwapo jicho la karibu sana wananchi Kwaruhombo. Nina

hakika kabisa kama unatoka Tanga ukifika Mbwele pale ukakunja kulia sasa kama unakwenda Mvomero ukaona ule umbali wanaotembea watu wangu, ukaona ukubwa wa Jimbo la Chalinze utatambua kwa nini tokea Uhuru mpaka leo wananchi wale wamekuwa wanalilia sana kitu hicho. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri utakapoanza kufanya kazi hiyo basi utupe jicho la karibu kwa Halmashauri mpya ya Jimbo la Chalinze. Ahasante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani, Kanuni ya 101(3) kinataka ufafanuzi wa suala mahsusi la sera. Kwa hivyo, tuendeele sasa kwa sababu lile la mwanzo lilikuwa angalau ni la jumla na ulishajibiwa. Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii.

Kwa kuwa katika mchango wangu niliongelea suala la *contradictions* ambazo zinaonekana zinakinzana na Sheria ya Ndoa zikimfanya mtoto wa kike aonekana kuwa *deprived of* na haki zake. Waziri kasema kwamba Sheria ya Elimu ndiyo ambayo itakuja kufanyiwa marekebisha ili imfanye mtoto huyu ambaye yuko chini ya miaka 18 aweze kupata elimu ya sekondari na akae shuleni asome ili asirolewe. Sijaridhika na jibu hilo namuomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu ya kuridhisha na kama atashindwa kunipa majibu ambayo yatanifanya mimi nione kwamba amemuona huyu mtoto wa kike ni wa thamani nitashikilia shilingi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza thamani ya mwanamke imezingatiwa sana na Serikali hii na hata ujenzi wa zile shule za kata za sekondari zinampa fursa mwanamke sasa badala ya kuolewa aendelee kusoma.

La pili, Serikali imesema hawa watasoma kuanzia *nursery school* mpaka elimu yote ya sekondari. La tatu, ni hili ambalo Serikali inakuja nalo kwenye Mkutano huu wa Wabunge, kuleta Muswada ili kuimarisha hiyo thamani. Siyo tu kwamba litakuwa ni kosa la jinai kumpa ujauzito mwanafunzi anayesoma shule, lakini hata kumuoa au kwa namna yoyote ili kumfanya asiendelee na masomo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiki ni kielelezo cha kuonesha kabisa kwamba Serikali imejiandaa sana kuhakikisha kwamba mtoto wa kike anaendelea na masomo. Siyo hayo tu na sheria nyingine nyingi zimetungwa ambazo zinalinda thamani ya mwanamke kama mtu mwenye haki sawa. Kwenye Ibara ya 12 niliyowasomea kwamba kila mtu anastahili kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wake akiwemo na mwanamke.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo sasa kwamba ni kwa nini nitaendelea kuishikilia shilingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema kwamba unajaribu kum-*protect* mtoto ambaye anatakiwa kuwa shuleni, kwa hiyo kwa Sheria ya Elimu kurekebisha itamfanya mtoto ambaye yuko shuleni yeye aendelee kusoma na kweli wanaume hawatamfuata kumchumbia na wala kumchukua kumuweka unyumba. Hata hivyo, siyo watoto wote wa kike ambao wana umri chini ya miaka 18 wanakwenda shuleni, wengine hawaendi shuleni bado wanabaki nyumbani. Mimi nia yangu ni kuwasaidia hawa watoto wa kike na wao wapate kubaki nyumbani basi wakiwa salama huku wakijishughulisha na shughuli za kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata haki za watoto, mtoto ana haki, kwa nini aolewe, kwanza kiafya unakuwa umemharibu huyu mtoto wa kike. Pia *psychologically* mtoto huyu bado hajawa na uwezo wa kuyakabili masuala mazima ya ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijaridhika, namuomba tu Waziri aangalie suala hili.

**MWENYEKITI:** Sasa unatoa hoja ya kutoa shilingi?

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, watakaochangia wasimame, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ridhiwani halafu Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Ester Bulaya. Tuanze na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama hapa kusema nikiwa kama Naibu Waziri wa kwanza wa kiume ambaye anafanya kazi kwenye Wizara inayoshughulikia mambo ya wanawake. Wanawake wenyewe wamenipa jina la Balozi wa Wanawake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka nimepewa nafasi hii na heshima hii kubwa na Mheshimiwa Rais wa Serikali wa Awamu ya Tano, nimekuwa nikishughulikia mambo mbalimbali yanayohusu haki za watoto na hususani haki za watoto wa kike. Katika shughuli zetu pale Wizarani tunalitambua jambo ambalo analolizungumzia Mheshimiwa Kiteto Koshuma kwamba kuna *contradiction* baina ya sheria mbalimbali ambapo kuna Sheria ya Ndoa inayoruhusu watoto



chini ya miaka 18 kuolewa. Kwa maana hiyo, tumeanza mchakato ndani ya Serikali wa kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ili iweze kuoana na sheria nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba wakati muafaka utakapofika...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Wakati wanaongea wenzenu muwe na heshima ya kusikiliza, ndiyo demokrasia hiyo wengine sisi huwa hatukopeshi nitawapeni ya uso.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla, naomba uongee na Mwenyekiti.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** No, kuweni na heshima bwana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla, naomba uongee na Mwenyekiti.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Bunge lazima tuheshimiane wakati tunaongea wengine sisi huwa hatukwepeshi nitawapa za uso sasa hivi waambie watulie. (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Naomba uwaambie watulie, Halima na Ester tuheshimiane, nitawapa za uso sasa hivi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla, naomba uendelee na hoja.  
*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee na hoja, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, naendelea na hoja lakini waambie watulie patachafuka humu sasa hivi. (Kicheko/Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojaribu kusema ni kwamba

anachokisema Mheshimiwa Koshuma tumeanza kukifanyia kazi chini ya Wizara yetu. Tayari tumeanza mchakato ambapo pengine mwezi wa tisa ukifika tunaweza tukaleta mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ili kuweza kuondoa vifungu vyote ambavyo vinamyima haki mtoto wa kike. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Bulaya.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliku-miss, ahsante kwa kunipa nafasi. Moja kwa moja naunga mkono hoja ya mtoa hoja. Kabla sijawa Mbunge nilikuwa Mwandishi wa Habari katika magazeti ya Uhuru na Mzalendo, nilipata fursa ya kufanya *research* kupitia Shirika la *Action Aid*. Nilienda Liwale, sheria hizi kandamizi mbali ya kufanya wanawake kuolewa katika umri mdogo pia zinachangia mimba za utotoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika Mheshimiwa kaka yangu anazungumzia shule za kata zinawasaidia wanawake, shule zile ni za wote, hapa tunazungumzia hoja ya msingi ya watoto wa kike kukosa fursa. Siyo wote watabahatisha kama akina Ester Bulaya, siyo wote watabahatisha kama wengine, tunapaswa kuweka misingi sasa hivi ya kuondoa sheria zote kandamizi siyo hii tu moja na wakati huo ni sasa hivi. Tunahitaji watoto wa kule kwetu Gushigwamara wafike hatua tuliyofikia siyo kwa kukandamizwa na sheria kandamizi kama hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Koshuma. Ukweli ni kwamba hata hizo shule za kata anazosisema mtoto anapomaliza kidato cha nne huenda anakuwa hajafanya vizuri anarudi nyumbani wakati wazazi wanajiandaa ni namna gani wamuandae mtoto huyu mara jamaa anatokea anampa mimba hakuna sheria inayomtetea mtoto yule akiwa mdogo. Sasa ukitamka shule za kata nashindwa kukuelewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka ni sheria inayomlinda mtoto wa kike, lakini inayomlinda mwanamke pia kwa sababu huyu mtoto wa kike anahitaji na yeye akae katika mazingira ya kuwa mama au ya kuwa mke. Miaka 16 ni mke wa namna gani? Huyu ni mtoto anayeenda kuteseka katika maisha yale ya ndoa. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie jambo hili, hatuchezi, tunatetea ukweli nendeni mkaone kule watoto wanavyotesea, wanavyodhalilika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaunga mkono hoja hii, Serikali itutendee haki. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. *Throughout history* ukisoma hata nyakati za Biblia mwanamke amekandamizwa sana. Ilifika mahali hata Wayahudi walivyokuwa wakiomba wanasema nakushukuru Mungu kwa kuwa mimi sikuwa mwanamke. Ukiendelea mbele zaidi wanawake wameendelea kukandamizwa na hoja aliyoileta dada yetu ni ya msingi katika karne hii ya 21 ni lazima tupandishe *standard* ya mwanamke aishi kwa uhuru na kwa kujiamini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama baba wa watoto wa kike watatu, naunga mkono sana hoja hii. Naamini wengi tunao watoto wetu wa kike, ni lazima tu-*protect* watoto wetu wa kike. Kwa hiyo, namuomba Waziri hizi sheria ambazo ni kandamizi, zina-*contradict* hasa hii sheria inayoruhusu mtoto wa kike wa chini ya umri wa miaka 18 kuolewa inatakiwa iletwe *Bill* hapa iondolewe ili tuweze kuwa-*protect* watoto wetu wa kike. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kama baba mwenye mtoto wa kwanza wa kike. Namwangalia mwanangu Aziza miaka 12 baadaye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua changamoto iliyopo hasa katika sheria za dini mbalimbali na miongozo mbalimbali ya maisha na mila zetu ambazo zinatufanya wakati mwingine kuolewa chini ya miaka 18 iwe ni jambo la lazima. Hata hivyo, kupitia Bunge lako ambayo ndiyo sehemu inayotunga sheria lazima tuzifikishe mwisho wa sheria hizo potofu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nimesoma sheria, sheria yetu inayotambua watoto inazungumzia mtoto umri wake ni sifuri mpaka 18 lakini Sheria ya Ndoa inazungumzia kwamba unaweza ukaoa mtoto aliye chini ya miaka 18. *Very interesting point*, ile siku ya kuoa ndani ya saa 24 lazima uwe umelala na mwanamke huyo. Najaribu kutumia tafsida ili kuweka mambo sawa, humu ndani watu wazima mnanielewa.

**MBUNGE FULANI:** Ndio tunakuelewa.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine* umemuoa mtoto wa miaka 14, 16, ndani ya saa 24 mtoto huyu, *Subhanallah*. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwa hisia za ndani sana kwa sababu sisi wengine tunao watoto wa kike na natambua ugumu wa maisha wanayopitia inapofika kipindi hicho. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri mimi pamoja na kumuunga mkono dada yangu pale Mheshimiwa Mjumbe mzito kabisa Kiteto lakini Mheshimiwa Waziri atakapoamka atuambue ni mkakati gani alionao kama Wizara kuhakikisha jambo hili linafikishwa mwisho na ikiwezekana kuzifuta kama alivyopendekeza Mchungaji Msigwa ili sasa mwanamke wa Kiafrika, mwanamke wa Kitanzania aweze kupata hadhi na heshima yake katika nchi yake? Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKIITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipingani na Waheshimiwa Wabunge kwa hoja hii na napenda tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba wiki iliyopita nilijibu swali hili hapa Bungeni likiulizwa na Mheshimiwa Toufiq. Nilifikiria tuna kumbukumbu ndiyo maana mimi nimeliongelea kwa kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijibu kwamba tulikuwa tumeanza mchakato wa kubadilisha Sheria ya Ndoa siku nyingi na kilichotuudhi sana ni kifungu cha 13 ambacho kinasema mtoto wa kiume anaweza akaoa na miaka 18 ila mtoto wa kike aolewe na miaka 15, kinaleta ubaguzi. Ukienda kifungu cha 17(2) cha sheria hiyo kinasema ukienda Mahakamani unaweza kuruhusiwa hata mtoto wa kike akaolewa chini ya umri wa miaka 15, *that is very serious!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *what happened?* Wizara ikaamua kupeleka Muswada Cabinet kwa ajili ya kubadilisha Sheria ya Ndoa. Baraza la Mawaziri likasema hapana! Hili suala ni *sensitive!* Baadhi ya Wabunge hapa tunajidai *liberal* tukitoka nje mnaanza maneno mengine tofauti! Ni *sensitive* kwa sababu linagusa *interest* za dini na jamii yetu. Kwa hiyo, tukaagizwa tutoke na *white paper* kuwahoji wananchi wenyewe waseme hapana hili suala sasa basi! Tukipata ridhaa ya Serikali sisi hata kesho asubuhi tunaweza kuleta hiyo *amendment* lakini ninyi wenyewe ndiyo mtatakiwa kuwa wa kwanza kuunga mkono. Pengine hata maandamano yanaweza kutokea kupinga suala hili, tujiandae. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoona mchakato wa *White Paper* umefika mbali na wakati huo huo tumeanza mchakato wa Katiba Mpya, tukaona huwezi ukaendesha vitu hivi viwili vya kuhoji mawazo ya Watanzania *at the same time*. Kwa hiyo, sisi tukaamini kwamba katika mchakato wa Katiba Mpya wananchi watalalamikia hiyo *aspect*, hawakulalamika. Ndiyo maana nilijibu wiki iliyopita kwamba tumeanza upya *process* ya *white paper* na tunashirikiana kwa karibu sana na Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla katika suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwezi kusubiri *the white paper process*, ndivyo nilivyowaambia hapa. *White paper* iendelee lakini *in the meantime* katika Mkutano huu tute Sheria ya Elimu ili tuibadilishe ambapo tunasema mtoto wa kiume na wa kike ni marufuku kuoa au kuolewa *as long as* yuko shule ya msingi na sekondari. Hii ni *interim measure*. Sasa Mheshimiwa Koshuma ulitaka tufanye nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, upande wa Serikali tumefika hapo tunadhani hili ni suala ambalo Watanzania wote wanahitaji kulijadili. Wizara yangu imefikia *advanced stage*, hili suala litarudi tena *Cabinet* kwa sababu linahitaji litengewe pesa maalum tuweze kufanya hiyo *white paper process*. Wakati tunafanya hiyo *process* kuwahoji Watanzania lazima tuendelee kubadili sheria nyingine kutusogeza karibu na hiyo azma ya kumkomboa mtoto wa kike. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto unakubaliana na maelezo ya Waziri?

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niwashukuru Wabunge wote ambao mmechangia kwenye hoja yangu kwa mawazo mazuri. Mmenitia moyo kama mtoto wa kike ambaye ninamshukuru Mungu alinisaidia na akawasaidia wazazi wangu wakapata pesa za kunisomesha nikaolewa nikiwa na umri wa miaka 28. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi sasa kwa wadogo zangu na watoto wangu, Mungu kanijalia nina mtoto wa kike ambaye ndiye nilikuwa namuwazia kweli kwamba aje mtu ana miaka 55 anataka kumuoa mtoto wangu eti kisa tu kamaliza darasa la saba, hataki shule, siwezi kumlazimisha hataki kusoma, huyu mtu aje aseme anataka kumuoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla angalau basi ameu-*soften* moyo wangu na kunifanya nifikirie kurudisha shilingi kwa sababu amesema wataileta sheria hii ili iweze kufanyiwa marekebisho mwezi wa tisa. Narudisha shilingi kwa Waziri lakini na uzuri *Hansard* zipo, naweka lakini kwa sababu nataka mwezi wa tisa sheria hii iletwe hapa Bungeni tuweze kuibadilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kiteto kwa kurudisha shilingi. Tunaendelea Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwanza nasema nataraji *reciprocation* katika suala hili, nashawishi upande ule uunge mkono hoja ambayo naitoa kama ambavyo sisi tumeunga mkono hoja waliyoitoa, ni suala la haki za binadamu. Asubuhi imesemwa sana

hapa kwamba katika Fungu 55 - Haki za Binadamu hawakuwekewa pesa zozote za kufanya *activity* zozote zile. Mtu mmoja asubuhi alisema bora ile ofisi ifungwe maana watakuwa wanakwenda bure bila ya kufanya lolote lile katika kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa haki za watoto, kuna haki za wafungwa, kuna *dispensation of justice* lakini tumeshindwa kuipa Tume hii pesa ili wafanye kazi. Kwa hiyo, kwa maana nyingine tunajizua sisi wenyewe haki zetu kulindwa na kusimamiwa. Tume hii imekuwa ikifanya kazi nzuri, imekuwa ikieleza matatizo katika suala zima la haki za binadamu lakini pia hatuwezi kuwa na maendeleo kama hatujakuwa na chombo ambacho kinasimamia haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo ya kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri la sivyo nitatoa hoja ya kuzuia kifungu chake cha mshahara. Kwa sababu hata leo asubuhi Waziri Mkuu ameshindwa kujibu swali kwamba hata ripoti za Kimataifa hatupeleki. Mheshimiwa Dkt. Macha aliuliza swali hilo asubuhi hapa kwamba hata ule wajibu wetu wa Kimataifa hatuutimizi na kuna *commitment* yetu, naomba kutoa hoja.

**MBUNGE FULANI:** Bado.

**MWENYEKITI:** Bado Mheshimiwa inabidi akupe maelezo.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Sawa.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui nitumie lugha gani kumshawishi Mheshimiwa Ally Saleh atuelewe kwamba hii ni bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano ikijaribu kuibeba Tume hii. Sisi tumesema, Tume hii tunaelewa umuhimu wake. Tume ya Haki za Binadamu ni moja ya taasisi za Serikali ambazo zimebahatika hata Serikali kujengea jengo lake yenyewe karibu na Ikulu pale, zito kabisa. Siyo hivyo tu, Tume ya Haki za Binadamu sasa hivi inaendesha programu kwa kushirikiana na UNDP ya kuhamasisha haki za binadamu kuanzia mwaka 2013 - 2017 na hiyo *action plan* imeasisiwa na Serikali yenyewe. Kwa hiyo, huwezi kuwa na Serikali ambayo huku inahamasisha halafu huku inainyonga Tume. Kama ni suala la punguzo la pesa ni *across the board* ili tutoe pesa kwa ajili ya *project* za maendeleo ndiyo hicho tu, si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimhakikishie kwamba sisi tunaelewa umuhimu wa Tume hii, imefanya kazi nzuri sana. Kama nilivyosema juzi kwamba katika miaka mitano na nusu hivi toka mwaka 2010, Tume

imepokea na kushughulikia zaidi ya malalamiko 13,709. Tume hii ni kundi la wazalendo ambao kwa kweli wanastahili pongezi kwa sababu ina wastani wa kupokea na kushughulikia malalamiko 2,493 kwa mwaka sawa na malalamiko 208 kwa mwezi. Ukija kwenye utatuzi wa malalamiko, wametatua malalamiko 6,169 wastani wa malalamiko 1,121 kwa mwaka, hivyo malalamiko 93 kwa mwezi. Hii ni *performance* nzuri sana. Sisi kama Serikali tungependa kui-*encourage* Tume kwa kutatua matatizo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Makamishna wa Tume ambao *both* ni kutoka *Mainland* na Zanzibar wako saba. Mishahara yao iko kwenye *Consolidated Fund* kwa hiyo, tumepunguziwa mzigo na Serikali. Pia *Treasury* ndiyo inasimamia kuhusu mafao yao, mishahara na posho za hawa Makamishna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu kwamba hii ni bajeti ya mwanzo hatuwezi kufanya *everything more than that*. Mimi nina uhakika Serikali tuko *so interested* na maendeleo ya hii Tume na ndiyo maana tarehe 9 tuna-*appear* mbele ya *United Nations (UN) - Commission for Human Rights* (Geneva). Sisi Serikali tutajitetea na Tume itakuwa pale pia, hatuingilii! Kila mwaka ikienda inatoa *paper* yake kwa uhuru kwa sababu wako *very independent*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda kusema hii *excuse* ya kwamba *across the board* inachosha sasa kwamba kwa sababu *i-cut across the board* basi hata katika *vital areas* tunasema tume-*cut across the board*. Tumezungumza na Tume kwenye Kamati, wanasema kwamba wanaishi maisha magumu siyo ya mishahara, hawana gari, hawana kazi ya kufanya, wanaishi mitaani wengine wamekodi Kigamboni wanasema maisha yao hayako salama, wamelalamika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalonishangaza ni kwamba hata jana Mwenyekiti wetu alijaribu kupeleka *issue* hii kwa Kamati ya Bajeti, taarifa niliyopata, wakati sisi watu wa Kamati tunatetea kwamba maarifa yafanywe apate pesa, Waziri anakataa Tume hii isipate pesa kwa sababu pia na taasisi nyingine zinasimamia. Kwa hiyo, mimi namshangaa Waziri kwamba sisi tunamtetea yeye hayuko tayari kutetewa. Tuna-*commitments* nyingi kama nchi tunashindwa kuzitimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sijaridhika kabisa, naomba kutoa hoja kwa kutumia Kanuni ya 103 kwamba nazuia shilingi ya Waziri.



**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, watakaochangia ni Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Ridhiwani, Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi. Tutaanza na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilianzishwa mwaka 2001. Kwa muda mrefu katika kipindi cha uhai wake Tume hii imekuwa inategemea sana fedha za nje, fedha za *SIDA-Sweden* na *UNDP*. Tumefika mahali hata hawa ambao wameibeba Tume miaka yote hii wamechoka. Makamishna wa Tume wanadai hawana magari ya kufanyia kazi, yaliyopo hayana matairi, hayafanyiwi service, wanashindwa kwenda kufuatilia malalamiko ya matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu *simply* kwa sababu hawana *operating budget*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii pamoja na matatizo yote haya na Mheshimiwa Waziri anakiri, imefanya kazi kubwa sana. Mtu yeyote ambaye amepata kusoma taarifa ya Tume juu yaliyomkuta Profesa Lipumba mwaka juzi, atakubaliana na mimi kwamba hii Tume kama tutaiacha ife njaa kwa sababu tu ya hiki kinachoitwa makato *across the board*, tutakuwa tumepoteza sauti kubwa na muhimu ambayo ni huru katika masuala ya uhifadhi wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh kwamda Waziri atafute fedha, Tume ipate fedha ifanye kazi yake ya kusimamia masuala ya haki za binadamu. Nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh, lakini nataka niweke mambo fulani vizuri hapa ili tuelewane sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachojua sisi Tume inavyofanya kazi, yako mambo mengi ya msingi ambayo yanafanyika ndani yake. Kukosekana kwa magari haiwezi kuwa moja ya sababu ya msingi kabisa kwamba Bunge hili linakaa kujadili tutafute magari badala ya kutafuta jinsi gani Tume inaweza kuwezesha ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Ametuambia hapa Mheshimiwa mtoa hoja juu ya kazi ambazo zimekwishafanyika, juu ya kesi ambazo zimekwishasikilizwa na juu ya jinsi mambo yanavyoendeshwa ndani ya Tume kiasi kwamba tumefika sehemu sasa tunahakika kwamba hata mnapokwenda mbele ya *Commission* ya *UN* kueleza juu ya hali ya *human rights* katika Tanzania mambo yetu yakoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nimuambie ndugu yangu Mheshimiwa Ally Saleh, Mjumbe mwenzangu, tuipe Serikali nafasi ijipange kwa

sababu hii ni bajeti ya kwanza na bajeti hii inatoa mwanga wa jinsi gani Serikali imeweza kujipanga vizuri kutekeleza majukumu ya Tume. Mimi nina hakika kabisa na kwa kuwa Serikali hii itakuwepo kwa miaka mitano hayo mambo mengine na vilio vyetu vitatekelezwa tu. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyopewa chini ya Kanuni ya 104(1), naongeza muda wa nusu saa ili tuweze kumaliza shughuli za Kamati ya Matumizi. Tutaendelea na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Saleh. Kwanza mimi nataka kuuliza hii Tume kama imeanzishwa kwa sababu tu ya kupewa hela nje ya Serikali imeanzishwa kwa kulazimishwa au? Maana mimi ninachojua Tume ya Haki za Binadamu ni chombo ambacho kiko chini ya Serikali na ni ajabu sana kuja kupanga bajeti hapa ya Serikali hiyo Tume kutopangiwa hela!

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi nimesimama hapa siyo mwanasheria lakini najua kazi ya Tume za Haki za Binadamu, kazi ya kutetea wananchi. Mimi natokea ndani ya Wilaya ya Kilombero, Jimbo la Mlimba watu wanapigwa kule, watu wananyanyaswa, wanahitaji msaada wa kisheria. Sana sana nimeona watu waliokuwa wanaenda kule ni wale wa Kituo cha Haki za Binadamu lakini kama Tume ingeimarishwa na Serikali ikaiwezesha kupata magari, haya magari ni msaada mkubwa sana kwa sababu hata Jimbo langu watu wanavyoteseka, wanavyopigwa hakuna gari linaloweza kwenda kule zaidi ya *Land Cruiser*. Sasa kama hawa watu hawana magari, hawawezi kujipambanua mbele ya wananchi kwamba sisi tuko hapa na tunafanya mambo haya. Kwanza wananchi wa Tanzania wengi wanashindwa kuitumia hiyo Tume kwa sababu hawajui, leo mnaibanabana hapo mnaibania nini? Hebu ipeni nafasi hiyo Tume, tuitengee pesa ili itoe matangazo wananchi waone kwamba wana chombo chao kinaweza kikawatetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Susan. Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh kwa kuzungumzia mambo machache. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu dhamira njema ya Serikali yetu ya Jamhuri iliyo chini ya Chama cha Mapinduzi ya maendeleo lakini naomba niseme tu *development can not negotiate human rights and good*

*governance*. Haki za binadamu haziwezi kuwa *negotiated* kwa maendeleo. Ibara ya 13 inazungumzia kwa kina kuhusiana na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba ukiangalia bajeti ya Tume inaonesha wazi kabisa kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi bilioni tatu ambacho hakitatosha kuendesha ofisi za Tume hii. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri anisaidie kupata ufafanuzi Tume hii itawezaje kushiriki katika vikao vya Kikanda na Kimataifa ukizingatia kwamba hakuna kiasi cha fedha kilichotengwa? Pia Tume hii itawezaje kusafiri nje ya nchi ikizingatiwa kwamba kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kusafiri nje ya nchi ni shilingi milioni nne tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania leo hii tunatambulika ni *grade A* katika mambo ya haki za binadamu. Inamaanisha kwamba Mwenyekiti na timu yake wakishindwa kusafiri kwenda kutengeneza hoja kule Umoja wa Mataifa tutashuka katika kiwango cha haki za binadamu. Kwa hiyo, naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri lakini sina haja ya kushika shilingi yake, ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa, wewe ulikuwa unaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh. Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lazima niseme kwamba mimi pia ni mmoja wa watu wenye *interest* katika haki za binadamu lakini niseme tu kwamba Tume hii imekuwa ikifanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia maneno ya mwenzangu Mheshimiwa Ally Saleh akisema kwamba *excuse* kwamba hali hii ni *across the board* inachosha, *but we are facing two options*, tuje hapa tudanganye au tuje hapa tueleze ukweli. *We are developing nation*, nchi ina-*competing interest*, kila mtu anataka dawa, kila mtu anataka elimu, kila mtu anataka usafiri. *It is not possible* kwamba kwa mwaka huu, kesho changamoto zote ziwe *solved at the same time*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naposema hivyo haina maana kwamba nina-*prioritize rights*. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Ally Saleh kwamba mimi ni mmoja wa watu ambao naamini katika *unity of rights* kwamba hakuna kitu kimoja ni muhimu kuliko kitu kingine, lakini lazima tuwe tunazingatia *practical realities of things* na Waziri amesema kwamba kuna pesa zingine zinatoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri lilizungumziwa leo kuhusu suala la *reporting*, kwanza suala la *human rights reporting* lipo katika Ofisi ya *Attorney General*. Kuhusu *reporting* ya *CRPD*, nilishaongea na watu wa Tume na bahati nzuri mchakato unafanywa, siwezi nikasema fedha inatoka wapi lakini tayari tuli-*discuss* namna gani mengine yanaweza yakafanyika ili hiyo *reporting* ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naposema *state reporting* ya Tume, sisemi kwa sababu ni kisiasa. *It is very interesting* kwamba wakati wengine sisi tulipopewa hizi teuzi, huwa nawaambia watu ni kama tuliambiwa tukayatekeleze tuliyoyaandika katika maandiko yetu. Kwa hiyo, ninaposema kwamba tunasaidiana kwa karibu kuhakikisha kwamba hii *state reporting* inafanyika ni suala la kweli na ni suala ambalo linatoka kwenye dhati ya moyo wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Wabunge tuunge mkono bajeti hii ipite kwa sababu isipopita sasa una-*create* tatizo lingine badala ya kusaidia kulikwamua hili lililopo. Kwa hiyo, naomba Wabunge wenzangu tuunge mkono ili bajeti ya Wizara ya Sheria ipite. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia vizuri Mheshimiwa Ally Saleh na Waheshimiwa Wabunge wote wakielezea umuhimu wa Tume hii ambayo mimi mwenyewe sikatai. Ni kweli kabisa kama Mheshimiwa Ally Saleh alivyosema nilikwenda kwenye Kamati Bajeti, nilishindwa ku-*support move* yao kwa sababu mimi niko kwenye Serikali naelewa hakuna hiyo hela. Kwa hiyo, kama ni suala la kusema tu tunataka shilingi bilioni kumi ambazo unajua hazipo utapata shilingi bilioni tatu tu *at the end of the day* tunamdanganya nani? *This is serious government* ikisema itakupa shilingi bilioni tatu itakupa hizo hizo na ndiyo maana sisi tumejipanga ndani ya hizo bilioni tatu tutafanya nini!

Mimi ndiye Waziri, niko na hiyo Tume kila siku, naielewa vizuri, mimi nasema tutakwenda! Wewe mwenzangu unasema umewasikia wanalalamika, kila mtu analalamika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ya Katiba na Sheria, kuna watoto zaidi ya tisa pale, sijui wote umewasikiliza kama wana magari! Nachosema tu ni kwamba sisi tunaielewa, kwa kuanzia bajeti hii itatutosha lakini mwaka kesho tuna kazi kubwa kweli kweli kwa sababu *external funding* itaanza kuisha na sasa hivi Serikali ndiyo tunaanza kujiandaa namna ya kumbeba huyu mtoto kwa mbeleko yetu sisi wenyewe, sasa tukianza sasa hivi madai mnatuvunja moyo. Nakuomba Mheshimiwa Ally Saleh achana na mambo ya shilingi hayo, naweza kukupa nyingine nje lakini hii achana nayo ili tusaidiane. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye Kamati moja tusaidiane kuijenga hii Tume. Hii Tume wote tunakubaliana ni ya msingi, ni muhimu, mimi nikuambie nini? Mimi ndiye Waziri na Katibu Mkuu wangu naelewa naye ni *human rights activist* kama mimi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nimuombe Mheshimiwa Ally Saleh atuelewe sisi tunaamini vilevile bajeti hii haitoshi kwa Tume lakini haitatufanya tushindwe ku-operate kwa sababu kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, sisi tunaomba utuunge mkono tuweze kuitekeleza bajeti hii. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasema mimi situmii shilingi natumia dola kwa hivyo hata ukinipa shilingi yako haisaidii kitu. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ni mwalimu wangu lakini *I see here the government is evasive of a very crucial issue in our country. Mimi for the sake of principles I won't compromise.* Bora mpitishe kwa kura, sawa lakini mimi na-hold shilingi. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

**MWENYEKITI:** Hoja hiyo imekataliwa, tunaendelea. Mheshimiwa Tundu Lissu. (Makofi)

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba maelezo ya Waziri kuhusiana na Sera ya Usimamizi wa Nidhamu ya Majaji wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wetu kama Kambi Rasmi ya Upinzani na katika mchango wangu binafsi nimezungumzia tatizo la usimamizi wa nidhamu ya Majaji. Tuna utaratibu uliowekwa kwenye Katiba. Majaji ambao wanatuhumiwa kwa utovu wa maadili, Katiba imezungumzia ambao wanaweza kuondolewa kwa sababu wana tabia mbaya, wanatakiwa waundiwe Tume ya Uchunguzi ya Kijaji. Tangu mwaka 1991, Jaji Mwakibete alipoundiwa Tume na kuondolewa wakati wa Urais wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi hakujawa na Tume nyingine ya Kijaji kuchunguza matatizo ya kinidhamu ya Majaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limepitisha Azimio tarehe 30 Novemba, 2014 kuhusiana na Majaji wa *Tegeta Escrow* kwamba Majaji hawa ambao ushahidi uliletwa Bungeni hapa waundiwe Tume ya Uchunguzi, hatukusema wafukuzwe, hatukusema wafungwe, tumesema waundiwe a *Judicial Commission of Enquiry to investigate their ethical status*. Leo mwaka na nusu hakuna majibu. Kwa hiyo, Bunge tulikaa hapa kupoteza muda tu, haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mapema kama maelelezo hayakutosheleza kwa nini Tume ya Uchunguzi wa Kijaji ya Majaji wa *Escrow*, Jaji Aloysius Mujulizi na Jaji Profesa Eudes Ruhangisa haijaundwa, kama imeundwa ripoti iko wapi? Hili lilikuwa ni Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna maelezo ya kutosheleza, nitashikilia shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza haya mambo tuyaweke wazi, Bunge hili siyo mamlaka ya nidhamu ya Majaji. Katiba iko wazi, Ibara ya 113 imieleza vizuri suala hili, kuna *Judicial Service Commission* (Tume ya Utumishi wa Mahakama) kama kuna Jaji anatumia basi hiyo Tume inafanyia kazi suala hilo na inapendekeza kwa Mheshimiwa Rais. Inategemea Tume yenyewe imemshauri nini, ndipo Rais anapoweza kuunda hiyo Tume na ina *cut across* inaleta watu kutoka *Commonwealth*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in this case let me tell you*, baada ya zile tuhuma, lakini twende na mstari ule kwamba Bunge hili siyo mamlaka ya nidhamu ya Majaji na maazimio yanaishauri tu Serikali la sivyo kutakuwa na mwingiliano wa madaraka. Bunge likishaazimia Serikali inaenda inatafakari kwa sababu ni lazima itekeleze pia kwa kuzingatia Katiba na sheria za nchi zilizopo. Mheshimiwa Rais Kikwete alisema siku ile pale *Diamond Jubilee* kwamba hawezi kwenda moja kwa moja hivi akakiuka utaratibu ule wa Katiba. Kwa hiyo, suala hili likaenda kwenye *Judicial Service Commission*. *Judicial Service Commission* ilipo-*investigate* lile suala ikashindwa kupata ushahidi wa kuridhisha wa kuwa-*convict* wale Mheshimiwa Majaji na hizo tuhuma za kifisadi. Kwa hiyo, wakamshauri Rais na Rais akaridhika hakuona sababu kwa sababu si suala rahisi kumchukulia Jaji hatua hovyoyovyoyo tu kwa sababu umezungumza humu ndani. Kwa hiyo, hiyo Tume haiwezi kuundwa, Rais alishalitolea maamuzi suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwenye hili ni lazima tuweke mipaka yetu sisi, haya mambo yaliyomalizika kwenye Bunge la Kumi yameisha, ndiyo Ibara ya 65 inavyosema.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Yanayoi-bind Serikali ni yale yaliyotungiwa sheria. Bunge hili haliwezi likafunga Bunge lingine. Kwa hiyo, kama unataka hiyo, *you just bring* hoja mahsusi, ndiyo Kanuni ya 64 inavyosema, ndiyo hivyo tu la sivyoyamambo hayataisha, kwa hiyo, ni lazima tuelewe hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia si vyema kuwa-accuse Majaji ambao wako hapa, *we cannot afford this one, so much serious!* Tunapotumia uhuru wetu wa kuzungumza humu na kutetea Kanuni zetu ziko wazi. Nimewasomea Katiba, Ibara ya 30(2)(d) heshima ya Mahakama lazima ilindwe na heshima ya mtu yeyote, sisi hatuwezi tukakaa hapa tukajifanya sisi wenyewe ni Majaji, sisi siyo *disciplinary authority* ya Majaji, *that is very clear*, haiwezekani, ni lazima tuwaheshimu. Sisi wanasheria tunaitana *learned brother*, mara nyingine tunaitana Waheshimiwa, *that is so much important and this is in the Constitution. I think you can have scores but not in this way!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri Mheshimiwa Tundu Lissu, hili alielewe, kwanza mambo mengine yako Mahakamani, hata haya ya *Escrow* anayoyazungumza yako Mahakamani, nafikiri ifike mahali ifikie mwisho tu. Mheshimiwa ameshauri Bunge lakini *at this time around there is no need* hata ya kuiondoa hiyo shilingi. Mimi naomba kushauri hivyo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni ya ajabu kabisa! Naomba niweke rekodi sawasawa. Jaji Mkuu amesema mwezi Disemba mwaka jana akizungumza na waandishi wa habari kwamba Tume ilishaundwa inaongozwa na Jaji Mbarouk Salim Mbarouk na ina Majaji wengine wawili.

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Jaji Mkuu akasema kwa maneno yake kwamba taarifa ya Tume ilikwishaiva. Huyu *Attorney General* wa wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jaji Mkuu amesema taarifa iko tayari, Bunge lilipitisha, nani aliyesema hapa kwamba Bunge linatoa hukumu? Bunge lilisema Rais aunde Tume, ndiyo Katiba inavyosema. Haya maneno ya *Attorney General*



ndiyo maana wakati mwingine tunakuwa na shaka, hivi viatu vinamtosha kweli?  
(Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye anasema Bunge lihukumu, Azimio la Bunge lilikuwa *absolutely clear*, Rais aunde Tume ya Uchunguzi ya Kijaji ili kuchunguza tuhuma za kupokea miamala ya Escrow shilingi milioni mia nne, mia nne! Hakuna mtu anatoa tuhuma hizi juu juu, hizi ni tuhuma zilizoletwa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge. Sasa *Attorney General* bahati mbaya ulikuwa Naibu wakati ule kwa hiyo hukuwepo na pengine labda hukusoma. Bunge linapotoa Azimio au Bunge linapotoa kauli haiwezi ikawa ni kauli ya bure.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe hoja, Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono tujadili hili suala. Tuambiwe Sera ya Nidhamu ya Majaji wa nchi hii ikoje? Naomba kutoa hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, wasimame watakochangia. Mheshimiwa James Millya, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Olenasha na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi.

**WABUNGE FULANI:** Na sisi Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu unakimbia kwa hiyo nimechukua wachangiaji watano wa hoja hii. Tunaanza na Mheshimiwa Millya.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu kwa asilimia 100. Tunachojaribu kusema hapa si kwamba nchi hii haijawahi kuwa na Majaji wazuri, tumeshakuwa na aliyekuwa Jaji Mkuu, Jaji Nyalali na Jaji Mwalusanya. Kwa kipindi hiki kidogo kilichopita tumekuwa na Majaji wabaya ambao wanatumia nafasi yao vibaya.

Hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu ni kwamba tunaomba Maazimio ya Bunge hili ambayo yamesema kwamba Majaji hawa walikuwa wabaya na wamevuruga *fraternity* ya kisheria, Bunge hili lishikilie maamuzi yake na Majaji hawa wachunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wakenya tunawacheka kwa vitu vingi, lakini wenzetu wameanzisha kitu kinachoitwa *Magistrate and Judges Vetting Board*. Mimi niko kwenye nyanja hii ya sheria na wewe mwenzangu najua ni mwanasheria, watu wengi wanaharibu sana! Tunaomba Bunge hili liweke historia ya kusimamia haki katika nchi yetu ili haki ya Watanzania wanyonge ipatikane. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja iliyo mezani kama ifuatavyo; kwanza, kutokuwepo kwa *incidences* nyingi za kuchunguzwa Majaji tokea wakati wa Jaji Mwakibete haimaanishi kwamba kuna tatizo. Wingi wa *incidences* hau-*justify* umakini wa usimamizi wetu wa sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu cha pili, tunavyozungumzia kuhusu uhuru wa Mahakama na mgawanyo wa madaraka inatakiwa tuwe waangalifu sana kama Bunge. Tunaporuhusu kirahisi Bunge liweze tu kuanza kujadili na kushambulia mhimili mwingine ni hatari sana katika uhuru wa Mahakama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba katiba Bunge hili, baadhi yetu tumeshakuwa na kesi za uchaguzi mahakamani na wengine tunakuwa na hisia kuhusu namna mhimili ulivyotutendea haki, tukiachia Bunge hili liweze kusukuma suala kama hilo kuna hatari ya kuhatarisha uhuru ule wa Mahakama. Kwa hiyo, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Lissu ya kutaka suala hilo lifanyiwe kazi, mimi nafikiri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Kushikilia shilingi haisaidii lakini nafikiri Serikali kama tulivyosema imepata ujumbe kwamba hili suala lifuatiliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lililopita tulikesha sana kuhusiana na suala hili la *Escrow* na suala hili la *Escrow* ndiyo lilimuondoa hata mtangulizi wa AG. Suala hili la *Escrow* ndiyo hata akina Profesa Tibaijuka wamelazimishwa kulipia kodi hela walizosema za mboga. Kwa hiyo, ilikuwa ni suala ambalo kama Bunge tulitimiza wajibu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge wengine tusitake ku-*spin* mambo hapa kwamba tunaingilia mhimili mwingine. Bunge tunatimiza wajibu

wetu na maamuzi tunayofanya hatupotezi muda hapa. Majaji siyo kwamba wao ni *untouchable* na hatujasema wamefanya kosa! Wachunguzwe, wakionekana wako salama hakuna tatizo, hakuna mtu ambaye ni *untouchable* hapa. Sasa Bunge tunaanza kukimbia wajibu wetu kusimamia utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Lissu hapa hatumu-accuse mtu! Tuliambia wote hapa! Sasa ni Wabunge wa aina gani Bunge hilo hilo linaamua kesho linageuka? Juzi walikuwa wanashangilia hapa wakakesha watu hapa na wakapiga makofi, kesho tena hao hao wamelalia upande mwingine, *what do we believe? What are we standing for?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Lissu ni ya msingi sana, ni lazima ile Tume itoe ripoti. Naomba Mheshimiwa AG hebu *peruse peruse* kidogo tafuta mambo yalivyokuwa yameandikwa vizuri kusudi usipotoshe umma. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua lazima tuheshimu tu sheria. Juzi hapa tulikuwa tunazungumza juu ya *Commission of Inquiry*, nadhani nilikuwa najibu swali. Hapa una Katiba inaeleza utaratibu wa kuwachukulia hatua ya nidhamu Majaji *then we have the Judiciary Administration Act* sasa utawezaje tena kuwaundia *Commission of Inquiry*?

**MBUNGE FULANI:** Katiba.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** No! Katiba inachozungumza ni Tume nyingine siyo ile *Commission of Inquiry, that is it!* Tusichanganye! Kuna *Commission of Inquiry* yameorodheshwa yale mambo. Jana Mheshimiwa Mbunge mmoja alikuwa anauliza habari za *cooperation performance* na tukamjibu hapa na ile sheria iko pale. Majaji hawa nidhamu yao inasimamiwa na Katiba na ile *Judiciary Administration Act*. Kwa hiyo, kama kuna *allegation* kuna *committee* ndani ya *Judicial Service Commission* yenyewe inachunguza, inaripoti kwenye ile *Commission* yenyewe *and then Commission* inamshauri Rais. Rais akiridhika ndiyo anaunda Tume sasa ambayo inajumuisha siyo Majaji wa Tanzania tu kwa sababu *Commission of Inquiry* unayosema hiyo wajumbe wako wanakuwa ni Watanzania tu *in this case* lazima upate na wajumbe kutoka *Commonwealth*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri Waheshimiwa ni lazima tuzingatie mipaka ya mamlaka yetu. Hizi sheria pia tuzielewe, tunazitunga sisi wenyewe. Mambo haya yalishapita na Bunge la Kumi, hatuwezi kulifufua hili! Kama unataka kulifufua lije kwa hoja mahsusi, *that is it!* Ndiyo Kanuni ya 64 inavyosema na mimi ni mjumbe wa *Judicial Service Commission*. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *I am an authority on this one because I am a member of the Judicial Service Commission, so I know what happened.*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mimi ni Mjumbe wa hiyo *Judicial Service Commission*.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa AG muda wetu siyo rafiki. Mheshimiwa Tundu Lissu mtoa hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ibara ya 110A(3) inasema; "Iwapo Rais anaona kuwa suala la kumuondoa Jaji kazini lahitaji kuchunguzwa, basi katika hali hiyo utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Rais anaweza baada ya kushauriana na Jaji Mkuu kumsimamisha kazi Jaji huyo;

(b) Rais atateua Tume ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili ..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni *very simple*. Hoja yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaikwepa kwepa tu. Jaji Mkuu wa nchi hii amesema kuna Tume imeundwa ina Wajumbe watatu, inaongozwa na Mwenyekiti Jaji wa Mahakama ya Rufaa Mbarouk Salim Mbarouk. Mwezi Disemba amesema Tume hii imeshakamilisha taarifa yake, taarifa imeiva, imebakia kupakuliwa! Maneno ya nani?

**MBUNGE FULANI:** Jaji Mkuu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Ya CJ! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *Attorney General* anatuambia nini hapa? Haya maneno kwamba Bunge linataka kuwaadhibu Majaji yametoka wapi? Bunge lilipitisha Azimio, Rais aunde Tume, Rais ameunda Tume kwa maneno ya Jaji Mkuu. (Makofi)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa, samahani naomba ukae.

**WABUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae Mheshimiwa Mchengerwa, malizia Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MBUNGE FULANI:** Kwenye Kamati hamna Taarifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Bunge hili lisimamie *principle*. Kama kuna Azimio lilishapitishwa, inaelekea limefanyiwa kazi kama tunaamini maneno ya Jaji Mkuu, inaelekea kuna Tume iimeundwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Naam!

**MWENYEKITI:** Tumefika mwisho sasa, naomba umalizie hoja yako.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Ahsante. Kwa hiyo, mimi bado nashikilia shilingi yangu kama Wabunge wanaona kwamba haya majibu mepesi mepesi ni sahihi wapige kura na kama wanaona majibu haya ni mepesi mno wayakatae.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Sawa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

**MWENYEKITI:** Hoja hiyo imekataliwa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye *guillotine* sasa kwa mujibu wa Kanuni ...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, naomba ukae tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 104(2) inatupeleka kwenye kupitisha vifungu na kusitisha majadala, Katibu.

Kif. 1001	Administration &HR Mgt .....	Sh. 6,207,700,000
Kif. 1002	Finance and Accounts .....	Sh.183,688,000
Kif. 1003	Policy &Information Services .....	Sh.369,360,000
Kif. 1004	Internal Audit Unit .....	Sh.114,900,000
Kif. 1005	Govt. Communication Unit .....	Sh.56,468,000
Kif. 1006	Procurement Mgt. Unit .....	Sh.102,516,000
Kif. 1007	Mgt. Information System Unit .....	Sh.104,480,000
Kif. 2004	Public Legal Services Unit .....	Sh.439,240,000
Kif. 4001	Constitutional Affairs .....	Sh.177,240,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 55 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif.1001	Administration &HR Mgt .....	Sh.1,424,334,000
Kif. 1002	Finance and Accounts .....	Sh.135,360,000
Kif. 1003	Internal Audit Unit .....	Sh.129,852,000
Kif. 1004	Legal Services .....	Sh.176,880,000
Kif. 1005	Procurement Unit .....	Sh.24,600,000
Kif. 1006	Mgt. Information System Unit .....	Sh.84,192,000
Kif. 2001	Administrative Justice .....	Sh.648,840,000
Kif. 2002	Human Rights .....	Sh.398,340,000
Kif. 2003	Research and Documentation .....	Sh.113,496,000
Kif. 2004	Public Education and Training .....	Sh.120,236,000
Kif. 3001	Zanzibar Office .....	Sh.121,500,000
Kif. 3002	Mwanza Office .....	Sh.0
Kif. 3003	Lindi Office .....	Sh.0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001	Administration & HR Mgt .....	Sh.1,658,192,000
-----------	-------------------------------	------------------

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

## KITABU CHA NNE

### MIPANGO YA MAENDELEO

#### Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1003 *Planning Division* .....Sh.1,000,000,000

Kif. 3002 *Treaties and Contracts Division* .....Sh.0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1003 *Policy & Information Services* .....Sh.1,396,472,613

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 2002 *Human Rights* .....Sh.100,000,000

Kif. 2003 *Research and Documentation* .....Sh.79,959,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, Taarifa.

### TAARIFA

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila marekebisho. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.



Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono sasa nitawajohi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa bajeti yake kupitishwa na Bunge hili. Nichukue pia fursa hii kumtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu ambayo ameyaomba fedha kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja hapa ambalo limetoka kwa *Chief Whip* wa Chama cha Mapinduzi kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi baada ya kutoka hapa watakutana kwa ajili ya *caucus* ukumbi wa Msekwa usiku huu. Kwa hiyo, wakitoka hapa wote wanapaswa kwenda kuhudhuria kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, nimekumbushwa hapa kwamba tuzingatie Kanuni hasa ya 64, wote tukasome, vitu vilivyokatazwa na ile Kanuni tusivifanye ndani ya Bunge kwa sababu vinatupotezea muda ule ambao tunatakiwa kuisimamia na kuishauri Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu, tarehe 6 Mei, 2016

*(Saa 2.26 Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa,  
Tarehe 6 Mei 2016, Saa Tatu Asubuhi)*